

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Arobaini na Tano Tarehe 12 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusimame dakika chache, tumkumbuke shujaa wetu Major General Silas Mayunga (Mti Mkavu) ambaye amepoteza maisha yake na wanamzika leo kule kwao Mara.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walisimama kwa muda wa dakika moja)*

**SPIKA:** Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi Amina.

Waheshimiwa Wabunge, historia ya marehemu wetu wote mnaifahamu, alishiriki katika mapigano makubwa ya ukombozi wa nchi yetu dhidi ya Nduli Iddi Amini. Kwa sababu hiyo, Bunge letu tumewakilishwa na Mwenyezeki wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa na Mjumbe mwingine wa Kamati hiyo Mheshimiwa John Shibuda na bahati nzuri yeze pia ni Mbunge wa eneo hilo. Kwa hiyo, tumewakilishwa kwa utaratibu huo.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 406

**Utaratibu wa Kuwapa Kazi ya Muda Wanafunzi  
wa Elimu ya Juu Wawapo Likizo**

**MHE. MUSSA Z. AZZAN** aliuliza:-

Miaka ya nyuma Serikali ilikuwa inawatumia wanafunzi wa elimu ya juu wanapokuwa likizo kufanya kazi ambazo zinawapa uzoefu na kujipatia kipato cha kujikumu maisha:-

Je, Serikali haioni haja ya kurudisha utaratibu huo, pia kwa kuzielekeza Halmashauri na Idara zake kutenga bajeti maalum ya kutekeleza mpango huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Z. Azzan, Mbunge wa Ilala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa utaratibu wa wanafunzi kujitolea wakati wakiwa likizo ulikuwepo katika miaka ya nyuma, ili kuziba pengo la wataalam katika Utumishi wa Umma kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ulisitishwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo kupatikana kwa wataalam wa kutosha katika kada nyingi za Utumishi wa Umma. Hata hivyo pale ambapo wanafunzi hao watapenda kujitolea, mamlaka za ajira hazizuiwi kuwatumia ili mradi waweze kukidhi viwango vya kazi vilivyopo katika mamlaka hizo.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa mazingira ya sasa hivi na kwa hali ya maisha yalivyo sasa hivi, je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuweza kuziwekea bajeti Halmashauri ili wanafunzi hao wanapokuwa likizo waweze kwanza kupata uzoefu, pili kutojiingiza katika makundi mabaya au maadili mabaya mitaani lakini vilevile kujipatia chochote ambacho kinasaidia kujikimu katika maisha yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, ni kama nilivyosema kwamba utaratibu huo haupo, lakini pia haukatazwi na waajiri pale ambapo wanaona ni muhimu kuwatumia wanafunzi hao pale ambapo kuna mahitaji ya lazima hawakatazwi kuwatumia na uwezo unaporuhusu pia hawakatazwi kulipa angalau pesa kidogo za kijikimu au za kuwasaidia nauki ya kwenda na kurudi katika kazi hizo.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania sasa hivi kuna mashirika mbalimbali na makampuni yanayotoka nje ya nchi kufanya kazi hapa mbali ya kuwapeleka hawa vijana katika Serikali, je, Wizara husika haioni kwamba ni wakati muafaka sasa kujadiliana na mashirika hayo au wawekezaji hao walau kuchukua asilimia 50 ya vijana hawa ili wapate uzoefu zaidi kuzidisha CVzao na angalau watapata chochote cha kuwasaidia mitaani wakati wa likizo zao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, wazo lake ni zuri na tutajaribu kushauriana na Wizara nyingine husika ili tuone kwa kiasi gani vijana wetu tunaweza kuwatumia kipindi cha likizo ili waache kuzagaazagaa.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Sasa hivi kuna Walimu wengi ambaao wamemaliza Chuo Kikuu cha Dodoma na Vyuo vingine vya Ualimu ambaao wakati huu wanabiri ajira za Serikali. Je, Serikali nayo haiwezi ikaangalia utaratibu wa kuweza kuwatumia Walimu hawa wakati huu wakisubiria ajira kwa utaratibu wa mikataba mifupi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo Walimu ambaao sasa hivi wanabiri ajira. Kwanza tunasubiri matokeo yao lakini pia kwa utaratibu ambaao tumejiwekea ni kwamba tunasubiri hii bajeti yetu itakapomalizika ndipo sasa tuenze kuwapanga katika vituo vyao vya kazi. Sasa kama wapo waajiri ambaao wana uwezo wa kuweza kuwatumia na wakati huohuo wakawalipa basi wanaweza wakawatumia. Swali la msingi liliulizwa kujitolea na hatumkatazi kijana yejote ambaye yupo mtaani kwenda kujitolea haswa katika sekta ya elimu ambako tuna shida kubwa sana na Halmashauri ambazo zina uwezo kwa kweli tunawashauri wawatumie na kuweza kuwalipa wakati tukisubiri utaratibu wa Serikali wa kuwaajiri moja kwa moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nashawishika kusema, mnaona alivyouliza muuliza swali, maswali ya nyongeza yalivyokuwa mafupi na Waziri alivyojibu? Tumepata wachangiaji watatu wa maswali ya ziada kwa sababu ya ufupi wa maswali na majibu mafupi. Tukifanya hivi, tutakuwa tunamaliza maswali yetu vizuri. Hivi ndiyo inavyotakiwa, siyo kuhutubia wenzeni hapa si mahali pake. (Makof)

Na. 407

#### Huduma ya Simu za Mkononi Nkasi Kusini

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Katika jimbo la Nkasi Kusini wananchi wa Kata ya Kala, Wampembe na Ninde hawana kabisa mawasiliano ya simu za mkononi, vilevile Makao Makuu ya Jimbo yaliyoko Kata ya Kate hakuna mtandao wa kuaminika.

- (a) Je, Serikali iko tayari kuzungumza na makampuni yanayotoa huduma hiyo ili kuwaunganisha wananchi hao na wananchi wengine?

(b) Je, ni lini wananchi wategemee huduma hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutoptana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika zoezi la kufikisha huduma za mawasiliano katika baadhi ya maeneo nchini, Serikali inashirikiana na Makampuni ya Simu nchini kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*) ili kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu tayari umeainisha jumla ya vijiji kumi na nane (18) katika Mkoa wa Rukwa vyenye ukubwa wa eneo la jumla ya kilometra za mraba ishirini na sita elfu mia nane sabini na tatu (26,873) kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013 yakiwemo baadhi ya maendeo ya Jimbo la Nkasi yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kutoptana na sababu za kiutalaam, Kampuni ya *Vodacom* ina mpango wa kuanza kujenga mnara katika Kata ya Wampembe ambaotutawezesha mawasiliano katika maeneo ya Ninde na Kala. Aidha, Kata ya Kate ipo kwenye orodha ya maeneo yatakayofanyiwa utafiti mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kampuni ya *Airtel* tayari wameyaweka maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge katika mpango wake wa kuyafanya tena tathmini kabla ya mwisho wa mwaka 2011.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha shughuli ya kufikisha huduma za mawasiliano, kuna mchakato mkubwa sana unaofanyika kuanzia tafiti za Kibashara, Kijiografia na Kiufundi kabla ya eneo kuwekewa mnara wa mawasiliano ya simu. Hivyo muda wa kutekeleza mpango wa kuweka minara ya simu hutegemea zaidi matokeo ya tafiti hizo. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau husika ina mpango mkakati ulioainishwa katika jibu la sehemu (a) ifikapo mwaka 2013 na itaendelea kuwashimiza wadau wote wa Sekta ya Mawasiliano kukamilisha tafiti zao katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge mapema iwezekanavyo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Kata ya Kala, Kwampembe na Ninde pia imekuwa na matatizo ya kiusalama na mawasiliano ya simu yangekuwa jibu zuri na kwa kuwa amesema kwamba mwaka 2013 ndiyo tuna uhakika wa kupata mawasiliano hayo, mimi naona bado ni mbali. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha kwamba tunapata mawasiliano ya haraka hasa kwa vile suala hili linahusu suala la usalama katika mwambao mwa Ziwa Tanganyika?

Swali la pili, katika mpango wa *UCAF* kwa maana ya mawasiliano kwa wote, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi au Wilaya ya Nkasi imekuwa ikipata miradi kwa kuchelewa. Je, Waziri anakubaliana na ushauri kwamba katika utekelezaji wake utekelezaji uanze katika Wilaya ya Nkasi na Jimbo la Nkasi Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mbunge kwamba mpango niliousema mpaka mwaka 2013 ni ule mpango wote kwa ujumla lakini maeneo niliyoyataja kwa mfano Kampuni ya *Airtel* wakati nakuja hapa nimewasiliana nao wamenieleza kwamba katika mwezi huu watawatuma wataalam wao kufanya utafiti katika maeneo niliyoyataja. Kampuni ya *Vodacom* vilevile wamenieleza kwamba wana mpango wa kuhakikisha kwamba baadhi ya Kata zitakuwa zimebekewa mawasiliano mwaka huu au mwaka kesho mwanzoni kabisa. Kwa hivyo, naposema mwaka 2013 simaanishi kwamba ndiyo Wilaya ya Nkasi au Jimbo la Nkasi litapata mawasiliano mwaka 2013, huo ni mchakato mzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi, namhakikishia kwamba si lazima tuanzie kule bali pamoja na *UCAF*, wadau wengine ambao ni Kampuni za Mawasiliano zinajipanga zenyewe bila kusubiri *UCAF*. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge mambo yake yatakuwa mazuri hivi karibuni.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ili na mimi niulize swalı dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la mawasiliano yaliyoko katika Jimbo la Nkasi Kusini yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko katika Jimbo la Lupa katika Kata za Luwalaje, Mamba, Mtandila, Matwiga, Mafyeko, Kambikatoto na Ufungo. Je, ni lini mawasiliano yatafika katika Kata hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Lupa ni kati ya Majimbo ambayo yako katika mpango wetu wa majoribio wa *UCAF*. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo tutakuwa tumejipanga vizuri na tenda imeshatangazwa maeneo hayo yataangaliwa kwa jicho la aina ambayo ye ye angependa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa tatizo linaloikumba Wilaya ya Nkasi ni sawa na tatizo lilloloko katika Jimbo la Mpanda Vijijini hasa katika Kata za Kabungu, Sibwesa na Katuma. Je, ni lini Wizara itapeleka huduma hiyo katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nipende tu kumhakikishia Mbunge kwamba Mkoo wa Rukwa kwa kweli katika tafiti zetu tumeona maeneo mengi sana hayana mtandao wa mawasiliano. Maeneo mengi yaliyoko katika Mkoo wa Rukwa hata ukiangalia katika jibu langu la msingi nimesema zaidi ya kilometra za mraba 26,000 zimefanyiwa utafiti kwa ajili ya kuwekwa kwenye mpango wa awali wa majoribio katika huu mpango wetu wa kupitia *UCAF*. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mbunge kwamba kwa mwaka huu tutajitahidi kadri tunavyoweza tuweze kufikisha mawasiliano katika eneo lake lakini kwa mpango mzima kufikia mwisho wa mwaka 2013 maeneo yote tungependa yawe yamefikiwa na mtandao.

Na. 408

#### **Ulipaji wa Bili Hewa za Maji – Sumbawanga**

**MHE. ABIA M. NYABAKARI** aliuliza:-

Katika Mji wa Sumbawanga, kuna mita za maji ambazo zinafungwa katika kaya za watu lakini huzunguka kwa upepo bila ya maji na wakati mwingine hutoa maji yenyе tope:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawapatia wakazi wa Sumbawanga maji safi yasiyo na matope hususan sehemu za Kizitwe?
- (b) Je, ni lini wakazi wa Rukwa wataacha kulipa bili za maji hewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wakazi wa Mji wa Sumbawanga hupata maji kutoka vyanzo vya mito midogo sita iliyopo katika msitu wa Mbizi, umbali wa kilomita 10 Mashariki ya Mji wa Sumbawanga. Mito hiyo ni Kanantumbi, Muva, Mwambazi, Momoka, Ndua na Namasapu. Shughuli za binadamu katika msitu huo zimesababisha vyanzo kuharibika na maji kupungua. Wakati wa mvua maji huwa na tope kutokana na mmomonyoko wa ardhi unaosababishwa na kuharibika kwa uoto wa asili katika mito.

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Sumbawanga hutibu maji kupitia mitamo yake miwili iliyopo Majengo na Kizwite. Maji yanayotumika Kata ya Kizwite hutoka Mto Ndua na hutibiwa

katika mtambo wa kusafisha maji wa Kizitwe. Wakati wa kiangazi, maji ya mto huo hupungua hivyo Mamlaka kulazimika kutumia maji ya Mto Namasapu ili kukidhi mahitaji. Maji ya Mto Namasapu huingizwa moja kwa moja kwenye mtandao wa kusambaza maji kwa sababu mto huo hauna miundombinu ya kufikisha maji kwenye mtambo wa kusafishia maji. Mto huo pia, uko katika usawa wa chini na kutokana na mwinuko maji hayawesi kufika kwenye mtambo bila kuwa na mashine ya kusukuma.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza kero ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga, Serikali inatekeleza Mpango wa Dharura (*Immediate Works*) kuititia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*). Katika mpango huo, jumla ya visima saba vimechimbwa kwa ajili ya kuongeza maji kwenye mtandao wa usambazaji maji. Usanifu wa miundomibinu ya kuunganisha maji hayo umekamilika na Mkandarasi wa Ujenzi *Herkin Builders Ltd.*, ameajiriwa. Kazi hiyo itagharimu shilingi bilioni 4.9 na itakamilika mwezi Desemba, 2011. Baada ya hapo Mto Namasapu hautatumika tena na huduma ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga itakuwa imeboreka.

(b) Mheshimiwa Spika, huduma ya maji katika Manispaa ya Sumbawanga hutolewa wakati wa mchana tu. Usiku hakuna huduma ya maji kwa kuwa muda huo Mamlaka huwa inajaza maji kwenye matenki yake. Wakati kwenye mtandao wa mabomba kukiwa hakuna maji hewa huingia na iwapo kutakuwa na koki zilizo wazi hewa hiyo itatoka kuititia koki hizo na kusababisha mita kuzunguka. Ili kuepuka tatizo la hewa kuzungusha mita, elimu imetolewa kwa wateja wote kuhakikisha koki zinafungwa wakati kunapokuwa hakuna maji kwenye mtandao.

**MHE. MUSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nina swali dogo sana.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu katika kazi zetu za Bunge humu ndani, kila siku maswali ya maji ni 40% isipokuwa leo tuna 10%, inaonekana ni tatizo kubwa katika nchi hii. Je, Serikali inatoa tamko gani kuondoa tatizo hili la maji kwa nchi yetu kwa sababu tatizo hili limedumu kwa miaka 50 na sasa inakuja miaka 50 mingine?

**SPIKA:** Mbona hotuba yake hajasoma? Jibu kifupi tu kwa sababu mtaeleza kwenye hotuba yenu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli maswali mwengi ambayo tunayapata Bungeni hapa yanahusu maji na hii inaonesha kwamba, maji ni huduma muhimu na ndio maana katika mpango wetu wa miaka mitano baada ya miundombinu ambayo tumeipa kipaumbele, maji inafuata baada ya umeme. Kila mtu inamgusa na ni lazima tuzungumze. Kwa hiyo, kuna mpango mzuri ambao tutakuja kuueleza tutakapowasiliha bajeti yetu kuona mikakati ambayo nchi nzima tumeipanga kuweza kupunguza tatizo hili la maji kwa wananchi wa Tanzania.

Na. 409

#### **Shirika la NSSF Kujihusisha na Miradi ya Ujenzi**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. DAVID Z. KAFULILA** aliuliza:-

Shirika la NSSF limekuwa mdau mkubwa katika uwezeshaji hasa kwenye miradi ya ujenzi:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani watumishi ambao ni wanachama wa Shirika hilo wanapata faida na hasara gani kutokana na uwekezaji wa NSSF?

(b) Je, hadi sasa NSSF imepata hasara kiasi gani tangu kuingia kwa Awamu ya Nne?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Watumishi ambao ni wanachama wa *NSSF*, wakiwa bado watumishi na baada ya kustaafu wanapata faida kutokana na uwekezaji unaofanywa na Shirika. Mafao ambayo yameainishwa kwenye Sheria iliyoanzisha Mfuko huu ni saba. Mafao hayo yamegawanyika katika mafao ya muda mrefu na mafao ya muda mfupi. Mafao ya muda mrefu ni mafao ya kustaafu, mafao ya ulemavu na mafao ya urithi. Mafao ya muda mfupi ni msaada wa mazishi, mafao ya uzazi, mafao ya kuumia kazini pamoja na mafao ya matibabu. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tangu 2005 mpaka 2010, Shirika limelipa jumla ya shilingi bilioni 339,099,780,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, tangu kuingia Awamu ya Nne, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii – *NSSF*, halijapata hasara yoyote bali uwekezaji umeweza kukua toka shilingi bilioni 424,899,090,000/= mwaka 2005/2006 hadi kufikia 1,029,206,200,000/= mwaka 2009/2010. Kwa kipindi hicho, mapato kutokana na uwekezaji yaliongezeka kutoka 26,464,500,000/= mwaka 2005/2006 na kufikia 83,233,750,000/= mwaka 2009/2010. Aidha, katika kipindi hicho, Shirika limeweza kupandisha kima cha chini cha pensheni kutoka 33,200/= hadi kufikia shilingi 80,000/= kiwango ambacho ni kikubwa kuliko viwango vya Mifuko yote Tanzania. Ongezeko hili ni sawa na 141%. Pia Shirika limeweza kuongeza pensheni zingine zote kwa 52%.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, yanaonesha wazi kabisa kwamba, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya *NSSF*, haujawea kupata hasara hata kidogo. Iwapo itathibitika kwamba, kuna maeneo ambayo Shirika la Hifadhi ya Jamii la *NSSF* limeweza kupata hasara, Mheshimiwa Waziri, utakuwa tayari kuwajibika?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, hapana sitakuwa tayari kuwajibika kwa sababu, hakuna hasara iliyopatikana. (*Makofii/Kicheko*)

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba *NSSF* haina hasara. Inaonekana *NSSF* inapata faida kubwa sana Tanzania na hivi sasa kuna tatizo kubwa la ukosefu wa umeme katika nchi yetu ya Tanzania kuititia vyanzo vya maji, sasa Serikali itakubaliana na mimi kwamba, sasa ni wakati muafaka wa kuiagiza *NSSF* ama kuikubalia *NSSF* kuwekeza katika kusambaza gesi ili sisi wananchi wa Tanzania tutumie vyanzo vya gesi badala ya kutumia tu maji? Je, Serikali itakubalia *NSSF* kuwekeza? Nafikiri nimeshaeleweka. (*Makofii/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, Shirika la *NSSF* liko tayari kuwekeza kwenye uwekezaji wowote ambao una tija kwa wanachama wake pale ambapo utafiti unafanyika na kuonekana kwamba kuna eneo la uwekezaji ambalo wanachama watapata faida lakini pili ni kwa faida ya nchi kiuchumi, basi sisi tutakuwa tayari kuwekeza. Kwa hiyo hilo analolizungumzia la kuwekeza kwenye umeme halina tatizo kubisa katika Shirika la *NSSF* na liko tayari kufanya hivyo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, anafahamu kwamba *NSSF* ina wanachama mpaka Kisiwani Pemba na hasa kwenye Jimbo langu la Wawi na kwamba wanachama hao bado hawajapata huduma zinazostahili kama vile za kupatiwa nyumba. Je, anawaambia nini wanachama wa *NSSF* walioko Jimbo la Wawi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, Shirika la *NSSF* kwa kweli linaangalia sana mahitaji na mafao ya wanachama wake. Wanachama kwa kweli wapo mpaka kule Pemba na *NSSF* wako tayari kuweza kuwasaidia. Sasa hivi kwa upande huo wa nyumba, Shirika kwa kuititia *SACCOS* za wananchama liko tayari kuwakopesha ili wanachama waweze kujijengea

nyumba. Hata hivyo, NSSF imekuwa ikijenga nyumba maeneo mbalimbali ili wanachama waweze kununua. Kwa hiyo, uwekezaji kama huo kama utaonekana unafaa kule Pemba na baada ya tathmini, tutakuwa tayari kufanya hivyo.

Na. 410

### Kuendeleza Sekta ya Kilimo Tarime

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** Aliuliza:-

Wananchi wa Tarime ni wakulima wazuri wa mazao ya chakula kama ndizi, mahindi na mihigo na sasa wanajhusisha na kilimo cha mazao ya biashara kama Kahawa, Tumbaku na Chai kwa kiwango cha juu na kufanya Bodi na Taasisi zinazosimamia mazao hayo kwenda kutoa program ya kupanua zaidi kilimo hicho:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kurekebisha Sheria inayozuia Kahawa ya Magamba kwenda kukobolewa nje ya eneo linalolima Kahawa?

(b) Je, kwa nini Serikali isishawishi Taasisi za Fedha na wawekezaji wa mitaji kuimarisha Viwanda vya Kukoboa Kahawa vinavyomilikiwa na vijiji na kujenga kiwanda kipyra cha Kukoboa na Kusindika Kahawa ili kuboresha kilimo hicho na kuinua kipato cha mkulima?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA)** aijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kahawa ya Tarime ni ya ubora wa kipekee kabisa na ipo kwenye kundi la Arabika, ngumu yenyewe ubora wa hali ya juu. Kwa hali hiyo, ikiipelekwa maeneo mengine kwa ajili ya ukoboaji na kupanga madaraja inaweza kuchanganywa na Kahawa nyingine hivyo kupoteza utambulisho na uhalisia wake. Umuhimu wa Kahawa ya Tarime kukobolewa na kutayarishwa Tarime ni kwamba, itawahakikishia wakulima wa Tarime kulipwa kutokana na ubora wa Kahawa yao. Vilevile Kahawa ya Tarime ikitayarishwa Tarime ajira itabaki Tarime.

(b) Mheshimiwa Spika, Bodi ya Kahawa inashirikiana na Halmashauri ya Tarime kuhamasisha vikundi vya wakulima kuanzisha Viwanda vidogo vya Kukoboa Kahawa Vijiji ili kuiongezea thamani. Kwa mfano, katika Kijiji cha Mriba, kiwanda kidogo kimoja tayari kimeanza kukoboa kahawa katika mwaka 2010/2011. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime inashauriwa kuendelea kuhamasisha wakulima kuititia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) kujenga viwanda vingine vidogo vitakavyomilikiwa na wakulima wenye.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya kidogo ya Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kiwanda hiki cha Mriba kikipanuliwa, kwa kiasi kikubwa kitasaidia sana kupunguza ulanguzi wa Kahawa ambayo Naibu Waziri amekiri kwamba, Kahawa inayozalishwa Tarime ina ubora wa hali ya juu sana. Je, ni lini Serikali itasaidia kupanua Kiwanda hiki cha Kahawa cha Mriba ili kiweze kusaidia wakulima wa Kahawa wasilanguliwe na walanguzi wa Kahawa?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tarime imebahatiwa kupata kilimo kingine cha mazao ya tumbaku na chai. Je, Serikali inasema nini hususan kuwasaidia wakulima hao kupata kiwanda kingine cha tumbaku na chai katika Wilaya ya Tarime?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunafuata utaratibu wa *D by D* na tayari tuna mipango ya *DADPS* kwenye ngazi ya Halmashauri na kwenye kila Wilaya, naomba kusisitiza tu kwamba, Wilaya ya Tarime ikishirikiana na Mheshimiwa Mbunge, wao wenyewe waweze kuibua program hiyo ya kupanua Kiwanda hicho cha Mriba. Mipango hiyo itakapokuwa imekamilika katika ngazi ya Halmashauri, kwa uhakika ngazi ya Wizara, tupo tayari kuunga mkono jitihada hizo na ikibidi fedha za nyongeza zitatafutwa ili Kiwanda hicho kipanuliwe kwa sababu, kwa asili yake pia zao la Kahawa, sio zao unaloweza kuvuna na kusafirisha pengine kwa sababu, unapovuna ni lazima ukamilishe mchakato mzima wa kukoboa, kukausha na kukaanga. Kwa hiyo, kwa hilo tupo radhi lakini kazi ya msingi ifanywe na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ujenzi wa viwanda vingine kwa mazao mengine kama Chai na Tumbaku kama alivyosema, jibu pia linafanana kwamba, wakulima wadogowadogo wa Chai na Tumbaku Wilayani Tarime, wao waibue mikakati na mipango ya kujenga Viwanda vya Kusindika Mazao haya aliyoyataja na sisi kama Wizara tutakuwa radhi kuandaa mazingira wezeshi kwa sababu, Sera ipo wazi kwamba, usindikaji ndio njia nzuri ya kuhakikisha kwamba, wakulima wananaufaika na mazao yao badala ya kuuza mazao ghafi.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Sheria ya Kahawa inaitaka Bodi ya Kahawa kuwaandikisha wakulima ili wawewe kutambuliwa na njia hii itasaidia sana wakulima kuweza kuaminika mbele ya Benki na kuweza kukopeshwa. Ni lini Serikali itailazimisha Bodi ya Kahawa kuwaandikisha wakulima wa kahawa katika Wilaya ya Mbanga?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, taratibu zipo wazi na nadhani wakulima anaowaongelea watakapokuwa tayari wamejiandaa, utambuzi hautakuwa na shida. Nadhani kazi ya msingi tu ikamilike na Bodi haitakuwa na kipingamizi ila kuwatambua kama walivyowatambua wakulima wa kahawa katika maeneo mengine.

Na. 411

#### Ruzuku ya Mbolea kwa Wakulima wa Chai

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI (K.n.y. MHE. JANUARY Y. MAKAMBA)** aliluliza:-

Mheshimiwa Rais, alipokuja Jimboni Bumbuli tarehe 13 Septemba, 2010 aliahidi kwamba, Serikali ingeanza kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa chai.

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu mfululizo, uzalishaji wa zao la Chai umekuwa unashuka kutoka tani 34,165 kwa mwaka 2008/2009 hadi kufikia tani 32,000 kwa mwaka 2010/2011. Hii inatokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukame, matumizi kidogo ya mbolea, lakini pia uhaba wa miche bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa zao hili na mchang'o wake katika pato la Taifa. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kutatua matatizo yanayodumaza uendelezaji wa zao hili la Chai. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kugharimia ruzuku ya mbolea, mbegu bora, miche bora ya Kahawa na Chai pamoa na dawa za Pamba na Korosho. Katika utekelezaji wa

ahadi ya Mheshimiwa Rais, ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa Chai, Taasisi ya Utafiti wa Zao la Chai Tanzania (*Tea Research Institute of Tanzania - TRIT*) imeanza kufanya utafiti wa matumizi ya mbolea kwenye zao la Chai. Matokeo ya utafiti huo yatasaidia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kupanga utaratibu mzuri wa kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima wa Chai. Aidha, Wizara pia katika mwaka huu wa 2011/2012, itazalisha na kutoa miche bora ya Chai milioni 10 kwa wakulima wa Chai.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la wakulima wa Chai wa Jimbo la Bumbuli linafanana kabisa na Jimbo la Korogwe Vijijini, hasa kwenye Kata ya Mhale, Mali, Bungu na Vugiri. Je, ni lini Serikali itapeleka mbolea ya ruzuku katika Kata hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivosema katika jibu la msingi, *TRIT* itafanya utafiti ambao si kwa Wilaya ya Lushoto tu peke yake, lakini katika maeneo yote yanayozalisha Chai. Kwa hiyo, kwa maana hii utafiti huu utafanywa na utafiti unafanywa kwa sababu, ruzuku imetolewa zaidi katika suala la kutafuta miche bora ya chai lakini haijawahi kutolewa ruzuku kwa upande wa kuweka ama kutumia mashambani mbolea, kama tunavyofanya katika mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo nijibu tu kwa kusema kwamba, utafiti huu utakapokuwa umekamilika, tutafahamu kama Wizara ni nini kinachopaswa kufanywa, wakulima wako wangapi, kiasi cha ruzuku inayotolewa kwamba itahitajika kiasi gani na hivyo pia maeneo aliyyataja yatanufaika kama zitakavyonufaika Kata na Vijiji vingine vinavyozalisha zao la Chai.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Serikali inatoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima, ambalo ni jambo jema sana, kuitia kwa mawakala na mawakala wanakopa kutoka katika mabenki na mpaka sasa mawakala hawajalipwa fedha zao na riba zinaendelea kuwaelemea, Serikali inasema nini juu ya mawakala wa pembejeo za ruzuku ambao hawajalipwa mpaka sasa?

**SPIKA:** Hawa ni wale wakulima wa Chai au wengine, wakulima wa Chai hawana hiyo ruzuku, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, suala la ruzuku kwa sasa linafanyiwa *management audit* na tunatarajia kwamba *audit* hiyo itakapokamiliika baadhi ya matatizo yaliyojitezea katika eneo hilo la ruzuku yanaweza yakatatuliwa likiwemo hilo alilolitaja la kuwalipa wakala wanaosambaza ruzuku.

Na. 412

#### **Hitaji la Umeme Tarafa ya Ndagalu**

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Tarafa ya Ndagalu katika Jimbo la Magu ni moja kati ya Tarafa ambazo hazijapata umeme kwa takribani miaka 50.

Je, ni lini sasa Serikali itawapelekea umeme wananchi wa Tarafa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festu Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Ndagalu, itapelekewa umeme kutokea Tarafa ya Magu Mjini ambako tayari kuna umeme, umeme huo utaoka kwenye njia ya umeme wa msongo wa KV.33 inayotokea Magu Mjini kwenda Mahaha. Tarafa ya Ndagalu katika Jimbo la Magu ni moja kati ya Tarafa ambazo hazina umeme wa Gridi ya Taifa katika maeneo yale. Tathmini ya awali iliyofanyika

illionyesha kuwa ili kuweza kupatia umeme maeneo ya Tarafa ya Ndagalu ambalo linajumuisha Vijiji vya Ng'anya, Kabilia, Shishani hadi Mahaha yenye inahitajika ujenzi wa njia ya umeme wa njia ya Msongo wa KV. 33 yenyewe jumla ya urefu kilomita 50, ufungaji wa transfoma kVA 50 katika vijiji hivi vya Ng'anya, transfoma mbili (2) za kVA 1000 *center* ya Kabilia, transfoma moja (1) ya 50KVA kijiji cha Shishani na transfoma moja ya 100 kVA kijiji cha Mahaha, pamoja na ujenzi wa njia za kusambazia umeme ili kuwafikishia umeme wananchi kwenye Vijiji hivyo vinne vilivyokusudiwa ambapo gharama yake inakadiriwa kufikia jumla ya shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo yaliwasilishwa *REA* tarehe 2 Juni, 2010. Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya kipaumbele iliyopendekezwa na Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kuombewa fedha kutoka Wakala wa Nishati Vijiji (REA). Kwa sasa hivi au kwa wakati huo labda niseme jumla ya wateja 250 walitarajiwa kuunganishiwa umeme chini ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatafuta fedha za utekelezaji wa mradi huu na tumeigiza *TANESCO* wafanye tathmini ya uwezekano wa kutekeleza mradi huu kwa awamu. Tutawasiliana kwa karibu na Mheshimiwa Mbunge ili kumpatia maendeleo ya tathmini hii.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Jibu la Serikali limesema kwamba mradi huu ambaeo ni wa kipaumbele kutoka Mkoa wa Mwanza umeombewa fedha kutoka Wakala wa Nishati Vijiji (REA) lakini Mheshimiwa Waziri amehitimisha kwa kusema kwamba ameagiza *TANESCO* wafanye tathmini ya uwezekano wa kutekeleza mradi huu kwa awamu, vipengele hivi viwili vimenichanganya kwamba anatekeleza *REA* au *TANESCO*?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kunichanganya huko, naomba kuuliza swali, tathmini iliyokuwa imefanyika awali ya mradi huu kuanzia Magu Vijiji kwenda Ng'anya, Kabilia, Shishani mpaka Mahaha, ilionyesha kwamba ni shilingi bilioni tatu na Serikali kipindi hicho ilisema kwamba shilingi billioni tatu ni nyingi sana kuweza kupatikana. Ikawepo njia mbadala ya kutoa umeme huu kutoka Taro, kuitia Kadashi, Maligisu kwenda Kabilia, ili hatimaye baadaye usambazwe kwenda Shishani, kwenda Ng'anya, pamoja na Nyang'anga. Sasa Mheshimiwa Waziri, anarudi kwenye mradi uleule wa bei kubwa ambaeo sasa unanitia mashaka kama kweli Wizara ina mpango wa kutekeleza mradi kama ambavyo tuliomba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema wameagiza *TANESCO* ifanye tathmini ya uwezekano wa kutekeleza mradi huo kwa awamu. Je, kwa sababu tathmini ilishafanyika kwa *line* zote mbili kutoka Taro, ama kutoka Magu Mheshimiwa Waziri kwa sababu *REA* ina mpango wa kuongezewa fedha kwa ajili kutekeleza miradi, je, badala ya kufanya tathmini anaweza kuwahakishia wananchi wa Ndagalu kwamba kwenye bajeti ya mwaka huu nguzo zitaanza kusimikwa ili mwaka ujao wa fedha umeme uweze kuwashwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi tu, maana maswali yenye yako wazi, naomba ujibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza lazima niseme kwenye maeleo yangu ya msingi sikukusudia kumchanganya, nilichosema ni kwamba pesa zile zimeombwa *REA* ni shilingi bilioni tatu, kuna vijiji vinne, lakini kwenye zile shilingi bilioni tatu wateja waliokadiriwa kuunganishiwa umeme ni wateja 250 tu. Kwa hiyo, ni mradi mkubwa lakini kuunganisha kufikia wateja ni mradi ambaeo siyo mkubwa sana. Kuna miradi mingine mikubwa ya *REA* ambayo inaweza ikawa ya shilingi bilioni moja au mbili lakini kuna wateja elfu mbili, elfu tatu. Sasa kwa sababu tuliukubali na kwa sababu tumeutengea na ni mradi wa kiupaumbele ulioombewa na Mkoa wa Mwanza, tumesema kwamba labda njia moja ukitoka huku Magu Mjini kwenda ndani ya Ndagalu pale, kuna vijiji vinne tuangalie kama wanaweza kuufanya kwa awamu, kwenda vijiji viwili kupeleka nguzo na lile pendekezo lake la kupeleka nguzo kwanza, halafu kupeleka nyaya baadaye ndiyo huko kwenyewe kutekeleza kwa awamu lakini hata hili ni lazima mafundi, wataalam wa *TANESCO* waseme kwamba ndiyo utekelezaji unawezekana ili upatikane ufanisi, kuliko kupeleka nguzo halafu zikae tu pale miaka mitatu, minne hazifanyi chocchte.

Mheshimiwa Spika, lakini hili lingine ni kweli, kuna mradi mwingine ambao unatokea Taro, Kadashi kwa Mheshimiwa Ndassa unakuja huku kwa Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, nao ni mradi ambao umefanyiwa tathmini unakwenda pale *Kabila Center* ambako kuna matumizi makubwa sana na mradi umekusudiwa kutekelezwa lakini kwa sababu ni miradi miwili sjapata bado tathmini ya utekelezaji kwa leo imefikia wapi. Naomba niwasiliane na Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu na Mheshimiwa Ndassa ili niwaambie utekelezaji huu wa Taro, kupitia pale *Kabila Center* utekelezaji ni lini kwa sababu unawahusu wote wawili.

**SPIKA:** Ndassa anauliza swali la nyongeza sijui ndiyo hilohilo? Mheshimiwa Ndassa!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Umeme kuupeleka Tarafa ya Ndagalu, badala yake ni kuutoa Taro, Kadashi, Nyashana, Nyaligisu mpaka *Kabila Center*, lini mpango huu utaanza au kwenye bajeti ya mwaka huu utakuwemo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, sema usikike.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya awali, huu ni mradi ambao unakidhi pia kufikisha maeneo haswa kwenye hili eneo la *Kabila Center* na ni mradi ambao unapita kwenye maeneo ya Mheshimiwa Ndassa ambayo yanapokea umeme ule uliotoka Kwindwa kwenda Malia kwa njia hii nyingine ya kuja Sumve. Kwa hiyo, naomba niseme kuna mradi pale uliokuwa unatekelezwa na huu ni mradi ambao Mheshimiwa Ndassa ameuombea pesa muda mrefu, naomba nisijifunge njue kama *REA* au *TANESCO* ni nani tumekusudia watekeleze mradi huu lakini ni mradi ambao umepatiwa kipaumbele kwa kutekelezwa. Kwa hiyo kama nilivyosema wakati najibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, naomba niwapatie maelezo ya uhakika baadaye kidogo.

**SPIKA:** Sisi tunajuaje kama wamepata maelezo, Mheshimiwa Naibu Waziri? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, maelezo ambayo nakwenda kuyatafuta kwa sababu mradi wenyewe ulishakusudiwa kutekelezwa lakini...

**SPIKA:** Swali langu ni dogo, sisi tutajuaje, maana nyie mnaambiana mtaleezana huko, sisi tutajuaje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tutarejea kulielezea Bunge kwamba tulishaafikiana. (*Kicheko*)

Na. 413

#### Wananchi Kuwekewa Umeme

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Baada ya kuanzishwa kwa mradi wa umeme wa gesi ya Mnazi Bay wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi walihidiwa kuvutiwa umeme majumbani kwa gharama ya shilingi 60,000/-

Je, kwa nini ahadi hiyo hajatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastasia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Agosti, 2003 kwa kufuatia kuthibitika kwa uwepo wa gesi asili ya kutosha Mnazi Bay, Serikali na Shirika la Maendeleo ya Petroli, *TPDC* ilisaini mkataba wa makusudio (*agreement of intent*) na kampuni ya ARTUMAS, kwa ajili ya kuendeleza gesi ya Mnazi Bay na kuzalisha umeme pale wa kusambazwa katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Septumba, 2007,

Serikali ilisaini mkataba wa kupatiwa msaada wa fedha kutoka Serikali ya Uholazi, kiasi cha Dola za Marekani 28.8 kama bilioni 44 hivi kuititia Taasisi ya *ORET*, kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya kusambaza umeme pamoja na kupunguza gharama za kuunganisha wateja wapya. Katika mpango huu wa *ORET* wateja walikuwa wanatakiwa kulipa shilingi 60,000 tu za *VAT*, badala ya gharama ya jumla ya kuunganishiwa umeme wakati huo ya shilingi 395,000.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza utekelezaji wa hatua mbalimbali za mradi, mambo yafuatayo yaliyojitokeza:-

(i) Hali ya kifedha ya ARTUMAS kuwa duni kutohana na kudorora kwa hali ya uchumi duniani. Hali hiyo ilisababisha kampuni ya ARTUMAS kuuza sehemu za hisa zake, ambapo kwa sasa inamiliikiwa na kampuni ya *Wentwork Resources*. Hatua hii ililenga kuimarisha uwezo wa kampuni ya ARTUMAS kifedha. Aidha, Serikali iliipatia mkopo wa Dola za Marekani milioni saba ili kujaribu kuhakikisha kuwa shughuli zinazohusiana na mradi ule zinaendelea.

(ii) Tarehe 31 Mei, 2010, msaada wa *ORET* wa Dola za Marekani, milioni 28 ulisishwa baada ya mwekezaji kushindwa kuthibitisha kuwa na fedha *matching fund/non grant fund* kwa ajili ya kuwekeza kwenye mradi, kama alivyotakiwa na *EWURA* kabla ya muda wa kikomo na kutotimizwa kwa masharti ya kutolewa kwa leseni ya kuzalisha na kusambaza umeme kwa mwekezaji na *EWURA* kuidhinisha utaratibu wa ukokotoaji wa bei za umeme wa jumla *power tariff methodology* na wa rejareja.

Mheshimiwa Spika, kutohana na kukosekana kwa msaada wa fedha za *ORET*, Serikali ililazimika kuanza maandalizi ya utaratibu mwingine mbadala kwa ajili ya upelekaji wa umeme katika maeneo hayo, kama ilivyokuwa imepangwa ikiwa ni pamoja na kuunganisha wateja kwa bei nafuu kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kutumia umeme kwa shughuli zao za maendeleo. Gharama za kuunganisha umeme kwa sasa ni wastani wa shilingi 470,000. Utaratibu mbadala unaweza ukawa wa kulipa kwa awamu kwa kipindi kitakachopangwa au unafuu mwingine utakaoridhiwa kadri bajeti itakavyoruhusu.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya umeme Mkoa Mtwara ni chakavu kiasi cha kusababisha upotevu mkubwa wa umeme pamoja na bili kubwa kuliko kawaida kwa wateja, je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha tatizo hili?

Swali la pili, pamoja na kuwepo kwa umeme wa uhakika katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa takriban miaka minne sasa, bado *TANESCO* ina wateja 17,000 na wakati huohuo kwa kutumia umeme wa gesi badala ya *diesel*, Serikali inaokoa zaidi ya shilingi bilioni moja kwa mwezi, je, ni kwa nini sasa Serikali isione kwamba ni busara kutumia kiasi hicho cha pesa kukarabati miundombinu ile chakavu katika Mikoa hiyo ya Lindi na Mtwara na kuwaunganisha wananchi vijijini umeme kwa gharama nafuu na hii itapelekea *TANESCO* sasa kuongeza wateja na pia kupata faida zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI NA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba miundombinu iliyokuwepo pale Mtwara ya kwenda Masasi iliyokuwa inapita Ndanda na wapi ambayo ndio iliyokuwa imeingiwa kwenye miradi ya gesi ilipoanza mwaka 2009 mwanzoni, ilikuwa hata wakati ule tayari ilishakuwa chakavu. Sasa hizi pesa bilioni 44 ambazo zilikuwa zimetolewa na Serikali ya Uholazi kama ni msaada zilikuwa zimekusudiwa pia zishughulikie suala la kuondoa ile miundombinu chakavu kwenye *fider line* zote mbili, *southern fider* kwa maana hii inayopitia Tandahimba na Newala na *northern fider* hii inayopitia Ndanda mpaka Lindi na kuendelea. Matatizo yake ni kwamba ilipokosekana ile *ORET* mwaka jana, miradi hii yote ya bilioni 44 pamoja na zile za kuunganisha zikawa zimeleta tatizo hili ambalo kwa sasa hivi ni kama vile tunaanza kujipanga upya kwanza kuunganisha lakini pili kubadilisha hii miundombinu chakavu. Tumekwenda kule mwezi wa kwanza, tumefanya ziara katika utaratibu ule na mafundi wa *TANESCO* na kweli wamebaini kwamba kuna kazi ya dharura ambayo inahitajika kubadilisha nguzo kama 400 hivi ili

kurudisha mfumo ule katika ufanisi unaotakiwa. Kwa hiyo, ni suala ambalo Serikali imeshalionna na tunalifanya kazi na inabidi tulitafutie fedha mbadala ili liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, la pili ni hili la wateja, ni kweli kwamba pana wateja sasa hivi 17,000 lakini wateja ambao wapo tayari kwa kukadiria, Mtwara wateja kama 11,000 hivi na Lindi wateja kama 6000 kwa hiyo nao ni wateja wengine 17,000. Baada ya utaratibu huo wa *ORET* kushindikana, wateja wamechelewa kidogo kuunganishwa kwa sababu gharama ni kubwa kuliko ilivyokadiria. Ndiyo maana kwenye majibu ya maswali ya msingi nimesema kwamba tunatafuta utaratibu mbadala ili kuhamasisha wateja hao 17,000 kuingia kwenye mfumo na kutumia umeme.

**MHE. SALUM K. BARWAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nataka kujua tu nini hatma ya mazungumzo ambayo yamedumu takriban miaka minne baina ya *TANESCO* kupitia Serikali na Kampuni ya *Umoja Light* ambayo ilikuwa na mkataba wa kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ambayo ingepelekea kuwa na auheni na kupata nafasi nzuri kwa watumiaji umeme kulipa gharama nafuu za uunganishaji wa umeme huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Ni kweli mkataba wa awali ulikuwa baina ya Serikali na ARTUMAS, ARTUMAS ndiyo walikuwa wanafanya kazi hiyo, hapa katikati na wao wakatengeneza Kampuni Tanzu ya *Umoja Light* ili ifanye kazi hizo kwa niaba ya ARTUMAS. Kwenye swali la msingi nimesema ARTUMAS ilivyofilisika kidogo, imeonekana kazi hizi pia zinaweza zikafanywa na *TANESCO* lakini sasa hivi kuna mtu mwingine *Wentwork Resources* ameuziwa mkataba wake na ARTUMAS. Lengo ni kuwapatia wananchi wa Lindi na Mtwara umeme. Tunajua kwamba *TANESCO* wanaweza kufanya kazi hiyo, tunaangalia kama mkataba huo wa *Wentwork Resources* tuendelee kuwa nao au tuireshees *TANESCO* ambao wana uwezo mkubwa lakini pesa zao inatabidi tuzitenge kwenye bajeti kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Na. 414

#### **Hatma ya Wafanyakazi wa Viwanda Vilivyobinafsishwa**

**MHE. VINCENT J. NYERERE** Aliuliza:-

Viwanda vingi nya umma vimebinafsishwa na kusababisha punguzo la wafanyakazi waliokuwa wameajiriwa na viwanda:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa wafanyakazi hao mafao yao na kuwajulisha hatma yao hasa wafanyakazi wa kiwanda cha *MUTEX* na vingine kote nchini?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya wafanyakazi katika mashirika yaliyobinafsishwa walipunguzwa kazini wakati wa utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji. Hata hivyo, siyo kila ubinafsishaji wa kiwanda uliambatana na upunguzaji wa wafanyakazi bali pale palipokuwa na sababu ya kupunguza ilibidi kufanya hivyo ili viwanda hivyo visibebe mzigo mkubwa usioendana na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi wa *MUTEX*, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kiwanda hiki kilibinafsishwa kwa utaratibu wa ufilisi mwezi Juni, 2006 na taratibu zote za ufilisi zilifuatwa, ikiwa ni pamoja na kulipa mafao ya wafanyakazi. Wafanyakazi 512 kati ya jumla ya wafanyakazi 935 walilipwa mafao yao na wafanyakazi 423 walikataa kuchukua mafao yaliyotolewa kwa utaratibu wa ufilisi na kuamua kufungua kesi Mahakamani. Kutokana na hukumu kutolewa dhidi yao, wafanyakazi hao hawakuridhika na wakaamua kukata rufaa. Rufaa yao ilitupiliwa mbali na Mahakama wakashauri wachukue mafao yao kama yaliyobainishwa katika ufilisi. Wafanyakazi hao bado hawajachukua mafao yao hivyo kupitia Bunge hili tunashauri wafanyakazi hao 423 waende *Consolidated Holding Corporation* kuchukua mafao yao.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa fedha iliyopangwa kuwalipa wafanyakazi hawa ni kidogo, haitoshi hata nauli ya kurudi makwao, je, Serikali haioni sasa ni vizuri kuwaongeza fedha hizo ili wawashawishi wakachukue warudi makwao?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, fedha hii imekuwa kidogo zaidi kutohakana na suala zima la kuisusia tangu mwaka 1996 hadi sasa kwa hiyo hata thamani yake imeshuka. Kwa hiyo, ni vigumu mimi sasa hivi kusimama hapa na kusema kwamba Serikali itatoa fedha lakini mimi namwomba Mheshimiwa Nyerere ajaribu kufuata taratibu za kuomba mamlaka husika kama kuna uwezekano wa Serikali kufanya hivyo Serikali itafanya hivyo kwa sababu nasema hili kwa sababu kuna maeneo ambayo Serikali inaweza ikatoa fedha kiwanda kikibinafsishwa pale ambapo kunakuwa na ushahidi kwamba kiwanda kile hakina uwezo kabisa. Sasa kiwanda cha *MUTEX* kwa uflisi kilikuwa na uwezo kikatoa fedha na fedha hizi zikapungua. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Mheshimiwa Mbunge akajaribu kufanya taratibu za kiutawala za kuwaombea hawa lisije likawa ni suala la kisera ila liwe ni suala la kiutawala.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, Mwekezaji wakati anakabidhiwa kiwanda hiki aliahidi atafunga mashine mpya na mpaka sasa hivi bado hajafunga kitu ambacho kinapelekea kudorora kwa uzalishaji katika kiwanda kile. Je, Serikali inatoa kauli gani sasa kuhusiana na mwekezaji huyu?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, wakati bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara inapitishwa hapa Bungeni juzi nillileze Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli kuna wawekezaji ambao hawakutimiza yale masharti ambayo tulikubaliana wakati tunasaini mkataba. Sasa Wizara ya Viwanda ya Biashara tumefanya tathmini na tathmini ile tumeipeleka *Consolidated Holding Cooperation* wao ndio wana uwezo wa kuongea nao kisheria wale ambao walipewa mikataba ile na PSRC na kazi za PSRC sasa hivi zinafanywa na CHC. Kwa hiyo, CHC tumeelekezana wataanza zoezi hilo mara moja la kuongea na wenye viwanda ambao hawakutimiza yale masharti ambayo tulikubaliana nao. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Matiko awe na subira na kweli ashirikiane katika zoezi hilo la kuhoji kwa nini mashine mpya ambazo zilikubaliwa katika mkataba hazikuwekwa.

Na. 415

#### **Hitaji la Kiwanda cha Kutumia Zao la Pamba**

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR** aliuliza:-

Nchi yetu inalima Pamba ya kutosha lakini Serikali huagiza Sare za Wanajeshi kutoka nje:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuwa a kiwanda kinachowezza kutumika zao la Pamba?
- (b) Je, Serikali pia haioni umuhimu wa kuwa na viwanda vidogo vya kushona ili tuweze kujitengenezea sare za Wanajeshi wetu sisi wenywewe?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na viwanda vinavyotengeneza nguo kwa kutumika Pamba inayolimwa kwa wingi hapa nchini. Kwa kutambua hilo, Serikali illanzisha viwanda vya nguo na baadaye kukabidhi kwa sekta binafsi chini ya zoezi la ubinafsishaji. Kwa sasa viwo viwanda 14 vya kutengeneza nguo, viwanda vivili vya kusokota nyuzi na viwanda vitano vya kushona mavazi. Kwa pamoja viwanda hivi vina uwezo wa kutumika tani 30,000 ya Pamba kwa mwaka, sawa na 30% ya Pamba inayolimwa hapa nchini. Kwa ujumla sekta

ya viwanda vya nguo na mavazi ilizalisha vitambaa vyenye mita za mraba 103,177,000 mwaka 2010 na kutoa ajira kwa watu 22,000.

Wizara inaendelea kuhamasisha na kuvutia wawekezaji katika sekta hii muhimu ili angalau kufikia 70% ya Pamba inayolimwa hapa nchini kutumika kuzalisha nguo. Hivi sasa Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Gatsby Trust*, inaandaa mkakati mahususi kwa ajili ya kuimarisha na kuendeleza sekta ya nguo.

(b) Mheshimiwa Spika, vipo viwanda viwili vya Jeshi ambavyo vinashona nguo za Wanajeshi. Viwanda hivyo ni Ruvu JKT na Cami-Suma ambacho hivi sasa kimesimamisha uzalishaji kwa muda. Kiwanda cha JKT Ruvu kilichopo Wilaya ya Kilaha, eneo la Mlandizi kinachofanya kazi kwa ushirikiano kati ya Tanzania na China, kina mitambo na vifaa vipyta vya kushonea (Mashine zipatazo 138). Mavazi yanayotengenezwa kiwandani hapo ni pamoja na sare kama vile Kombati na T-sheti za Wanajeshi na mgambo na vyandarua kwa ajili ya Wanajeshi. Viwanda hivi vya Jeshi vinanunua vitambaa kutoka katika viwanda vya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhimiza matumizi ya nguo zinazozalishwa hapa nchini kutengeneza sare za Majeshi yetu, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) walitembelea baadhi ya viwanda vya kutengeneza nguo kwa lengo la kuangalia hali halisi ya uwezo na teknolojia inayotumiwa na viwanda hivyo ili kuhimiza utengenezaji wa vitambaa vinavyokidhi mahitaji ya Majeshi hayo. Sampuli kutoka katika viwanda viwili vilivyoonekana vina uwezo wa kutengeneza vitambaa kwa ajili ya sara za Majeshi ziliwashilishwa ili kufanyiwa uhakiki na Majeshi, ikikubalika viwanda hivyo viweze kushona nguo hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wenyewe viwanda vya kutengeneza nguo tutashirikiana vema kuhakikisha kuwa bidhaa bora zinazokidhi matakwa ya Jeshi zinazalishwa.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, hivi sasa Watanzania sote tunaelewa kwamba tuna tatizo la kushuka kwa bei ya Pamba. Je, kuna hatua gani za hivi sasa za dharura zilizochukuliwa ili kuweza kuwapa matumaini hawa wakulima na kama hakuna je, Serikali iko tayari kununua Pamba kama inavyofanya kwenye zao la Mahindi au ile *gap itakayojiteza* basi kuweza kufidia ili kuwapa matumaini hawa wakulima wa Pamba?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema bei ya Pamba imeshuka katika Soko la Dunia na ni kweli kwamba wanaonunua Pamba sasa hivi hawawezi kununua kwa ile bei elekezi ambayo iliwekwa na Bodi ya Pamba na wale wadau wa Pamba waliokutana Mwanza hivi karibuni ya shilingi 1,100/=.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameunda Tume ambayo inalifanyia kazi suala hili na wakati wa bajeti ya Wizara yangu nililisema hapa na nikawaomba Wabunge wote wawe na subira ili Tume ilette taarifa yake ili Mheshimiwa Waziri Mkuu akitoa ile taarifa iwe ni taarifa ambayo imezingatia hali halisi na ambayo wananchi wataelezwa kitu ambacho kweli kitafanyika. Nikisema hapa kwamba bei itaongezwa au Serikali itafidia, nitakuwa natoa ahadi ambayo namuingilia mkuu wangu wa kazi katika Tume ambayo ameundi. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira.

**SPIKA:** Muda umekwisha na maswali pia yamekwisha. Sasa tuna wageni ambaa ni Madaktari saba kutoka Jamhuri ya watu wa China ambaa wako nchini kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa muda wa miaka miwili. Karibuni sana na ahsante sana ila hatukuambiwa ni wapi watakapofanya kazi lakini mradi mtafanya kazi nchini mwetu, tunawatachia mafanikio mema katika kazi yenu. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutoka Shirika la Filamu nchini, yuko Rais wa Shirika hilo, Ndugu Simon Mwakifwamba, siku nyingine mnawakalisha *Speakers Gallery*. Kuna Ndugu Wilson Makubi yeche ni Katibu, Ndugu Susan Lewis Natasha, yeche ni Mjumbe wa Kamati ya Maadili FAFF. Ahsante sana na karibuni sana. (*Makofii*)

Wako wageni wengine kutoka Shirikisho la Sanaa za Maonyesho nao ni Ndugu Denis Mango. (*Makofi*)

Wengine ni kutoka Shirikisho la Muziki, hawa ni Ndugu Makamu wa Rais anaitwa Chemundu Gwao na Katibu wake anaitwa Salim Mwinyimvua. (*Makofi*)

Pia kuna wageni wengine kutoka Shirikisho la Sanaa za Ufundu, nao ni Bwana Adrian Nyangamale. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ameleta wageni wake kutoka Shirika la Filamu, Shirika la Sanaa za Maonyesho, Shirikisho la Muziki na Shirikisho la Sanaa za Ufundu. Nafikiri Mheshimiwa Mbilinyi hapa atakuwa amekubali.

Pia wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 52 na Walimu sita (6) wa Shule ya Msingi ya *DCT Holy Trinity Dodoma*. Karibuni sana na ahsante sana tumefurahi kuwaona, sikujua kuna shule ya namna hiyo lakini karibuni sana. (*Makofi*)

Pia kuna wanafunzi wengine 56 na Walimu nane wa Shule ya Sekondari ya *Central Dodoma*, karibuni sana na msome kwa bidii. (*Makofi*)

Tuna kikundi cha watu 11 cha Timu ya *Sport Kizaazaa waklongozwa* na Ndugu Juma Simba. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Zungu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati tarehe 14/8/2011, saa 3.00 katika ukumbi wa Msekwa B, siku ya Jumapili, kawaida tunafanya saa 5, kwa hiyo ni saa 5.00.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret S. Sitta anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 8.30 mchana watakuwa na kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa C.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, anaomba niwatangazie Wajumbe wake kuwa leo kutakuwa na kikao cha Kamati kuanzia saa tano katika Ukumbi wa Msekwa B. Hawa nimewaruhusu kufanya kikao saa tano.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo hii saa 8 mchana watakuwa na kikao chumba namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 kutakuwa na kikao ukumbi namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi H. Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kukusanyika mbele ya Jengo la Utawala saa 7.15, mnajua mnakokwenda.

Mheshimiwa John J. Mnyika, yeye ni Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa leo hii saa 9.00 alasiri kutakuwa na kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Kaimu Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho Jumamosi tarehe 13/8/2011, saa 9.30 alasiri kutakuwa na uzinduzi wa ujenzi wa nyumba 290 za Shirika la Nyumba la Taifa katika eneo la Medeli hapa Dodoma. Mgeni rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wabunge wote wanaombwa kushiriki katika hafla hiyo

muhimu. Hili ni tangazo kutokea Ofisini lakini limeletwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Waheshimiwa Wabunge, leo hii mtoto wa mkulima ni siku yake ya kuzaliwa. (*Makofi*)

(*Hapa Wimbo wa Happy Birthday Uliimbwa*)

**SPIKA:** Ahsante, *happy birthday* Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakutakia maisha mengine marefu yenye fanaka, umri wako hatuna haja ya kuujua. Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana, tunamtakia kheri! (*Makofi*)

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

#### HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la mwaka 2007.

**KWA KUWA** Mkutano wa Nne wa Bunge wa kushughulikia bajeti ya Serikali pamoja na shughuli nyininge za Bunge zilizopangwa umepangwa kumalizika tarehe 26/8/2011;

**NA KWA KUWA** ratiba ya shughuli zote zilizopangwa kufanya katika Mkutano huu wa Nne zimepangwa kwa kuzingatia Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007;

**NA KWA KUWA** tarehe 18/7/2011, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa niaba ya Serikali aliomba Bunge kulipatia Serikali muda wa ziada wa kuweza kuzingatia na kuifanya kazi michango mbalimbali iliyotolewa wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini;

**NA KWA KUWA** katika kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi wa Bunge kilichofanyika katika ukumbi wa Spika tarehe 18/7/2011, Wajumbe wote wa Kamati hiyo waliohudhuria waliazimia kuliomba Bunge likubali kufanya kazi siku ya Jumamosi tarehe 13/8/2011 yaani kesho ili kuiwezesha Wizara ya Nishati na Madini kuwasilisha majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zilizotokana na kikao cha tarehe 17 na 18/7/2011 na kuwasilisha hatua zilizochukuliwa na mkakati wa utekelezaji wa hatua hizo pamoja na kuitisha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2011/2012;

**KWA KUWA** kwa mujibu wa Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, Bunge haliwezi kukutana na kufanya kazi siku ya Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko;

**NA KWA KUWA** ili kuwezesha Bunge kuweza kukutana siku ya Jumamozi tarehe 13/8/2011 yaani kesho, ni lazima Bunge litengue Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007 kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1);

**HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Nne, Kanuni ya 28(15) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelezea kwamba Bunge halitakutana siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za Mapumziko itenguliwe na badala yake Bunge likutane siku ya Jumamosi yaani kesho kuanzia saa tatu asubuhi na hakutakuwa na kipindi cha maswali na majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Mmh! Hoja imeungwa mkono na pande zote. Ngoja kwanza bwana, kaa kwanza! Hamuwezi kuwa mnagonga wakati mtu amesimama tu, hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

(Hoja illtolewa iamuliwe)  
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki kutengua Kanuni za Bunge zilizotajwa)

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, hii hoja tumeileta kwa sababu kwa mujibu wa siku ambazo Bunge linapaswa kukaa, ni siku hamsini (50), sasa tukisema tuongeze siku nyingine *other than* kutafuta siku yetu katikati hapa ingekuwa ni tatizo kidogo. Kwa hiyo, tumekubaliana kesho tutukane na hatutakuwa na maswali lakini naona kuna wengine wanahoji randama iko wapi? Hatuanzi upya! Ile Wizara tumeijadili yote, tulipokomea tukasitisha ni pale ambapo tulitaka tuingie kwenye Kamati ya Matumizi, ndio tukaona kwamba kazi fulani ifanyike na ni kazi fulani, siyo Wizara nzima, ni suala la umeme tu! Kwa hiyo, mwongozo mzima wa nini tunafanya kesho tutaeleza baadaye baada ya Kamati zinazohusika kukaa na kuona tuna-manage vipi. Hatuanzi upya, randama zilishatolewa, kama unaitafuta iko mahali panapostahili. Randama ziko kumi (10) tu, mkachukue mjisome. Vilevile na maswali yote mliyomuuliza Mheshimiwa Waziri atajibu kesho, lakini hili maalum tunataka maelezo maalum.

Mheshimiwa John Mnyika ulikuwa unataka kusemaje? Iko Kanuni inayosema usicheleweshe muda.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limetokea hivi sasa kutoptana na Kanuni ya 68 (7).

**SPIKA:** Limetokea wapi? Humu ndani? Wapi limetokea?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, suala la kutengua Kanuni kwa ajili ya kufanya shughuli kesho ambalo limeungwa mkono na pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, katika hoja iliyowasilishwa inahusu muda wa kuanza Kikao kwamba kesho tutaanza saa tatu (3.00) lakini haikutaja muda wa kumaliza kikao kwa hiyo siku ya kesho.

Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba kulikuwa na mawazo mawili, wazo la kumaliza saa saba (7.00) ambapo kungekuwa na muda mfupi sana wa kukaa kama Kamati na wazo la kuongeza muda ili kumaliza saa nane (8.00). Sasa naomba Mwongozo wako katika jambo hili la muda ili Serikali iweze kutoa hoja yenye kuhakikisha kesho kunakuwa na muda wa kutosha kwenye Kamati wa kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, la pili kwenye jambo hilohilo la kuhusu utaratibu wa siku ya kesho, naomba Mwongozo wako vilevile. Huko nyuma tulipunguza muda na tulibadili utaratibu wakati Bunge linapokaa kama Kamati. Sasa kwa kuwa maelezo uliyoyatoa ni kwamba kesho hakutakuwa na hotuba ya Kamati wala hotuba ya Kambi ya Upinzani, tutakwenda moja kwa moja kwenye Kamati. Ili kuwatendea haki Watanzania, ni vizuri vilevile katika Mwongozo wako ukaweka utaratibu ambaa utarejea kwenye misingi ya Kanuni zilivyouka awali kutoa muda wa kutosha wa mahojano na majadiliano kwenye hatua ya Kamati ili kuweza kutimiza lengo kweli la kwenda kuipitia upya ile bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kama ambavyo hoja illolewa Bunge liliipoahirishwa. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika, unachokisema ni sahihi. Azma ya kusoma hoja hii ilikuwa iishie saa nane (8.00), nimemwambia asisome saa nane (8.00) kusudi kuwe na muda wa kutosha. Ndiyo maana hakusoma ili uwepo muda wa kutosha na siku hiyo imepangwa rasmi kwa ajili ya kumalizia Wizara hii. Kwa hiyo, haipo kwenye Kanuni kwamba tutamaliza saa saba (7.00), tutaanza saa kumi (10.00), hakuna hiyo. Ndiyo maana nimeweka muda wa kutosha. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea!

## HOJA ZA SERIKALI

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012

## Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutajadiliana mpaka saa saba na robo (7.15) halafu jioni tunaingia kwenye Kamati. Jana walitajwa wafuataao, Mheshimiwa Susan Lyimo ataanza, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi na Mheshimiwa Nyambani Chacha Mariba Nyangwine, wajiandae.

Mheshimiwa Susan Lyimo! Hayupo! Mheshimiwa Moza Abedi Saidy! Mheshimiwa ndiyo unaitwa hivyo! (*Kicheko*)

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuweza kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuungana na Waislamu wenzangu wote waliofunga Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani na wale ambao hawakujaliwa nao pia namwomba Mwenyezi Mungu waweze kujaliwa. Wale ambao wameungana nasi kwa kuamka salama siku ya leo na wale ambao Mwenyezi Mungu amewatanguliza mbele ya haki tuwaombee dua.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnapotoka nje, Kanuni inasema kwamba mnapaswa kutoka kimyakimya.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ni muhimu sana katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa kuwa tunalo jengo la *TPDC* ambalo kwa kweli ni la muda mrefu, halijakarabatiwa na hivyo kupungua hadhi yake kwa kuota majani, tungeomba Wizara iweze kukamilisha ujenzi ule na kuonesha hadhi ya jengo lile.

Mheshimiwa Spika, nije moja kwa moja kwenye suala la Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari wanafanya kazi katika mazingira magumu mno, wengine wamekuwa wakinyanyasika, wengine wakifukuzwa na kukemewa katika maeneo mbalimbali, jambo ambalo kwa kweli linafanya utendaji wao wa kazi kuwa mgumu. Pia hawana vitendea kazi vya kutosha, isitoshe wengine wamefikia hatua ya kumwagiwa tindikali, wengine kupoteza maisha na kudhoofisha kazi hii ili isifanyike kwa ufanisi. Pia ukiangalia hata kwenye malipo yao, fedha wanazopata hazikidhi mahitaji ya shughuli ambazo wanazifanya. Kwa kweli inaelekea kwamba hii yote ina lengo la kuwadhoofisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kumuinua Mwandishi wa Habari ili aweze kufanya kazi yake kwa ufanisi bila kujihusisha kwenye vitendo vya rushwa na vitendo vingine ambavyo vinaweza vikamshawishi kutoa habari ambazo hata si sahihi. Kuna upande mwengine ukiangalia kabisa shughuli zao wanakuwa kama vile wana upendeleo fulani, inaonekana hata humu ndani ya Bunge, yupo ambaye atatoa hoja ya msingi haitaweza kutangazwa, lakini atakayetoa hoja ya swali la nyongeza utakuta ndiye anayetolewa habari kamili. Hili suala kwa kweli lipo, ni afadhali wangeacha ili waweze kutenda kazi hii na kukiletea sifa chombo chao kwa ufanisi mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa michezo ni afya, ni uchumi, ni ajira, tunao vijana wengi ambao wanapenda sana michezo hususani michezo wa mipira. Tunao vijana wengi ambao wana nguvu za kutosha, uwezo mzuri, kuanzia ngazi za chini hasa tukianzia shulen ambako watoto wanajitahidi kucheza michezo ya mipira, tunao watoto wazuri mno, lakini inafika wakati watoto hawa wanakata tamaa ya kuendelea kwa sababu pindi wanapomaliza shule hawafuatiliwi kuoneshwa kwamba wana umuhimu katika sekta hii ya michezo wa mpira na hakuna sekta ambayo inapendeka zaidi kama eneo hili la michezo wa mpira.

Mheshimiwa Spika, tunao watoto ambao waliweza kucheza michezo mingi shulen hasa katika Kata ya Bereko, Wilaya ya Kondoa. Kuna vijana walijitokeza wakacheza vizuri, wakachukuliwa wakapelekwa mpaka Mwanza, kufika kule wakapata zawadi na zawadi waliyoambulia ni *Helmet* badala ya kupewa Pikipiki na waliambiwa nendeni mtapewa lakini

mpaka leo hii kuanzia miaka ya themanini (1980) hawajaona kitu chochote. Vijana wale walikuwa wakimbiasi wazuri, wachezaji wazuri, lakini hawakupata zile zawadi. Hii ni moja ya sababu ambazo zinasababisha kukata tamaa. Ili tuweze kuona ni jambo ambalo linapendeka katika michezo yetu, basi ni vizuri zaidi ile ahadi iliyotolewa basi itimizwe.

Mheshimiwa Spika, utakuta pia watu wanacheza mchezo ya mpira wanafika mpaka hatua ya uzeeni lakini wanapozeeka wanatelekezwa. Kwa sababu wanakuwa wamekosa nguvu ya kufanya kazi ile, ajira ile ndiyo inaishia palepale. Kwa kweli Wizara iangalie wale ambao wamecheza vizuri na walikuwa wanafanya vizuri ndiyo wawe Makocha wa kuwafundisha hawa walioko chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mila na desturi za nchi yetu haziruhusu mtu mzima au kijana wa kuanzia umri wa miaka 18 na kuendelea kumbaka mtoto wa miaka sita mpaka kumi na moja (6 - 11) na kuendelea. Kwa kuwa Wizara hii inashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na kwa kuwa kila mara kwenye vyombo vyaya habari inatoa habari mbalimbali kama hizo za ubakaji, udhalilishaji, naona ni muhimu sasa hivi sekta hii ikajiunga moja kwa moja na kushirikiana kuanza kutoa matangazo kuanzia ngazi za chini na kuweka sheria za kushirikiana na Vitongoji, Vijiji mpaka Kata ili kukemea mila ambazo zinapotosha umma na zinakiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, mfano, mwanzoni mwa mwaka huu mtoto wa Kimasai aliripotiwa kwamba aliolewa akiwa na umri wa miaka sita (6) na akazaa akiwa na miaka kumi na moja (11). Hivi kweli mtoto huyo atasoma tena? Kitendo alichotendewa mtoto huyo si ni sawa na kupotezewa heshima yake na kumfanya asiwe tena na maamuzi katika familia akiwa kama mama? Atakuwaje mama wakati yeye bado ni mtoto? Napenda Wizara ishiriki katika mambo kama haya na kuweza kuelimisha umma.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la sanaa. Sanaa ni mchezo, ni ufundi, lakini utakuta vitu vyetu nya sanaa tunavyotengeneza hapa nchini vinapofika nije vinakuwa na ubora zaidi kuliko sisi wenyeewe ambao tumevitengeneza. Jina letu sisi linaenda kutukuza jina la nchi nyiningine badala ya nchi yetu ya Tanzania. Kwa mfumo kama huu, napenda basi hata sisi tuboreshe vitu vyetu kuanzia hapa hapa nchini, tuviuze kwa bei ya ghali. Mfano, juzi tulipokuwa kwenye maonesho ya Sabasaba Dar es Salaam, tulikuta kinyago chetu sisi kinauzwa kwa shilingi 200 au 500, lakini wanakuja watu kutoka nchi za nje, wanunuua vinyago vile wakifika kule wanaviuza kwa bei ghali zaidi, je, sisi Watanzania tunanufaikaje kwa hilo?

Mheshimiwa Spika, napenda tu kumalizia na suala zima la Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari wazingatie shughuli zao na wala wasizingatie kikundi ambacho kinakuwa kama taasisi fulani. Hii ni tabia ambayo inatutia wasiwasi kidogo. Ili tufanye kazi zetu kwa ufanisi, inatakiwa twende pamoja.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri habari za utangazaji zisiishie Mijini tu kama vile Dar es Salaam na maeneo mengine na huko vijiji pia wanahitaji wapate kutangazwa ili wajulikane wanafanya nini. Kuna maendeleo mbalimbali yanayofanyika kule Vijiini ambayo yanahitaji pia yatangazwe. Kuna michezo, mambo ya wakulima, mambo ya ukiukaji wa sheria za haki za mirathi, watu wanauana, watu wanapigana na kadhalika. Habari kama hizo hazitangazwi, habari tunazosikilia zinatoka Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na maeneo mengine, je, Wilaya ambazo hazina mawasiliano ni lini zitakuwa na mawasiliano hayo ili ziwe zinatoa habari? Mfano, kule Kondoa na maeneo mengine ya huko vijiji kabisa.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu kwamba naipongeza Wizara hii lakini naomba iongezewe fungu ili iweze kufanya kazi yake kwa uzuri na kuweka utandawazi na kupata vifaa nya usafiri. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii adhimu. Mimi napenda kuzungumza kwa ufupi kuhusu mambo kadhaa. La kwanza, Sera ya Utamaduni, la pili ni umuhimu wa utamaduni na kama Serikali tulyonayo inadhani kwamba utamaduni ni kitu

muhimu. Suala la tatu litahusu lugha na la nne litahusu uzalendo na jinsi unavyohusiana na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, mimi ninavyodhani Sera ya Utamaduni kama ilivyo kwanza haitoshelezi. Kuna mambo mengi sana ambayo yameshapitishwa hapa Bungeni yanayohusiana na Itifaki mbalimbali za Kimataifa ambazo hazizingatiwi katika Sera hiyo. Halafu pili Sera yenyewe haina nguvu Kikatiba wala kisheria. Naomba Waziri katika majumuisho yake atueleze kuhusu mipango ya Wizara kurekebisha kasoro hizi.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu utamaduni. Dhana ya utamaduni ambayo imeenea hapa nchini ni dhana finyu sana na watu kwa kweli hawajafundishwa dhana pana ya utamaduni. Kwa tafsiri pana na sahihi, utamaduni ni ujumla wa maisha ya jamii. Ni ujumla wa mafanikio yote ambayo jamii husika imejipatia katika maeneo mbalimbali ya sayansi, teknolojia, sanaa, muziki, mila, desturi, imani, falsafa, michezo na mambo mbalimbali ambayo jamii hiyo imeyapata katika mapambano yake na mazingira. Hiyo ndiyo tafsiri ya utamaduni na ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, utamaduni madhubuti hujenga Taifa ambalo ni madhubuti lakini mkiwa na utamaduni amba si madhubuti Taifa litakuwa ni legelege na ndiyo maana hata leo hii tunasikia habari kwamba watu siyo wazalendo tena, ni kwa sababu hawajaweza kujengwa vizuri katika utamaduni amba si madhubuti.

Mheshimiwa Spika, kumetokea nini toka tupate uhuru? Toka tupate uhuru, Idara ya Utamaduni kwa kweli haijapewa umuhimu ipasavyo. Imekuwa ikihamishwahamishwa toka Wizara hadi Wizara. Hata bajeti ambayo imepata mwaka huu ni kielelezo tosha kuonesha kwamba, kwa kweli hatudhani kwamba utamaduni ni kitu muhimu. Katika Halmashauri hadi leo hii mimi nimepata taarifa kwamba Maafisa Utamaduni hawajui watakuwa wapi kwa sababu hawako kwenye orodha ya TAMISEMI iliyopelekwa kule kwenye Halmashauri. Napenda kupata majibu kuhusu jambo hilo kutoka kwa Waziri. Je, Wizara inafanya nini ili kuishawishi Serikali ione kwamba utamaduni ni kitu muhimu?

Mheshimiwa Spika, pili ni kwamba huko kwenye Halmashauri hawa Maafisa Utamaduni amba kawaida huwa wako chini ya Maafisa Elimu, watakuwa wapi? Kwa sababu hata utamaduni haumo kwenye hii orodha ya TAMISEMI iliyopelekwa kule! Kwanza kabisa nikzungumzia hili suala la Maafisa Utamaduni kuwa chini ya Maafisa Elimu, ni kuwadhalilisha hawa Maafisa, ni kielelezo tosha kwamba utamaduni sio kitu muhimu.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea kuhusu lugha. Lugha imeongeleta jana, kidogo wengi wanasema kwa kweli Serikali haijatilia maanani sana lugha ya Kiswahili na mimi ninaafiki. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Taifa, lugha za Mataifa mengine katika nchi hata ndogo kama Aisilandi, wengi wenu hamjui kwamba *Island* ni nchi ndogo sana hapa duniani na ina idadi ya watu 280,000 na kitu, lakini ina lugha yake ya Kaisilandi ambayo ni lugha ya Taifa na lugha hiyo inatumika kote Bungeni, Mahakamani na inatumika kama lugha ya kufundishia kwenye ngazi zote za elimu. Hapa Tanzania bado tunasusua, hata humu Bungeni Miswada inaletwa kwa Kiingereza, inaletwa kwa Kiingereza ilhali tukijua kwamba baadhi yetu hatujui Klingereza. Nikiwa nimesema uongo naomba nisahihishwe.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mahakama za Wilaya na nyingine za juu kumbukumbu au rekodi za Mahakama zinaandikwa kwa Kiingereza. Sijui tunamwandikia nani? Naomba Waziri anijibu, tunamwandikia nani? Hilo suala pia linamhusu Waziri wa Sheria. Suala hili la lugha ya kufundishia limekuwa katika mjadala. Mjadala wa Kitaifa umefanyika, hoja za pande zote zimetolewa na kutathminiwa na kimsingi, hakuna hoja kwa nini elimu hapa nchini isifundishwe kwa Kiswahili? Hakuna hoja ila tunaendelea kuvuta miguu. Sera ambayo karibu itatangazwa kutoka kwenye Wizara yetu ya Elimu haijabadilisha msimamo. Bado inashikilia kwamba Kiingereza kiendelee kutumika. Sijui tunataka kuwapatia elimu hawa vijana wetu au tunataka tu kuwafurahisha mabwana zetu? Naomba Waziri anieleteze kuhusu hili la lugha ya kufundishia kwa sababu yecheleza na Waziri wa Elimu walipaswa kukaa na kulitattua.

Mheshimiwa Spika, kuna lugha zetu za kienyeji ambazo ni hazina kubwa sana. Labda kwa watu ambao hawajui ni kwamba sisi Tanzania kama tutaoa mchango katika utamaduni wa dunia utakuwa katika masuala makuu machache tu. Pamoja na zile sanaa zetu za asili kuna lugha nyingi zaidi ya 100 ambazo ni pamoja na Kiswahili. Naomba Waziri anieleze, Wizara inafanya nini katika kuziendeleza lugha za kienyeji. La mwisho, ambalo nitalizungumzia ni kuhusu suala la uzalendo na linalohusiana na utamaduni na lugha ya kufundishia. Inavyoonekana ni kwamba hapa nchini tunafanya mchezo wa kuigiza. Tunataka kujenga uzalendo kwa kutumia lugha ya Kiingereza, kwa sababu lugha ambayo kijana anaitumia ni nyenzo ya msingi katika kumjenga kiutamaduni. Sasa nyie mnatumia lugha ya Kiingereza ambayo ni ngumu kwake, anakariri. Elimu ya siku hizi imekuwa ni elimu ya kukariri tu. Sasa uzalendo utaujengaje kwa kutumia lugha ya kukopa? Kuna methali moja ya Kiswahili inayosema "Nguo ya Kuazima..." mtamalizia wenyewe ndugu zangu.

Nilikuwa nashauri, somo la uraia ambalo zamani ilikuwa linafundishwa kwa Kiswahili lirezeshwe, lifundishwe kwa Kiswahili kwa sababu ndiyo somo linalomjengea kijana uzalendo. Zamani ilikuwa ni elimu ya siasa, lakini ilikuwa ni elimu ya uraia. Lirezeshwe lifundishwe kwa Kiswahili kwa sababu uzalendo hauwezi kujengwa kwa kutumia lugha ya kukopa. Uzalendo hauwezi kujengwa katika utamaduni, legelege. Tuimarishe utamaduni wetu na ninaomba Waziri atueleze mikakati ya kuimarisha utamaduni wetu. Siyo mambo ya michezo tu au hayo mengine ya mipira na kadhalika, japo ni mazuri. Lakini la msingi, zaidi ni haya ambayo ninayoyasema sasa hivi ambayo yatawajenga watu wawe wazalendo wapende nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanasema kwamba ukiamua kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia katika ngazi zote mpaka Chuo Kikuu, basi tutaua Kiingereza. Nani alisema hivyo? Mbona China wanatumia lugha zao lakini wanajua pia Kiingereza? Huko Aisilandi (*Iceland*) kwenyewe wanatumia lugha yao ya Kaisilandi lakini pia wanajua Kiingereza. Tuanzishe Taasisi za kufundishia lugha za kigeni. Utaratibu huu tulionao wa kufundishia Kiingereza haufai. Mtu unasoma Kiingereza toka darasa sijui la ngapi mpaka la 12 hujui lolote, huwezi kuandika sentensi sahihi. Kwa hivyo, utaratibu huo umeshapitwa na wakati. Mtuombe ushauri sisi ambao ni wataalam wa lugha. Kuna taratibu za kisasa za kufundisha lugha kwa miezi mitatu mtu akaielewa na kuweza kuisema na kuiandika.

**SPIKA:** Hata Kichina?

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Hata Kichina, lugha yoyote ile, hata Kibena. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo ndugu zangu mchango wangu ni huo, namwomba Waziri atupati mkakati wa kufufua utamaduni wetu na kutujengea msingi mzuri wa uzalendo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Basi tujifunze na Kichina maana wanakuja wengi. Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, simwoni, Mheshimiwa Iddi Azzan atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kwenye Wizara hii. Kwa namna ya pekee kabisa niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti yao. Tunakwenda kwenye miaka 50 ya uhuru wa nchi yetu ambayo mwezi wa Desemba kutakuwa na sherehe hizo kubwa. Nilikuwa nataka kufahamu Kiwizara...

**SPIKA:** Mheshimiwa Chiku Abwao mbona unanivunjia heshima? Wewe hujioni ulivyo katikati na mtu na nani! Haya tuendeleee.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu Wizara imejipanga vipi ama kuwaenzi ama kuwakumbuka Waandishi wa Habari ambao wakati ule wa uhuru walikuwepo, walitangaza na walitoa taarifa kwa wananchi wetu wakaipamba sherehe ile na waliendelea kufanya hivyo kwa miaka kadhaa? Nataka kufahamu Waandishi hao na naomba niwataje. Kulikuwa kuna Heri Mboto, David Wakati, Hamza Kasongo, Salim Seif Mkamba, Steven Mlatie

hawa walishiriki kwenye ile sherehe yenye na matangazo yao, kwa kweli ukiyasikiliza hata leo unasiakira raha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Wizara inawaenzi vipi hawa katika kusherehekeza miaka 50 ya uhuru wa nchi yetu? Lakini sio hao tu, kulikuwa kuna Dunstan Tido Mhando, Jacob Tesha, Ahmed Jongo, Debora Mwenda, Eda Sanga, Juma Ngondae, Suleiman Hegga, Godfrey Mngodo, Khalid Ponella, Paul Sozigwa, Abdul Omar Masoud Jawewa, Mshindo Mkeyenge, Mustapha Nyang'anyi, lakini kwa namna ya pekee pia kulikuwa kuna mtangazaji mmoja ambaye yuko Kenya, Leonard Mambo Mbotela, alisaidia sana kukuza lugha yetu ya Kiswahili. Nataka kufahamu tunawaenzi vipi hawa?

Mheshimiwa Spika, nije sasa kwenye masuala ya michezo. Nimempungeza Waziri kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake, lakini nafahamu vizuri sana Waziri huyu jinsi alivyokuwa mchapa kazi huko alikopita mpaka hapa alipofika. Isipokuwa namwonea huruma utendaji wake mzuri wa kazi huko alikotoka hapa unaweza ukaingia doa. Kwa sababu Wizara hii imegubikwa na watendaji ambaao ama kwa makusudi wamechoka ama, basi tu wameamua wasitende kazi zao vizuri. Haya malalamiko yote unayoyasikia ndani ya Bunge hili ni kwa sababu ya watendaji wetu hawa wa Wizara hii, kama ingekuwa amri yangu, basi ningesema wote nawafukuza. Kuanza upya siyo ujinga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 wakati tunachangia bajeti ya Wizara hii tulizungumza mambo mbalimbali, lakini kubwa ikiwa ni kubadilisha ama kuhuisha Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ya Mwaka 1967 ambayo ilirekebishwa ikawa mwaka 1971 Sheria Namba 6. Tulilisema hilo, lakini tukasema pia na sera yenu hii ya michezo imepitwa na wakati na yenye na ifanyiwe marekebisho. Waziri wakati ule alisema hilo ameliona, wameshaanza kulfanyia kazi na wakati wowote itakuwa tayari. Bajeti zote zilizofuatia ukisoma wanakwambia tunakamilisha marekebisho ya Sheria Na. 12 ya Baraza la Michezo. Miaka hiyo yote imekwenda hivyo na hata kitabu cha bajeti Waziri alichowasilisha ameendelea kusema hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunauliza, hivi kurekebisha sheria iendane na wakati, tuna michezo ya kulpwa hivi sasa, hatuko kwenye ridhaa, tena kurekebisha sheria inawataka miaka mingapi? Wakati Sheria ya Mwaka 1967 inarekebishwa, ilioneckana ina kasoro mwaka 1970 wakaamua kuifanya marekebisho. Mwaka 1971 sheria ile ikarekebishwa na iliwachukua kipindi cha mwaka tu tena ikatoka kwa ukubwa zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 1967. Lakini leo tunaendelea kubembelezana na Wizara hii kwa ajili ya kufanya marekebisho ya sheria.

Mheshimiwa Spika, nasema Waziri, Watendaji wako bado wamelala usingizi mzito na kwa kweli kama hatutawaamsha, basi suala hili la michezo ambalo Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Tanzania wanalipigia kelele, haliwezi kuendelea. Hatuwezi kuendelea kama hatuna sera nzuri na hatuwezi kuendelea kama sheria yetu imepitwa na wakati. Tunasema siku zote na narudia kusema kwamba hili na kwa vyovoyote ilivyo mimi sitakubali na niungane na wenzangu ambaao walipinga bajeti hii na mimi nitaendelea kuipinga bajeti hii, kwa sababu hatuwezi kuwa Wabunge kila siku tunarudia jambo hilo hilo, hamtaki kulirekebisha. Kitu cha kufanya kazi mara moja kinawachukua miaka kadhaa. Tumechoka kusubiri, hivi sasa vijana wetu wanakwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Filamu, wanazuia filamu za Kitanzania, kijana wa Kitanzania amekwenda kukopa, ametengeneza filamu yake anaisambaza mnakwenda kuizua pale, kwa nini hamweki utaratibu wakati anaandaa *story* yake au *scripts* zake zile mzipitie mapema mumwelekeze, mumsaidie ili asiingie gharama za kutengeneza filamu kwenye usambazaji, mnakuja kuzuia. Hii siyo sawasawa. Lakini filamu zinazotoka nje ambazo hazina maadili kabisa mnayaruhusu, yanaingia yanasantazwa na yanapoteza maadili ya nchi yetu na kuwapoteza watoto wetu. Hizo hamzizui! Lakini hii ya kijana wa Tanzania aliyetengeneza ikawa na kasoro kidogo tu ambayo mngemweleza mapema angeweza kuirekebisha mnaizua.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wengine walikopa, wengine waliazima hela mnawafanya waadhirike. Kwa hiyo, niwaombe sana Bodi ya Filamu, huo usingizi mliokuwa nao sasa muamke,

mjue kwamba hivi sasa vijana wetu wanakwenda hatua tatu zaidi mbele wakati nyinyi bado mko kwenye usingizi, hatuwezi kuendelea na wala hatutakuwa tunawatendea haki. Niombe sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia na Baraza la Kiswahili, watu wamezungumza sana hapa. Mimi nasema isije ikatokea siku moja Rais akalogwa, akanichagua mimi kuwa Waziri humu ndani. Kiswahili tutakizungumza popote hata tukienda Ulaya hatutaona aibu, ndiyo lugha yetu. Lakini leo utakuta mahali Watanzania wako mia, kuna Mzungu mmoja, basi ndio anahangaika hangaika tu, ananeng'eneka kuongea Kiingereza, sema Kiswahili ili watu wote wakusikie. Kama kuna mkalimani atamsaidia yule ambaye haelewii Kiswahili, lakini tunafanya lugha yetu inazidi kupotea.

Kwa hiyo, naomba sana, Baraza la Taifa la Kiswahili, sheria zilizotengenezwa zimetengenezwa kwa Kiingereza. Hivi nyie Baraza la Kiswahili hamna maneno ya Kiswahili kutafsiri sheria hizi? Wananchi wetu huko chini hawaelewi tunapitisha Wabunge huku tunaelewa elewa, lakini ukienda chini kwa wananchi wetu ambaa ndio wanatakiwa wazielewe hizi sheria wanashindwa kuzielewa kwa sababu mmeandika kwenye lugha ambayo sio. Kwa hiyo, naomba sana hili nalo tuliangalie ili tuone unafanyaje.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwamba angalau sasa eneo liko Kiromo kwamba mtaanza kujenga jumba la utamaduni. Lakini mlisema kwamba kuna michoro ambayo kwenye bajeti ya mwaka uliopita mnaandaa, nilitegemea kwamba labda kwenye bajeti hii mngetuonyesha basi hiyo michoro ili tujue ni kitu gani kinajengwa. Lakini michoro hamna, angalau mmesema tu kwamba kuna eneo lipo Kiromo. Nina hakika kama eneo limepatikana, basi litajengwa jumba hilo la utamaduni. Tuweke mkazo jumba hili lijengwe, hatuna eneo ambalo vijana wetu wakafanya maonyesho yao ama mambo yao kwa sababu ya hiyo.

Mheshimiwa Spika, timu zinazowakilisha nchi kwenye Mashindano ya *All African Game*, bahati nzuri mashindano haya yanafanyika jirani, Msumbiji. Ni mategemeo yangu na ni mategemeo ya Watanzania wote pamoja na hawa wanamichezo ambaa wako kambini kwa muda mrefu kwamba wale waliofikia viwango watakwendwa kushiriki kwenye mashindano haya na kushindana kwenye mashindano hayo, hatutapenda kusikia kwamba wapo wanamichezo ambaa wamefikia kiwango cha kwenda kuwakilisha nchi yetu kwenye mashindano haya halafu eti ashindwe kwenda kwa sababu Serikali haina fedha ama kwa sababu chama chake hakina fedha, amekosa nauli. Watanzania hatutapenda kusikia hilo. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba wanamichezo hao waliofikia vigezo wanakwenda kwenye mashindano hayo ili kuwakilisha nchi yetu vizuri kuiletea nchi yetu sifa katika mashindano haya.

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (*TFF*), wanayo ligi inayoendelea *Premium League* ama Ligi Kuu. Ligi ile inashirikisha timu 12 na angalau hivi sasa wameongeza zimefika 14. Lakini hivi ni nchi gani duniani ambayo ina timu 12 kwenye ligi? Hivi maendeleo ya mpira, hawa vijana wetu vipaji vyao tunavipata wapi ikiwa ligi ina timu 12 au 14? Mimi naona kuna haja kabisa na Serikali hili muwaambie watu wa *TFF* pamoja na kwamba watakwambia wao wameagizwa na *FIFA* lakini waone umuhimu wa kuongeza timu kwenye Ligi Kuu ili tuweze kupata wachezaji wengi. Vijana wetu hawa waonyeshe vipaji vyao na mwisho tunaweza tukawapata wachezaji wazuri kwenye Timu yetu ya Taifa. Suala la kubakiwa na timu 12 labda wakati ule lilikuja kwa sababu barabara zilikuwa mbaya. Timu kusafiri kwenda Mtwara au Bukoba ilikuwa inachukua muda, lakini hivi sasa barabara zote ni nzuri.

Kwa hiyo, tuone umuhimu wa kuongeza timu, lakini hata na hawa wadhamini wanaodhamini Ligi Kuu niwapongeze kwa hicho wanachokifanya, lakini basi kwenye udhamini wao yale matangazo wanayobandika tangazo mbele kwenye fulana ya mchezaji hapa, hebu lile tangazo la hapo mbele walitoe. Kwenye kifua iachiwe timu itafute mdhamini ambaye ataweka tangazo lake ili waweze kupata fedha za ziada. Mdhamini anaweza akaweka tangazo lake sehemu nyingine, lakini sehemu ya kifua iachwe kwa ajili ya klubu kutafuta wadhamini wao watakaoweza kuwasaidia. Hii iko dunia nzima. Ukienda unakuta hiyo, hapa kwetu sisii mdhamini wetu amebandika tangazo lake hapo mbele, fulana inakuwa nzito, fedha yenye ndogo, kwa hiyo, tuone umuhimu wa kuwasaidia vilabu vyetu ili viweze kuwa na wafadhili wengine ama wadhamini wengine waweze kuwasaidia kuendesha timu zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilituahidi kwamba mtafanya mjadala wa kitaifa kuhusu maendeleo ya soka na misema hiyo mwaka 2006/2007 kwenye bajeti. Mkasema kwamba Mkutano huo utafanyika mwaka 2007 na Mheshimiwa Rais ndiye atakuwa Mgeni Rasmi. Mpaka leo kimya na kwenye hotuba hii wala hulijasemwa tena hilo. Tunataka kuona huo mjadala, msiseme maneno mazuri Bungeni kwa ajili ya kupitisha bajeti zenu, lakini mkienda kwenye utekelezaji hakuna kitu. Kwa kweli inatia aibu sana. Pesa mlizoomba shilingi bilioni karibu ishirini, lakini ni shilingi bilioni tatu na pointi ndiyo za miradi ya maendeleo zilizobaki, zote ni za matumizi ya kawaida. Angalieni kwenye bajeti zenu zinazokuja, wekeni pesa nyngi kwenye miradi ya maendeleo na pesa hizi za matumizi ya kawaida ambazo nyngi zinakwenda ovyo tu zipungue kidogo. Huwezi kuwa na shilingi bilioni 16, lakini huwezi ukawa na bilioni tatu tu ya maendeleo. Ni vitu ambavyo havina uwiano mzuri. Kwa hiyo, naomba hilo nalo mlipe umuhimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu wa Shirikisho la filamu wapo hapa, wapeni uwezo. Tumeona wasanii wetu wanakwenda kwenda hovyo tu, wengine wanasema wanaridhika na kipato wanachokipata, lakini walio wengi hawaridhiki. Haki Miliki haiko sawa. *COSOTA* ambao ndiyo wanasmamia, wao wamejiegemeza upande mmoja tu kwa msambazaji mmoja anaitwa *Steps* na ye ye utasema kama ni mbia wa huyo *Steps*. Msanii akitengeneza kazi yake na akitaka kazi yake isambazwe na mtu mwingine, inakuwa haiwezekani kwa sababu *COSOTA* hamsaidii. *COSOTA* inamsaidia yule ambaye amekwenda *Steps* peke yake. Sasa tunasema *COSOTA* naye huko *Steps* ana nini? Ni lazima isaidie wasanii wote, Haki Miliki iwalinde wote na yule ambaye anaona anaridhika na kipato anachokipata, basi acae kimya, awaache hawa ambao hawaridhiki waendelee kulalamika ili wasadiwe na wao waridhike na kipato chao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, nitapenda kupata maelezo ya kutosha kwa Wizara kuhusu haya ambayo nimeyasema. Lakini suala la mziki, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, ametoa *Mastering Studio*, amewapa *THT*, lakini nina hakika wasanii wengine wakimwomba atawapa. Kwa sababu hawa waliomba na hawa *THT* waliomba hata Wabunge mwaka 2006 walituomba na tulikwenda na sisi tukawachangia. Kwa hiyo, hawa wanaonekana wako mbele kuomba misaada, wasanii wengine nao waige mfano huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii na naomba niseme kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ambayo imechambua bajeti hii na kwa kusema hayo, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu ya wataalam wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, uliponipa jukumu la kuongoza Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, mara ya kwanza kabisa nilipokutana na Mheshimiwa Dkt. Nchimbi, Waziri mwenye dhamana ambaye nitafanya kazi kwenye Sekta ya Habari, Michezo, Utamaduni na Maendeleo ya Vijana kwa kweli tulipozungumza kwa mara ya kwanza tulikubaliana majukumu ya Wizara yake ni makubwa sana. Lakini kitu kilichonipa imani, ni utendaji kazi mzuri wa Waziri huyu kwa historia yake ya miaka mingi na wote tunaamini kwamba atatusaidia kuboresha haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayasema. Lakini ukweli ni kwamba Wizara hii pamoja na namna inavyotengewa fedha kidogo za kufanya kazi, ni lazima leo Waheshimiwa Wabunge tukubaliane majukumu ya Wizara hii kwa maana ya kuiflikia jamii moja kwa moja ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu zipi? Nianze kwa kukubaliana na ripoti ya Kamati yangu. Katika ripoti ya Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii, tumegundua kwanza Wizara hii imeongezewa Idara nyeti na muhimu sana kwa Taifa letu, Idara ya Maendeleo ya Vijana. Sasa hivi katika nchi yetu, idadi ya watu kadri inavyokuwa iko kama ifuatavyo:-

Watoto kuanzia mwaka mmoja mpaka miaka 15, ni asilimia 45 ya Watanzania wote. Miaka 15 mpaka miaka 60 ni asilimia 45 nyngine zilizobaki. Umri unaoendelea ni asilimia hizo chache zilizobaki. Sasa unakuta kwamba umri huo ambao nimeusema, wenyewe Watanzania wengi asilimia kubwa ni vijana. Lakini tukikaa na kujuliza hivi tunafanya nini na vijana hawa wengi wanaoendelea kuongezeka, hawa niliosema asilimia 45 kutoka mwaka mmoja mpaka miaka 15

hawa ni umri ule waujana kabisa, wataingia kwenye ujana kesho na mpaka kesho kutwa. Lakini tunasema nini kwa hawa vijana? Ndiyo maana nilimwambia Mheshimiwa Waziri ana kazi kubwa. Idara hii baada ya kuletwakwenye Wizara hii ni Idara nyeti. Lakini ukiangalia sasa bajeti ya maendeleo kwenye Idara hiyo ya Maendeleo ya Vijana tena inaitwa hivyo Idara ya Maendeleo ya Vijana katika nchi yetu ya Tanzania, utasikitika sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi, hawa vijana ndiyo wenye tatizo kubwa la ajira. Hawa vijana ndiyo wanaohitaji kuingia kwenye Sekta ya Michezo, hawa vijana ndiyo wengi ambaowameamua kujajirikwenye Sekta ya Sanaa ya Muziki, Filamu na kadhalika. Sasa ukijuliza, tunahangaika na ajira lakini tunao uwezo wa kuwaajiri vijana wetu kwenye sekta hizo nilizosisema na kwenye Sekta ya Habari. Lakini wamevezeshwaje? Idara hii ya Maendeleo ya Vijana imewekwaje ili isaidie kwa kweli kuleta maendeleo kwenye nchi yetu kwa sekta hii ya vijana? Ukianza kwenye kitengo cha sanaa, muziki, ni matatizo makubwa. Katika nchi nyiningine nyangi na kwenye taarifa yetu ya Kamati tumetoa taarifa kwamba ukienda Nigeria, ukienda Malawi wasanii hawa ni watu wakubwa na wana pesa nyangi na vijana wamejajiri kwenye sekta hiyo wanamudu maisha yao, wanachangia kwenye pato la Taifa kwa kiasi kikubwa. Lakini njoo katika nchi yetu, vijana hawa wanatia huruma.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli lazima niseme, kwenye Kamati tumelisema sana hili, wanatia huruma. Najua Sheria ya Bunge ilipitisha kuwepo kwa Shirikisho la Hati Miliki, *COSOTA* kuwasaidia wasanii wetu ili waweze kuwa na kipato kutokana na sanaa zao. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atuletee hii Sheria tubadilishe. Tubadilishe Sheria hii tuweze kuangalia hii *population* ya vijana wetu tuone Sheria hii itaisaidiaje Serikali yetu kuwaajiri hawa vijana kwenye Sekta ya Habari, kwenye ya utamaduni, kwenye michezo, filamu na kwenye Sekta ya Muziki. Tukifanya hivyo, tutaondokana na hili bomu tunalolisema la ajira kwa vijana kwa kiasi kikubwa. Tuletee Sheria hiyo tubalishe. Hawa *COSOTA* kwa kweli pamoja na Sheria kuwaruhusu, bado hawajatimiza wajibu wao inavyotakiwa. Wasanii wanapata shida sana, vijana wetu wanahangaika.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye sekta hiyo hiyo ya vijana hakuna Mbunge hata mmoja hapa ataniambia kule kwenye Jimbo lake hakuna kijiwe. Sijui nani alianzisha hii *concept* ya vijiwe! Vijana asubuhi wanakusanyika vijiweni, watakaa tangu saa 12.00 asubuhi mpaka 12.00 jioni na sio utamaduni wetu huo. Sisi tumeurithi wapi, Mungu wangu? Vijana kumi, thelathini watakaa pale na kijji kimoja kinawenza kuwa na vijiwe hata kumi. Kijiwe kingine wataweka miwa, kijiwe kingine hakina hata shughuli yoyote.

**SPIKA:** Miwa mitatu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Miwa mitatu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Serikali itusaidie, mwezesheni Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Waziri anayeshughulika na maendeleo ya vijana. Tukiamua kuvitumia vijiwe hivi kama vikundi vyamaendeleo hakika tutawaondoa vijana wengi kutoka kwenye vijiwe na tukawapa ajira na wakawenza kujitegemea kabisa na tukapunguza hili tatizo. Kwa sababu vijana hawa ukifika mijini ndiyo wanavuta bangi, wanakula madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, Lakini Idara hii ya Maendeleo ya Vijana hebu tuiwezeshe, tunasema kilimo kwanza, kule vijiini wale vijana wamechoka kulima na majembe, ndiyo maana wanaweka miwa mitatu, wanakaa kwenye kijiwe. Hawa tukiwatengeneza vizuri pamoja kuwapatia nyezo za kufanya kazi, tukawapa viwanda vidogo vidogo, tukawapa vijiwe vyakutengeneza balskeli na pikipiki tutaondokana na vijiwe visivyokuwa na tija kwa Taifa letu, lakini tutawawezesha vijana wetu katika nchi hii ya Tanzania ili waweze kujikwamua na maisha yao na tutaondokana na tatizo hili kubwa ambalo ni tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, tusipoamua kuboresha Idara ya Maendeleo ya Vijana kwenye Wizara, hakika mimi nasema hatutakuwa na maana. Wanaocheza sana sasa hivi kwenye michezo mingi iwe *netball* au *football* ni vijana.

Mheshimiwa Spika, mimi sijakuona kwenye *netball* hata siku moja, kwa sababu tayari umri wako haukuruhusu, umri wangu hauniruhusu, Mheshimiwa Dkt. Nchimbi mwenyewe pamoja na umri wake ule haumruhusu. Lakini vijana wetu ndio wanaocheza na michezo ni ajira. Hebu tubadilishe sera hii ya michezo tuwasaidie vijana wetu wengine wajari kupitia kwenye Sekta ya Michezo. Mimi ninasema Wizara hii ikiwezeshwa itasaidia kupunguza umaskini kwa vijana wetu na kuleta maendeleo yenye tija kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, miaka mitano iliyopita na mwaka huu nimeendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Tumekuwa na tatizo kubwa sana. Pamoja na kuwapongeza sana wenzangu wa habari, magazeti, televisheni na kadhalika. Hapa katikati kumetokea wingu kubwa la vyombo hivi hivi vya habari, aidha, kuhitilafiana na jamii ya Watanzania kwa namna moja ama nyingine. Kwa muda mrefu Kamati yangu imeduwa ikiombwa Muswada wa Uhuru wa Habari uletwe Bungeni. Lakini pia Muswada wa Umiliki wa Vyombo vya Habari Miswada hii ikiletwa, nchi yetu ikawa na Sheria hizo mbili, haya malumbano yasiyokuwa na tija hayatakuwepo. Mimi sijui kwanini, Serikali tunaogopa kuleta hii Miswada, kuna nini? (Makof)

Leteni tutengeneze Sheria itakayowasaaidia wenzetu wanahabari, lakini itakayowasaaidia nchi yetu na wananchi wa Tanzania wapate habari kulingana na utaratibu tutakaojiweke. Sasa haya yote tunayolalamika hapa ndani, huko nje, kama hatutakuwa na Sheria hizi mbili tunafanya nini? Tusifanye soko hili, kiwanda hiki cha habari kama ni kiwanda tu holela hakina mwenyewe. Tutapeana hapa lawama zisizokuwa na msingi. Mimi sioni ni kwa sababu gani tunakuwa na hofu ya kuleta Miswada hii miwili. Kamati imefanya kazi sana hata kipindi kilichopita. Naiomba Serikali leteni hiyo Miswada miwili tuikalie hapa Bungeni, tuwashirikishe wadau wa habari, watuambie Serikali ituambie, watanzania tujulize tunataka kuwa na *industry* ya habari katika nchi yetu inayofananaje? Hapo tutakuwa tumemaliza kazi na kufanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali isisite katika hili itusaidie ili tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusikitika, na mimi kama mchangiaji wa leo naendelea kusikitika sana na jinsi liliyotelekezwa jengo la *TBC Mikocheni*. Ukipika kwenye jengo lile, huwezi kuamini ni kwa kiasi gani Serikali haioni umuhimu wa lile jengo pale Mikocheni. Kumbukumbu zote za Habari ziwe za matukio ya redio, ziwe za matukio ya magazeti na ziwe za matukio ya televisheni toka wakati wa uhuru zipo kwenye jengo hilo ambalo ukiingia, huwezi kuelewa ni kitu gani kinachoendelea. Jiwe la msingi liliwekwa nadhani na Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi miaka mingi iliyopita. Jengo lile linatia huruma. Serikali inapoteza kitu cha maana kabisa pale. Tumeomba sana Serikali, tunao *NSSF* wanajenga majengo kila siku, kwanini wasimalizie lile jengo na urithi huo wa Watanzania uendelee kubaki mahali ambapo ni salama?

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli ninaomba sana Mheshimiwa Waziri na kwa sababu Serikali nzima iko hapa inisikie, jengo lile limalizwe, litengenezwe na tuhifadhi hizo nyaraka za Serikali vizuri. Ni urithi mkubwa wa kihistoria wa watoto wa nchi hii. Kikazi hiki ninachokisema cha asilimia 45 hawakuwepo wakati wa uhuru, hawajui hata wakati wa vita ya Kagera kulikuwa na nini. Hawajui na wakati mwingine tunawalaumu hawa watoto hawayajui haya mambo. Sasa hivyo ndio vitu vya kihistoria vya kuwaeleza watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba lugha ya Kiswahili iheshimike na naomba mila na desturi za nchi yetu ziheshimike. Sasa hivi kuna wimbi kubwa la kusahau mila na desturi zetu. Tunajiingiza kwenye mila za kigeni na matokeo yake tunaharibu heshima na utu wa nchi yetu ya Tanzania. Mimi nadhani tukuballane, ifike wakati tuendelee kujali utamaduni wetu kama kielelezo cha Taifa. Waheshimiwa Wabunge jana hapa wamelalamika, Mheshimiwa Mariam Msabaha amesema, watoto wanavaa nguo fupi hovyo, hakuna anayejali. Miaka ya nyuma mtoto katika ukoo, katika jamii katika kijiji akifanya kosa alikuwa ni mtoto wa wanakijiji wote. (Makof)

Mheshimiwa Spika, leo hii watoto wetu wanapoteza utamaduni wa nchi yetu. Mavazi yao siyo ya kitanzania. Wako watoto hata lugha za asili za wazazi wao hawajui. Hata kusalimia kwa lugha za wazazi wao hawajui. Hivi baada ya muda mtoto huyu asipojua hata lugha ya baba na mama yake akishazaa na yeze lugha ile itakuwa imepotea kwenye ukoo huo. Kwa hiyo, nadhani tukiacha mbali lugha yetu ya Kiswahili na umuhimu wa kuendeleza Kiswahili chetu, kutenga fedha ya kutosha kuhakikisha Kiswahili kinapata nafasi, mila na desturi za Watanzania ziendelee kuwepo.

Makabila yaliyokuwa yanaamkia kwa kupiga magoti, watoto wafundishwe kuendelea kuamkia kwa kupiga magoti, makabila yaliyokuwa hayatakiwi kufanya vitu ambavyo havina msingi, tuangalie kama tulikuwa na mila na desturi ambazo zina afya kwenye Taifa letu, tuendelee kuwa nazo, tutengete fedha za kurithisha utamaduni huo na kurithisha mila hizo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuomba Wizara ndani ya miaka hii mitano mtuletee vazi la Taifa. Mataifa yote na Mataifa mengi ya Afrika wana mavazi yao ya kutambulisha utamaduni wa nchi zao. Tumeanza mchakato wa vazi la Taifa. Huu ni mwaka wa kumi hatujapata. Hapa mimi naomba tufikie mahali tuwe na hizi *identity*. Ukienda zako nje, watu wakujue wewe ni Mtanzania. Pale uwanja wa ndege, wageni wakiingia, wajue wamefika Tanzania. Inaleta raha jamani! Tunapoteza mambo mazuri mengi ambayo kwa kweli yametupa heshima ya nchi yetu toka enzi za Mwalimu. Sasa leo masuala yale yote toka Mwalimu anapigania uhuru, leo ni miaka 50 enzi zile za Mwalimu zote tunataka kuzififisha. Mimi nashauri sana haya ni mambo ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri, mikataba yote inayohusu maendeleo ya vijana, mikataba yote inayohusu utamaduni wa Taifa letu tuleteeni turidhie na naiomba Serikali iendelee kuvacha Vyuo vya VETA vya kuwasaidia vijana kwenye Wizara ya Elimu, Wizara ya Elimu ina majukumu mengi. Vyuo hivi ama vihamishiwe Wizara inayowalea vijana ama vipelekwe Wizara ya Kazi na Ajira, vikasaidiwa na kusimamiwa katika mfumo wa kutengeneza ajira. Kule kwenye Wizara ya Elimu, jamani hawa wamezidiwa. Vyuo Vikuu tumefungua vingi, vimejaa huko, Vyuo vya Ualimu, Elimu ya Sekondari na Vyuo sijui vya nini. Kule jamani kumejaa. Mimi nadhani hebu tuhamishe hiki kitengo cha ufundi kwa maana ya kuleta maendeleo ya vijana, ama turudishe vile vyuo kwenye Wizara hii, ama tupeleke kwenye Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii. Lakini, awali ya yote, kwa kuwa toka Mwezi wa Ramadhan uanze, ndiyo mara ya kwanza kuchangia. Naomba nichukue nafasi hii niwapongeze na niwatakia heri Waislam wote wanaofunga na kumaliza salama Kumi la Kwanza, Kumi la Rehema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri. Hakuna kizuri kisichokuwa na kasoro, hilo wavumilie. Yanayotolewa hapa ni kwa ajili ya kuboresha bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza, nianze kugusia suala la vijana. Vijana ni kiwanda kinachoalishwa kila siku, vijana wako wengi sana, na kijana ili awe kijana lazima awe na ajira inayoeleweka, iwe kwenye sekta binafsi, iwe kwenye Sekta ya Serikali au kwenye Mashirika ya Umma. Lakini Wizara hii lazima ijikite kindakindaki, iweke mkakati ni vipi itawasaidia hawa vijana. Kuna ajira nydingi sana, hatuna haja ya kubabaika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara hii, peke yao hawawezi kama Wizara, lazima washirikishe Wizara ya Kilimo, Viwanda na Biashara na Wizara ya Elimu, kwa sababu humu kuna sekta ambazo zinaweza zikatoa ajira kwa vijana wetu. Ukienda kwenye maeneo mbalimbali kwenye Mikoa yetu, kwenye Wilaya zetu, utakuta kuna maeneo makubwa ya kilimo, maeneo makubwa ya kufuga, maeneo makubwa ya kuzalisha mbogamboga na hata matunda.

Kwa hiyo, ni vizuri wakachukua vile vijiwe ambavyo tayari vipo, wenyewe wameshavitengeneza, na uzuri ni kwamba wao wanachotakiwa ni kupeleka taaluma tu. Lakini vijana wenyewe wameshajitambua kwamba kundi hili wako wapi na kundi hili wako wangapi? Wanaomaliza vyuo, wale ambaao wamesomea kilimo, wanazagaa mitaani. Sioni sababu kwa nini wazagae mitaani. Waliosomea ufugaji nyuki, waliosomea ufugaji wa kuku na ng'ombe wanazagaa mitaani. Kwa nini Wizara hii ya Vijana kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika wasiungane wakatoa ajira hata kwa kuwapa mikopo midogo midogo? Wakizalisha wanavyozalisha, mikopo itarudi. Wazihushe Benki zetu zinazoweza kutoa mikopo ili vijana wetu waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, uzuri wa Wizara hii, pamoja na kundi la vijana liko kwao, lakini kuna ajira nyingine iko ndani ya Wizara hii ya sanaa, ndani ya Wizara hii pia kuna utamaduni. Mimi nina baba yangu anaitwa Halfan Matitu, yuko Chuo cha Sanaa Bagamoyo, toka akiwa kijana anasomesha watu kupiga marimba. Amekwenda mpaka nje ya nchi kwa sababu ya kupiga marimba. Hiyo ni taaluma ambayo inatoa ajira. Nawaomba Wizara ihakikishe vijana wetu hawapotei, wanapatiwa ajira kutokana na sekta ambao zimejitengeneza zenyewe.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye lugha, hili ni jambo la kusikitisha ndani ya Bunge letu. Tumesomewa tamko humu humu ndani kwamba tutumie lugha yetu ya Kiswahili. Cha ajabu, sheria zetu mpaka leo hii zinaletwa kwa Kiingereza. Sheria hizo tunamtungia nani? Sheria hizo kama tunawatungia Watanzania waliko kule Vijijiini, unampa sheria ya Kiingereza akaifanyie nini? Waingereza walishatuachia nchi siku nyingi, sheria zao tulishaziona, wajibu wetu ilikuwa zile zilizokuwepo kuzitafsiri na tunazositengeneza, tuziweke katika lugha ya Kiswahili. Yakija matamko kutoka Umoja wa Mataifa, hatuna budi yaje kama yalivyo, lakini yafanyiwe utaratibu wa kutafsiriwa ili yaweze kueleweka kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, hilo la Kiswahili ni sisi wenyewe kulikazania humu ndani. Tusipoangalia, Mikutano yetu tunayokwenda, basi kama Wachina, kama Wafaransa, kama Waarabu wanajivunia lugha yao, sisi tuna tatizo gani?

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani zina radio zao zimeweka Idhaa Maalum ya Kiswahili. Sisi Watanzania wenye Kiswahili chetu hatukienzi. Kwa kweli hilo ni la kulisikitikia sana. Ninaomba Wizara hii iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha Kiswahili kinaenziwa.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye suala la mavazi, Serikali miaka ya huko nyuma ilikuwa na utaratibu mzuri sana. Humu ndani kila mtu anayesimama analalamika, watu wanavaa nguo nusu uchi. Pengine hawa wanaotoka majumbani wamevaa vizuri, wakitoka nje wanavaa vibaya. Kama Serikali ina meno na ina amri, inashindwa nini kurudisha utaratibu wa zamani, wanaotembea na nguo fupi wote walikuwa wanakamatwa. Wizara ya Utamaduni inaruhusu vipi wanaume wanapocheza ngoma, muziki, wanavaa suruali japokuwa mdebwedo, lakini na fulana wameficha viuongo vyao? Iweje waruhusu wanawake wavae nguo nusu uchi, viuno nje? Jamani, sisi wanawake tusipojistahi wenyewe, nani atatupa staha? Kuna vitu vingine havistahili kuonekana na watu. Wanawake, vitu vingine havistahili vionyeshwe ovyo! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Wizara hii, bahati nzuri Wizara hii imekamilika, ina mwanamke na ina mwanaume. Waheshimiwa mawaziri, hakikisheni mnashirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, askari wapite barabarani, siyo mgambo wanadhalilisha akina mama wanaotafuta riziki. Wale akina mama wanakwenda sokoni na vijana wetu wanaouza vitu vidogo vidogo, mgambo wanawakamata, wanawapiga. Haifai! Wawakamate wanaokwenda uchi. Tuache kulalamika humu ndani, tufanye vitendo vya kuonekana na tufanye kazi ya kuonekana. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumekwenda sambamba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka hapo, naomba sasa nigosie Idara ya Habari. Kiwanda hiki cha habari tofauti na taaluma nyingine, Daktari atakupima malaria, atakupa dawa baada ya siku saba ndiyo itajulikana.

**SPIKA:** Na wewe useme kama ni mwanahabari pia.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Ahsante, nilifikiria watu wanalikumbuka hilo.

**SPIKA:** Hatukujui! (*Kicheko*)

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimesomea taaluma ya uandishi wa habari. Nashukuru. Habari ni kiwanda ambacho kinatoa majibu hapo hapo. Mimi naongea sasa hivi, mtu anasikia huko. Hawezi aka-forward wala aka-rewind, imetoka.

Sasa basi, toka Awamu hii ya Nne ilipoanza, tuliwaahidi kwamba italetwa sheria ambayo itatulinda sisi, itawalinda waandishi wa habari, itawalinda wenye vyombo vya habari. Lakini mpaka leo hii halijafanyika, tunategemea nini? Tusishangae tunapoona rushwa zimezidi, tusishangae tunapoona mwandishi anapotumia kalamu yake ambayo siyo kitu kizuri, anakuwa

ye ye hakimu, anakuwa ye ye askari, anakuwa ye ye kila kitu. Nataka nitoe mifano, kwa nini nimesema hivyo? Kwa kuwa hakuna sheria inayolinda. Mwandishi anatumia kalamu yake saa hiyo hiyo kukupa jina analolitaka ye ye. Atakuita wewe fisadi, atakuita wewe mwizi, hujapelekwa Mahakamani wala hujathibitishwa wewe fisadi.

Mheshimiwa Spika, kuna mwandishi mmoja na gazeti lake, ninavyosema ananisikia, na nadhani yuko katika viwanja hivi, amenipa cheo mimi cha kuwa Yuda Iskarioti. Mimi jina langu Zaynabu. Yuda Iskarioti wapi na wapi? Waandishi wa habari wawe makini. Lakini, mkileta sheria, tunaweza tukawabana. Huwezi ukaandikwa vibaya ukakaa kimya, huna sheria inayokulinda.

Mheshimiwa Spika, kuna Baraza la Habari Tanzania, lakini Baraza lile halina meno. Mheshimiwa Waziri, nataka unijibu, lini uthalipa meno Baraza la Habari ili liweze kuhakisha wanaoandika taarifa za kupotosha, wasiandike taarifa kwa maslahi ya mtu.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la mishahara midogo. Waandishi wanapopewa mishahara mikubwa, jamani, bahasha hazitakuwepo. Waandishi wa habari nao ni binadamu, wanataka waishi, lakini mshahara mdogo, elimu ya uandishi wa habari haipo ya kutosha, ndio hao wanaitwa makanjanja. Leo kaja, kapewa kazi ya kuja kuandika Bungeni, kapewa posho. Posho hiyo ya siku kadhaa, kule nyumbani anahitaji pesa, huku mtu akimpa hela ye ye ataikataa? Lakini, mkiweka sheria, yule atakapopokea zile pesa, hataandika kile anachokitaka, ataandika kalamu yake inavyomwelekeza na maadili yake.

Mheshimiwa Spika, nawaombe waandishi wa habari wenye vyombo vya habari, hasa waangalie maadili ya uandishi wa habari. Sheria ya nchi haisemi mwandishi wa habari ni nini na mwandishi wa habari ni nani. Wenzetu Uganda, huwezi kuwa mwandishi wa habari lazima uwe na taaluma kwanza, halafu ndio unakwenda kusomea Uandishi wa Habari.

Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameweuka mambo ya mitaala. Lakini hajasema hiyo mitaala inaanza lini, kwa sababu tukiwa na Waandishi wa Habari waliobobeaa kwenye taaluma fulani, matatizo mengine hayatakuwepo. Tuwe na Mwandishi wa Habari wa Uchumi, tuwe na Mwandishi wa Habari wa Afya, tuwe na Mwandishi wa Habari wa Sheria, hakutakuwa na migongano. Lakini, ye ye anajua tu zile taaluma za uandishi, hana taaluma nyingine. Leo mhariri atampangia aende Mahakamani, kesho atampangia aje Bungeni, keshokutwa atampangia aende kwenye uzinduzi sijui wa Kilimo Kwanza. Hana mwelekeo! Hata uchambuzi wake unakuwa haunogi. Lakini bado wanapaswa na wao waweke ile habari yao wanayoandika iwe inalenga kukidhi mahitaji ya msomaji au msikilizaji au mtazamaji.

Mheshimiwa Spika, hilo naliomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja zake aniambie, Sheria ya Habari imefikia wapi? Tusiogope, tunatunga wenyewe na sheria zinatungwa kwa ajili ya watu. Kwa hiyo, naomba nijibiwe suala la sheria liko wapi, suala la mitaala litaanza lini, hayo yatatusaidia.

Mheshimiwa Spika, twende kwa wanaomiliki Vyombo vya Habari. Mimi nataka kujua, utaratibu wa kuwa na Vyombo vya Habari ukoje? Kwa sababu, hakuna taaluma isiyokuwa na sheria na kanuni zake. Hata wachezaji ngoma wana sheria na kanuni zao. Kule kwetu sisi tuna ngoma inaitwa Tokomile. Sheria ya ngoma ya Tokomile, ni lazima mchapane viboko. Sasa, kwenye hili suala la kutoa leseni kwa waandishi wa habari likoje? Mtu anaanzisha gazeti, hata kama kaishia *Form Four*, kaishia *Form Six*. Huwezi ukaanzisha duka la dawa au kuwa daktari kama huna cheti ambacho umesomea kwenye taaluma hiyo. Naomba na hilo pia nipatiwe majibu, hili litatoa migongano katika magazeti yetu na vyombo vyetu vya habari. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Redio Tanzania kulikuwa na utaratibu unawekwa, lakini angalau wiki sita wanakupa mafunzo ya kukaa mbele ya kipaza sauti na vipi ukarekodi watu huko na utauliza vipi maswali. Sijui kama utaratibu huo hivi sasa upo! Kama haupo, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie, kwa nini? Hasa na waandishi wa habari wengine wanatuhabibia Kiswahili. Kwenye 'la' anasema 'ra' na kwenye 'ra' anasema 'la', kwenye 'n' anasema 'm', kwenye 'nchi' anasema 'njii'. Liangaliwe kwa makini, tusipotoshe vizazi vyetu. Hilo naomba lizingatiwe sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba suala la maslahi ya waandishi wa habari lizingatiwe, wapewe mishahara itakayowakidhi, tuepukane na kuwalalamikia kwamba wanataka rushwa kila siku. Jamani na wao binadamu. Lakini kukiwa na utaratibu mzuri, Wizara ikitengeneza, hakuna atakayebabaika, hatutapata watu sijui wanaitwa makanjanja, wote watakwenda shule, wote wataandika habari vizuri na habari zitakuwa na uwiano kwa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa waandishi wa habari ni kwamba muache kuwa Mahakimu, msimpe mtu cheo cha ufsadi kabla hajawa fisadi. Maana mkitetewa na ninyi mpokee yale mnayoambibiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Lakini, nipatiwe majibu ya kina. (*Makof*)

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru na mimi kuniona ili nichangie mada iliyopo mbele yetu. Kabla ya kuanza na mada hii, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalla kupata nafasi hii katika siku Tukufu ya Ijumaa, ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, katika kumi Tukufu la Makhfira la kughufiriwa Waislam na moto, wale wanaojitahidi kufunga vema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kuchangia mada hii kwa kuanza na *TFF*. Lakini kabla sijakwenda mbele zaidi, nataka kusema kwamba Tanzania ni muungano wa nchi mbili, Zanzibar na Tanganyika. Kama ingekuwa hapana Zanzibar, basi Tanzania isingekuwepo, na kama ingekuwa hapana Tanganyika, vile vile Tanzania isingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, *TFF* ni chombo kinachoongoza mpira Tanzania. Lakini, kinaonekana, kana kwamba ni chombo cha Tanzania, lakini utendaji wake kinafanya kazi zake kwa Tanzania Bara peke yake, lakini kimejivika koja la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nathibitisha haya ninayoyasema kwa kutoa vipengele moja kwa moja ili nanyi mmpate faida. Katiba ya *TFF* inazungumzia Bara peke yake, Zanzibar haipo. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, viongozi wote wa *TFF*, basi wanatoka Bara, Zanzibar hakuna kiongozi hata mmoja. Jambo lingine, wale waliowachagua viongozi wa *TFF* wote ni kutoka Bara, Zanzibar hakuna mtu ye yote aliyepiga kura kuuchagua uongozi wa *TFF*.

Mheshimiwa Spika, mipaka ya katiba yake inafanya kazi ndani ya Tanzania Bara peke yake inafanya kazi ndani ya Mikoa 21, Mikoa mitano ya Zanzibar haimo. Utendaji na utekelezaji wa kazi zake vile mire kipaka yake ni Tanzania Bara tu, Zanzibar haihusiki. Lakini, kama hayo hayatoshi, misaada yote inayotoka *FIFA* na *CAF*, inatumika kwa kutengeneza maendeleo ya upande wa Tanzania Bara peke yake kimichezo. Zanzibar haipati misaada yoyote kutoka *CAF* wala kutoka *FIFA*, haipati misaada hiyo.

Mheshimiwa Spika, *TFF* ni chombo ambacho kimevaa joho la Serikali ya Muungano, lakini kinafanya kazi upande mmoja tu wa Muungano. Sasa hili ni tatizo kwa maendeleo ya soka letu la Tanzania, kwa sababu utakuta Zanzibar inadorora kimaendeleo ya mchezo wa mpira. Wako vijana ambao wana vipaji, vijana wazuri, vijana wenye mori wa kucheza mpira, lakini utakuta wanabanika kwa sababu wanakuwa hawana vitendea kazi, misaada yote inamalizikia Tanzania Bara, Zanzibar hakuna kitu chochote. Sasa hii inadumaza maendeleo ya mpira ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar inaathirika vipi? Zanzibar inaathirika kwa sababu kwanza inakosa uanachama wa *FIFA* na *CAF* kwa sababu Tanzania Bara imekwishatangulia na imechukua joho hili, imevaa joho hili. Kwa hiyo, Zanzibar inakosa uanachama wa *CAF*. Lakini pia kama hilo halitoshi, Zanzibar inatowe ka katika dira ya kandanda duniani. Inatowe kabisa kabisa. Vijana wa Zanzibar hawashiriki katika michezo yoyote ya Kimataifa, ikiwa ya mwaliko au ile inayoandaliwa na *FIFA* na *CAF*, haipati kabisa kabisa. Kwa hiyo, utakuta Zanzibar inadidimia kwa maendeleo ya mpira.

Mheshimiwa Spika, chama cha mpira – ZFA ambacho kinaongoza mpira Zanzibar, kinazidiwa nguvu, hakiwezi kusaidia chochote juu ya hili. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama, aje aniwekee uwazi juu ya jambo hili kwa sababu inawezekana labda mimi nazungumza, lakini yeze ndiye anafahamu zaidi, aje anielezee kuhusu hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili ambalo nalizungumza hapa mbele ya Bunge hili Tukufu hata wao Zanzibar – ZFA wamellilalamikia hili. Wamellilalamikia siku nyingi sana, lakini utatuzi wake haufiki mwisho. Unaendelea tu. Kwa hiyo, madhambi ukiyakusanya mengi, yakizidi, unaangamizwa. Ni hatari kabisa kwa kweli. Tunapoliona tayari kosa limetokea, basi ni vizuri kuliwahi pale pale tuliondoe ili tuendeleze vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninayo barua hapa ya ZFA kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, naomba ninukuu barua hii ili Bunge lipate faida. Barua hii ya tarehe 16 Julai, 2011, Ref. No. ZFA/TFF/22/VOL.V/196, inatoka ZFA Zanzibar kuja TFF Bara. Anasema Bwana Leodger Tenga, "Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Dar es salaam, Tanzania.

Kuhusu masikitiko kutoka Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA) dhidi ya Chama cha Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), tafadhali husika na mada ya hapo juu, Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA) kimelazimika kuleta kwako masikitiko yetu kutokana na kuvumilia na kustahimili kwetu kwa muda mrefu bila kuona mafanikio ya yale yote ambayo tumekuwa tukiyapoteza muda wa kukutana, kupanga na kusubiri utekelezaji wake usioonekana, si kwa ZFA wala jamii ya mpira wa miguu Zanzibar, kinachoonekana ni vikao vingi vimepita na sasa kusogezwa mbele na kupangwa upya vikao visivyoukuwa na tija.

Tumeanza tokea mwaka 2009 mpaka leo mwaka 2011. ZFA tumefikia kueleza kuwa sasa wakati wa vikao ni basi, kilichobakia ni kueleza kwako yafuatayo, pamoja na barua hii naambatanisha maelezo yafuatayo kutoka ZFA Taifa kwako Rais wa TFF, ahsante."

Mheshimiwa Spika, barua hii inatoka Zanzibar na nakala yake kwa Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii, Michezo Zanzibar na Mheshimiwa Waziri Habari, Vijana Utamaduni na Michezo Tanzania. Kwa hiyo, bila shaka Waziri hili analijua.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo la siku nyingi, lipo, lakini linashindwa kufika muafaka ili tukaendelea na michezo, na tulilaumu siku nyingi, itakuwa maisha ya wasindikizaji kwa sababu haki haitendekei. Jambo la shirika moja, akinuna, hilo Mwenyezi Mungu halipi Baraka, litakuwa linaendelea ndani ya matatizo tu siku zote. Kwa hiyo, naomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anielezee na lifanyiwe marekebisho tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nazungumzia kuhusu makocha wa kigeni wanaoletwa kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, makocha wanaokuja Tanzania kwa ajili ya timu ya Taifa, vile vile, Wanafanyakazi upande mmoja, tunawalemaza, wakifika wanafanya kazi upande wa bara peke yake Zanzibar hainufaiki. Alikuja kocha Maximo ambaye Rais ndiye aliyesababisha aje hapa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania, lakini akifika, bado anafanya kazi upande wa Bara. Timu zote za Bara zinazocheza daraja la kwanza anazipitia, anatazama vipaji vya vijana wanaohusika, anachagua timu ya Taifa, Zanzibar hajakwenda hata kocha mmoja. Sasa sijui Zanzibar ni Tanzania au ni wapi. Kwa sababu anakuja kwa ajili ya Tanzania, lakini anafanya kazi upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Zanzibar wenye vipaji wanakosa kushiriki timu ya Taifa, hawashirikishwi. Kocha mwingine aliyejuja Poulsen naye ndiyo hivyo hivyo anachukua wale aliorakuta, wale aliorarithi tu. Vijana wenye vipaji hawachaguliwi ndani ya timu ya Taifa. Huu ni uonevu.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba Zanzibar hakuna vijana wenye vipaji, wapo. Kuna mwaka mmoja, kidogo nimesahau, Simba ilikuja ikacheza na timu mmoja ya Zambia, sijui kama ni Mfulira au ni nini, ikafungwa mabao manne kwa bila, katika uwanja wa Taifa. Ilirudi kwenda Zambia lakini illifanya vitu ikafunga mabao matano kwa bila, kule Zambia, mfungaji alikuwa ni kijana kutoka Zanzibar ambaye kafunga mabao yote anaitwa Thuweni Ally.

Mheshimiwa Spika, wapo vijana ambao wana uwezo, na sijui timu ya Taifa inachaguliwa kwa vigezo gani. Nichukue *Challenge* ya mwaka 2009 iliyofanyika Kenya, pamoja na timu zote zilizoshiriki kule, lakini kulikuwa bado kuna timu mbili ambazo zimealikwa, timu ya Chipolopolo ya Zambia ilikuwa ni timu moja kali ambayo ni hatari. Kila timu iliyokutana nayo ilikuwa inafunga, ikaingia robo fainali kwa bahati nzuri ikakumbana na timu ya Zanzibar Heroes kutoka Zanzibar, huo ndio ulikuwa mwisho wake. Ulichezwa mpira dakika tisini hawakufungana, zikaongezwa dakika thethini hawakufungana, ikatolewa Chipolopolo kwa mikwaju ya penati na Zanzibar. Sasa inakuwaje wachezaji ambao wana vipaji kama hivyo wanaipeleka timu kama hivyo halafu akakosekana hata mchezaji mmoja ndani ya timu ya Taifa, Taifa Stars? Hakuna mchezaji hata mmoja wa timu zinazocheza ligi ya Zanzibar!

Mheshimiwa Spika, tuna wachezaji wawili ambao wanachezea timu ya Yanga, Babi na Haroub (Cannavaro) ni hao tu. Lakini hakuna mchezaji yeote wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hili linauma! Tukiyazungumza sana haya, tunaonekana Wazanzibar, jamani hii ni haki yetu, ni sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano na sisi tuna-share, ni lazima hili tuliseme.

Kwa hiyo, Waziri atakapokuja aniweke sawa ili na mimi moyo wangu kidogo utulie kwa sababu kwa kweli moyo wangu siyo mzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi namfahamu Waziri alipokuwa katika umoja wa Vijana, aliwahi kuja katika Jimbo langu la Nungwi Kilimani na akatoa *speech* kuhusu Wapinzani. Nilifurahi sana kwa sababu alikuwa anaelimisha, lakini naomba jambo moja anisaidie. Nina timu mbili ambazo zinacheza daraja la kwanza Zanzibar, *Mundu Sports Club* na *Sharp Boys* za Nungwi, nakuomba Waziri kwa vile ni mtu mzuri na ninaamini atanisaidia naomba vifaa vya jezi kwa timu hizi anisaidie. Nina imani kwamba imani yake na ukarimu wake atakapokuja kwenye majumuisho, basi naomba jawabu. Kama nimepata au nimekosa, na ukarimu wake utaonekana hapo. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Mimi nilifikiri angesema akirudi jioni hapatatosha hapa, kumbe tayari jezi tu. Haya tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara hii. Naomba kutangaza maslahi kuanzia mwanzo mpaka mwisho kwamba mimi ni mdau kifedha, kijamii na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba kwanza niwatakie kheri vijana wote nchini Tanzania kwa sababu leo tarehe 12 Agosti, ni siku ya kimataifa ya Vijana. Kwa hiyo, vijana wote duniani wanasherehekea siku hii katika hali yetu ngumu, vijana Mitaani huko, tuitambue hii siku kwa sababu labda mwakani Agosti, 12 ya mwaka 2012 itakuwa na matumaini zaidi kuliko hii.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea suala la vijana, tupo *very serious*, na ndio maana tunaongelea vitu endelevu kama kuanzisha Benki ya Vijana ya Taifa, hili nimeliongelea jana. Kuna mwenzagu mmoja Mheshimiwa akanyanyuka akikipongeza Chama cha Mapinduzi na Umoja wa Vijana nadhani kwa kuanzisha Benki ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi. Ni kitu kizuri, lakini ningewashauri kwamba wao ni Chama Tawala, wao ndio wana Serikali, wangetumia fursa hiyo kuanzisha Benki ya Kitaifa na siyo ya kichama, hasa ukizingatia kwamba historia inawahukumu kwamba siyo wazuri katika kuendesha biashara kama ambavyo walishindwa mradi wa mabasi, umoja wa vijana. *SUKITA* ilikufa, kwa hiyo, hili wangeliweka kitaifa zaidi ili mawazo yetu kwa pamoja yatumike na kuanzisha Benki ya Vijana ya Kitaifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitajikita zaidi kama nilivyotangaza maslahi zaidi kwenye muziki hasa muziki wa bongo fleva. Naomba nichukue fursa hii kuwakaribisha Dodoma na humu ndani pia ingawa mmeshawakaribisha Viongozi, Marais wa Mashirikisho yote ya Sanaa ambao wapo pale.

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru kwa heshima niliyopata jana kama Waziri Kivuli kwa Wasanii nilioaalika kukaa kwenye *gallery* yako, walikaa kwenye viti vyekundu, jambo hilo tu limebadilisha *vibe* mtaani, yaani kukaa wale wasanii kwenye viti vyekundu kumeleta *vibe* tofauti kabisa mtaani na vijana wamefurahi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba nina uhakika Rais wa Shirikisho la Wasanii aliyeo hapa amekuja kwa *bus*, tena siyo Shabiby ambayo ni *Luxury*, na hiyo ni *reflection* ya namna gani ya wasanii wa Tanzania bado tuko chini. Miaka michache ya nyuma kulikuwa kama huko mtaani kuna *concert* ya Dudu Baya, msanii mmoja tu, miaka sita saba iliyopita wakati hili gemu linakua, kama kuna *concert* ya Dudu Baya hapa Dodoma, basi utaona *balloon* kama sita saba zinaranda randa mitaani, amekuja Dudu Baya na wapambe wake wote wapo kwenye *ma-balloon*. Lakini leo hii unasikia kuna *Fiesta* tuseme katika Mkoa wa Dodoma, wasanii 60 huoni hata pikipiki ya msanii inazunguka mtaani. Hiyo ndiyo hali ya muziki huu. Hiyo ndiyo hali ya wasanii.

Mheshimiwa Spika, leo nitaongea kwa uchungu sana na kwa makini sana na ninaomba Bunge hili na Taifa litusikilize. Haiwezekani vijana wote wa Taifa hili la Tanzania tufanikiwe kwa kuuza unga. Niuze madawa ya kulevyaa ndiyo niwe tajiri, ndiyo nijenge. Tumeshindwa kubuni vitu kwa ajili ya watu wetu, tunashindwa hata kuendeleza vitu ambavyo vimejitokeza vyenyewe kama muziki wa Bongo *Flavour*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaachia watu binafsi wana-*tamper with this*, wanaharibu hiki kitu. Huu muziki ulikuwa unakwenda wenyewe. Tulivoanza huu muziki, Wadosi wanaoitwa Wahindi, walikuwa wanatufuata Sinza, mtaani, *bar*, saa sita usiku tunakaa nao Sinza Bar tunaongelea biashara. Leo hii unakwenda ofisini kwa Wahindi, wasanii wenyewe majina ambao wako kwenye *TV* kila siku wamekaa foleni utafikiri wapo hospitali ya Mwananyamala ambako Daktari hayupo. Wasanii wa Taifa hili wanakaa foleni kusubiri *contract*, anakaa masaa kumi, sa kumi na mbili asubuhi yupo mpaka saa kumi na mbili jioni ndiyo anakwenda kuonana na promota. Pale ata-*discuss* kitu gani? *Confidence* iko wapi?

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kumwona tu Mhindi, amesharidhika kwamba mimi nimeshafanikiwa. Saikolojia imebana na hatukufikishwa huko kwa bahati mbaya. Tumefikishwa huko kwa makusudi na watu ambao Serikali imewaacha wateke hiki kitu chetu. Watu ambao wametumia ikulu kufanya ufsadi hata kwenye *Bongo Flavour*, na hawa watu wanajulikana na wanatetewa na watu waliopo ndani ya jumba hili. Hiki kitu hakiwezekani, leo tunataka majibu kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, watu wanasema mnazungumzia *studio*. *Studio* siyo *issue*. Tunazungumzia suala la *studio* ya Rais kwa sababu ndiyo tumepata *weakest link*. Pale ndiyo kuna uthibitisho ambao tunaweza kuweka mbele, ni namna gani watu wameteka hata dhamira njema ya Rais Kikwete katika kuusaidia huu Muziki. Sijawahi kumwona Rais Kikwete baada ya kuwa Rais, lakini nilimwona wakati anaanza harakati zake akiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje akihuusika na muziki huu na picha ninazo. Rais hawezi kufanya hivi vitu wanavyosema amefanya leo.

Mheshimiwa Spika, unasema *studio*, eti mara amewapa *THT*, mara sijui kawapa *Tanzania Flavour Unit*, nini maana yake? Mnaficha nini? Mnaficha nini? Mnatuletea uozo, matokeo yake mnachoresha tu Rais mitaani. Kwa sababu watu wanaelewa hii Tanzania siyo Tanzania ile ya Uhuru na Mzalendo peke yake. Hii Tanzania ni tofauti, msimchoresha Rais Kikwete na nia yake njema kuusaidia huu muziki.

Mheshimiwa Spika, iishie hapa leo na tuanje upya tupewe fursa makampuni *sponsor* acheni vitu mnayofanya kwenye *u-marketing manager*. Ni uzalendo gani unaokufanya wewe *Marketing Manager* kusaini dola laki laki nne alipwe Jay Z halafu unasaini shilingi laki mbili au laki tatu alipwe msanii wa Tanzania kama Afande Sele? Katika onyesho hilo hilo na zaidi kila wanapokuja tunawafunika katika yale maonyesho. Hata Wasanii wa Nigeria wanakuja hapa mnawalipa dola laki moja, dola elfu hamsini, ni nani anayeidhinisha? Wanalipa kodi kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kuna wakati mimi nilikwenda Marekani kwa shughuli binafsi, kufika kule Watanzania wakasema Mkongwe ni lazima ututumbuize. Nikasema sawa, nikafanya *show* moja ya kufa mtu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kesho yake napokea *email* kutoka kwa ubalozi wa Marekani unaniambia nipige simu, nikawapigia simu wakaniambia *you are doing a good thing, you are okay, we are appreciate what you doing* kuendeleza sanaa zenu na kila kitu. Lakini umefanya makosa, unatakiwa ufuate sheria moja, mbili, tatu, ili ulipe kodi. Mimi nimetoka Tanzania nakwenda kulipa kodi Marekani kwa dola elfu mbili niliyolipwa? Wale wanakuja hapa wanalipwa dola laki nne, laki tatu, wanabeba zote wanaondoka nazo, hawalipi hata kodi kwa nchi. Halafu Wizara ina bajeti ya shilingi billioni 14.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 14 huwezi kujenga hata *theatre*. Mheshimiwa Nchimbi, huwezi kujenga Kiromo kwenye uwanja mpya ulioupata kwa bajeti ya Shilingi bilioni 14. Ningekuwa na uwezo leo hii kwenye ile fungu la Kaka yangu Mwakyembe na mimi ningekwenda kuchukua Shilingi bilioni ishirini kule nipeleke kwa Mheshimiwa Nchimbi ili tuongeze bajeti kwa sababu zile fedha hazina maelezo na zimepelekwa uchukuzi. Kwanini tudharau Wizara ya Utamaduni?

Mheshimiwa Spika, utamaduni unatoa mchango kwa Taifa, utamaduni ni uti wa Mgongo wa Taifa, halafu mnakaa mnasema Rais ametoa *studio*, mara sijui iko *THT*. Kaka yangu hapa na ye ye anatetea, sijui tuliombwa! Rais anaweza kuongea popote pale na akawa ameongea na Taifa. Iwe ni kwenye *party* ya *THT*, iwe kwenye *birthday* aliyoandaliwa na *Clouds*, Rais alikwenda kuongea na wazee lakini ujumbe ukaenda *TUCTA*. Si ndiyo? (*Makofii*)

#### **WABUNGE FULANI:** Ndiyo. (*Makofii*)

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *regardless* ameongea wapi, ameahidi nini, alipokuja ndani ya hili jengo aliongea kama sehemu ya mafanikio yake, aliongea kama sehemu ya msaada wake kwa wasanii. Alisema alitoa *Studio* ndani ya Bunge hili. Hakusema amewapa *THT*, alisema wasanii wa Tanzania, alisema amewapa pango kwa maana ya nyumba. Ile nyumba ni ya Serikali, hawezi Rais Kikwete kumpa mtu binafsi ile nyumba, hawezi kuwa hivyo! Mnasema eti hasikii, hawezi kuwa kwa *level*/hiyo, acheni hivyo vitu humu ndani. Eeh! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais hawezi kuwa kwa *level*, hiyo atoe nyumba ya Serikali, yaani ajue kabisa na aongee humu ndani aseme nimewapa wasanii. Mtoto wa mkulima yumo humu ndani, mmachinga naongea hapa, natumaini na ye ye ananisikia, maana yake labda Mawaziri hawawezi kuongea naye Rais.

Mheshimiwa Spika, kuna siku nyingine nilikutana na Miraji Kikwete, ni rafiki yangu, nilimwuliza hiki kitu. Hii inakuwaje? Kwa sababu wote tunajua, kila mtu anajua tatizo la huu muziki ni nini. Tatizo la huu muziki umetekwa. Nikamwuliza hivi inakuwaje? Akasema hata mimi sielewi hii, unajua utendaji; nikamwambia hivi yule dingi yako, huwa mnakula pamoja mezani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nikamwambia kwa nini usimwambie *on a dinner table*, kwa sababu wewe uko mtaani, wewe uko na sisi unaelewa kila kitu Miraji, mwambie Baba yako hali halisi kwamba Ruge anakuyeyusha. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilimwambia Miraji, lakini sasa angalia tunavyokwenda, tunaleta siasa, wanasema *THT*, mara ile *studio* kwa Tanzania *Flavour Unit*. Hakuna Chama kinachoitwa *Tanzania Flavour Unit*. *Flavour Unit* ndiyo Richmond ya Bongo *flavour* ndugu zangu. *Flavour Unit* ndiyo *Dowans ya Bongo Flavour*. *Flavour Unit* ilikataliwa kusajiliwa na BASATA, tena BASATA ipeni nguvu, ipeni hela. BASATA ina hela ya mishahara tu, wakishagawana mishahara inabaki Shilingi milioni mbili. Watafanya nini BASATA na Shilingi milioni mbili? Wataendesha semina gani? Wapeni nguvu watu kama *Rural Arts* ambao wanajitokeza kwa dhati, wanaomba huku na huko misaada ili kujenga sanaa na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, wanasema Tanzania *Flavour Unit*, hii ilikataliwa wakaenda kujisajili BRELA kama kampuni. Wanachofanya sasa hivi, wanatugawa wasanii, wanachukua washikaji zetu wasanii ambao kilio chao tunakijua, tunalia kilio kimoja, wanachukua wanamweka pale *front* wanasema wewe utakuwa Mwenyekiti. Wampe Ukurugenzi kwa sababu ule Uenyekiti waliompa ni boyo. Mkurugenzi yuko nyuma anasubiri misaada kutoka kwa Rais kwa sababu ameshampiga changa Rais kwa miaka mingi sana. Kampotosha Rais kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Spika, hii kwa kweli, mimi naomba kuanzia leo, kwanza naomba niwashukuru sana wana Mbeya kwa kuniruhusu kutumia muda wangu humu Bungeni kupigania hiki kitu, kwa sababu hawaelewii kabisa. Ninawasihi wasanii wenzangu tuache kutumiwa. Mimi nimetoka huko, hakuna kitu kule, hakuna hela tena kule. Msanii unakaa unashubiri matukio mawili kwa mwaka, *fiesta* na sijui *College Bash*, wewe msanii gani?

Mheshimiwa Spika, nchi kama hii haina hata msanii mmoja wa kimatifa. Juhudi toka ziishe za akina Dkt. Remmy hakuna mtu tunasikia anakwenda kwenye *International Festival*. Tunasikia wanasubiri tu *fiesta au collage bash*, huo siyo usanii, ni feki, mnadanganywa na amkeni kwa sababu kuna *future* nzuri mbele yenu na ndiyo maana Mungu ametuleta katika huu mjengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mungu ametuleta humu kwa sababu kuna *future* nzuri kwa hiyo, tuache uoga. Kama kubaniwa, huko mnaita kubaniwa, kama kubaniwa kungekuwa kunafanya kazi mimi leo nisingekuwa ndani ya huu mjengo, mwanzo wa kampeni mpaka mwisho wa kampeni hao hao mnaosema kwamba wanakuza sanaa walikuwa wananchana kwenye redio yao kila siku, siwezi kuwa Mbunge wa Mbeya Mjini na nimekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini niko ndani ya mjengo leo. *Future* nzuri inakuja wasanii, *Tanzania Flavour Unit* siyo chama, chama kinachotambulika kisheria kimeitwa *Tanzania Urban Music Association (TUMA)* mimi hata siyo kiongozi, viongozi wapo. Kile chama kilikosa nguvu kwa sababu kiliachwa yatima, hakina mtu anayemjua Rais, hakuna mtu anayeijua Ikulu, kile chama kiko BASATA kimebaki, vijana wanahangaika mitaani hata ofisi hawana. Lakini ndio wenyenye muziki wao. (*Makofi*)

Narudia tena, haiwezekani wote sisi tupate mafanikio kwa kuuza unga tulikataa, tulifuatwa tukakataa tukaambiwa bwana wewe unakwenda sana Ulaya kwa hiyo, wewe huwezi ukastukiwa nikasema *no my future is gonner be clean* na imekuwa *clean* kwa sababu kwa siasa za upinzani nina uhakika tungekuwa vichafu lazima mngetuchimba sana na katika mjengo huu tusingeingia. Lakini tumeingia, niwashukuru sana Wanambeya kwa kuniruhusu kutumia muda wangu kutetea muziki huu. Tuamke Serikali imo humu, ujumbe umefika, kufikia mwaka huu utakapoisha kwenda mwakani tutaongelea mahotelii ya kitalii Mbeya na hapo *airport* itakuwepo kwa sababu sasa hivi michakato inaendelea. (*Makofi*)

Lakini niwashukuru sana Wanambeya kwa kunipa fursa hii kwa sasa kutetea huu muziki kwa sababu ningeacha wangesema bwana kashatususa, kasahau alikotoka huyu siyo aina ya Mbunge ndani ya Sugu na haitakuwa hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu muziki kwa mwaka kwa utafiti wa uchumi wa Chuo Kikuu kwa tathimini ya mwaka jana tu *revenue* yake ni shilingi bilioni 91, zipo wapi shilingi bilioni 91 *reflection* yake iko wapi? *Reflection* ya kwanza ilitakiwa iwe kwetu sisi wasanii mngetuona na ma-*Range Rover*, Rais wa taasisi nionyeshe *Range Rover* hapo nje. Siungi mkono hoja mpaka Waziri anijibu haya kwa ufahamu na tumsafishe Rais wetu katika hili. A-deal na haya mambo ya *DOWANS* na mengine. (*Makofi*)

**SPIKA:** Usichafue mambo baada ya kumaliza vizuri, yaani kama wana wa Mbeya wangokusikia wewe habari ya maji, habari ya kiwanja cha ndege katika Wizara hii Spika angekuambia siyo mahali pake. Kwa hiyo, hayo ulizungumza ndio mahali pake. Kwa hiyo, tulipoanza wakaguzi wa hesabu nilikuwa peke yangu nilikuwa naona hata aibu leo wamejaa mpaka Spika ni mkaguzi kwa hiyo, wanasanaa sasa mmeshaanza. Kwa hiyo, mko humu na mambo yatabadilika tu. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Nina mambo manne kwa haraka haraka ambayo ningependa kushirika na kuchangia katika mjadala huu. La kwanza namna gani tunaweza tukashirikisha vijana wetu katika harakati za uchumi ndani ya nchi hii? (*Makofii*)

La pili, namna gani tunaweza tukashawishi na kushirikisha vyombo vya fedha ili kusaidia vijana ambao wapo katika kila Wilaya. Tatu, namna gani Serikali hii inaweza ikasaidia kutafuta masoko kwa ajili ya haraka za uchumi wa vijana wetu ambao wapo kila Wilaya. Mwisho namna gani tunaweza tukasaidia katika nyanja za michezo ili vijana wetu walio kila Wilaya waweze kufaidika na kwenda michezo kama tunavyotarajia. (*Makofii*)

Sasa la tatu, ni namna ya kushirikisha vijana wetu katika nyanja za uchumi, Serikali mpaka sasa hivi imeshafanya kazi kubwa kwa kuanzisha mambo mengi ambayo yanashirikisha vijana katika uchumi. Lakini mpaka dakika hii vijana wetu bado wana matatizo makubwa ya uchumi kwa sababu bado hatujawashirikisha vya kutosha. Nasema hivyo kwa sababu la kwanza kabisa ukienda kila Wilaya utakutu Wilaya haina takwimu kamili ni vijana wangapi wenye uwezo wa kufanyakazi kitakwimu inao? Ni vijana wangapi wamemaliza shule kila Wilaya wapo ndani ya Wilaya, ni vijana wangapi wenye ujuzi wa fani mbalimbali wapo na waweza wakafanya nini? Takwimu hazipo katika Wilaya. Tunazo takwimu za *rate of unemployment* hizo ni *globally Kitaifa*. Lakini kila Wilaya takwimu hazijaandalisha vya kutosha. Nashauri tuwe na takwimu za kutosha ili tuweze kujua katika makundi hayo namna ya kuanza kupanga kuwashirikisha vijana katika shughuli za uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la nne, baada ya hapo nashauri kila Wilaya wafanye tathimini ya nini kinaweza kikafanyika kiuchumi katika kila eneo (*economic feasibility studies*) kila Wilaya ni lazima tuwe tunajua kabisa nini kinaweza kikafanyika na makundi ya vijana ambao tunaweza tukawashawishi wakawa *engaged* katika *economic activities*. Tunafahamu *studies* hizo zinaweza zikafanyika katika kujua aina ya kilimo kila Wilaya wanaweza wakafanya nini, aina ya ufugaji wanaoweza wakafuga kitu gani na aina ya viwanda vidogo vidogo. Mpaka sasa hivi Serikali imekuwa ikijitahidi kupeleka mbolea. Lakini bila kufanua kwamba kundi lenye uwezo wa kufanya kazi ni kundi la vijana kwa kiwango gani mbolea tumewapelekea vijana ambao wanaweza wakafanya kazi katika kilimo ambao hao ndio kundi la uzalishaji. Kwa mfano hata nikiwa jimboni kwangu hakuna *data* kamili ambayo ninaweza nikaitoa mimi kama Mbunge kwamba vijana wangu katika Jimbo la Kalenga wangapi ambao walinufaika na mfuko wa mbolea kwa sababu hatuna *data* ambazo zinalenga kundi lenye uwezo wa uzalishaji. Ni wakati sasa kuwa na *data* na kulenga kuwawezesha vijana ambao wapo tayari kwa ajili ya kujenga uchumi. (*Makofii*)

La tano, kwa kuwa ninazungumzia masuala ya kuwawezesha vijana kiuchumi lazima tuangalie namna gani tunaweza sasa kushawashi vyombo vya fedha ambavyo vitakuwa tayari kwenda vijiji kuwashawishi kwa njia mbili, kwanza wapunguze riba ya ukopeshaji (*lending rates*) Serikali ina uwezo wa kuzungumza hili. La pili Serikali inaweza ikapunguza *corporate tax* kwa mabenki ambayo yatakuwa tayari kwa ajili ya kukopesha vijiji. Ninafahamu mabenki mengi yanatasita kwenda vijiji kwa sababu *volume* ya *profit* ni ndogo lakini Serikali inaweza ikazungumza na mabenki haya, taasisi za fedha zikaelekea vijiji kwa *concessional taxes*. Hili linawezekana, ninafahamu sehemu zingine duniani wamelfanya ni wakati sasa *deliberately* Serikali yetu iweze kutazama namna gani tunaweza tukasaidia makundi yaliyo vijiji kwa kuwawezesha kwa kushirikiana na mabenki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la sita, ibakie wajibu wa Taifa sasa kama vijana tumeshawashirikisha katika nyanja hizo za uzalishaji tutazame namna gani tunaweza kujishirikisha sisi kama Serikali kujua masoko yako wapi. Vijana wanapokuwa wanazalisha wajue kile wanachokizalisha kitauzwa wapi ndani ya nchi na nje ya nchi. Serikali ina uwezo wa kujua Kenya kunahitajika kitu gani, Uganda kunahitajika kitu gani na nchi zingine kunahitajika kitu gani ambacho vijana wetu katika Tanzania wanazalisha. Tusitarajie vijana ambao *they are confined* katika Wilaya wanaweza wakajua masoko yako wapi, ni wajibu sasa wa Serikali tuweze tukawatayarishia vijana wajue masoko na wanapokuwa wanafanyakazi za uzalishaji wanajua soko katika *level* ya uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimesema nitazungumzia masuala ya michezo. Wengi wamezungumzia masuala ya michezo, sina sababu ya kurudia umuhimu wa hoja zote walizosisema. Lakini Kitaifa bado ni lazima tuzungumze, hatuna mfumo wa kushirikisha vijana katika michezo mashulenii. Umefika wakati sasa tuseme tutengeneze mfumo ambao Serikali itakuwa inajua na kwa kiwango gani shule zetu zinashiriki michezo na ipi. Katika huo mfumo tuwe na uhakika kila shule ina viwanja, hili limezungumzwa na Wabunge wengi. Lakini bado Serikali tunatarajia Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha atachukua nafasi na kulizungumzia hili. Ni wakati kila shule iwe na viwanja kwa ajili ya aina ya michezo ambayo tutaipitisha na kusaidia kila shule wawe wanacheza watoto wetu. (*Makofii*)

Lakini lingine vijana hawa ambao wanamaliza shule kila kata ina *secondary school* na kila kijiji kina *primary school* na wote hawa hawafanikiwi kwenda shule za juu na wengi wao wanabakia pale vijiji. Wakati tunazungumza namna gani kiuchumi tunaweza tukashirikisha hawa vijana wakati mwingine hawa wanakuwa hawana kitu cha kufanya lazima tuwashirikisha katika michezo wale ambao hawako katika shule. Kwa namna gani, tutazame namna gani tunaweza kila Wilaya au katika tarafa tukawa na viwanja vikubwa kwa ajili ya kuhamasisha mashindano ya vijana ambao wapo kila Wilaya, wapo kila kata na hawana kitu cha kufanya baada ya kazi. Ni lazima Serikali tutazame namna gani tunaweza tukashirikisha wananchi kujenga viwanja kwa nguvu za Serikali pamoja na wananchi wenyewe kila tarafa ili kuwe na michezo ambayo inakuwa inaendeshwa kule. Tuwe na mfumo mwingine ulio ndani ya shule wa michezo na pia tuwe na mfumo ulio nje ya shule lakini ukishirikisha *all able youth* ambao ni vijana wapo katika kila Wilaya/Kata wawe na wakati wa kutumia vizuri michezo na kazi.

Kwa mfano katika Jimbo langu la Kalenga tuna nafasi ya maeneo mazuri sana kwa mfano kata ya Ifunda, pale Ifunda tunaweza tukajenga uwanja mzuri sana na kata ambazo zipo ndani ya Tarafa ya Kiponzero wanaweza wakashiriki na kwa namna hiyo, kila Wilaya na kila mikoa tunaweza tukafanya hivyo tutakuta vijana wengi wapo *engaged full time* baada ya kazi wapo katika michezo. Hawapo sasa hivi katika hali hiyo kwa sababu mifumo hii Kitaifa hatujaitengeneza. Nashauri Serikali itazame namna gani inaweza ikatumia utaratibu huu na mifumo hii ikasaidia vijana wetu kuwa katika wakati mzuri wa kutumia wakati wao vizuri kiuchumi na kimichezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeona nichangie nafasi hii katika haya ambayo ni machache lakini naomba Mheshimiwa Waziri atakapopata nafasi ya kujumuisha aweze kueleza anayatazamaje haya kwa sababu kwa mawazo yangu nafikiri yatasaidia wananchi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii kama kitinda mimba. Maana yake kitinda mimba ni yule mtoto wa mwisho, huwa anapendwa sana na mama na baba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kidogo sana Wizara hii ni Wizara muhimu sana katika nchi zote ndio inayotangaza kila nchi. Vitu vinavyoitangaza nchi yetu ni michezo, utamaduni wetu ndio unafahamika kutoekana na Wizara hii. Mimi binafsi nakipenda sana kile kipindi kwenye TBC kinaitwa Utamaduni wa Mtanzania, zile zinavyochezwa nikitazama ngoma zetu zinazotoka Zanzibar kule na ukitazama mama yule anavyochezwa ngoma ile basi mimi mwenyewe huwa nafarijika. (*Makofii*)

La pili, ukiangalia hivyo utaona kwa sababu ya kucheza zile ngoma tu lakini ni ishara kwamba Watanzania wana afya nzuri, kama huna afya ngoma za Kitanzania huzichezi, utacheza hii *bongo flava*. Lakini ngoma ya Mtanzania ambaye anaruka, akacheza, akakata mambo ya ajabu mazuri mazuri yale hadi uwe mzima na sisi tunagombania Taifa lenye watu wenye afya. Naomba Wizara hiyo, isaidie sana ngoma zetu za kitamaduni za vijiji ili watu kupata afya njema. (*Makofii*)

La tatu, Wizara hii haitunganishi kama *union*. Ni Wizara ambayo robo tatu ya Tanzania Bara tunakutana kwenye *union*, kwenye michezo hasa mpira na mambo mengine. Mimi ninaomba sana Wizara hii ikaunganisha nguvu. Huku kwa wenzetu kuna *talented* kubwa ya watu wenye uwezo wa michezo kwa sababu kuna *big choice* akitaka kutafuta wachezaji wa mpira

huku na ukawa ni *fair* utapata wachezaji hata milioni tatu, wakimbiaji wa kila aina michezo. Nafikiri tumefika mahali katika idara hii ikaunganishwa ikaweza kusaidia Tanzania kwa maendeleo. (*Makofi*)

Watanzania wengi ambao ni wanamichezo ni maskini sana, hawana uwezo hata wa vifaa, Watanzania wengine wanafanya mazoezi ya mbio kwa miguu chini lakini kwa sababu mguu wa Mtanzania anayetoka huko hata ukichomwa na msumari basi msumari hukatika wenyewe. Sasa naomba tuliangalie na tutumie sana shule zetu kuanganisha michezo hii ili watoto wakitoka huko wakija wa juu wana utamaduni huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuchangia suala hili kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ikajibowi na Wizara ya Utamaduni. Lakini nakata nirejee tena leo *football* sasa ni mchezo wa uchumi. Naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri. Leo wachezaji wa Tanzania anagombaniwa kununuliwa dola milioni 20, milioni 10 jambo ambalo hakukuwa na mchezo hata mmoja aliyewahi kununuliwa na klabu zaidi ya labda shilingi 10,000. Sasa tuitazame hii *promotion* ilivyofikia ikiwa mchezaji anakwenda kufanya mazoezi kwanza kule akirudi wanazungumza klabu na klabu anauzwa si chini ya milioni 20, milioni 30 tena *dollars*. Mchezo huu wa mpira ni biashara ambayo inafanywa kwa dakika 90. Mapato yake ni milioni 300, milioni 400 kwa Tanzania biashara gani inayofanywa kwa dakika 90 ikaleta faida milioni 300, milioni 400? Hakuna, tuna bahati tumepeata uwanja mzuri wa Taifa ni wa kisasa, wa kileo. Sasa Wizara imebakia kuchangia Serikali katika mapato na iwe njia moja ya mapato ya nchi yetu. (*Makofi*)

Leo *Europe* mpira ni njia ya mapato inaisaidia zile nchi. Lakini sisi bado tunafikiria mpira ni mchezo wa starehe tu ukacheze pale uvunjike, hapana. Mpira ambao unaweza ukatusaidia sana, sana, sana, katika matatizo haya ya *secondary schools* za Kata kwa sababu mapato yake ni makubwa kuliko mapato mengine yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo yetu haya lazima Wizara hii kwa sababu ni Wizara inayohusiana na vijana watueleze Mheshimiwa Waziri ana programu gani ya kuwasaidia Wamachinga. Wamachinga wote ni vijana wenye afya njema, wenye akili nzuri, wanaoshindwa na mapato ya kujidoresha. Sera ya Chama chako cha Mapinduzi ni kuhalikisha kila Mtanzania anakula vizuri, analala vizuri, anasoma vizuri, ana gari nzuri. Sasa hawa Wamachinga una sera gani ya kuondoa matatizo yao. Tumeona si watu ambao wanahitaji kusaidiwa kiakili au muwawekee *camp* muwapelekee chakula. Wanahitaji usalama wao angalau nguvu zao ziweze kuzalisha na kuondoka na matatizo. Tuambie mnafanya nini kwa manufaa ya hao vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Kamati mbili tofauti, kuna Kamati ya Uongozi ya Bunge ambayo ni Wenyeviti na Makatibu wetu wa Kamati na kuna Kamati hii *Councilors*. Wenyeviti wanatusaidia maslahi yetu kwenye Kamati...

**SPIKA:** Unamaanisha *Commission?*

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Naam!

**SPIKA:** Unamaanisha *Commission?* *Commission* ya Bunge, hii ya pili?

Ya kwanza Kamati ya Uongozi ambayo ni Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu na kama Mwenyekiti hayupo basi Makamu Mwenyekiti anakuwepo. Nyingine ni Tume ya Bunge sijui ndiyo ipi unayoisemea? (*Makofi*)

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunisaidia, kwa sababu nilijua utanisaidia kwa sababu na wewe uko ndani yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge maisha yetu yanakwenda na Tume hii na siyo kitu cha kufanya mchezo ndani ya Bunge letu. Wabunge wanaishi hapa Dodoma wanaishi katika maisha magumu sana. Tunasikitika sana Tume yetu ya Wabunge yenye nia njema ya kusaidia

Wabunge wetu eti inashindwa kutekeleza kwa sababu mtu mmoja kasema hatutaki mafao, hatutaki hivi, sisi sote Wabunge tufe na njaa, tupate matatizo. Hatuwezi! Nakusudia kusema kwamba sisi tumeunda Tume yetu kwa maslahi yetu na wote hawa waliokataa, waliokubali, walipiga kura kwa maslahi ya Tume hiyo. Tunakwama, juzi tulichelewa kutiliwa posho katika Benki ya CRDB, jana tumetoka mie, Mheshimiwa Sanya, nanyi mpaka benki ya CRDB kwenda kufanya ghasia angalau tusiaibike. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunakaa, tuna maslahi yetu, tuna Tume yetu ambayo haingiliwi na Serikali. Ni Tume ya Bunge inaangalia maslahi yetu. Halafu haitekelezi matakwa yetu kwa sababu eti mtu kakataa. Naomba Mheshimiwa Waziri ukija uniambie nini sababu yake. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wakati wa kusali umefika na nimaliza kwa kusema nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Katika orodha ya wachangiaji huyu ndiyo alikuwa wa mwisho. Lakini hii ya mwisho haikuhusu Mheshimiwa. Amepenyeza hivi, kapenyeza tu. Lakini pia Kanuni inamruhusu kama kuna jambo la maslahi ya Wabunge anaweza kusema kama alivyosema. Kwa hiyo, haupo nje kabisa ya Kanuni zetu. Tatalishughulikia sisi wenyewe na liko katika uwezo wetu. (Makofii)

Sasa msitafsiri vibaya kwamba hilo suala la maslahi ya Wabunge ni shughuli ya Tume ya Wabunge. Kwa hiyo, hatujakaa toka maneno yalipoanza, hatujakaa. (Makofii)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumponqezza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kama ifuatavyo, naomba nianze na vijana. Vijana ni Taifa la leo na hasa ukizingatia vijana ni wengi katika nchi yetu takribani 60%. Kutokuwa na mpango kabambe kwa vijana hawa ni kutengeneza bomu kubwa sana. Vijana wapo *desperate* sana kwa mfano Tanga, viwanda vyote vimekufa, vijana karibu wote hawana kazi, hawana uwezo wa kujajiri na mpango wa kuwawezesha haupo na kama upo basi ni mbovu. Vijana hawa wengi wanakaa vijjeni kwa kuwa hawana cha kufanya kazi kubwa ni kula miraa. Kwa kweli vijana wa Tanga wana hali mbaya sana. Mheshimiwa Waziri naomba katika mipango mikakati yenu kwenye Wizara naomba muwaangalie vijana hawa wa Tanga kwa jicho la huruma na imani.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe mchango wangu kwenye michezo, michezo ni muhimu sana katika maendeleo ya Taifa lolote, kwani michezo ni kazi, ajira na pia ni furaha na vilevile afya.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu kwenye Wizara itusaidie ili Serikali isitoze kodi kwenye vifaa vyao michezo ili tuweze kupata vifaa hivyo kwa urahisi na kuweza kukuza maendeleo katika michezo nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa Jiji la Tanga limeteuliwa na *TFF* kujengwa kiwanja kingine cha Kimataifa cha michezo kikubwa sana zaidi ya kiwanja cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri habari hizi ni za kweli kwani nilienda hata kuonyeshwa eneo lilitengwa kwa ujenzi wa kiwanja hicho na kama habari hizo ni za kweli ni lini ujenzi huo utaanza kwani hiyo itakuwa neema kubwa kwa wakazi wa Jiji la Tanga na pia nimepata taarifa kuwa uwanja huo umeshatengewa pesa je, ni kwell? Tafadhalii Mheshimiwa Waziri naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa wa Jumhuri ya坦桑尼亞 waandishi wa Mafunzo ya Ufukasi na Ufukasi wa Mafunzo (Wanahabari) ambazo ni kazi nzuri sana, ila kuna baadhi ya waandishi ambao wanatoa habari ambazo hazina uhalisia kiasi fulani wanapotosha umma. Waandishi (Wanahabari)

wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana kiasi kwamba inawalazimisha kupokea bakshishi. Ni muhimu sana kuboresha sekta hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa masikitiko yangu katika utamaduni, kwa ujumla utamaduni wetu Kitaifa unamong'onyoka siku hadi siku hasa kundi la vijana limepoteza mwelekeo kabisa na hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, mavazi yetu kwa kiasi kikubwa sana tunaiga kutoka nje hasa nchi za Magharibi. Wanawake ndio hasa wanadhalilishwa sana katika mavazi, wanashindwa kuelewa kuwa maumbo ya Kiafrika yanatofautiana sana na maumbo ya wenzetu wazungu. Inabidi Serikali isaidie katika kurekebisha mavazi haya hasa kwa wanawake kuwe na masharti katika uvaaji.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kuzienzi na kuziendeleza ngoma na nyimbo zetu Watanzania badala ya kung'ang'ania *bongo flava* na nyimbo za wenzetu wa Magharibi na ngoma zao.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu ambayo inabeba asilimia 60 ya vijana ambao ni nguvu kazi kubwa ya nchi yetu.

Nimpungeze Waziri na Naibu Waziri na wataalam wake wote kwa kuweza kuandaa hotuba hii na kuweza kuisoma humu Bungeni. Pia nichukue nafasi hii kumpungeza sana Msemaji Mkuu wa Upinzani katika Wizara hii kwa hotuba yake nzuri ambayo ina mambo mengi mazuri ambayo Serikali ikiyafanyia kazi naamini yatasaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema vijana ni nguvu kazi kubwa sana ya Taifa letu lakini nguvukazi hii imeshindwa kutumika vizuri na hii ni hatari kama hatutakuwa na mipango ya kuwasaidia au kuwawezesha vijana wetu. Sisi ni mashahidi tunawaona vijana wakiwa wanazurura mitaani na kukaa vijiweni bila kuwa na kazi na hii inawasababishia kuijingiza kwenye mambo mabaya ambayo yanahatarisha maisha yao na jamii kwa ujumla. Hivyo ni jukumu la Wizara hii kuhakikisha kundi hili la vijana linawezeshwa ili liweze kujitoa kwenye hilo tatizo kubwa walilonalo. Kuendelea kusema tu kuwa vijana wanatumiwa na wanasiasa haiwasaidii vijana, tutawasaidia tu kwa kuwa na dhamira ya kweli bila kuingiza siasa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kupongeza sekta hii ya muziki ambayo imeweza kutoa ajira kubwa kwa vijana wetu. Lakini lipo tatizo kubwa linalowakabili katika ajira yao hiyo nalo ni wizi wa kazi zao. Vijana hawa wamekuwa wakijituma sana lakini maisha yao yanabaki pale pale huku wengine wakinufaika kwa jasho la vijana hawa, naomba sana Serikali iwasaide sana vijana hawa hasa kwa kuleta Bungeni Marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki ili tuweze kuongeza kipato cha vijana wetu ambao wanaabiwa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naamini hayo yakifanyika mapato ya wanamuziki, watunzi wa filamu na washirika wao pamoja na Serikali yataongezeka na hivyo mchango halisi wa sekta hii kwenye uchumi wa nchi hii utakuwa na utajulikana na utathaminiwa kuliko hali ilivyo sasa kwa wasanii wetu. Pia tunaomba Wizara iwasaide wasanii wetu wanapofanya maonyesho au kazi na wasanii toka nje wahakikishe wasanii wetu wawe wanapata mgao mzuri ili tuweze kuwatia moyo wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi duniani imeendelea kwa kutumia lugha ya kukopa, hivyo basi imefika wakati sisi kama nchi kuienzi lugha yetu ya Kiswahili na wala tusione aibu kuitumia mbona Mataifa makubwa kama China wanatumia lugha yao na wameendelea?

Jambo lingine ni kuhusu sheria zetu zinazoandikwa kwa Kiingereza hivi ni Watanzania wangapi huko vijijini na mijini wanaojua lugha hiyo? Tunaomba sana Wizara ilifanyie kazi suala hili la lugha ambalo ni utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ya michezo bado haijapewa msukumo mkubwa, nasema hivyo kwa sababu sekta hii ingetumika vizuri ingeweza kupunguza tatizo kubwa la ajira hasa kwa

vijana. Kama unavyoju michezo ni ajira, michezo ni afya na michezo hujenga umaja wa Kitaifa na Kimataifa. Ukiangalia Bajeti ya Wizara hii ni kidogo sana na hii inachangia kudidimiza sekta hii ya michezo.

Mheshimiwa Spika, ipo michezo mingi sana mbali ya *netball* na *football* ambayo ingewezeshwa ingeweza kuondoa tatizo hili la ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru hayo ndiyo niliyokuwa nayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba yenyenye manufaa kwa wananchi. Kwa ujumla niipongeze Serikali kusimamia kazi zote pia Wizara kwa ujenzi wa kiwanja cha michezo cha Dar es Salaam. Baada ya kuanza na hayo, sasa nachangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi maadili ya makabila mbalimbali ya Watanzania yanapotea. Naishauri Serikali kwa kutumia Maafisa Utamaduni waanzishe vikundi vya wazee na vijana wa kila kabilila kuweka kumbukumbu za mila na desturi na kuandika vitabu kwa faida ya kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali itangaze vazi la Taifa kwa vijana wa kike na kiume kwa kuzingatia mishono, mavazi ya vijana yanatuadhiri sisi wazazi wao hasa vikundi vya ngoma.

Mheshimiwa Spika, matangazo yanayoingilia kati wakati taarifa ya habari inasomwa yanavuruga taarifa ya habari na kukatisha tamaa waskilizaji. Naomba Serikali ifafanue kwa nini wameingiza utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya michezo vikiwepo na viwanja vya mpira, ili kukuza michezo ni vizuri Serikali iagize kila Kijiji, Wilaya na Mikoa kuwa na viwanja vya michezo mbalimbali ili vijana wasisumbuke kutumia viwanja vya muda. Vilevile ni vizuri michezo ya riadha ifufuliwe ambayo vijana wenye vipaji vya aina mbalimbali wavitungie na itakuwa ni aina ya ajira.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali iwe na mpango wa majengo ya michezo katika wilaya ili vijana na wazee wapate mahali pa kuelimisha vijana michezo ya jadi na vilevile itakuwa ni uchumi kwa makundi yatakayoshiriki itakuwa ni burudani kwa wananchi kwenda kuona sanaa zinazooneshwa.

Mheshimiwa Spika, kuna wanaochonga vinyago vya aina mbalimbali ambavyo ni biashara kubwa na ni uchumi kwa wanaotengeneza. Naomba Serikali itueleze kama inawatambua wachongaji hawa wa vinyago na ikawa wamewatafutia masoko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameumba mbingu na ardhi, pia ametujalia kutufikisha katika Bunge lako Tukufu, tukiwa katika hali ya uzima.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa ufanisi, pia ni matumaini kwa Watanzania ambao kwa muda mwingu wanasubiri maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hotuba hii nikijikita upande wa vijana. Vijana ndio Taifa la leo, baada ya ule usemi wa zamani, vijana ni Taifa la kesho, bado Serikali hajjawashughulikia vijana kama inavyotakiwa, vijana bado hawajui nini hatma yao kimaisha, wamekuwa omboomba katika miji na baadhi yao wamekuwa wakishirikiana katika matendo mabaya ambayo kwa kijana yanamharibia sifa yake.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu katika kuendeleza vijana, nawaomba Mheshimiwa Waziri, kwanza ajaribu kukutana na vikundi vya vijana ili kuweza kuwasikiliza maoni yao pamoja na mwelekeo wao wa kimaisha, hapo ndipo atapata mahali pa kuanzia, pili Mheshimiwa Waziri

atenge fungu maalum kwa ajili ya kuweza kuwasaidia hata kwa kuwakopessa ili waweze kufanya biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho naomba tupate majibu ni kitu gani wametengewa vijana amba wanakaa vijiweni?

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichangie upande wa habari. Kwa upande wa habari namuomba Mheshimiwa Waziri aitupie macho idara hiyo kwani waandishi wa habari wamekosa maadili ya kuandika habari, wamekuwa wakilazimisha kuwa lazima magazeti yao yanunuliwe, wanawenza kuandika habari, hata kama kuielimisha pia wanajaribu kuweza hata kuwakashifu watu ili waweze kuuza magazeti yao. Tanzania ya leo imekuwa ikipata habari kutoka kwenye magazeti wakidhani hizo habari zote ni za ukweli, kumbe ni kinyume na maelezo yaliyokuwemo katika gazeti hilo.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri awachukulie hatua wale wote amba wanajaribu kuchafua amani illopo nchini kuititia magazeti, kwani waandishi hawa wamedhani kuwa nchi hii haina mwenyewe na kumbe wenyewe tupo tunainenzi na kuitunza.

Mheshimiwa Spika, mwisho namuomba Mheshimiwa Waziri ayazingatie haya yote niliyochangia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inashughulikia sekta zenyne fursa ya kuchangia katika ustawii wa nchi. Hata hivyo katika miaka 50 baada ya Uhuru mchango wa habari, vijana, utamaduni na michezo katika uchumi wa nchi na maisha ya wananchi haulingani na nafasi ya Wizara husika. Hivyo mikakati inapaswa kuboreshwa na Bajeti ya Wizara husika iongezwe kuweza kukidhi mahitaji ya habari, vijana, utamaduni na michezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 imekuwa ikihidi kukamilisha mchakato wa Sheria ya Uhuru wa Taarifa pamoja na Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari. Serikali katika majumuisho itoe majibu ni kwa nini mchakato huu haujakamilika katika mwaka 2010/2011 na iweke mpango wa kuletwala Miswada husika katika Mkutano wa Tano wa Bunge mwezi Novemba, 2011 ili mchakato mzima uweze kukamilika katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Serikali ielewe kwamba uhuru wa taarifa kwa wananchi pamoja na huduma bora za maendeleo ni nyenzo muhimu ya kuhamasisha maendeleo na kuhamasisha uwajibikaji katika Taifa. Mapambano dhidi ya ujisadi, jitihada za kuendeleza rasilimali za Taifa pamoja na ujenzi wa utamaduni wa uwajibikaji katika Taifa utafanikiwa ikiwa tutapanua wigo wa uhuru wa taarifa na huduma za vyombo vya habari. Misingi hii inapaswa pia kuzingatiwa katika Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, masuala ya vijana ni ya muhimu sana katika Taifa letu kwa kuwa vijana pekee ni zaidi ya 60% ya nguvukazi ya Taifa. Vijana na watoto kwa pamoja ni zaidi ya 60% ya Watanzania hivyo matatizo ya vijana ni matatizo ya Taifa. Kwa upande mwingine, maendeleo ya vijana ni maendeleo ya Taifa. Hivyo, kipaumbele kimojawapo cha nchi yetu katika kizazi cha sasa ni kushughulikia masuala ya elimu, ajira na afya ya vijana. Wizara ina changamoto kubwa ya kushirikiana na Wizara zingine kushughulikia changamoto hizo ikiwemo kukuza vipaji vya vijana. Hivyo, Wizara inapaswa kuweka mifumo bora ya kufanikisha azma hiyo hususani kwa kuigawa Idara ya Vijana kuwa chombo chenye nguvu na rasilimali zaidi, kuanzisha Baraza la Vijana la Taifa na kuanzisha Benki ya Taifa ya Vijana. Mifumo hiyo inapaswa kuwepo ngazi ya Taifa na pia kwenye Halmashauri na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, utamaduni na michezo ni uhai wa Taifa. Serikali ilete Bungeni mkakati wa Taifa wa kuendeleza utamaduni na kuinua michezo. Vazi la Taifa na mavazi ya makabila mbalimbali yaendelezwe, Wizara ishirikiane na Bunge kuonyesha mfano kwa kufanya marekebisho kwenye Kanuni ya 146(3) ili Bunge na Wabunge kuwa mstari wa mbele katika kuendeleza

utamaduni wa nchi. Serikali ianzishe mkakati na mfuko maalum wa kuendeleza vipaji vya vijana, chombo ambacho kitashirikiana na mamlaka zingine za Kiserikali kuhakikisha vijana kwenye sekta za utamaduni na michezo wananufaika na jasho lao.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa maendeleo kitabu cha nne kwa fungu 96; kifungu 1003; kasma 5417 na 6380 zinapaswa kuongezewa fedha za ndani ili kuongeza ajira kwa vijana na vituo vya vijana ikiwemo katika mitaa mbalimbali ya Jimbo la Ubungo ikiwemo kupitia vijiweni. Kifungu 6001; kasma 6314; Mfuko wa Utamaduni unapaswa kuongezewa rasilimali na kuchangia katika kuendeleza utamaduni ikiwemo mijini. Matumizi ya kasma za ruzuku 271200, 270600, 270800 kwa vifungu 6001, 6004, 7003 yanapaswa kuzingatia tija na ufanisi.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara kwa hotuba nzuri ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012 ya Wizara yao. Nifuatие kutamka mapema kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri imejieleza kuwa vyombo vya habari ni tegemeo kubwa la ajira kwa vijana na nyenzo muhimu ya kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha jamii na hivyo kukuza uelewa wa wananchi katika masuala mbalimbali. Aidha, vinatoa fursa ya pekee kwa Serikali kupata mrejesho stahili kutoka kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya kisheria, kijamii na kiuchumi.

Lakini kadri ya umuhimu na wingi wa vyombo vya habari kuongezeka katika jamii ndivyo umuhimu wa kurekebisha sheria, kanuni na mazingira ya kupata na kutawanya habari unavyoongezeka ili kuendana na hali halisi ya leo.

Napenda kuwatia moyo viongozi wa Wizara hii kuhangaikia Miswada ya Sheria ya Uhuru wa Habari (*Freedom of Information*) na Sheria ya Vyombo vya Habari (*Media Law*) ili vyombo hivi viwe mhimili muhimu wa kupashana habari, kuelimishana, kuleta demokrasia, kukuza utawala wa sheria kwa kuzingatia maadili na miiko ya taaluma ya uandishi wa habari. Narudia kusema, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii kutohana na umuhimu wake kiasi cha fedha kilichotengwa ni kidogo mno. Vijana wengi wanahitaji mikakati maalum ili waweze kujajiri. Vijana wana matatizo mengi na ndio walio wengi katika jamii. Kundi la vijana limegawanyika makundi matatu, wapo waliohitimu elimu ya msingi, waliohitimu elimu ya sekondari na elimu ya Chuo kikuu. Makundi haya yasipowekewa mikakati mizuri ipo siku hawatakubaliana na hali ya maisha wanayoishi. Ugumu wa maisha utawasukuma kufanya mambo ambayo itakuwa ni msiba wa Kitaifa.

Nataka kujua Serikali ina mikakati ipi ya kukabiliana na matatizo yanayowakabili vijana kama vile kukosa ajira, kuvuta bangi, kutumia dawa za kulevyia na kadhalika, je, elimu inayotolewa inakidhi haja ya kutoa ajira kwa vijana? Nataka kujua kama Serikali ina mikakati ya kubadili mfumo wa elimu hapa nchini ili vijana wanapomaliza elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu waweze kujajiri!

Mheshimiwa Spika, *media* hii ya habari ni muhimu sana katika kuelimisha, kufundisha, kuhabarisha, kuonya, kukosoa na kuhimiza shughuli za maendeleo. Je, Serikali inaisaidiaje sekta hii ya habari ili nayo iweze kuwa ni mhimili muhimu katika Taifa hili? Chombo hiki cha habari hakijatiliwa umuhimu sana, naomba sekta hii ya habari ipewe uzito unaostahili. Waandishi wa habari wapewe kinga ya kisheria ili kusudi wanapotoa habari ambazo zina ukweli lakini huenda hazifurahishi Serikali iwalinde.

Mheshimiwa Spika, michezo ni muhimu sana kwa vijana, michezo inatoa ajira, lakini vilevile inalitangaza Taifa. Naomba Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kudumisha michezo kuanzia ngazi ya shule za msingi hadi vyuo vikuu. Naomba pia ushirikiano wa Wizara katika

kudumisha michezo Wilayani Mbarali hasa kupewa vifaa vya michezo ili pamoja na juhudini tunazofanya jimboni Mbarali basi tuungwe mkono, tunahitaji mipira na vifaa vingine vya michezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ieleze ni hatua gani zimechukuliwa kwa watendaji wa Wizara hii kutokana na kitendo kilichojirudia cha kutopigwa nyimbo za Taifa wakati wa mechili ya mpira wa miguu kati ya Tanzania na Morocco mbele ya Rais Jakaya Kikwete wakati Waziri aliliambia Bunge lako mwaka 2010 baada ya tukio kama hilo kutokea katika mechili ya Tanzania na Brazil na lilitokea tena mbele ya Rais Jakaya Kikwete, Waziri aliomba radhi na kuahidi kuwa jambo hili halitatokea tena. Kufanya kosa sio kosa ila kurudia kosa. Sasa kosa limerudiwa, ni hatua gani mmechukua?

Mheshimiwa Spika, mashindano ya Kagame yamemalizika kwa aibu, uwanja wetu ni mzuri lakini umetiwa dosari na watendaji wabovu, siku ya fainali umeme ulikatika, jenereta hazikuwashwa. Nyavu za magoli zilikuwa mbovu kiasi cha waamuzi kusimamisha mpira na kuzitengeneza kwa kamba mbovu. Bomba za chini za kuzuia nyavu za goli hazikuwepo mpira ukipigwa nyavu zinainuka, hii ni aibu. Pamoja na matatizo hayo lakini pia matunzo ya uwanja kwa ujumla si mazuri, maji hakuna, vyoo baadhi ni vibovu, viti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Waziri atueleze ni lini Sera ya Michezo itakuwa tayari? Sheria ya BMT, Sheria ya BASATA, BAKITA na Bodi ya Filamu ni lini zitakuwa tayari?

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni hatua gani Wizara inachukua kulinda viwanja vya wazi vya michezo kama vile pale Jangwani ambavyo vinavamiwa kwa kasi sana na ujenzi unaendelea wa majengo na *stand ya bus*, eneo lile lilitengwa maalum kwa ajili ya michezo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha viwanja vyetu vya michezo mikoani ambavyo vingi vinamilikiwa na CCM Serikali kwa nini isiingie mikataba na CCM na kuvitengeneza viwanja hivyo na ikibidi kuviwekeea nyasi bandia ili viweze kutumika wakati wote na hata Serikali ikiaagiza kwa Halmashauri zetu kujenga viwanja hivyo kwa kuviwekeea nyasi bandia inawezekana, viwanja vyetu vingi bado vina majukwaa mazuri isipokuwa sehemu za kuchazea ndio mbaya navyo ni Mkwakwani, Jamhuri - Dodoma, Ally Hassan Mwinyi - Tabora, Kambarage - Shinyanga, Majimaji - Songea na Jamhuri - Morogoro. Nawasilisha.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ili kukuza vipaji vya vijana wetu kwa upande wa michezo hasa *football*, *netball*, *boxing* na kadhalika kuna umuhimu sana wa kuwa na *academy* katika nchi yetu. Je, hadi sasa tuna *academy* ngapi na Serikali ina mpango gani wa kuwa nazo mikoa yote ili nchi yetu ipate wachezaji bora na wakacheze michezo ya kulipiwa na kutangaza nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, hapo nyuma nchi yetu iliendelea sana kwa upande wa *athletics* na walipepeza bendera yetu. Je, kitu gani kimeathiri kupata vijana wengi zaidi wa kushiriki mashindano ya Kimataifa? Je, Serikali ina mkakati gani wa kupata vijana na si kushiriki tu bali kushindana na kushinda.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kazi njema.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata nafasi ya kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kisha naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa ushirikiano mzuri waliokuwa nao katika kazi mbali na ushirikiano huo pia nawapongeza kwa umahiri, uwezo, ueledi wa majukumu yao Wizarani hapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo naomba nijielekeze kwenye eneo moja tu ambalo ni utamaduni. Utamaduni kwa uelewa wangu ni kwamba neno lenyewe lina asili ya Kiarabu lenye maana ya Mji (Madina). Kutoholewa kwake lina maana ama shughuli maalum za

asili katika mji fulani, zikiwa ni pamoja na mavazi, ngoma, mila na desturi, lugha na vitu ambavyo vinaambatana navyo.

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni kitu hai kitu ambacho kinaweza athirika kutokana na kuingia na kutoka kwa watu tofauti cha msingi ni kwamba Taifa lazima lilinde utamaduni wake. Kufanikisha Tanzania kuwa na utamaduni wake hatuna budi kuhakikisha kwamba Serikali inasimamia ipasavyo kubainisha wazi na kuelimisha wananchi yapi yameamuliwa kuwa ni utamaduni wa nchi kufanya hivyo na kuwaelimisha namna ya kuelewa na hata kutungia sheria tuhakikishe kwamba tunasimamia kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, hapa ni kufafanua ni lipi vazi la Kitaifa ni vyema tukaamua ni ipi lugha ya Taifa aidha, tuambiwe ni ngoma au wimbo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutekelezwa hayo pale inapoonekana haja inajiri basi kuwe na sheria au kanuni ambazo zinaleza mipaka ya matumizi ya mila na desturi na vitu ambavyo vimeelezwa na sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, ni busara Wizara ikashughulikia suala hili mapema vinginevyo suala hili linaweza kupoteza utamaduni na heshima ya nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, michezo ni ajira tena michezo ni kipaji cha mtu kwa hiyo, ni vizuri Serikali kupitia Wizara hii kutenga fungu la kuweza kuwasaidia wanamichezo wale wanaoshinda kwenye mashindano ya kuhitajika kwenda nje waweze kusaidiwa kwani hata timu ya Taifa husumbuka sana kutafuta wafadhili kwa safari za nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ILugha ya Taifa ni Kiswahili na ni kweli Wabunge wanajua kuzungumza lugha ya Kiingereza lakini hiki Kiingereza cha Sheria ni kigumu, wengi hatuelewi vizuri sana.

Nashauri, Miswada inapoingia Bungeni iandikwe kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili yule asiyefahamu sana Klingereza aweze kujadili Muswada huo kwa lugha ya Kiswahili ili aweze kushiriki kikamilifu kwenye mijadala hiyo kwani utamaduni wa Watanzania ni kuzungumza Kiswahili na ndio lugha yetu ya Taifa, Miswada yote ikiandikwa lugha ya Kiswahili kila Mbunge atafanya maamuzi ama asome ulioandikwa Kingereza au Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, michezo ipo ya aina nyingi, ndani ya nchi yetu tuweke utaratibu wa kuitambua michezo yote iliyopo ndani ya nchi yetu kwani kuna michezo mingine wachezaji huwa wanaiwakilisha nchi au kuitangaza nchi lakini huwa wanapata taabu sana kwani kuna michezo mingine Watanzania wengi hawaijui kwa hiyo hata kutafuta mfadhili huwa ni taabu sana.

Ushauri wangu Serikali kupitia Wizara hii mshirikiane na Wizara nyingine za Majeshi yetu ya Magereza, Polisi, Jeshi la Tanzania, ili waweze kurejesha ajira za wanamichezo ndani ya majeshi yetu kwani kuna Watanzania wengi wana vipaji yva michezo lakini hawawezi kuendelea mbele kwani hawana mtu wa kuendeleza mbele.

Mheshimiwa Spika, kama kweli michezo ni ajira basi tuwasaidie vijana wetu wa michezo kuwaajiri kwenye ajira hizi za majeshi ili tuweze kupunguza vijana wasio na ajira ambaa wana vipaji tuweze kuwaendeleza mbele kwani ni jukumu letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Spika, naomba nitanabaishe Serikali kwamba bila ya kutafuta jibu sahihi la ajira kwa vijana, tunalipalilia bomu kubwa nchini na ili lisitupasukie

mikononi mwetu lazima tupate programu ya dharura kuibua ajira kwa vijana haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni zito na ni zito kwa sababu tunasema bila kufanya ama kusimamia ilhali nyanja za ajira zipo lakini bado Serikali hajjaliona hili kuwa ni gumu! Hebu tuwawezeshe kikweli kufuatana na matakwa yao wenyewe!

- (i) Usanii
- (ii) Uandishi wa habari
- (iii) Kilimo bora na nyenzo za kisasa
- (iv) Mifugo
- (v) Uvubi wenye tija (EEZ)

Mheshimiwa Spika, bila ya viwanda vya kusarifu mazao yetu ambayo yanapatikana ndani ya nchi na ambayo yanapatikana kwa wingi sana, bado tutaendelea kuimba ajira na maendeleo!

Mheshimiwa Spika, naomba kwa makusudi tuwashajirishe Watanzania wenye uwezo kuwekeza kwenye nyanja tofauti nchini. Wawekezaji wa nje, tuwatizame kwa macho ya umakini kwani wapo wengine ni wababaishaji na matapeli, badala ya kuwekeza wanakuja na dhamira ya kutuobia huku tukiawezesha kimkopo badala ya mikopo hiyo kuipeleka kwa wazalendo. Lazima wawekezaji wa nje tuwape masharti ya idadi gani kufuatana na kima/ukubwa wa waajiriwa ili moja ya sharti letu ni kuchukua idadi fulani ya vijana wetu, hili liwe ni sharti la ulazima.

Mheshimiwa Spika, bila kusimamia mila, silka na utamaduni wa malezi, Taifa hili tutalifikisha mahala pabaya sana!

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulezi, si suala la wazazi wawili tu, huko watokako wazee wetu ulezi wa kijana kwenye jamii husika lilikuwa ni suala la jamii iliyomzunguka kijana huyo, kwa hili wazee walifanikiwa sana, heshima, nidhamu, adabu na uelewa wa mambo yanayomhusu kijana kujengeka katika maadili, mila, silka na utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, ni mafunzo ya kufundishwa, awekwe na wazee ama kwenye unyago ama jando hii ni kwa madhumuni ya kumjenga kijana wa kike ama wa kiume. Leo si lugha, mavazi wala ngoma zinazotoa tafsiri au kielelezo cha utamaduni wa kabilia fulani au kijiji fulani, ngoma ni vurugu, nyimbo ni balaa. Michezo leo duniani sio siri ni ajira, Watanzania wanao uwezo na vipaji vipo!

Mheshimiwa Spika, kuhusu riadha, vijana mashulenii ndiko tutakopowapata lakini tuisahau kuhakikisha tumeanzisha *Sports Academy* nchini.

Mheshimiwa Spika, mpira wa miguu ni mchezo unaoongoza leo duniani kote, ila Tanzania hivi ni kweli Serikali hajajua kosa letu ni nini na ndio sababu hatuendi bali tunarudi? Vilabu vya mchezo wa mpira wa miguu, viongozi ndio kikwazo kimojawapo kinachochangia kufeli kupatikana kwa mafanikio ya mchezo wa mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akubali kwamba mzigo aliopewa ni mzito na unahitaji mashirikiano makubwa na Wizara nyingine nyingi na sisi Wabunge wenzake tupo tayari atakapohisi ushauri wangu unafaa! Ahsante sana.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia machache katika Wizara hii ya Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kuwa Wizara hii haijatendewa haki katika Bajeti yake ambapo ilionomba jumla ya shilingi 18,552,728,000/= lakini imepatiwa fedha kiduchu kiasi kwamba kiasi walichopewa hakiwezi kukidhi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kweli tunaamini katika mabadiliko basi tusifanye mzaha na Wizara hii hasa masuala ya vijana. Vijana ndio tumaini ya jamii yoyote katika kuleta maendeleo basi na tujitoe kwa hali na mali. Namna gani tutaweza kufanya hivi? Ni kwa kuchukua hatua za makusudi kuwasimamia katika mambo ambayo ndiyo yatawawezesha *ku-break even* katika maisha. Ajira ni namba moja katika kuwawezesha vijana kujitegemea na tuwasaidie vijana wa *bongo flava* au kizazi kipyä kuvuna jasho la kazi zao ambazo sasa linakabiliwa na tatizo kubwa la kushikwa na walanguzi wenge uwezo mkubwa bila ubaguzi niwaseme baadhi yao ni wafanyabiashara wenge asili ya Kiasia ambaa ni wajanja sana. Vijana wetu hawawezi wenyewe bila msaada wa Serikali kushindana nao.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuamke, tuwabebe watoto wetu kwa vile Serikali ina vyombo vya dola basi itumie vyombo hivi na *TRA* kunusuru kizazi chetu. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa na kuleta hotuba hii hapa Bungeni ili Bunge liijadili.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya vijana wetu katika fani mbalimbali na kwa kuzingatia vijana ndio nguvukazi ya Taifa hili. Hata hivyo kwa Serikali kushindwa kuwezesha Wizara hii kikamilifu imeshindwa kuinua vipaji na kujenga uwezo wa vijana wengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, michezo zaidi ya kuwa ni afya kwa kila mtu lakini pia ni ajira tosha sana kwa vijana wengi. Hapa nchini vijana wengi waliopo kwenye michezo hali zao za maisha bado ni duni na hajawenza kuwakomboa kutoka kwenye umaskini.

Mheshimiwa Spika, michezo inajenga akili za watoto wetu, viwanja vya watoto wetu kwenye makazi, mitaa na shulenii lazima viheshimiwe na vitunzwe. Katika Sheria ya Ardhi ya Vijiiji 1999 (5) lazima ielekeze viongozi wa vijiji kutenga maeneo ya michoro kila mahali.

Mheshimiwa Spika, tabia ya watu kuvamia maeneo ya viwanja vya michezo na kuyajenga inawanyima watoto haki. Mwaka jana Waziri alieleza hapa Bungeni kuwa wameandaa utaratibu wa kupitia viwanja vyote vya michezo kwa watoto na kuhakikisha maeneo yote yaliyovamiwa yanarudishwa mikononi mwa Serikali ili watoto wayatumie. Naomba Waziri aeleze zoezi hilo limefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wanamuziki wanajidhalilisha na wanadhalilisha wanawake wote. Ni kwa nini Serikali na Wizara wanalfumbia macho tatizo hili? Kwa nini wanaume kwenye bendi hiyo hiyo wanavaa vizuri wanafunika miili yao na wanacheza vizuri wanapendenza, wasichana wanavaa nusu uchi, vitovu nije, maziwa nije, mapaja nije maana yake nini? Wanaovaa mavazi hayo wanafundisha nini watoto wanaokua sasa? Tunaomba iletle Sheria ya Kulinda na Kuheshimi Utamaduni wetu na nidhamu kwa wanamuziki wote.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania kwa sasa michezo ya maigizo imeanza kushika kasi kubwa. Ni vizuri sana tu wawezeshwe zaidi na elimu na mafunzo ili waweze kuigiza kwa ufanisi zaidi na kufikisha ujumbe wanaoutarajia.

Mheshimiwa Spika, nasikitishwa sana na tabia ya kutumia watoto wadogo kwenye maigizo kwenye maeneo yanayotisha. Kwa mfano mtoto kupelekwa msituni, kuzamishwa baharini, kutishiwa kwa bastola. Ukiangalia vipengele hivyo vinatisha sana lakini pia watoto hawa tunawajengea taswira mbaya bado wadogo. Kwa akili ya mtoto anajenga akili bado anawenza kujifunza kuwa katili kutohana na mazingira tunayomuweka. Watoto wasitumike kuigiza kwenye maigizo ya wakubwa. Badala ya kuwajenga tunawaharibu! Tuache wasome wakifika umri wa kutosha wataamua nini wafanye.

Mheshimiwa Spika, utendaji kazi wa BASATA bado haujaweza kusaidia wasanii waweze kunufaika na kazi zao wanazozifanya, wasanii wameshindwa kuinuka kutohana na kazi zao kuibowi na wafadhili na wajanja wengine huko mitaani. Baraza hili la Sanaa Tanzania limefanya

nini kusaidia kuondoa tatizo hilo sugu na kuna mikakati gani endelevu ya kuendeleza wasanii na kazi zao?

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali imerudisha michezo shulenii ili watoto wetu waweze kukuza vipaji vyao na kupata uelewa wa mambo mbalimbali. Tatizo lillipo sasa ni upatikanaji wa walimu/wataalam wa michezo shulenii na vifaa vyaa michezo. Miaka ya 1980 kwenye shule zote kulikuwepo na walimu na vifaa vyaa michezo vyaa kutosha kwa kila michezo. Watoto waliweza kuingia kwenye michezo wowote anaopenda na akafundishwa kuumudu vema. Leo hakuna mipira, fimbo, tenesi, bao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Serikali itueleze imejiandaa vii kuwezesha vifaa vyaa michezo shulenii pamoja na walimu wa michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie na kuwezesha michezo ya wanawake hapa nchini. Tusiridhike na *Twiga Star* peke yake. Michezo yote ni mizuri na tukiwezesha vizuri tutawavutia wanawake wengi kuingia kwenye michezo na hivyo kuleta ajira na maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie mikataba na ajira za waandishi wa habari hapa nchini ili waweze kufanya kazi zao kwa ujuzi zaidi kuandika yale yanayosaidia jamii. Waandishi wa habari hapa Bungeni waandike hoja za msingi zinazotolewa na Wabunge ili Watanzania wasome na sio kuchukua suala dogo hata la utani na kujaza kwenye magazeti yao.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda niunge mkono hoja hii ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Naunga mkono hoja hii nikijua kuwa ndiyo yenye jukumu la kuweka misingi endelevu kwa vijana amba wanajumuisha takribani asilimia 60 ya idadi ya watu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana, inakadiriwa kuwa takribani 15% ya vijana hawana ajira, wakati ambapo kwa vijana wa kiume ukosefu wa ajira ni 12.3% kwa vijana wa kike inakadiriwa kuwa 14.3%. Tatizo hili ni kubwa zaidi mijini 16.5% ukilinganisha na vijiji 7.5%. Kwa Dar es Salaam hali inaonekana kuwa mbaya zaidi ambapo inakadiriwa kuwa ukosefu wa ajira kwa vijana ni takribani 31.5%. Hii ni hatari sana kwa usalama, amani na utulivu wa nchi yetu. Matukio yanayotokea sasa huko Mashariki ya Kati chimbuko lake kubwa/au yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa ajira kwa vijana. Tujifunze kutokana na yanayotokea kwa wenzetu ili yanayowakuta yasije yakatokea kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba kasi yetu ya kuzalisha ajira ni ndogo, hatujaelekeza ipasavyo katika kuhakikisha kuwa rasilimali zetu zinaweza kuondokana na tatizo la ajira. Tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa tunakuwa na jitihada endelevu za kukuza sekta zitakazotuwezesha kuzalisha ajira kwa wingi, lazima tuweke mkazo katika kuhakikisha kwamba mitaala yetu inajielekeza katika elimu ya ujasiriamali. Mitazamo ya vijana lazima ibadilike hata pale wanapomaliza elimu ya Chuo Kikuu wawe tayari kupata elimu mbadala na kuijendeleza kupitia vyuo vya VETA, wenzetu katika nchi zilizoendelea wamefanikiwa sana katika hili.

Mheshimiwa Spika, wakati ambapo kundi la vijana ndilo linalotengeneza idadi kubwa ya watu hapa nchini, ni aibu kwamba kundi hili halina fursa za kutosha za kupata huduma za kifedha. Wakati ambapo 54% ya Watanzania hawapati huduma za kifedha hali ni mbaya zaidi kwa kundi la vijana.

Mheshimiwa Spika, ipo mifuko mingi inayojihuisha na utoaji mikopo kwa vijana lakini kwa bahati mbaya sana *targeting* yetu sio nzuri na matokeo yake mikopo hii haiwfikii vijana hali kadhalika hatujafanya tathmini ya kina kujua mifuko hii imewafikia vijana kwa kiasi gani. Kama kweli tunataka kufanikiwa lazima sasa tafiti za kina zifanyike ili kujua kama kweli tunafikia makusudio ya kuanzisha mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kushauri kwamba sasa tujielekeze katika sekta ya uvuvi ili kuondokana na tatizo la ajira kwa vijana. Haiingii akilini kuwa Vietnam yenye kilomita za mraba 3600+ za uvuvi inaweza kuwanzia pato la takriban *USD* triliioni 5.2 kutokana na ufugaji wa samaki wakati sisi tuna eneo linalofikia kilomita za mraba 341,189 tunaingiza *USD* milioni 185 na

hivyo kudumaa katika kuondokana na tatizo la ajira. Lazima sasa tuwekeze katika ufugaji wa samaki katika mwambao wa bahari na maziwa kwa kufanya hivi tutaweza kuwaondolea vijana umaskini.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine tutumie mfumo wa umwagiliaji wa matone ambao umeoneshwa hivi karibuni pale Nanenane Dodoma. Mfumo ule ili ukamilike hauhitaji zaidi ya shilingi milioni 70. Hivi endapo tutakuwa na mfumo ule kwa kila wilaya ambao kwa mujibu wa maelezo ya wataalam unaweza kumwagilia ekari 50 je, ni vijana wangapi watawezeshwa kujajiri kupitia kilimo kwa kila wilaya?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri ni nzuri naipongeza na kuunga mkono hoja, hata hivyo nina michango ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijana wa Tanzania wanahitaji kushiriki katika kujenga nchi yao wakiwa na maadili ya Kitanzania, naiomba Wizara ili kufikia malengo hayo inatakiwa kubaini vijana wake na kutambua kazi zinazofanywa na vijana, vijana wakinambuliwa wataweza kuja na ajenda zinazowahusu vijana wa Taifa lao na kushiriki katika ujenzi wa Taifa lao. Kwa mfano, vijana na ajira, wapo vijana vijiji na mijini wanaonekana kama wapowapo tu, nguvukazi hii ikiunganishwa kwa kuwatambua na kubuni aina ya kazi ambayo vijana hao wanawenza kuzifanya kwa kulingana na mazingira yao na ya Kitanzania, kasi ya maendeleo ya Taifa itaongezeka. Wale wa mijini watambuliwe na kushiriki shughuli zinazofanana na shughuli za mijini na wale wa vijiji kwa shughuli zao kama kilimo, ufugaji, uvuvi na kadhalika. Kwa namna nyingine unaanzisha kijiji cha vijana wape nyenzo za kazi na utaalami wachape kazi za kuzalisha kwa kilimo hakika vijana wataenda na watafurahi sana au kwa awamu chukua vijana peleka Jeshini JKT *intake* ile yote ipeleke Bonde la Mto Ruvu wape zana na utaalami watazalisha na hapo umesuluhisha ajira na maendeleo yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, au wasomi wetu wanaomaliza katika Vyuo Vikuu vyetu siyo lazima wakatafute ajira rasmi ambazo zimekuwa taabu kupatikana kama sehemu za kilimo zimeanza huku na kule kwa vile maeneo ya kuwekeza katika kilimo ni mengi na vijana hawa wakawa vinara wa kusimamia uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati Watanzania kuwa na aina ya utamaduni unoaoeleweka na siyo kuigaiga utamaduni wa kigeni hasa katika suala la mavazi, liwepo Vazi la Kitanzania kama vile tunaona mavazi ya Kinigeria. Utamaduni wa nchi una makatazo yake, yale yote yanayopotosha taswira nzuri za Kitanzania katika mitindo ya mavazi yakemewe kama kuvaa nusu uchi siyo utamaduni wetu, tabia kama kuuza mwili, ukahaba siyo desturi ya Mtanzania na wizi, ujambazi, uvuvi siyo silka ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, badala yake kuchapa kazi iwe ni kitu kinachomtangaza na kumtofautisha kijana wa Kitanzania na vijana wenzake pale wanapokutana.

Mheshimiwa Spika, maadili mema na tabia nzuri mbele ya jamii na hamu ya kujifunza zaidi itasaidia sana kuiwekea Tanzania taswira nzuri. Yote haya yatawezekana kama Wizara itakuja na Sera (*policy*) nzuri ya kuyaendeleza.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Nkasi Kusini hawajaunganishwa na michezo, pawepo utaratibu wa kuendeleza ushindani wa michezo kwa vijana tena wasio shulen. Lazima iweipo Bajeti walau kidogo kushindanisha makundi ya vijana katika kila wilaya inasaidia kuendelea kulea vijana.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Jimbo la Nkasi Kusini hawajapata mikopo ya vijana miaka mingi. Naomba maelezo ya Waziri.

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa na Chuo cha Michezo kama cha Malya kwa nchi nzima kama Bajeti itaruhusu miaka ya mbele. Ahsante.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nitachangia katika maeneo yafuatayo, sera ya utamaduni, umuhimu wa utamaduni, lugha na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, sera ya utamaduni toka ipitishwe mwaka 1997, sera hii haina nguvu Kikatiba wala kisheria. Masuala kama haya huingizwa katika Katiba katika nchi nyingine mfano, Afrika Kusini, Umoja wa Ulaya na kadhalika au huundiwa Sheria. Bila kufanya hivyo, utekelezaji wa sera unakuwa mgumu kuhusu sera ya utamaduni, sidhani kama hata kanuni za utekelezaji zimeshaandaliwa. Kadhalika sera inahitaji kuduruswa kuingiza vipengele vya Itifaki za Kitamaduni za Kimataifa zilizopitishwa toka mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri pana na sahihi, utamaduni ni namna watu wanavyoishi, namna inayojumuisha mafanikio yote ya jamii husika katika teknolojia, sayansi, siasa, mila na desturi, michezo, imani, lugha, falsafa na sana mbalimbali. Kwa tafsiri hii, utamaduni si gombesugu wala kunengua tu.

Mheshimiwa Spika, kama Marehemu Baba wa Taifa alivyowahi kusema utamaduni ni roho ya Taifa. Utamaduni ni utambulisho wa Taifa. Taifa lenye utamaduni madhubuti ni Taifa linalojamini na kujithamini. Linaendeleza na kukuza utamaduni bila kusubiri kusifiwa na watu wengine. Taifa lisilo na utamaduni madhubuti ni Taifa legelege. Taifa kama hilo haliwezai kuhimili wimbi la utandawazi mamboleo.

Mheshimiwa Spika, toka tupate Uhuru, juhudzi za kukuza utamaduni katika Taifa letu hazijatosheleza. Yumkini hili linatokana na ukweli kwamba umuhimu wa utamaduni haujatambuliwa ipasavyo toka tupate Uhuru, isipokuwa kwa kauli za watu wachache (Marehemu Mwalimu Nyerere) tu ambazo kwa kiasi kikubwa zimeshasahaulika. Ukweli kwamba umuhimu wa utamaduni haukutambulika ipasavyo toka tupate Uhuru, unajonesha jinsi Idara ya Utamaduni ilivyofanywa kuwa ngurukizi kwa kuhamishwahamishwa toka Wizara moja hadi nyingine. Hata Maafisa Utamaduni siku hizi katika Halmashauri wapo chini ya Maafisa Elimu, nafasi ambayo ni ya kuwadhalilisha na kielelezo tosha kuwa utamaduni si muhimu.

Mheshimiwa Spika, lugha ni nyenzo kuu ya utamaduni kwa maana kwamba ndicho chombo kinachotumika katika kurithishia utamaduni. Kadhalika, lugha ni utambulisho mkuu wa Taifa. Hapa tutazungumzia lugha ya Taifa lugha ya kufundishia na lugha za kienyeji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya Taifa, je, lugha ya Kiswahili ina hadhi gani kama lugha ya Taifa? Mbona matangazo/maelezo katika mabango bado yako katika Kiingereza? Mbona Miswada katika Bunge huandikwa kwa Kiingereza ilhali majadiliano yako katika Kiswahili? Mbona rekodi za hukumu Mahakama za Wilaya na Mahakama za juu huandikwa kwa Kiswahili? Waziri atoe msimamo wa Wizara hii kuhusu haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya kufundishia, hakuna sababu ya msingi kwa nini Serikali bado inasuasua kuhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia toka elimu ya awali hadi Chuo Kikuu. Watafiti wameshafanya kazi yao na mahitimisho yameshafikiwa. Kama nchi ndogo ya Iceland (yenye watu 285,000) inaweza kutumia lugha yao toka elimu ya awali hadi Chuo Kikuu, kwa nini sisitusiweze?

Kuhusu lugha za kienyeji, Wizara inafanya nini kusaidia kuhifadhi na kukuza lugha za kienyeji? Lugha nyingi zinakufa, Serikali iandae mkakati kukuza na kuzihifadhi kutumia mbinu za kisasa.

Mheshimiwa Spika, uzalendo hauwezi kujengwa katika mazingira ya utamaduni legelege unaoyumbishwa na wimbi la utandawazi mamboleo. Uzalendo madhubuti ndio msingi mkuu wa maendeleo ya nchi yoyote bila ya kuwa na hili nchi itayumbayumba na inaweza hata kuuzwa. Lugha ya Taifa inayotumika katika shughuli zote za maendeleo ya nchi ni mionganii mwa vipengele muhimu katika ujengaji wa uzalendo huu.

Mheshimiwa Spika, katika majumuisho yake, Waziri atuambie Wizara yake imejiendaaje kuwaandaa vijana wa Tanzania wawe wazalendo, watakaolienzi, kulithamini na kulitumikia Taifa lao?

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hotuba ya Waziri Kivuli Mheshimiwa Joseph Mbilinyi iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana katika kuleta maendeleo, kukuza uchumi, mahusiano, umoja, Utaifa na amani. Nasema hayo nikimaanisha kuwa ukianza na kipengele cha michezo, michezo inaweza ikamaliza kabisa matatizo yanayoliangamiza Taifa kama UKIMWI, utumiaji wa dawa za kulevy, kukosekana kwa ajira na majanga mengine mengi yanayowakabili vijana.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali itaweka mikakati na kuitekeleza kwa vitendo, pia kupima matokeo, vijana wawekewe mfumo mzuri wa kuwashirikisha vijana kwa kutoa mafunzo/mkazo kuanzia shulen ihasa chekechea, msingi na sekondari na kuwepo na ufuutiliaji na kutambua vipaji vyao. Kila kijana atakuwa na kitu cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwepo na masomo maalum yanayotambua michezo mbalimbali na kuwepo na mitihani ya mwisho kila atakayefaulu kulingana na michezo wake aendelezwe na hatimaye ataajiriwa/kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaofaulu kuwepo na shule maalum pamoja na masomo mengine ili kuendeleza vipaji na michezo.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikithamini sana michezo wa mpira wa miguu kwa wanaume. Serikali ione umuhimu wa kuthamini timu za miguu na za mikono za wanawake(*netball*). Wizara hii iweke mafungu ya kuwezesha mikoa na wilaya ili kuziwezesha timu hizo.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari nchini vimetoa na vinatoa mchango mkubwa katika Taifa kwa kupitia redio, *TV*, magazeti na kadhalika, ingawa wapo baadhi wanapotisha lakini vimefanya kazi kubwa ya kuelimisha jamii. Hivyo wanahabari waboreshwe kimaslahi na iwe lazima waajiri wawawekee bima wanahabari.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione haja ya kuhimiza halmashauri zote nchini kuanzisha redio, *TV*, ili kuwezesha wananchi walio wengi hasa vijiji wanapata habari.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mkakati na kuelekeza Halmashauri iweke wazi vikao vyake kupitia redio muda wote inapofanya vikao vya Halmashauri ili kila mwananchi ajue kinachojadiliwa katika Halmashauri yao kama liliyo Bunge.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kama Taifa tukubali umefika wakati kutambua vipaji vya watoto/vijana na kuwaendeleza kulingana na vipaji vyao na sio kupeleka vijana vila kutambua vipaji walivyonyavyo, tuanje sasa inawezekana.

Mheshimiwa Spika, Serikali iokoe vijana walio vijiweni, mijini na vijiji kwa kuwatambua kuwapa semina, kuwasikiliza ni nini wanapendelea ili kuwapa mafunzo ili wapate kujiajiri/kuajiriwa. Serikali itoe maelekezo kwa Serikali za Mitaa, Halmashauri waanze kazi hiyo mara moja na wapime matokeo.

Mheshimiwa Spika, si vizuri Serikali kulalamika kuwa vijana wanatumia dawa za kulevy, wavivu, wanaiba/wanakwapua bila kutafuta mbinu mbadala ya kuwawezesha vijana hao. Ahsante.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu tasnia ya habari. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inaeleza bayana umuhimu wa wananchi wake kupata habari wakati wowote anapohitaji. Na vyanzo vya habari katika nchi yetu ambavyo vinaendeshwa kisheria ni kama televisheni, radio, magazeti, nitaje vichache ingawa pia kuna mitandao mbalimbali kama ya *internet* na simu inayoweza kuwa vyanzo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa magazeti ni moja ya vyombo vya habari ambayo husomwa kwa wingi na wananchi wengi kwa nyakati tofauti, na waandishi hawa wa habari kuripoti jambo ambalo limetamkwa na kiongozi au ye yote yule anayewajibika kwa jambo fulani katika nchi yetu, lakini kwa mshangao mkubwa, kumekuwa na tabia ya wale wanaonukuliwa kutoa matamshi mbalimbali, kukataa matamshi yao na kuyakanusha bila aibu hata kama magazeti yote yamekuwa yamemnukuu matamshi yale yale hata kama watatofautiana neno moja ila maudhui yanaweza kuwa yale yale.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri leo atoe tamko, ikiwa kila mto matamshi kwenye vyombo vya habari hususani magazeti anaponukuliwa (hasa kwa jambo ambalo lina madhara kwa wengine) na baadaye kukataa, wananchi wawe wanamwamini nani? Je, Wizara inaweza kuwaeleza wananchi chombo au vyombo vipyta vya habari na kuachana na magazeti ambayo kwa namna moja tunataka kuaminishwa kwamba yanatoa habari za uongo?

Naomba niungane na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuitaka Serikali iito studio alioitoa Mheshimiwa Rais kwa wasanii wote kutoka kwa *Tanzania House of Talents (THT)* pamoja na nyumba ya Serikali ilipo ofisi hii na kurudishwa kwa wasanii wote ili kulinda heshima ya Mheshimiwa Rais, kwani alipotoa ahadi hii alijua anachomaanisha na alikuwa na makusudi ya kuwasaidia wasanii wote baada ya kusikia kituo chao cha muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mwanafalsafa mashuhuri na wa kukumbukwa sana duniani Plato aliwahi kusema kwamba ili mwanafunzi aweze kujifunza vizuri ni lazima awe na mwili imara kuptit michezo, yaani alisema; “*A health mind is a health body.*” Msemo huu una maana kubwa sana kwa jamii yote ya binadamu. Bila michezo tutakuwa ni Taifa ambalo ni legelege, lisilokuwa na afya njema na hivyo kupata madhara ya kiafya na magonjwa ya kujitakia.

Mheshimiwa Spika, michezo ni lazima ichezwe katika maeneo yalijotengwa makusudi kwa shughuli hii ambayo ni viwanja vya michezo kwa mshangao mkubwa, nchi yetu ina upungufu mkubwa sana wa viwanja vya michezo hasa vya kila mkoa na hii mara nyingine inasababishwa na kuuzwa maeneo ya wazi yalijotengwa hususani kwa watoto wetu kucheza na kujifunza michezo. Ili tuwe na timu imara kama za wenzetu walioendelea kama Taifa tunatakiwa tujenge au tuimarishe viwanja vyote vya michezo yote na kuanza kuwafundisha watoto wetu michezo tangu wanapokuwa wadogo shulenii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, naungana na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba viwanja vyote vya michezo vilivyokuwepo wakati wa chama kimoja ambavyo vilimilikitwa kwa CCM, mfano Uwanja wa Majimaji - Songea, Sheikh Amani Abeid - Arusha, Uwanja wa Jamhuri Morogoro, Uwanja wa Jamhuri - Dodoma, Uwanja wa CCM Kirumba - Mwanza na kadhalika virejeshwe Serikalini na kuwa chini ya mamlaka ya viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na ninaipongeza Wizara hasa wewe Waziri kwa umakini wako kwa kushirikiana na Naibu Waziri kwa pamoja na wafanyakazi wote, taasisi na viongozi na wafanyakazi waliokuwa chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa bweni la Chuo cha Michezo Malya na ninapenda kuomba Serikali kupeleka pesa zote za maendeleo shilingi 365,398,000 tofauti na Bajeti ya mwaka jana ambapo fedha zilizoidhinishwa ni shilingi 318,300,000 lakini shilingi 100,000,000 (100 milioni) hadi Juni ndizo zilizopelekwa Chuo cha Michezo Malya ndicho kiwanda cha kutoa watalaaam wa kufundisha michezo nchini kuptit mashulenii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mategemo makubwa ya kukipanua Chuo cha Malya naiomba Serikali ihahakishe inatoa fedha kwa ajili ya upimaji wa eneo la Chuo ili kuondoa migongano na wananchi. Chuo kiwe na hati ya kumiliki eneo tofauti na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kama mdau wa sekta ya habari, naomba niwaombe waandishi wote wafuate maadili ya kazi yao, uandishi wa habari ni taaluma, ina heshima yake, wasijidhalilishe kwa kuandika habari zisizokuwa na manufaa kwa Taifa letu, waandishi wetu wawe wazalendo kwa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, dhima ya vyombo vya habari ni kuhabarisha jamii, kuelimisha na kuburudisha, ninaviomba vyombo vya *MCT, TEF* na *MOAT* visimamie sekta hii nyeti. Naiheshimu sana sekta hii kwani katika nchi zingine waandishi wake huweka maslahi ya nchi yao mbele na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili ikisimamiwa vizuri itatoa ajira kwa nchi jirani na nchi zinazojifunza Kiswahili. Nchi nyigi sasa zinataka sana kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na hata katika Mikutano ya Kimataifa. Naomba BAKITA iimarishwe na ipeleke watalaan wetu wa lugha ya Kiswahili wakafundishe, hii ni fursa ya ajira kwa Watanzania. Ni aibu eti Wakenya kujua na kupeleka watu wake nje kufundisha lugha ya Kiswahili badala ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo (BMT) ina majukumu na inatakiwa itekeleze majukumu nane kama yalivyoidhinishwa katika kitabu chako. BMT kwa sasa haina inalofanya, ipo likizo, ipo kwa jina tu, naomba itekeleze majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mpira wa Miguu (*TFF*), naomba ipange utaratibu mzuri wa kusomesha makocha wazawa kupitia fedha zinazotolewa na *FIFA*. Tuwe na utaratibu ili kuwawezesha makocha, kwani hivi sasa hatuna hazina ya makocha mfano ukiondoa akina Julio, Mkwasa, Kibadeni na wengine hivi baada ya hao nani mwagine, hatuna mpango wowote wa kuja wachukue nafasi zao na hao walijisomesha wenyewe. Nashauri Serikali kwa hili ilichukue na ni changamoto kwa Serikali na *TFF* na hapo naomba kujua Serikali ina utaratibu gani wa kusomesha makocha wazawa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Fenalla Mukangara pamoja na Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara hiyo kwa ufanisi mkubwa wa kazi yake na hotuba nzuri mliyoandaa ambayo inaipa heshima Wizara yako.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhuru wa habari, kwa kweli jambo hilo ni zuri katika nchi, lakini hivi sasa vyombo binafsi vya habari vimekuwa vichocheo vikubwa na Serikali yao. Hivyo Serikali kuitisha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari nchini pamoja na ile ya haki ya kupata habari zilizo sahihi. Sheria hiyo iletwe Bungeni kwa kushughulikiwa, kwa ajili ya kuwawezesha waandishi wa habari, kwa kuweza kuzingatia maadili ya uandishi wa habari kuwa makini na wenye tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, michezo ni burudani, afya na furaha kwani lazima nchi yoyote iwe inajishirikisha na michezo. Michezo ianzie shulen, utoton, lakini Watanzania michezo yetu inakuwa na ushabiki mkubwa bila kuangalia kwamba michezo ni furaha. Sekta ya michezo hajapewa umuhimu unaostahili kwamba michezo siyo mechi iwe tayari ndio kuwa na zoezi la nguvu, bila ya kuwa na mechi hakuna zoezi la nguvu. Kuwe na sheria inayomlenga mchezaji anatakiwa aishi vipi, mlo wake upi, makazi yake anaishi vipi. Kama inavyozungumzwa michezo fedha, basi tujikubalishe kama kweli tunataka Tanzania kushinda.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hotuba hii na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizarani. Lakini pamoja na hapo juu nahitaji kuchangia, kutoa maoni, ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu sekta ya habari. Hii ni sekta muhimu sana katika kuelimisha, kuburudisha na kuhabarisha. Tasnia hii ina nguvu sana kwa maana ya sababu zilizotajwa hapo juu na ndio daraja kwa wananchi kujua kinachojiri katika jamii. Yamkini inawezekana kabisa ikawa ni mhimili wa nne! Lakini ninachelea kusema kwamba tasnia hii sasa imeingia doa katika kufuata maadili ya uandishi wa habari. Imekuwa kwamba vyombo vya habari sasa vinatafuta taarifa tu za kuchafua/kubomoa ili pengine watu wanunue tu magazeti yao (*print media*).

Vyombo vya magazeti hususani gazeti la Mtanzania vimekuwa vikikiuka sana maadili ya uandishi wa habari na kinachosikitisha ni pale ambapo waandishi wa habari wanapokubali kutumiwa na baadhi ya watu kwa sababu ya kisiasa ama vinginevyo ili kuendeleza ajenda zao binafsi. Hili ni jambo lisilokuwa jema na halina mustakabali mzuri kwa amani na maendeleo ya nchi yetu. *Ethics* za uandishi habari zinakiukwa kiasi ambacho inafika mahala watu hawana imani na waandishi wa habari, inakuwaje wanachapisha *stories za one side* tena kwa kushabikia. Serikali ituambie ina mkakati gani juu ya kutatua tatizo hili maana kuna wengine wanaochafuliwa wanaona hakuna haja ya kulumbana na waandishi wa habari. Wawe pia na uzalendo pia na adabu.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, Serikali imejipanga vipi katika kuimarisha michezo kwenye ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa?

Mheshimiwa Spika, vifaa vya michezo vitolewe kwenye kila wilaya. Michezo idumishwe, ifufuliwe katika shule zote za msingi na sekondari. Hivi ni kwa nini suala la ufadhili wa michezo limekuwa ni tegemezi kubwa la ufadhili? Serikali haioni sasa kuna haja ya kubuni miradi itakayojiendesha kifaida katika michezo hii?

Mheshimiwa Spika, wanamuziki wa Tanzania wananyanya sana, tasnia ya sanaa haitendewi haki kabisa. *Copyright Regulatory Authority of Tanzania* inatakiwa ishirikiane na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kuandaa mfumo mzima wa jinsi ya kutumia.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini kiwango cha michezo nchini kinadidimia tu pamoja na kutumia fedha nyigi kuwalipa makocha (*expatriates*). Yangu machache kwa leo ni hayo tu hapo juu, majibu ya kina yatolewe katika kuhitimisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, michezo ni kazi, michezo ni ajira kama itaandaliiwa na kusimamiwa vizuri na kwamba kwa kuwa michezo kwa kiasi kikubwa ni ajira, inayowagusa sana vijana, hivyo kama itasimamiwa vyema na kwa dhamira inayokubaliana na usemi wa michezo ni kazi, michezo ni ajira na hasa pia ukazingatia kwamba tuna vijana wengi wasio na kazi, hapa tutaweza kusaidia kundi kubwa la vijana katika kuwapatia ajira bora na inayoeleweka.

Mheshimiwa Spika, Tanzania katika michezo ya Kimataifa tuna tatizo kubwa la kwamba Tanganyika inavaa koti la Tanzania katika kuiwakilisha Tanzania kujeungu na Vyama vya Michezo Duniani (CAF na FIF).

Mheshimiwa Spika, FIF na CAF ni Vyama vya Mpira Afrika na Duniani ambavyo wanachama wake ni nchi ambazo zina Vyama vya Mpira na ambazo zimejiunga na vyama hivyo na kwamba sisii kama Tanzania ambayo tafsiri yake ni Tanganyika na Zanzibar, nafasi ya kujeungu na vyama hivyo, imekuwa ikichukuliwa na Tanzania Bara pekee jambo ambalo hata pale misaada ya kuendeleza michezo inayotolewa na vyama hivyo kwa nchi wanachama ruzuku hizo zinaishia Bara kama kwamba Zanzibar haina haki, lakini pia jambo hili la Tanzania Bara kuvaan koti la Tanzania katika jambo hili kunainyima pia Zanzibar nafasi ya kujeungu na kuwa mwanachama.

Mheshimiwa Spika, ni mara moja tu Zanzibar imefaidika na fedha ambazo Tanzania inapata kutoka *FIFA* kama mchango wa kuendeleza michezo Tanzania. Gharama ya kuotesha nyasi katika uwanja wa Gombani Pemba pekee na fedha zote zinaishia Bara, hii sio haki na ni dharau na udhalilishaji wa *TFF* kwa *ZFA*.

Mheshimiwa Spika, uundaji wa timu za Taifa kila pale unapofika msimu wa kuunda timu ya Taifa ya Tanzania na hasa utaratibu wa sasa wa kuwa na kocha wa kigeni, makocha hawa huishia kuangalia mechili ya ligi ya Bara tu bila kwenda Zanzibar jambo ambalo linawanyima nafasi wachezaji na vilabu vya Zanzibar kuweza kushiriki na kuwakilisha Zanzibar wakati inapotajwa Tanzania katika michezo (*Taifa Stars*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu makocha na wachezaji wa kigeni, utaratibu wa kuchukua wachezaji pamoja na walimu kutoka nje, hili ni jambo ambalo linawadumaza walimu na wachezaji wazalendo, kwa kuwa ni wazi kwamba anapokuwepo kocha mgeni, kwa kuwa amechukuliwa kama mtaalamu lazima afanya kazi aliyoijia na akifanya kazi, maana yake ni kwamba kocha mzalendo akae benchi, hali kadhalika, wachezaji wa kigeni wanapokuwepo hapa ni lazima wazalendo wakae benchi, na kukaa benchi maana yake ni kuuwa viwango vyao.

Mheshimiwa Spika, kocha na mchezaji wa kigeni anapoondoka maana yake ni kwamba tuanze upya kujuliza kocha gani au mchezaji gani atawea kuziba pengo la aliyeondoka, sambamba na hilo utaratibu wa kuruhusu wachezaji watano wa kigeni kusajiliwa na klabu, hili sio sahihi katika ile dhana ya kukuza vipaji kwa wachezaji wetu, naishauri Serikali kupitia Wizara kwamba kusiwe na fursa ya kusajili wachezaji wa kigeni zaidi ya watatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la wataalamu, tuna tatizo la wataalamu wenye uwezo wa kutosha katika kusaidia jitihada za kuendeleza michezo mbalimbali hapa Tanzania. Ushauri wangu kwa Serikali kupitia Wizara hii kwamba fedha hizi tunazopewa na *FIFA* zitumike pia katika kuwapatia uwezo makocha wetu hawa wazalendo ili tuweze kuwajengea uwezo ili na wao wawe na ujuzi wa kutosha wa kulisasidia Taifa katika kukuza vipaji na hata viwango vya timu zetu na hata vilabu.

Mheshimiwa Spika, tunao makocha hapa nchini ambao ni wazalendo na walioonesha mchangano mkubwa katika kusaidia timu zetu na naomba nitaje baadhi yao kocha Jamhuri Kiwelu (Julio), kocha Shilingi (Jamhuri Pemba), kocha Kibadeni (King Mputa), kocha Abdulishani Msoma (Zanzibar) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hebu tuwapeleke hawa nchi mbalimbali wakaongeze ujuzi wao wa kufundisha katika nchi mbalimbali mfano, Ujeruman, Italia, Uingereza, Brazil na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) inatia aibu ofisi ambazo wanafanya kazi, ni kama eneo la mama ntile vile wana tatizo la sehemu ya kufanya kazi, eneo lao ni dogo, finyu na halifai kwa kufanya kazi chombo cha Taifa kama hiki. Nashauri Wizara, wapewa sehemu katika eneo la Uwanja wa Taifa ili wapate ofisi pale wafanye shughuli zao. Ahsante.

**MHE. PHILIP G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nazipongeza hotuba zote zilizowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Pamoja na maelezo mengi ambayo yamewasilishwa ninaiomba Serikali izingatie sana hotuba iliyotolewa na Kambi ya Upinzani, kwa kuyafanya kazi maoni yaliyotolewa kwani ni yenye manufaa kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vijana ndio tegemeo kubwa la Taifa na ndiyo nguvu kazi yake. Vijana wa Kitanzania wamepewa nafasi hasa katika nyanja zote, ni waathirika wa mfumo mbovu wa ajira. Kundi hili ni kubwa sana lisipoangaliwa kwa umakini na upendo mkubwa basi Taifa linaandaa bomu kubwa ambalo halitawezza kukabiliana nalo. Naiasa Serikali isifanyie mchezo suala la vijana, ifanye mikakati kupitia Wizara zote kuona ni namna gani vijana hawa wanapata ajira ili waweze kujitegemea na kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, burudani ni kitu muhimu sana kwa binadamu yoyote ili kuipumzisha akili, kuelimika na kuadilika. Pamoja na sifa hizo, kuna baadhi ya bendi za muziki ambazo mbali na kutoa burudani hizo wasanii wake hasa wa kike wamekuwa wakivaa mavazi ya kutia aibu, sasa katika hili jamii inajifunza nini? Muziki au dansi sio kuacha mwili katika hali ya kuuabisha na mbona wasanii wa kiume wa muziki wanavaa vizuri na mavazi yao hayatii aibu na jamii inapata ujumbe? Iweje kwa wanawake ndio wadhalilishwe? Tunaitaka Serikali itoe tamko kuhusu uhalali wa wasanii wa kike wa muziki wa *dance* kuvala vivazi nya aibu.

Mheshimiwa Spika, ninasikitishwa sana na kitendo cha baadhi ya vyombo nya habari hususan magazeti kwa waandishi wa magazeti hayo kuandika baadhi ya habari zinazodhalilisha watu. Kwa mfano gazeti moja ambalo hivi karibuni liliyoandika habari za kuwashushia hadhi baadhi ya Wabunge sambamba na kuweka picha zao ukurasa wa mbele wakiwahusisha na vitendo viovu. Tunaitaka Serikali itoe tamko kuhusiana na tukio hilo sambamba na kulifungia gazeti hilo kwa muda usiojulikana. Hata kama ni gazeti la udaku lakini ni gazeti halali na limesajiliwa kama mengine.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mtiindo wa kuwahusisha watoto wadogo kwenye filamu, sio mbaya kama filamu hizo zinaelezea maadili lakini filamu nyine zinahusisha watoto tena wa kike katika masuala ya mapenzi, hali hii inapotosha jamii ikiwa ni pamoja na kuwajengea kiburi wasanii hao hata mbele ya jamii kujiona kwamba ni wakubwa. Tunataka Serikali ipige marufuku kwa watoto kuhusisha na filamu za mapenzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Uvezeshaji maarufu kwa jina la Mfuko wa JK. Mfuko huu, ni chanzo muhimu cha kufanya vijana wa Tanzania kuweza kupata chanzo cha mtaji ili kuweza kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuwawezesha vijana kupata fedha za kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo lillojitokeza ni kwa vijana wa vijijini. Kutofaidika na mfuko kutokana na masharti yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kutokana na vigezo vigumu vilivyowekwa ambavyo kijana wa kijijini hawezi kukidhi. Hivyo ni vema sasa Serikali kuandaa utaratibu mpya utakaowezesha vijana wa vijijini kupata mikopo hiyo ikiwa ni pamoja na Serikali kutenga fungu pekee la vijana wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, vigenge nya vijiweni nya vijana wasiojihusisha na shughuli za uzalishaji mjini/vijijini (sheria ya nguvu kazi). Kumekuwepo na vijiwe vingi mjini na vijijini nya vijana kukaa bila kufanya kazi kusubiri kiongozi/mfanyabiashara, akipita mbele yao na kuanza kumwombwa fedha ni kwa lugha ya hatujala au utatuacha hivi hivi.

Mheshimiwa Spika, ukiwaangalia vijana hao wana nguvu, wana afya nzuri na wanao uwezo wa kufanya kazi mbalimbali za uzalishaji, aidha kwa kilimo na shughuli nyine yoyote cha msingi ni kuweka utaratibu wa kuwapatia elimu ya ujasiriamali/na kuwapatia mitaji.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, wakuu wa Wilaya nao wamekuwa wanasiwa, hawafanyi kazi ya utawala ya kusimamia sheria ya nguvu kazi kwa vijana wanashinda vijiweni bila kufanya kazi, matokeo yake ni kuanza kunywa pombe asubuhi, kuvuta bangi na kucheza kamali.

Mheshimiwa Spika, vyuo nya *VETA* vijijini, Serikali inatakiwa kuanzisha vyuo nya *VETA* sambamba na shule za sekondari kuweza kukokota vijana wote watakomaliza elimu ya sekondari ambao hawatabahatiwa kuendelea na masomo kidato cha tano na cha sita, waingie katika Vyuo nya Ufundji (*VETA*).

Mheshimiwa Spika, kupililiza kwa uhuru wa vyombo nya habari. Itambulike kuwa uhuru bila nidhamu ni fupo. Kumekuwa na uhuru uliopitiliza kwa baadhi ya vyombo nya habari vimekuwa vikifanya kazi ya kisiasa na siyo kufanya zilizokutia maadili. Taaluma ya kazi yao jinsi inavyoolekeza na kufanya kazi ya uchochezi, uchonganishi na hasa kuchonganisha vyama nya siasa na kuchanganisha Serikali na vyama ya siasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe inachukua hatua kwa baadhi ya waandishi wa habari wanaokiuka maadili, vinginevyo vyombo nya habari visivyo fufuta maadili vikiachwa vinaweza kusababisha uvunjifu wa amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa vipaji nya vijana wa vijijini. Wapo vijana wengi walio na vipaji vingi sana huko vijijini. Walakini inakuwa ni vigumu sana vipaji vyao kuonekana ili viendelezwe hii ni kutokana na kutokuwa na mpango mahsus wa kuendeleza vipaji nya vijana wetu ambao wapo vijijini ambao hawana fursa ya kuonekana japo wanavyo vipaji vizuri walivyojaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo ikuze na kudumisha tamaduni zote, mpira, ngoma, nyimbo, shairi na maigizo ikiwa ni pamoja na kuendeleza tamaduni za makabila yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la Shirika la Utangazaji *TBC* kutosikika baadhi ya maeneo kama vile Mkoa wa Rukwa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara kuiongoza na kuisimamia vizuri Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pili nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na timu yote ya ushindi ya Wizara hii, ikiwa ni pamoja na kumpongeza Mkurugenzi mpya wa *TBC*. Nawapongeza watangazaji wote wa *TBC1*, Gerson Msigwa kule Ruvuma, Dada Jane Shirima na wenzake, akina Elisha Eliya, Shehe Hassan kwa kweli na wote, lakini nitakuwa sijakamilisha kama sijawapongeza pia redio yetu *TBC* Taifa, inayohabarisha mpaka shambani, Babu Alex, Dada Elisia Bura, Nzota na wengine wote. Sisi wana CCM tunashukuru kwa ku-*balance story* japo siku moja mnatutosa kidogo.

Mheshimiwa Spika, habari za ngoma za utamaduni wetu, pamoja na utalii wa ndani bado hazijatangazwa vizuri. Tunashauri pamoja na bajeti ndogo ya Wizara, Wizara lazima ijithidi kutangaza fursa za utalii wetu hasa vivutio vilivypo maeneo ambayo bado hayajulikani.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mashindano ya Olympiki, kila wakati wanachukuliwa wana michezo wa mjini tu, kule Nyasa kuna vijana wana uwezo sana wa kuogelea. Tena wanaweza kuuleta ushindi wa kuogelea kwa kuvunja rekodi. Nashauri ni vema utaratibu ufanyike wa kuibua vipaji nya vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliahidi angesaidia kutoa zawadi ya michezo kule Kihagara siku ya makumbusho ya Taifa (1,500,000/=) tu, mpaka leo vijana wale wanandidai pesa zao mpaka napata aibu. Hivi Wizara hii inadanganya au Katibu wako Mkuu hakupata hiyo barua ya maombi? Mbona basi hakujibu kuwa hatasaidia? Na Mheshimiwa Waziri ulitoa matumaini.

Mheshimiwa Spika, ni vema nifahamishwe tu ili kuondoa kero kwa vijana wale. Hata hivyo walifurahi sana walipojua kuwa mnawaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, habari nyingi zinalenga sana watu binafsi kuliko ujumbe wake na faida pana kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa nini kusifanyike utaratibu wa kuwazesha *TBC1* kuwa na mitambo itakayosaidia kurekodi nyimbo za utamaduni pamoja na *CD* zetu za vijana wa bongo ili kuwahakikisha ubora na *traceability* (kama *bar codes*).

Mheshimiwa Spika, mwisho Bajeti ya Wizara hii iongezwe ili iweze kutimiza malengo yake kwani Wizara hii ndiyo yenye kazi ya kuwezesha uchumi wa wakala hao ambao ni nguvu zao wenywewe kama vile nyimbo michezo na ngoma na hao ndio wengi katika jamii.

**MHE. MUSSA KHAMIS SILIMA:** Mheshimiwa Spika, michezo, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri sikuona mipango imara ya kuendeleza michezo yote kwa ujumla hususan mchezo wa mipira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, timu yetu ya *Taifa Stars* siku zote imekuwa ikifanya vibaya katika mashindano ya Kimataifa kama ya Mataifa ya Afrika na Kombe la Dunia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa niliyoiona ni maandalizi mabaya ya timu na kutopewa stahiki za maandalizi bora.

Mheshimiwa Spika, hali hii ipo kwa timu yetu ya *Twiga Stars* na nyinginezo. Naomba maelezo yako juu ya tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu habari, Mheshimiwa Waziri pamoja na maelezo mazuri uliyoyatoa kuhusu sekta ya habari nilitegemea kuona kuwa unajenga Jengo la Kampuni ya magazeti Dodoma.

Mheshimiwa Spika, lakini badala yake bado Wizara yako inang'ang'ania kununua Jengo Dar es Salaam na kulifanya ukarabati badala ya fedha zilizotumika kwa ujenzi wa jengo jipya Dodoma ambako ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nami kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuongelea kuhusu lugha ya Taifa. Ni bora kabisa Wizara hii ikasisitiza Kiswahili, kwa kuwa ndiyo lugha ya Taifa letu, pia tunaomba hata Miswada humu Bungeni ije kwa lugha ya Kiswahili, kwa kuwa sheria hizi tunazitunga kwa ajili ya Watanzania. Je, ni Watanzania wangapi wanaojua Kiingereza? Pia hata Miswada yetu na hata *volume* zetu wakati wa Bajeti ni lazima zije Kiswahili na semina pia, huku ndiko kukienzi Kiswahili na pia ndio kukikuza Kiswahili. Na sio kukipa mgongo Kiswahili. Wabunge humu ndani ndio wakwanza kuharibu Kiswahili na kuongea kiswa-*english*? Ni vizuri ukakemea sana tabia hii. Kwani Wabunge ndio kioo cha jamii.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wetu ni muhimu kwa mila na desturi zetu, lakini utamaduni wa kuiga kutokea nchi jirani, kama hauendani na utamaduni wetu, si bora tukauiga hasa ule wa mavazi yasiyo ya staha hasa pale tunapoona vijana wamevaa vichupi na matiti kuwa nje. Huu si utamaduni wetu wa Kitanzania. Hata babu na bibi zetu walicheza ngoma kwa kufunika matiti yao na kuvala mavazi ya kimila, lakini matiti yalifunkwa. Sasa basi ni bora ukakemea hili na kuichukua hatua ili kuwarejesha vijana wetu kwenye maadili yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna filamu ambazo hazipendezi kabisa, zinawafunza watoto wetu mambo ambayo mfano kunyonyana ndimi na mambo mengine mengi, ni bora filamu kuzichuja kabla ya kuziingiza sokoni.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuongelea suala la habari ni muhimu vyombo vya habari vikawa na utendaji wa usawa na sio kutumika kama vielelezo vya wana siasa. Mfano swali la Mbunge A akiuliza, kama mwandishi si wake hatoandika, lakini swali hilo hilo la nyongeza akiuliza Mbunge anayemtaka, ndiyo atamuandika, lakini swali si lake. Huku ni kutotenda haki kwa mwenye swali. Huu sio uzalendo na sio haki.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Waziri katika Bunge hili kuna wanamichezo wa aina mbalimbali, lakini mpira wa miguu na mikono ndio unaoongoza. Je, Waziri na Wizara mnazisaidiaje timu hizi za Bunge? Ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutanguliza kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri ningesema machache. Kwanza nitangulize kuhusu vijana. Malalamiko mengi ya vijana ni ajira. Lakini haiwezekani wala hatutegemei vijana wote wapate ajira Serikalini.

Kwanza ajira inategemea taaluma na ushindani wa sifa za nafasi husika. Sasa vijana wetu hawataki kujajiri kwa kufanyakazi kwa mikono yao jambo ambalo vijana wetu wamezoea kukaa kwenye magenge na kulalamika ajira bila kufanyakazi, naomba Wizara itoe hamasa na kuwajengea vijana miundombinu ya kufanyakazi za mikono na kurudi vijijini kufanyakazi za kulima, kufuga na kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni mkopo wa fedha za JK ni kweli kila Wilaya wamepewa fedha kwa ajili ya mkopo. Lakini utaratibu wa mkopo ni mbovu sana kwa ajili ya ukiritimba ambao umewekwa na benki wakishirikiana na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Longido hawakuweza kupata mikopo kwa ajili ya masharti magumu ya kupata mikopo mpaka sasa fedha zipo benki zilifanyiwa biashara na walengwa hawakupata mikopo. Naomba Wizara wafuatilie kuona tatizo ni nini? Kwani fedha hizo hazitoki. Faida ya fedha hizo zinatoka lini au fedha za wananchi zinaongezeka.

Mheshimiwa Spika, napenda kumueleza Mheshimiwa Waziri jamii ya wafugaji hawakupata mikopo hata *SACCOS* moja kwenye maeneo yao, naomba ufuatilie ili nao wapate mikopo. Ni busara kufika Longido kuona matatizo ya ukiritimba wa kunyimwa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo wananchi wengi wanapenda michezo. Tanzania ina washabiki wengi lakini wachezaji ndio tatizo hasa kufanya mazoezi. Ni afadhali Serikali kuwasomesha walimu wa michezo ili tupate makocha toka hapa nchini pamoja na kuwatafuta vijana wenye vipaji vijijini kuliko kuwang'ang'aia wachezaji wenye umri mkubwa kila wakati.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri awasaidie jamii ya Kimasai wanaotumiwa utamaduni wao kutangaza biashara kwenye vipeperushi, kwenye mabango, mijini na kwenye matangazo mengi bila ridhaa yao wenyewe na wakati mwagine jamii zingine au watu wengi wanalipwa wakitumiwa kwenye matangazo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata majibu kwa hili jambo. Ahsante nategemea utanijibu.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri wake, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanikisha kuleta hotuba ya Wizara yao mbele ya Bunge lako Tukufu ili nasi Waheshimiwa Wabunge tupate fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu weledi na maandishi ya uandishi wa habari, tunashukuru kwa kuwa sekta ya habari imepanuka sana, tuna waandishi wa habari wengi wanaosomea mafunzo yao katika vyuo tofauti na kumekuwepo na utitiri wa vyuo ambao unazalisha waandishi wengi. Lakini rai yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari wawe wazalendo kwa kuandika habari zenye maslahi kwa Taifa letu, zenye kulinda heshima ya nchi yetu, zenye kufuata mila na desturi za nchi yetu na si kama ilivyo sasa kwa mfano, Gazeti la Mwananchi mara nydingi limekuwa likipotosha habari, likiandika habari za uchochezi kinyume na maadili na miiko ya tasnia hii ya habari.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kushirikiana na Wizara husika pawepo na uhuru wa uandishi lakini sio unaovunja mila, maadili na miiko ya uandishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni (kuenzi utamaduni wetu) natambua juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuenzi utamaduni wetu, kuuhuisha na hata kuulinda

Iakini kumekuwepo na changamoto nyingi zinazoendelea kuufifisha utamaduni wetu na hasa huu utandawazi (*globalization*).

Mheshimiwa Spika, utandawazi unasababisha vijana wengi kudharau tamaduni zetu na kuiga za nchi za ng'ambo mfano katika mavazi. Vijana wengi wanavaa mavazi yasiyo na staha ambayo yanapelekea kudhalilishwa kama vile mavazi ya kubana mwili maarufu *skin tight* na kutembea mchana kweupe na mavazi ambayo yanatakiwa yavaliwe katika klabu za usiku, ombi langu, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa vijana hususan katika mavazi ili kulinusuru Taifa letu na kulinda utamaduni wetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya maendeleo ya vijana, kumekuwepo na mikakati mingi inayolenga kuboresha maisha ya vijana Iakini haitekelezeki. Kwa mfano mamillioni ya JK yaliyotolewa yalilenga pia kuwawezesha vijana kujikwamua katika maisha magumu kiuchumi Iakini swali la kuijuliza. Je, ni vijana wangapi wamenufaika na Mfuko huu wa JK?

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Wizara ni kwamba kuhakikisha kwamba inasimamia kwa dhati mikakati yote inayolenga kuboresha maisha ya vijana kwani vijana ndio Taifa la leo, tukiwakwamua vijana kiuchumi ndio tunalikwamua Taifa letu. Ahsante.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, tunapoongelea vijana, tunaongelea nguvu kazi ya Taifa ambayo inapotetereka, basi na Taifa lote limetetereka. Kijamii tunapoongelea sura ya umaskini wa nchi huonekana pia kupitia vijana hasa wanapokosa ajira, elimu, kipato kiuchumi na upotevu wa maadili.

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilonalo katika nchi yetu hii ni sera ya mipango isiyotekelvezeka, kwani hawa hawa vijana tunaowazungumzia ndiyo hawa hawa waliosahaulika sana kimaendeleo. Ni wazi kuwa Serikali imewasahau sana hasa vijana wa Mikoa iliyo sahau lika kama Rukwa na Wilaya zake zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali haitoi fursa sawa kwa vijana wote kimaendeleo kwa mikoa yote inaangalia zaidi mikoa yenye maendeleo kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza. Huko kidogo ndiko Serikali imekazia macho.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa kuona ni jinsi gani tutawasaidia vijana katika kuwawezesha kielimu, kiuchumi na kilimo. Serikali imesema kuwa vijana wawezeshwe *waji-group* na kuanzisha miradi na kwamba Serikali itawapa *support*. Lakini *support* hiyo imekuwa chanzo cha viongozi, maafisa maendeleo ya vijana kujificha na kukimbilia ofisi zao kuwakwepa vijana. Vijana wamekuwa wepesi kuitikia wito wa Serikali kuunda vikundi, mfano kuna vikundi vingi vya vijana walivyoanzisha miradi kama ufyatuaji wa tofali, kilimo cha bustani za mbogamboga, ufundu seremala na ufundu magari/pikipiki. Lakini hawa wote hakuna waliofanikiwa na mfuko wa vijana unaotengewa 5%.

Mheshimiwa Spika, huku ni kuwainua vijana au ni kuwazika vijana? Naiomba Serikali initajie vikundi vya vijana walionufaika na mfuko wa maendeleo ya vijana katika Halmashauri ya Mpanda. Sasa naiomba Wizara kupitia Serikali yake ihakikishe kila mkoa na wilaya kunakuwa na Afisa Maendeleo ya Vijana na siyo kuweka makaimu au kuteua mtu asiyejua umuhimu wa vijana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wizara ijaribu kubeba sura ya ubunifu ili iweze kuinua vijana kiuchumi ili waepukane na muda wa kuvuta bangi na dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wa Mtanzania umekuwa ukiporomoka siku hadi siku. Si mashulen, si maofisini na hata majumbani na mitaani.

Mheshimiwa Spika, mimi naona Serikali imetoa mwanya au Wizara yenyewe kwa kuruhusu kuiga mambo yasiyofaa hii ni kutokana na Serikali kuficha au kutokutoa fursa ya kutangaza na kutokutamblisha, utamaduni wetu wa Kitanzania. Mfano mashindano ya U-miss yamekuwa yakikiuka utamaduni wa nchi yetu kimavazi na kudhalilishwa wanawake. Hivi hakuna njia nyingine

katika mashindano hayo inayoweza kutumika kuwapima vipaji hawa mabinti zetu, ila ni kuonyesha mavazi ya nusu uchi? Serikali ni mama wa Taifa letu naomba ifikirie hili.

Mheshimiwa Spika, michezo ni uhai, ni ajira. Michezo ipewe kipaumbele sana ili kuimarisha afya za watoto wetu ambaa afya zao za sasa ni tete kwa sababu ya kukosa mazoezi. Pia vipaji vitafutwe kuanzia shule za msingi, michezo irudishwe. Pia Serikali ihmize katika mashule vipindi nya michezo viwepo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma na iwe ni lazima. Nawasilisha.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Fenella F. Mukangara (Mb), Katibu Mkuu, Ndugu S. Kamuhanda na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yao iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo napenda kuyachangia katika Wizara hii japo kwa nimeona bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana ukililinganisha na majukumu yaliyonayo.

Mheshimiwa Spika, vijana. Naomba Wizara ituambie imejipanga vipi kuhusu ustawi wa vijana. Vijana wetu wengi hawaelewi Wizara hii inasimamiae hili kundi kubwa ambalo limeanza kupoteza imani na Serikali yao. Naomba Wizara sasa itupatie mikakati inawasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwanza yale Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) yangerudishwa ili vijana wanapohitimu masomo ya Kidato cha Sita wajunge ili wapate mafunzo na kurudisha uzalendo ambaa vijana wengi wamepoteza. Ni imani yangu kuwa kama wangepita katika makambi hayo, wangeweza kufundishwa masomo na mbini mbalimbali za elimu ya kujitegemea kama hawatapata nafasi ya kujunga katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Wizara hii ingeshirikiana na Halmashauri zetu pote nchini ili iweze kutumia fursa mbalimbali zilizo katika Halmashauri na fungu linalotumika kuwakopesha vijana ili waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba pia Halmashauri zetu zitenge maeneo kwa ajili ya viwanja nya michezo ili kuwasaidia vijana wetu waweze kuibua vipaji vyao na pia tunajua michezo ni ajira, burudani na afya. Hivi viwanja tutakavyotenga vitasaidia pia kutoa burudani kwa vijana na jamii kwa ujumla. Badala ya vijana kujihusisha na mambo yasiyo mazuri kama vijiwe nya bangi, ubakaji na uporaji kutokana na viwanja hivyo wataaka kupata hizo burudani.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia vijana katika nchi mbalimbali wakipata ajira ikiwemo ya mpira wa kulipwa, kupata mikataba ya matangazo mbalimbali. Hivyo naishauri Serikali yetu iwe na mpango mkakati wa kukuza na kuiyendezea vipaji nya vijana wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utamaduni, tunao vijana wengi sana ambaa wanapotoka kwa kuiga utamaduni wa nchi nyininge matokeo yake tumeona mmomonyoko wa maadili unavyoenea kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itujulische vazi letu la Taifa ni nini. Kuna wakati tulisikia kuna mchakato wa kutafuta vazi hilo, je, mpango huo umefikia wapi? Tunapenda na sisi Tanzania na tutasikia raha sana tutakapoona Mtanzania anatambuliwa kwa vazi lake kama yalivyo Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka kukuza sekta hii ya utamaduni, ni vyema Kitengo cha Utamaduni katika Halmashauri zetu kingeboreshwa maana naamini Halmashauri ndizo zipo karibu na wananchi na ikiwezekana ziripoti moja kwa moja Wizarani.

Mheshimiwa Spika, michezo. Kiwango cha michezo mbalimbali hapa nchini kimeshuka kutokana na bajeti finyu inayoletwa katika michezo yetu yote kwa sababu bado Tanzania hatujaweza kuwekeza katika michezo kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, Sera ya Vijana ya Taifa ya mwaka 2007 inaeleza kutaundwa Baraza la Vijana la Taifa. Ni miaka sita imeshapita sasa na hakuna hatua zozote za utekelezaji wa uundwaji wa Baraza hilo, naomba Serikali itueleze hatua iliyofikia katika uundwaji wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, Nampongezo Waziri wa Habari, Vijana na Utamaduni kwa kuwasilisha bajeti yake vizuri ikiwa ni pamoja na utendaji mzuri katika Wizara hii tangia ameingia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Pamoja na kutengewa bajeti isiyoweza kukidhi matarajio ya Wizara, bado ipo haja ya kusimamia maeneo ya kumbi za starehe kwani maeneo haya yamekuwa yaktumika vibaya, wamiliki huruhusu watoto wadogo kuingia maeneo haya usiku bila kujali Sheria na Haki za Watoto. Aidha, kumejitokeza maeneo wanaweka (*TV*) na kufanya ni sehemu ya kupatia kipato kwa kuonyesha kanda za 'X' huku vijana wadogo wakiwa wanaharibikiwa kwa kuondokewa na maadili na hatimaye nao wakiwa mitaani wanaanza kufanya maigizo kana kwamba ni jambo jema. Niombe Serikali kupitia Maafisa Utamaduni wakishirikiana na Maafisa Biashara (*Leseni*) kukagua mara kwa mara maeneo yaliyopewa leseni za *music* ili kuona kwamba hawaendi kinyume na sheria. Aidha, Maafisa Utamaduni Wilaya wakumbushwe wajibu wao, wasisubiri wakati wa sherehe ndipo wanajitambua vinginevyo suala la utamaduni litabakia wakati wa matuklo tu.

Mheshimiwa Spika, suala la mpira wa miguu, pete na riadha. Pamoja na kwamba michezo ni afya, naomba Serikali iwape mafunzo Walimu walioko mashulen na wanaohusika na michezo ili kuwawezesha kufanya vizuri katika kuwaandaa vijana kushindana ili kuwawezesha kuwapata watoto wenye vipaji vya michezo. Aidha, Walimu hawa wapewe motisha kwa kazi wanayoifanya badala ya Maafisa Michezo na Utamaduni.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri ameinisha kwamba wanatarajia kuweka "centers" za kumbukumbu ya ukombozi wa Bara la Afrika. Kama Mbunge wa eneo husika, nafarijika sana na ujenzi huo. Hata hivyo, mchakato huo kwa namna yoyote utakuwa unakwenda sambamba na kutwaa maeneo ya wananchi. Napenda kuhakikishiwa na Wizara hii kama taratibu zote za kupatikana kwa eneo husika zimezingatiwa na kwamba wananchi hawataathirika na ujenzi huo kwa namna yoyote.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, maeneo mengi kama sio yote ya Jiji la Dar es Salaam yaliyotengwa mahsus kwa shughuli za umma (*open spares*) na michezo yamevamiwa na wajanja wachache na kubadilishwa matumizi. Naomba Serikali iniambie, ni kwa namna gani wamejipanga kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, kubainisha maeneo yote ya wazi yaliyotengwa mahsus kwa ajili ya michezo ili yaweze kurudishwa na kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wasanii, mengi ya malalamiko hayo hata Wizara inayafahamu. Changamoto kubwa inakuwa ni utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na haja za msingi sana zinazotolewa na Shirikisho la Filamu Tanzania, juu ya mfumo wa biashara ya filamu ambao unammaliza kabisa msanii badala ya kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana, kwanza kutokana na soko lote kuwa limeshikiliwa na Mhindi mmoja anayemiliki kampuni ya *Steps Entertainment*, kampuni ambayo ilianza kazi rasmi mwaka 2007. Wakati Mhindi huyo alipoingia kwenye biashara hii, *DVD* moja kwa bei ya jumla ilikuwa inauzwa T.Shs.3,500/= na *VHS* ilikuwa inauzwa T.Shs.3,000/=, baada ya huyu Mhindi kuteka soko, sasa hivi bei ya jumla ya kazi ya sanaa inauzwa *DVD* moja shilingi 1,500 – mpaka shilingi 1,000/. Mfanyabiashara huyu kwa kutumia nguzo yake nyingine ya kuwa *dealer*

pekee wa *DVD* Tanzania, anatumia fursa hiyo ipasavyo katika kuwaumiza wasanii wetu pamoja na wasambaji wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanikiwa kuua soko la wasambazaji wazalendo kwa kutumia fursa alizonazo, mfanyabiashara huyu wa Kihindi ndiye mpangaji wa bei na mbaya zaidi, masharti ya kuingia mkataba na yeye ili asambaze kazi yako, kunaenda sambamba na kununua haki miliki ya kazi ya msanii!

Mheshimiwa Spika, kitu kibaya zaidi ni kwa namna Serikali inavyokosa mapato kwa kuibiwa na huyu mfanyabiashara. Kuna uthibitisho kwa Mhindi huyu kuwa na nakala mbili za mikataba zenyenye bei tofauti, lengo likiwa ule mkataba wenye bei ndogo ndio wa kuionyesha *TRA* kwa madhumuni ya kulipia kodi, nchi inailbiwa.

Mheshimiwa Spika, *COSOTA* inalalamikiwa sana kulinda uovu huu, inalalamikiwa kutokuweka tangazo kuzuia wezi mpaka kwenye filamu zinazosambazwa na *STEPS*. Mbaya zaidi inalalamikiwa kutoitisha mukutano wa wanachama, kwa zaidi ya miaka mitatu. Naomba kupata maelezo. Naomba Serikali iingilie katika tuwanusuru wasanii, tuisaidie nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mirahaba, jinsi inavyopatikana na kugawanya havieleweki. Ni muhimu Wizara ikaliweka hili wazi. Ni muhimu zaidi Wizara ikutane na viongozi wa mashirikisho haya yanayotambulika kisheria ili waweze kupanga mikakati thabiti na kutafutia mgogoro huu ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo Mhindi huyu amefanikiwa kuwagawa wasanii ili aweze kuwatawala vizuri, ndio maana limeibuka kundi la *Bongo Movie*. Ni muhimu kama Wizara ikakutana na vijana wetu hawa, iwasaide kama msimamizi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wayachukulie haya malalamiko ya mashirikisho yaliyoundwa chini ya Sheria Na.23 ya mwaka 1974.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu filamu yaani *Bongo Moves*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 76, katika majukumu ya Wizara, umeeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo ya maadili Kitaifa na kukuza utamaduni na mila.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwanza lazima nipongeze Tanzania yetu. Baadhi ya *Film* zetu ni nzuri lakini kuna baadhi ya *film* zinakiuka sana maadili ya Kitanzania kwa mfano filamu ya *Family Desire*, haina maadili hata kidogo. Wizara haioni haya kwa nini *film* zinazokiuka maadili yetu zisifungiwe maana filamu nyengine huwezi kuzitazama na watoto kwani zina matusi ya wazi. Kwani kabla ya kutoa *film* hakuna Baraza au Kamati ya Maadili ambayo inazipitia filamu zote kabla ya kuzitoa? Naomba Waziri baadaye aniambie amechukua hatua gani kwa *film* zilizokiuka maadili yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari nchini. Vyombo vya habari kazi yake ni kuhabarisha, kuelimisha na kufundisha. Ni jukumu la vyombo hivyo kuwaelimisha wananchi hasa wale ambao hawapitii magazeti yaani wa vijijini kujua hali halisi ya ukweli na kuvuruga. Kwa mfano magazeti huwa wanaandika jambo la uzushi ili mradi tu wauze magazeti. Pia kuna matangazo mengine hayafai kutolewa kwani yanadhalilisha, kwa nini hayafungiwi?

Mheshimiwa Spika, stadi za maisha kwa vijana. Kuhusu stadi za maisha kwa vijana, mimi ushauri wangu, kwa wazee wenye familia nao watoto stadi za maisha kwa watoto wao, baba kwa watoto wa kiume na mama kwa watoto wa kike ili kuepusha kufuata desturi za Magharibi kwani watoto wengi sana wanaangalia luninga. Hizi stadi za maisha zianze ndani ya familia zetu.

Mheshimiwa Spika, vikundi vya SACCOS za vijana, sekta ya maendeleo ya vijana, mikopo kwa vijana. Katika hotuba imesemwa jumla ya SACCOS 242 zilikopeshwa ni sawa lakini bado tunawaona vijana wengi wako katika hali mbaya kimaendeleo na hata ajira Serikalini hamna na hao wanaojajiri wenyewe mara nyingi Serikali huwahamisha mara huku mara kule na wengine wako vijiweni na huko vijiweni kubwa ni madawa ya kulevyta na mambo machafu. Hata hiyo mikopo kweli ni vijana lakini vijana wanaofaidika ni wa Mijini na wale tu amba wana ukaribu na kiongozi fulani. Bado hatujamkomboa kijana ila tunazidi kumkandamiza kijana ambaye tunasema ni Taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, kwa leo naishia hapa ila tudumishe mila na desturi zetu na tuepuke utamaduni wa Magharibi ambao hautusaidii. Michezo ni afya, michezo ni malezi, michezo ni kazi au uhai.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, (Mb), Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Katika nia njema ya kuondokana na ukabila, yako mambo muhimu ya msingi yanaharibika na kupotea mionganoni mwa makabila ya nchi hii. Utamaduni wa makabila mbalimbali nchini hapa unapotea kwa sababu Serikali haijawa na sera na mkakati wa kuhakikisha kwamba utamaduni wa makabila unadumishwa na kuenziwa. Iko hekima kubwa na busara nyingi sana ambayo inaendelea kupotea na inaonekana hakuna anayejali.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba namna ya pekee kabisa ya kuhakikisha mila na desturi ya kabile fulani inabaki na kudumishwa ni kuititia lugha yao. Ndani ya lugha ndimo kuna mila na mambo yote ya kabile husika. Nashauri TBC ianzishe matangazo kwa lugha mbalimbali zilizopo hapa nchini. Hili lifanyike kuititia FM Stations zilizoko Mikooani angalau kwa saa mbili kwa siku, ili Watanzania ambao hawajui Kiswahili waweze kusikia mambo yanayotokea nchini mwao. Kuititia vipindi hivi, hata watu watahamasika kuzungumza lugha zao na hivyo kudumisha tamaduni zao. Jambo hili lilenge zaidi lugha za kabile ndogondogo ambazo ziko hatarini kutoweka, kwa mfano lugha ya Kizinza, Kisumbwa, Wahadzabe, Watindiga, Wamwani na kadhalika.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wadau wote wa Wizara, kwa kazi ngumu waliyoifanya ya kuandaa bajeti hiyo ambayo ni nzuri japo ni finyu. Hongereni sana na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri lakini bado kuna changamoto nyingi sana lakini mimi nitajikita katika maeneo yafuatayo:-

- (a) Maendeleo ya michezo na utamaduni.
- (b) Viwanja vya michezo.
- (c) Waandishi wa habari.
- (d) Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya michezo na utamaduni. Tunaipongeza Serikali yetu kwa kujitahidi kuendeleza michezo na hasa nguvu kubwa ambayo imewekwa katika mpira wa miguu. Kwa kweli jitihada zimefanyika katika Football lakini Netball ambao wadau wake ni wanawake, kwa kweli ni huruma tunapotaka kufanya mashindano mpaka waombeombe kwa wafadhili. Tunaomba kama upande wa football, timu ya Taifa inagharamiwa na Serikali kwa nini Netball nayo isigharamiwe?

Mheshimiwa Spika, upande wa michezo, nashukuru mashindano ya Elimu ya Msingi na Sekondari UMISHUMTA, imerudi sasa bado yale ya utamaduni. Ngoma zetu za asili zinakufa, wa kufufua ni vijana wetu, utamaduni wa Mtanzania unakufa. Naomba Serikali iibue program ya kuimarisha utamaduni wa Mtanzania kwa kuokoa jahazi.

Mheshimiwa Spika, viwanja nya michezo. Naipongeza Serikali kwa kutujengea Uwanja wa Taifa Mkoani Dar es Salaam lakini uwanja huo unatakiwa utusaidie sana wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kutuungezea kipato. Cha kushangaza michezo ya Yanga na Simba inachezesewa na sheria tupate asilimia 3%, mbona Halmashauri ya Temeke hatujawahi kupewa, hawa *FIFA* wana agenda gani?

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika na Uwanja wa Karume, llala sioni kama unaboreshwu uweze kutumika na kuingiza mapato. Naiomba Serikali, uwanja huu umebeba jina kubwa la Karume katika kuenzi miaka 50 ya Uhuru basi uwanja huu uangaliwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Azam – Mbagala. Tunamshukuru Mwekezaji amejenga uwanja mzuri sana lakini mpaka sasa haujafunguliwa, tunaambiwa kuwa bado *TFF*. Tunaomba Mwekezaji yule Serikali imsaidie katika kutimiza taratibu ili uwanja ule uweze kufunguliwa kwani utasaidia kuleta ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari. Sekta ya habari ni muhimu sana lakini wafanyakazi wake wanafanya kazi katika mazingira magumu. Vipato vyao hawa vikoje? Mbona wanaonekana wanateseka sana na hawana maendeleo?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie Wizara hii ina mambo mengi na majukumu makubwa lakini inachukuliwa kimchezomchezo tu. Wapewe bajeti ya kutosha na kipaumbele cha aina yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%. Naomba ushauri wangu uzingatiwe.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba demokrasia katika sekta ya habari nadhani haikueleweka kwa Waandishi wengi wa Habari na ndio vyombo vingi nya habari vimeduwa na ufinyu wa kuandika habari sahihi.

Mheshimiwa Spika, utumiaji mbaya wa vyombo nya habari ambavyo vimekosa taaluma sahihi ya uandishi wa habari husababisha majanga miongoni mwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Usahihi wa kauli yangu hii tuangalie Burundi yaliyotokea kutohara na habari zilizokuwa zikitolewa na Redio Intarahamwe. Vyombo nya Habari hususan magazeti hapa Tanzania vinatumika kuandika taarifa za watu fulani hata kama maelezo yao yanalenga kuleta maafa kwa jamii. Sasa huu si uadilifu wa uandishi wa habari.

Mheshimiwa Spika, endapo wananchi watajuwa kwamba gazeti fulani linaandika taarifa ya Chama fulani na wananchi walio wengi wakajua kwamba misingi ya Chama hicho ni fujo na sio kuwatumiwa wananchi na kuwaletaa maendeleo basi ni dhahiri kwamba gazeti hilo halitapendwa na wananchi walio wengi kwa sababu malengo ya wananchi ni maendeleo na sio fujo, malumbano na vijembe ikiwa ndani ya Bunge au kwenye majukwaa ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, vyombo nya habari ni kichocheo cha maendeleo ya kweli pale tu ambapo vitatumika kwa kufuata maadili ya utoaji wa habari sahihi ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za ukweli, udhati na uhakika juu ya mambo yanayoigusa jamii. Vyombo nya habari ni dira na kioo cha kuionyesha jamii Taifa letu liko wapi na ni nini tufanye ili tuweze kufikia hatua za maendeleo ya kuigwa.

Mheshimiwa Spika, suala la baadhi ya Waandishi wa Habari kupokea hongo na kuwaandika baadhi ya viongozi wa siasa taarifa ambazo zinapingana na matakwa ya wananchi, ni tabia ambayo inastahili kuachwa. Ni vyema ikakemewa kivitendo na hata kufikishwa katika vyombo nya sheria endapo itaonekana kwamba inaweza kuleta mgogoro.

Mheshimiwa Spika, vijana ndio nguvu kazi ya Taifa. Ni ukweli kwamba asilimia 60% ya Watanzania ni vijana. Kundi hili linastahili kupewa heshima ya kutambuliwa ipasavyo, kauli ya kusema kwamba vijana ni Taifa la kesho imepitwa na wakati, ni kauli finyu, ni kauli potofu na haistahili kutajwa katika mazingira tulionayo sasa. Kwa sababu ya kung'ang'ania kauli hiyo, vijana

wengi wanatutoka, wanakwenda nje kukimbilia kutafuta maisha na wale ambao wapo nchini wanatafuta maisha kwa njia ambazo ni haramu aidha wanaendesa biashara harama za madawa ya kulevyia na wengine wanaishia kuwa vibaka na majambazi sugu ili kukabiliana na ukali wa maisha. Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba kundi hili linaendelezwa kwa misingi ya kulikwamua Taifa hili ili lisiingie katika harakati za kutafutana wachawi baina ya waongozaji na wanaoongozwa.

Mheshimiwa Spika, utamaduni. Ni kweli usiopingika kwamba utamaduni wa Mtanzania umeanza kuperomoka kwa kiasi kikubwa mno kutokana na kufuata tamaduni za wageni. Ilikuwa ni aibu, kashfa na fedheha kubwa kwa mwanaume wa Tanzania kusuka nywele au kuvaa hereni leo hili linaonekana hadharani, Serikali inaona lakini imenyamaza kimya. Vijana wa kieme wanavaa suruali wenyewe kwa lugha ya kuficha uozo wanaziita 'Kata K' wanakwenda nusu uchi, Serikali kimya kama haipo. Wanawake nao wamemsahau Mola Muumba wanaona kana kwamba Mola amewaonea kuwapa ngozi nyeusi wanakula vidonge kubadili ngozi zao jambo ambalo linawaletea ugonjwa wa ngozi na kuathirika kwa hali zao kiafya. Ni afadhali mwanaadamu kuridhika na hali aliyopewa na Mola Muumba.

Mheshimiwa Spika, sanaa. Katika sekta ya sanaa, kwa kiasi kikubwa Tanzania tunastahili sifa. Hata hivyo kuna sanaa ambazo zinakwenda kinyume na silka na utamaduni wetu. Mfano, kuna kanda za CD ambazo zinakwenda kinyume na maadili ya Watanzania. Kuna CD ambazo zinaonesha masuala ya jamii baina ya Mwanamke na Mwanaume kinadharia na zinaonyeshwa hadharani na watoto wetu ikiwa wanaona tutarajie kupata tija zipi kutoka kwa watoto wetu kama si kusubiri kulea watoto ambao ni wa nje ya ndoa? Sanaa ni sekta muhimu sana katika jamii na Taifa lolote. Tatizo ni kwamba Serikali hajawa tayari katika kuwasaidia wasanii.

Mheshimiwa Spika, michezo ni sehemu kubwa ya ajira katika nchi ambazo zinatambua thamani ya michezo nchi yetu bado hajatambua thamani ya michezo. Michezo inajenga afya ya mwanadamu, michezo hujenga mwili, hujenga siha na kumfanya mwanamichezo wakati wote kuwa mwenye furaha na uchangamfu. Serikali ina wajibu wa kuanzisha viwanja vya michezo vya kimkoa lakini vilevile kama Taifa kujengwe angalau viwanja vinne vya kimataifa ambavyo vitashirikisha jamii ya michezo yote na sio mpira wa miguu tu. Viwanja vinne hivyo viwe ni kama ifuatavyo kuwe na kiwanja kitakachotambuliwa Kimataifa Kusini mwa Tanzania, Kaskazini, Kati na Kanda ya Ziwa, viwanja ambavyo vitazidisha hamasa ya ukuzaji wa michezo Kitaifa na Kimataifa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika bajeti hii ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Wizara muhimu sana katika maendeleo ya michezo na vijana.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa masikitiko yangu kutokana na Wizara hii kushindwa kusimamia tasnia ya filamu za Tanzania kwani maigizo yanayoigizwa na waigizaji wetu kwa sasa yamepoteza mwelekeo halisi wa uigizaji unaoendana na utamaduni wetu na sasa unealekea kufuata utamaduni wa Kimaghribi. Ni vigumu kwa filamu za sasa za Kitanzania kuweza kuziangalia katika mazingira halisi ya kifamilia, kwani kitakachojitokeza ni fedhaha na aibu kubwa.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida sasa kuonyesha picha ambazo mavazi yanayoaliwa ni nusu uchi na hili si tu kwa waigizaji wa filamu bali hata kwa vikundi vya muziki, kwani wanenguaji wa bendi za muziki ndio wanaaibisha hasa utamaduni wetu, uvaaji wao nao hauridhishi kabisa na unatia aibu kuona dada wa Kitanzania akicheza huku asilimia 90 ya maungo yake yakiwa uchi.

Mheshimiwa Spika, *Taifa Stars*, kwa muda mrefu timu yetu ya Taifa ya Tanzania imekuwa haileti kile ambacho Watanzania wengi tungependa kukiona au kukipata kutoka kwa timu hii, ambacho ni ushindi. Kwa kweli Wizara haina budi kujipanga upya katika jambo hili kwa kutilia mkazo hasa katika nyanja za kuinua vipaji vya soka kwa kuanzisha shule kwa ajili ya michezo ukiwemo hasa mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, michezo ni ajira, mfano mdogo tu umeonekana wazi wakati timu zetu za Yanga, Simba zinapofanya vizuri vijana wengi huhamasika kununua

vipeperushi mbalimbli nya timu hizo jambo ambalo hutoa ajira zisizo rasmi kupitia biashara ndogondogo na kujipatia riziki halali.

Mheshimiwa Spika, bado hatujachelewa na tuanze sasa kuimarisha sekta hii muhimu katika kuimarisha afya zetu na kuleta raha kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ni Wizara muhimu sana, kwa kuwa inagusa vijana, Wanahabari na jamii kwa ujumla. Serikali itambue umuhimu wa sekta hii na kuitengea fedha za kutosha kuijendesha na fedha za maendeleo zitolewe kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa miradi mbalimbali mfano, ujenzi wa viwanja nya michezo katika kila Wilaya na Mikoa, nyumba za utamaduni na kuwezesha watumishi wa habari. Kiwango cha shilingi billion 18.4 ni kiasi kidogo sana na Wizara itashindwa kutekeleza mipango yake.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maendeleo ya vijana. Wizara iandae program ya kuelimisha vijana namna ya kujajiri wenyewe kwa kujitahidi kuishauri Wizara ya Elimu kufungua VETA au Vyuo vingi kwa ajili yao ili kuachana na makundi yasiyofaa ya uzururaji na kukaa vijiweni. Pia kushirikisha vijana katika michezo mbalimbali na kuhakikisha vijana wanapata mikopo katika mifuko ya vijana katika Halmashauri zetu kwa kuwa Halmashauri nyingi hawatekelezi hayo kwa kutumia fedha hizo kwa matumizi mengine. Naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hilo, lipo Wilayani Hanang nadhani na Wilaya zingine vijana kutopewa mkopo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya habari. Vyombo nya habari vina wajibu wa kufanya kazi kwa kuzingatia umakini, weledi na maadili ya uandishi wa habari. Vyombo nya habari vimekiuka kabisa maadili ya uandishi wa habari wanapokubali kutumiwa na baadhi ya watu wenyewe nguvu kama Mawaziri wenyewe fedha au Wanasiada, ili kuendeleza agenda zao binafsi. Hili ni jambo lisilopendeza hata kidogo na halina mustakabali mzuri kwa amani na maendeleo ya nchi yetu. Mfano kule Hanang katika Kituo cha *Full Council* habari zinazoandikwa na Waandishi ni kauli ya Mkuu wa Wilaya na Mbunge ambaye ni Waziri. Tulipochukua hao Waandishi kwenda Basotu kuchukua habari za uharibifu wa mazingira ya Ziwa Basotu, Mheshimiwa Waziri aliwafokea Waandishi hao wawili na kuwaambia wasitoe taarifa hiyo na kwa nini wamepanda gari la Mbunge wa Chadema na kadhalika. Je, hali hiyo si viashiria nya Waandishi wa Habari kunyimwa uhuru wao wa kutoa habari? Je, hiyo si ni dalili ya viongozi wa Serikali kutumia madaraka yao vibaya? Ni vema sasa tutambue uhuru wa Waandishi wa Habari na kuhakikisha tunawapa fursa ya kuandika na kutoa habari.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa katika Tanzania hii ni vijana, ambao wengi wao hawana kazi na wengine hubabaisha ili kupata mkate wao wa siku. Vijana hawa wanaweza kuwezesha ili kujikumu na kujajiri wao wenyewe na familia zao, kwa kupewa mikopo. Mikopo wa JK uweze kuwasaidia, ingawa mkopo huu huwa na matatizo kwa watendaji, kama Wizara iwe na mpango maalum na mikakati ya kuhakikisha kwamba vijana wote wanapata mikopo na sio kwa upendeleo.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaojariji wenyewe hukumbwa na maafa ya Askari wa Jiji. Vifaa wanavyouza huchukuliwa na kutiwa katika deni ambalo hawawezi kulisipa, kwani mkopo wote umechukuliwa. Serikali iliangular jambo hili kwani kuwaajiri haiwezi na hawawaajiri na hapo ndipo vijana wanapoitia kwenye mazingira mabaya ya ulevi, kuvuta bangi na unga pamoja na wizi, kwani Serikali inawaweka mahali pabaya. Je, Serikali inataka hawa vijana wafanye nini ili kujitoa katika janga la umaskini?

Mheshimiwa Spika, utamaduni. Kila nchi ina utamaduni wake wa kuliweka Taifa katika *symbol* nzuri. Kuna utamaduni/watu ukiwaona tu, unajua ni nchi gani, lakini cha kusikitisha Tanzania bado hatuko tayari kuuhfadhi utamaduni wetu kwani hata vazi la kuwasilisha nchi bado hatunalo. Serikali ina wajibu wa kukaa na kuunda vazi la Kitaifa kwa wanawake na wanaume. Namwomba Waziri atapokuja kujumuisha alieleza Bunge lipi hasa vazi la Taifa?

Mheshimiwa Spika, filamu. Utamaduni wa Kitanzania unapotoka hasa unapoangalia filamu za Kitanzania. Zamani ukiangalia huna wasiwasi hata ukikaa na watoto lakini sasa ni mashaka makubwa, tunafuata mila na utamaduni za nje. Wasanii kuvaan nguo za nusu utupu hasa wanawake, kubusiana na kufanya mambo yasiyostahiki. Hata hivyo, imejitokeza kuchukuwa utamaduni wa Nigeria na kuweka katika michezo yao. Je, hakuna chombo maalum cha kuangalia kabla ya michezo hii kutoka (sensa)?

Mheshimiwa Spika, Taarab. Utamaduni wa taarabu nao unapotoka, kuanzia waimbaji hadi watazamaji. Tabia mbaya inayojitokeza na kuendelea kujionesa ni albu, ya wanawake kucheza mauno na wanaume kujibana na wanawake. Lugha inayotumika katika mashairi nayo ni mbaya kulinganisha na taarabu asilia, zamani kila kitu kilikuwa kiko kwenye mabano au mafumbo. Je, Wizara haoni kwamba tunaiweka nchi katika hali mbaya na tunakaribisha gonywa la UKIMWI kuendelea?

Mheshimiwa Spika, maadili yamemomonyoka, baadhi ya vyombo vyahabari vimechangia kumomonyoka kwa maadili ya habari. Waandishi wakiwa na ufahamu mkubwa na uweledi wa kuandika habari zilizo za kweli nchi itaweza kuendelea, chuki zitaondoka na watu watapendana. Sio kila Mwandishi wa Habari ni Mwanahabari. Wizara itambue na kuwa na Waandishi wazuri. Waangalie Vyuo vyahabari vamelele na Walimu wao.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyahabari. Vyombo hivi ni muhimu sana lakini sasa hivi maadili yamepungua, Serikali ijtahidi kuviangalia na kuvirekebisha. Lugha inayotumika katika vyombo hivyo mara nyingine hutumia lugha za mitaani, Kiswahili hupotosha, kizungu nacho mashaka.

Mheshimiwa Spika, magazeti yapo mengi, TV zipo nyngi lakini hupotosha taarifa, labda kwa sababu ya kufurahisha mtu yaani mmiliki wa gazeti au chombo, Serikali au Chama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatimiliki bado ni tatizo kwa wasanii, kazi zao zinauzwa bila ya mpangilio, badala ya kupata faida wanakula hasara, mbele hawaendi, umaskini unazidi. Wizara ni vyema wakalisimamia hili ili kuwapa haki yao na kuwakamata wale wanaowatesa.

Mheshimiwa Spika, michezo. Baadhi ya michezo imefifia kama riadha, ndondi, *netball*, mpira wa pete, (*valley ball*) na kadhalika. Michezo ni ajira, afya, michezo pia ni utalii kwa kuwavutia watu kutoka nje ili kuweka michezo ya Kitaifa hapa Tanzania, pia kwa kuendeleza uchumi wa nchi. Tuwe na miundombinu mizuri katika michezo. Serikali iwekeze kwenye tasnia ya michezo, kuwe na vifaa vyahabari michezo, kuwe na shule za michezo kama nchi zinazoendelea, kuwa na vyombo vinavyosimamia michezo, viwanja vizuri na Walimu wa Michezo. Kuna haja ya kufufua michezo katika sehemu mbalimbali kama mashulenii, Jeshini na Viwandani.

Mheshimiwa Spika, suala la *FIFA* lina umuhimu wake kwa nchi zote mbili za Tanzania Mainland na Tanzania Visiwanii, lakini inavyoonesha kuna mambo ambayo Tanzania Bara inawahujumu Tanzania Visiwanii, katika mambo mbalimbali ikiwemo misaada. Kuna misaada inayoletwa kwa Tanzania, yenye kumaanisha Bara na Visiwanii lakini Tanzania Bara huwanyima wenzaa wa Zanzibar kitu ambacho si haki. Namwomba Waziri unapokuja kujumuisha alieze Bunge ni kiasi gani na misaada mingapi au ipi iliyopata na kuwapa *ZFA* ya Zanzibar kutoka *TFF*?

Mheshimiwa Spika, matangazo na wanawake. Wanawake kudhalilishwa katika mabao ya matangazo au matangazo ya gazetini, TV, ngoma kwa wanawake kuvaan nusu utupu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itunge Kitabu cha Kueleza Mila na Tamaduni za Tanzania ili watoto, vijana na nchi mbalimbali wazijue na kuzisoma ili wazifahamu na kuzithamini. Nchi na watu wake wajithamini wenyele ili wengine waweze kuwathamini.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehma kunijaalia kuwa ni mionganii mwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuniwezesha kuchangia hoja hii kwa njia ya maandishi. Kwa heshima zote naamini Waziri ataupokeea mchango huu na kuufanya kazi kuititia Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda katika kuchangia hoja hii nijielekeze katika suala la utamaduni wetu, utamaduni wa Mtanzania. Utamaduni umepotea njia kwa kiasi kikubwa na kila siku zikisogea mbele tunazidi kupoteza heshima ya Mtanzania kwa kuacha mila, desturi zetu na kujikita na kuiga tamaduni za kigeni na kuacha kufuata tamaduni zetu za asili zilizotujengea heshima katika Taifa letu la Tanzania. Suala zima la mavazi, watu wanathubutu kutembea utupu, wanavaa vigoo vya kiajabuajabu mbele ya watoto wao. Sehemu kubwa ya wasanii wetu wanaigiza mambo ambayo ni kinyume na maadili yetu kwa kuonyesha hadharani suala la mapenzi kwenye vyombo vya habari kama *T.V.* zetu.

Mheshimiwa Spika, suala la madawa ya kulevyo. Vijana wetu walio wengi sasa hivi wameathirika kwa kutumia madawa ya kulevyo, jambo ambalo limeathiri vijana ambaa ndio tegemeo letu kubwa la nguzu kazi ya Taifa letu. Napenda niishauri Wizara isimamie malezi bora kwa vijana wetu kuititia suala zima la michezo, ili vijana waweze kushughulishwa na kujipatia ajira kuititia suala zima la mkakati juu ya michezo.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari ni taasisi muhimu kabisa katika Taifa letu. Vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa kuweza kujenga au kubomoa ikiwa vitajiendesa na kutumiwa vibaya au kuingiliwa uhuru wake. Serikali pia ina wajibu mkubwa wa kuivilinda vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu vyombo vya habari na chaguzi zetu ndani ya nchi. Naomba niishauri Serikali iliyopo madarakani, isihodhi vyombo vya habari kwa kuvielekeza vibaya, waviachie vifanye kazi kwa uhuru bila kupendelea upande fulani, suala hili linaweza kuleta utatanishi na kuweza kuleta vurugu na upotevu wa amani na utulivu uliopo.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha soka nchini petu kinaendelea kushuka siku hadi siku ukilinganisha na miaka ya nyuma. Naomba niishauri Serikali kuititia Wizara husika iandae mkakati mpya juu ya suala la kuongeza bajeti yake ili iweze kutekeleza vyema na kuboresha sekta ya michezo ya soka kwa sababu michezo ni afya, michezo ni ajira, michezo ni hamasa kwa vijana. Ahsante.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pungezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa na kukamilisha hotuba hii. Napenda kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni sekta ya maendeleo ya vijana. Nini kifanyike? Hali ya ukosefu wa fursa za ajira kwa vijana hapa Tanzania inazidi kukua siku hadi siku. Vijana hawa ndio wanahodhi asilimia kubwa ya tegemeo katika nguvu kazi ya Taifa kwa zaidi ya asilimia 60. Takwimu za ukosefu wa ajira za vijana ni takriban asilimia 11 tofauti na matarajio ya MKUKUTA ambaa ulipanga kushusha ukosefu wa ajira mpaka asilimia 6.9 mnamo mwaka 2010. Kwa upande mwagine takwimu hizo hazitoi picha kamili ya uhalisia wa hali tete ya ukosefu wa ajira na fursa za uzalishaji pato kwani hali ya sasa na ongezeko la wahitimtu toka Vyuo vya Ufundii na Elimu ya Juu imeongezeka maradufu katika miaka ya hivi karibuni. Hali hii ya ukosefu wa ajira kwa vijana si tu inarudisha nyuma jitihada za vijana hawa kujiletea maendeleo yao binafsi bali pia kwa kiasi kikubwa inarudisha nyuma Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa Wizara kubuni/kuja na mipango madhubuti na endelevu ya kushughulikia tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana katika kujituma na kujajiri. Wizara inabidi pia kuandaa mikakati mabsusi ya kuwafikia vijana wanaoshinda vijiweni na hata wale wanaojihuisha na madawa ya kulevyo ili waweze kujajiri wenyewe na kuachana na vitendo visivyoofaa. Nashauri pia wakati tunajiandaa kusherehekea miaka 50 ya Uhuru, Wizara iandae/kuendesha mjadala wa Kitaifa nini kifanyike kuharakisha maendeleo ya vijana na kukuza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, pili ni juu ya sekta ya habari. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na vyombo vya habari katika kuihabarisha, kuelimisha na kuburudisha jamii bado kumekuwa na changamoto nydingi zihusianazo na ukiukwaji mkubwa wa maadili katika baadhi ya vyombo vya

habari hasa binafsi. Je, ni lini Wizara itakamilisha/kuleta Bungeni Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari na Sheria ya Haki ya Kupata Habari? Naamini kupitishwa kwa Sheria hizi kutawawezesha Waandishi wa Habari, Wamiliki wa vyombo vya habari kufanya kazi zao ipasavyo kwa kuzingatia maadili ya uandishi wa habari zenyen tija na manufaa kwa nchi na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, Tanzania lugha ya Taifa ni Kiswahili ambapo lugha hiyo hiyo imechukuwa nafasi ya Kitaifa, kwa msingi huo lugha ya Kiswahili inahitajika duniani na kwa vyovyote, unaposema Kiswahili, Tanzania ndio kwenye shina lake. Kwa hali hiyo inatakiwa kwenye Vyuo vinavyosomesha Kiswahili huko duniani ni lazima Walimu wa Kitanzania wanaosomesha Kiswahili wawe wengi. Sijui hali ikoje? Pia hata katika vyombo vya habari hususan redio iwe hivyo hivyo, watangazaji wengi wawe wa Kitanzania.

Je, Wizara imewasaidiaje wasomi wa Kiswahili kupata nafasi huko nchi za nje? Kama Wizara haitakuwa makini katika suala hili basi soko la Kiswahili huko nchi za nje litatawaliwa na nchi nyinyine.

Mheshimiwa Spika, hali inavyojitokeza hapa nchini katika vyombo vya habari hususan *TV* kwa baadhi ya vipindi, havilingani na silka na utamaduni wetu. Utamaduni wa nchi za Ulaya kwa baadhi ya sehemu haulingani na utamaduni wetu, kwa hivyo si sahihi kila kipindi kinachooneshwa kwenye *TV* kwa sababu vinatoka Ulaya ndio inavyostahili kuonekana kwenye *TV* zetu, ipo haja *TBC1* ioneshe mfano wa vipindi vyake.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kuwaendeleza vijana kwa kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana wamewezeshwa kwa kupitia *SACCOS* TShs.1,210,000,000/. Muda wa kurejesha fedha zilizokopwa umeshafika lakini jambo la kusikitisha na kushtushwa fedha iliyorejeshwa ni Shs.46,350,000/ tu. Mimi nina wasiwasi mkubwa kwa hali hiyo inawezekana vijana au *SACCOS* zao ni za kubabaisha na Wizara pengine hawakufanya utafiti wa kutosha juu ya *SACCOS* hizo. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa fedha hizo zinarejeshwa ili vijana wengine wawze kupata mkopo?

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 22 wa hotuba ya Waziri, Aya ya 32, Waziri amesema vijana 200 walikutana kujadili kwa pamoja utekelezaji wa mpango wa vijana duniani. Ukiachana na sifa za kielimu, je, ni sifa na utaratibu gani zilizotumika kuwapata vijana hao 200?

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari binafsi vinafanya kazi nzuri hapa nchini lakini tatizo kubwa liliopo wamiliki wa vyombo hivi vya binafsi hawana tabia ya kuwasomesha wafanyakazi wao. Ipo haja Wizara ianzishe utaratibu wa kuwashawishi wamiliki wa vyombo binafsi kuwasomesha wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Spika, matumizi sahihi ya Kiswahili ni wajibu wa BAKITA. Leo hii Kiswahili kinasemwa na kuandikwa kwa makosa ya kawaida. Ni vizuri BAKITA isimamie matumizi bora ya Kiswahili. Ahsante.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, hotuba nyingi za Wizara hii zimepita lakini bado hajjawahi kutokea sehemu inayowaenzi Waasisi wa Muziki nchini kama vile Muasisi wa HipHop, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi (*Mr. II/SUGU*) ambaye sasa ni Mbunge wa Mbeya Mjini. Hivyo basi tungependa Wizara ya Mheshimiwa Waziri itupe maelezo ni namna gani tunawaenzi waasisi hawa kwa kuwa tunathamini kazi yao kwani ni msaada mkubwa kwa jamii yetu katika kuburudisha, kuelimisha na kuongeza ajira nchini hususan kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya vijana. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hatujaona ni vijana wangapi wamepata ajira binafsi kupitia mikopo inayotokana na Wizara yake kwa kuwa vijana wengi nchini hawana elimu ya kutosha na kazi maalum za kufanya na kwa kuwa Taifa bila vijana wanaofanya kazi ni sawa na Jeshi bila silaha? Hivyo basi naomba Wizara ya Habari itupe ufanuzi wa takwimu ni vijana wangapi wameweza kujajiri kupitia mikopo hii. Naomba kuwasilisha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoifanya katika mazingira ya bajeti finyu. Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kutoa uhuru wa kutosha kwa vyombo vya habari, lakini kwanza nisemavyo siku zote *Government should not abdicate its responsibility* na kuhakikisha vyombo vya habari vinazingatia *ethics na good journalism*, kama ni kuikosoa Serikali basi iwe *constructive criticism*.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari visipotoshe ukweli wa mambo. Njia moja ya kuwasaidia Wanahabari ili wawe *good reporters* ni kuhakikisha katika *syllabus* zao au *curriculum* za vyuo vyao kuwepo na masomo yanayowasaidia kupata *skills* za *critical analysis* ya *issues* mbalimbali. Somo la *logic* ni muhimu sana. Mwanahabari akisoma masomo kama *economics* na *political science* atakuwa *reporter* mzuri.

Mheshimiwa Spika, utamaduni wa nchi yetu unatoweka sijui kama tumeanza kujenga utamaduni wa Kitaifa au tuna utamaduni wa makabila mbalimbali tu. Basi tuimarishe tamaduni zetu za makabila mbalimbali wakati tunajaribu kujenga utamaduni wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, *American Cultural Globalization*, dunia imetekwa na utamaduni wa Kimarekani. *Holly Wood* inazalisha filamu nyingi na inaziwa dunia nzima kwa malengo mawili. Mosi, kueneza utamaduni wa Kimarekani na pili, kupata fedha. Sasa hivi filamu za *Holly Wood* zinaingiza fedha nyingi katika uchumi wa Marekani. Vijana wetu wametekwa na utamaduni wa Kimarekani. Hiyo ni changamoto kwa Wizara ya Utamaduni. Tuongeze tamasha za utamaduni pamoja na semina mbalimbali. Kuwepo na programu za utamaduni wetu katika radio na TV.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, sharti isaidiane na Wizara ya Kazi na Ajira, kuwawezesha vijana waweze kujiajiri. Mimi binafsi kama Mbunge wa Ngara nina changamoto kubwa. Vijana wengi wa Ngara wako kijiweni. Nilikuwa sijui kama kuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Naomba Wizara hii inisaidie ili vijana wa Ngara nao waweze kufaidika na Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, sanaa ni kipaji cha watu wenye akili kwa mfano sanaa ya *music*. Naiomba Wizara iendelete *strategy* ya kuibua vipaji vya watoto kuanzia shule za msingi nchi nzima. Hii itawezekana kama kutakuwepo Walimu wa Sanaa na Michezo katika shule zetu na vyuo vyetu. Tufike *stage* ambayo wanansanaa wanalipwa vizuri kama ilivyokuwa wana sanaa wa nchi za wenzetu (Ulaya).

Mheshimiwa Spika, Wizara im-support Mheshimiwa Rais katika *Vision* yake ya kutaka timu yetu ya mpira iweze kushiriki katika *World Cup* na katika mashindano ya mpira Barani Afrika. Hii itawezekana kama Wizara itawatambua vijana katika shule za msingi ili kuwaandaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, mila na desturi za Kiafrika, mila na desturi zetu zinatoweka kwa vijana wetu, Wizara ina changamoto ya kusaidiana na wazazi pamoja na Walimu mashulenii kuwajenga vijana katika utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mkubwa ni kurudisha *National Service* itasaidia kujenga nidhamu ya vijana pamoja na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, filamu kutoka nje zidhibitiwe, filamu za kihuni zisiruhusiwe kuoneshwa nchini.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Michezo, Chuo kimoja hakitoshi. Vyuo vya Ualimu, *Teachers Colleges*, vishiriki katika ku-promote michezo na utamaduni.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, napenda nichangie kwa kuanza na mpira wa miguu.

Mheshimiwa Spika, ziko nchi nyingi za Afrika na Ulaya zina wachezaji ambao wanachezea *team* kubwa duniani za mpira ambao wanalipwa fedha nyingi na vilabu vyao nchini kwao zinalipwa fedha nyingi pia. Tanzania vijana wengi wanaocheza mpira ni wale walioshindwa elimu

ya sekondari/msingi. Kijana aliyesoma *degree* atacheza mpira kwa utaalamu vizuri zaidi (hasa anapofundishwa). Nashauri Serikali ihamasishe pia vijana waliopo Vyuo vyetu nya Ualimu, Vyuo Vikuu wachezee *team* ya Taifa, Simba, Yanga na kadhalika. Wale waliomaliza elimu ya msingi VETA waagizwe waanzishe elimu ya mchezo *including football, netball etc.* *Team* zikiwa na wengi wenye elimu hakika zitafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, yako makampuni au watu binafsi ambao wanaweza kuunda *team* za michezo tofauti wakawalipa wachezaji na kuwalea. Nashauri Serikali iungane na sekta binafsi kuona uwezekano wa kuanzisha *team* kama hizi. *Team* hizi zitakuwa zimetengeneza ajira, kipato na kodi kwa Serikali. *Team* kama hizi zikubaliwe zianzishwe kila Mkaoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipange kuwe na mashindano ya Mikoa hii na zawadi nono zitolewe kwa washindi bila urasimu na usumbufu. Mafunzo ya michezo yanaweza pia kuanza katika shule za msingi. Michezo ni furaha, michezo ni afya na ni kipato. Michezo ikianza mashulenzi watoto *wata-grow up with the culture*. Wale wacheza mpira ambao watakuwa wazuri (*good in football*) wanaoweza kutambulika mapema, wakawa *promoted* na kupewa *professional studies* baadaye watakuwa wachezaji wazuri. Nashauri Serikali lanze michezo hii mashulenzi (sio vipindi nya *Physical Education* nya kawaida) iwe zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, matangazo yanayotangazwa na *TV* na Redio zetu, wakati mwingine ni mabaya kwa maadili ya watoto wetu. Mfano tangazo la "wa hapa hapa" linalorushwa na *Airtel* linafundisha maadili yasiyo mema. Nashauri Serikali itoe angalizo kwa wanaochambua matangazo waangalie matangazo yote yasiyofaa yasitangazwe na *TV* zetu.

Mheshimiwa Spika, ziko *DVDs* nydingi zinazuwa na maduka ya *music* (yanayouza *CD, Cassettes etc*) wanauzuwa *DVD* mbaya za *ponography*. Nakumbuka Serikali ilipiga marufuku *ponography* nchini. Nashauri Serikali ipitie maduka yote kuhakikisha *DVD* hizi haziendelei kuuzwa kwani zitaharibu maadili ya watoto wetu. Ziko nydingine zinatumwiwa na matajiri wenye mabasi ya abiria. *DVD* kama hizi ni mbaya. Nashauri Serikali itoe tangazo kwa wenye mabasi *as to what kind of movies should be shown to their passengers*. Wakati mwingine inakuwa *embarrassment* kwa abiria.

Mheshimiwa Spika, *Big Brother* haina maana yoyote kama maadili yanayofundishwa ndiyo hayo tunayoyaona. Kama kuna uwezekano wa kuzuia picha hizo zisipate *access* katika *satellite* za Tanzania, nashauri Serikali ifanye hiyo.

Mheshimiwa Spika, vijijini wako raia wanaonyesha sinema kwa wananchi wa maeneo yao usiku. Watu hawa hawajasajiliwa na Maafisa Utamaduni wa Wilaya na wakati wanakusanya fedha nydingi sana kama kiingilio. Hawalipi kodi na wanaonyesha picha mbaya usiku kwa watu wazima na watoto. Nashauri kila Afisa Utamaduni wa Wilaya kwa kupitia Maafisa Tarafa, Watendaji wa Vijiji, watu hawa wasajiliwe, wajulikane, wapewe amri sinema hizi za usiku zisionyeshwe kwa watoto *under 18* na kama za watoto (hasa wa shule) iwe Jumamosi na Jumapili *during the day*. Watoto wengi (hasa Mikoa ya Magharibi) wanapata mimba kutohana na sinema hizi.

Mheshimiwa Spika, waganga wa kienyeji wanachangia mauaji ya vikongwe huko Mikoa ya Magharibi, wanatoza viingilio mpaka 140,000/= kama kiingilio kwenye umoja wao. Mfano ni Chama cha Waganga Nzega CHAWATIATA. Hiki ni mfano wa Chama kinachotapeli raia wake kwa mkataba na Katiba kutaka kila mwenye kufanya uganga ajiunge kwa gharama kubwa na fedha yote inatafunwa na wao na Afisa Utamaduni wa Halmashauri ya Wilaya. Nashauri Serikali isajili waganga wote wa kienyeji na kila Chama cha Waganga ada ya kujunga iwe *discussed* na Baraza la Madiwani, itanusuru mateso wanayopata waganga na raia kwa ujumla. Pia ni vema waganga walipe kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri ye ye binafsi kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii, jambo amblao halishangazi

kwani uwezo na uadilifu wake unafahamika, lakini vilevile kwa kutoa hotuba nzuri yenyewe kuonyesha mwelekeo. Aidha, nimponeze Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Fenalla Mukangara kwa kuteuliwa katika nafasi hiyo, kwa usikivu, unyenyekevu na uwezo mkubwa, "certainly you would never have gotten a better Deputy Minister than her". Nimponeze Katibu Mkuu, Kamuhanda, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara yako kwa kazi nzuri wafanyazo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimponeze Waandishi wa Habari, watoaji habari wa aina zote, iwe magazeti, majarida, redio, televiseni, ma-blog mbalimbali, kwa kazi nzuri ya kuhabarisha na kwa kiwango kikubwa ni kama mhimili wa nne na imesaidia sana Watanzania kufahamu mambo mbalimbali na kuchocha maamuzi ya haraka kwa maslahi ya Watanzania lakini nilikuwa najiuliza ni namna gani wanawezeshwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili ambayo kimsingi ni moja ya *core functions* za Wizara hii? Ni taaluma kama taaluma nydingine ambayo kwa sababu za msingi inaendeshwa na watu binafsi kufuatilia maslahi ya kifedha ya kimsingi (kwa mfano mshahara) ili kuepuka wanahabari hao kununuliwa kwa maslahi ya pesa ilhali wanaandika habari zisizo sahihi. Kama Wizara mnajua maslahi hayo? Mwisho wa siku kila mtu anahitaji kipato ili aishi na unapokuwa unaweza kukidhi mahitaji yako ya msingi angalau (ukiacha watu wenye hulka hiyo) kwa kiwango kikubwa na maadili yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi na nchi kwa ujumla sasa hivi inaendeshwa na vyombo vya habari. Cha kutisha zaidi habari hizo ndizo zinaaminika na kufanyiwa kazi, bila kujali zile habari ambazo ni za uchochezi na hazina ukweli na mara nyangi ambazo ni za uchafuzi. Kisha muda mwingi unatumwiwa kusafisha hali hiyo, kiasi cha kupoteza muda wa kuleta maendeleo. Je, Wizara imejipangaje kuhabarisha umma kuwa hayo mambo ni uzushi au ni hatua gani zilizopo kwa kushirikiana na Umoja wa Wanahabari kuhakikisha hali hiyo inaratibiwa?

Mheshimiwa Spika, utamaduni, mtakubaliana nami utamaduni wa nchi umepotea kabisa. Hata Maafisa Utamaduni walioletwa kwenye Halmashauri wakiwa hawana nyenzo, usafiri na fungu la kufanya kazi, mategemeo ni Halmashauri na kama Kilindi mapato yetu ni madogo, *OC* hajiji kwa wakati na kwa fedha zilizombwa kwenye bajeti, hivyo kupoteza maana ya kuwa nao ndani ya Halmashauri. Kuna mpango wa kujua shughuli wanazofanya Maafisa hawa? Bajeti yao inaelezwaje ikizingatiwa Halmashauri hazina uwezo? Pendekero, anzisheni mashindano ya utamaduni kuanzia ngazi za chini hadi Taifa kwa wananchi lakini pia mashulenii na vyuoni.

Mheshimiwa Spika, michezo, sambamba na hao Maafisa Utamaduni, Maafisa Michezo kwenye Halmashauri pia bajeti yao inategemea zaidi uwezo wa Halmashauri. Hawana usafiri wala vifaa, Wizara ilikusudia nini kupeleka Maafisa hawa Wilayani? Kuna vijana wengi wana vipaji vya mpira wa miguu, pete na basketball na kadhalika, tatizo vifaa na Walimu. Viwanja pia ni tatizo. Hivi kweli hili libaki kuwa la Mbunge ambaye kwa bahati mbaya wengine hawana *interest* kabisa ya michezo? Naomba Wizara itoe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mafunzo yanatolewa kwa ajili ya kuimarisha michezo na awamu iliyopita ilikuwa imefika zamu ya Kilindi. Pamoja na hayo, naomba sana tuwe na mwongozo, tuanzishe *FAT* Wilaya ambazo zitafuata sheria na kuwa na viongozi. Hali kadhalika kuwa na viongozi hadi kwenye Kata na Vijiji. Eneo kubwa ambapo vijana hupata kujumuika, kupoteza muda badala ya kufanya vitu viovu, ni kwenye michezo. Hivi naomba Serikali iwape kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, wakimbiza mwenge. Jopo hili la wakimbiza mwenge ni la vijana, wa kike na wakiume ambao kwa kiasi kikubwa ni wenye uwezo na ukakamavu mkubwa kuhimili mbio za nchi nzima. Cha kusikitisha baada ya mbio za mwenge jopo hili limeachwa, ilhali wanakuwa na upeo mkubwa wa masuala mbalimbali ya sehemu zote za nchi hii. Naomba nimpendekeze, paundwe kitengo maalum cha wakimbiza mwenge ili tuwatumie kwa kutumia usoefu mkubwa waliopata na changamoto walizoona. Wanaweza kuwa msaada mkubwa katika kutoa kipaumbele kwa masuala mbalimbali ya uchumi wa nchi yetu. Hili ni la msingi, naomba lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, vijana, nimponeze Serikali kwa kujitahidi kutoa misaada na nafasi mbalimbali kwa vijana wetu kutokana na wingi wao unaweza kudhani vijana hawaangaliwi na

Serikali, lakini naomba jitihadi ziongezwe kwa vijana wa vijijini. Kama ilivyo, utaratibu wa semina za wajasiriamali vijana huwa hawahusishwi sana. Naomba tushirikiane tuenze mradi maalum wa kuwawezesha vijana.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii adimu kukukaribisha wewe Waziri au Naibu wako au wote mtembelee Wilaya ya Kilindi muone tunayoyafanya katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri na hususan Wizara hii na mipango yake mizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kero kubwa ya vijana. Vijana wetu wengi hawana ajira, hawana mwelekeo wa kiuchumi. Naomba Serikali sasa ichukue hatua ya kuhakikisha kuwa mbali na mikopo finyu inayotolewa kwa vijana bado elimu ya ujasiriamali hawanayo. Ufanyike utaratibu wa kuhakikisha kuwa mikopo inaboreshw na elimu ya ujasiriamali na pia utaratibu wa kuwashindanisha wajasiriamali hawa wadogowadogo kwa lengo la kuwaendeleza ufanyike.

Mheshimiwa Spika, vijana wamekosa mwelekeo kimichezo. Aidha, nniombe Wizara ifanye utaratibu wa kuhakikisha angalau kila Wilaya inapata maeneo na viwanja vya michezo vinavyomilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana shujaa wetu wa michezo ya Riadha, Ndugu Felbert Bay, mwananchi wa Jimbo la Kibaha Mjini, yeye na mke wake kwa kazi kubwa ya kuendeleza michezo wamekuwa wakitumia viwanja vya shule yao, Filbert Bay Secondary School kwa shughuli mbalimbali za kimichezo na hata kugharamia michezo hii wakishirikiana na Mbunge wa Jimbo. Kwa nini sasa Serikali isitambue mchango wa wachezaji hawa wakongwe, wakawa wanaandaa vijana watakaowarithi? Kuna sababu gani ya kutoa gharama kubwa kwa wageni kufundisha timu zetu wakati tunao wakongwe waliokwishashiriki na kuletea Taifa letu sifa kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya, muundo wa Idara ya Utamaduni na michezo unatia mashaka. Vijana kwa wazee wamekuwa wanabuni ligi zao pasipo hata kupewa mwongozo na idara hizi. Maofisa Utamaduni hawana mpango wa kuwahusisha wananchi katika *programme* za michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja zisizopungua nne katika Wizara hii muhimu sana, inagusa mustakabali wa vijana wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza ni kuboresha kiwanja/viwanja vya mpira kama walau kile cha zamani cha Taifa pale Dar es Salaam kwa kiwango cha kile kilichoboreshw kwa sasa yaani iwe kila Mkoa hii itasaidia sana kukuza soka, mpira wa pete, mpira wa kikapu, riadha na michezo mingine mingi iweze kufanyika katika viwanja hivi. Hii si tu itasaidia kukuza na kutoa ajira kwa vijana wetu bali pia kuingiza kipato cha kifedha ili kukuza uchumi katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza michezo, Serikali inatazamia sana soka na tunasahau michezo mingine, nafikiri hii ni changamoto kubwa inayowakabili Watanzania na hasa Idara husika katika Wizara. Inabidi vipaumbele viwekwe katika michezo yote hii itasaidia sana kuibua vipaji ndani ya jamii ya Watanzania na hii itasaidia sana katika kuviendeleza ambapo itapelekea hata kufika katika ngazi za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni kuhusu kuenzi utamaduni wa Mtanzania. Utamaduni wa Mtanzania unatafishwa na tabia za kigeni na hii inasikitisha kuona Wizara husika imefumbia macho suala hili. Mfano mimi nashangaa hadi leo hii nimekuwa nikisikia mchakato wa vazi la Kitaifa, hii ni aibu kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika utamaduni napendekeza kuwepo na mashindano ya ngoma za jadi maana naona ngoma zetu za asili zinatokomea, watu tunabobeaa kwenye ngoma/muziki ya kisasa sio kwamba naipinga hii miziki ya kisasa, la hasha, ni kule kusahaulika kabisa kwa ngoma za jadi.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika utamaduni ni kuhusu mashindano mbalimbali yanayowahusisha watu mbalimbali katika jamii yetu, mfano mashindano ya *Big Brother Africa*. Hivi Wizara husika inajua dhima nzima ya haya mashindano ya *Big Brother Africa* maana tumeshuhudia vitendo vya kifilauni mbele ya watu. Mfano wa fedheha zaidi ni kwa binti wa Kitanzania katika shindano la mwaka huu alishuhudiwa akifanya vitendo vya ngono na kijana wa Kiganda, kwa utupu kabisa tena bila hata kujifunika na shuka. Hadi leo hii Wizara husika hajatoa tamko la kukemea kitendo kile na hata kuihoji Kampuni ya *Multchoice* ambao ndio huwachuja vijana hao na kuwapeleka ili wapeperushe bendera ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ni kuhusu vyombo vya habari. Inabidi taswira hii iangaliwe vizuri kwa maana ya kuongeza kipato kwa Wanahabari ili kuondoa hii hulka ya wao kufanya kazi kwa kusubiria au kuandika habari/na au kuitangaza pale tu au kwa yule anayewapa fedha. Hii inakuwa haitoi mchango wowote kwa Watanzania kwani inapelekea kuondoa weledi katika taswira hii na hivyo wakati mwingine kupotosha ukweli kabisa wa habari kitu ambacho ni hatari sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia inabidi Televisheni ya Taifa yaani *TBC* pamoja na Radio na magazeti yafanye kazi na kuripoti habari bila ya upendeleo kwani ikumbukwe kuwa vyombo hivi ni vya umma na vinatumia kodi za Watanzania na hivyo visikilize taarifa toka pande zote ziwe nzuri au mbaya kama ilivyo sasa ambapo vyombo hivi vya umma vinaegemea zaidi kuperdelea Serikali na Chama cha Mapinduzi. Hii inadhihirisha kwa *programme* nyingi na taarifa zihusizo Chama hiki Tawala.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu vipindi kwenye Redio/TV mbalimbali, vingine si kwa manufaa ya umma na hivyo ni vema *TCRA* waki-monitor.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niisihi Serikali kupitia Wizara na Idara zake walipe deni la *TBC*. Maana ni albu kuona madeni yapo kwenye ma-billions. Hii ni aibu. Hivyo nashauri wadeni husika walipe haya madeni haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa michezo ni furaha, michezo ni ajira, Taifa letu ni lazima liweke kipaumbele katika michezo. Michezo huongeza pato kubwa la Taifa, michezo hufanya/kuwezesha nchi kutambulika Kimataifa. Ni muhimu sana bajeti ya Wizara hii kuwa kubwa ili kuweza kutekeleza kazi zao walizozipanga.

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru sana kwa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), kwa kazi yao nzuri wanayoifanya katika Taifa letu. Nampongeza sana Mkurugenzi wa Baraza la Michezo Tanzania, nakubali kazi yake nzuri sababu ameweza kupeleka watendaji wake katika Mikoa mbalimbali ya Tanzania ili kutoa mafunzo ya michezo kwa vijana wetu. Wametoa mafunzo kwa vijana katika Wilaya ya Mufindi kutoka Kata mbalimbali ndani ya Wilaya ya Mufindi, sasa hivi vijana wanafanya mashindano ya michezo wa mpira kila Kijiji – Kata – Wilaya. Nashauri Watendaji wanaokwenda kutoa mafunzo Wilayani kutoka Dar es Salaam waongezewa posho/fedha ya kujikumu sababu mazingira wanayokwenda ni magumu sana. Pia bajeti yao ni ndogo sana Wizara sijui kama itaweza kufanikisha malengo yao kwa bajeti hii ndogo ya T.Shs.14,523,735,560/=. Wizara ipewe magari ya kufanya kazi ili wanapoenda Wilayani waweze kusafiri kwa gari lao sababu wanakuwa na mizigo mingi pamoja na vifaa vya michezo wanayoenda nayo kwa ajili ya mafunzo. Aidha, Maafisa Utamaduni Wilayani wapewe magari. Mafunzo yatolewe kwa Makocha wa mpira wa miguu na mpira wa mikono kwa wasichana kwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari waajiriwe siyo kujitolea na walipwe mishahara kama wafanyakazi wengine. Waandishi wa Habari waheshimiwe sababu kazi yao ni muhimu sana katika kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, jengo la *TBC*, naomba Serikali ilitolee maamuzi ya haraka lijengwe, haipendezi hata kidogo kubaki kuwa gofu kwa sababu ni muda mrefu sasa liko hali ile na *NSSF* wako tayari kulimalizia.

Mheshimiwa Spika, wasanii wetu ni watu mahiri kwa kutufunza kwa njia ya sanaa mbalimbali, lakini sanaa hii hivi sasa imepita mipaka ya maadili ya silka na mila zetu. Utamaduni wetu unapotea hasa pale wasanii wanapoonesha mili yao na vitendo vyta mapenzi ya ndani katika luninga. Hii inapotosha vijana wetu na pia inatia aibu, huwezi kuangalia mchezo ukiwa umekaa na watoto wako au watu unaowastahi.

Mheshimiwa Spika, kila nchi duniani ina lugha yake hata makabila yote yanatumia lugha zao lakini sisi hapa nchini kwetu tunajaribu sana kuidhalilisha lugha yetu ya Taifa kwa sababu hata hapa Bungeni wengi wetu tunachanganyachanganya, hii inapotosha sana vijana wetu na pia walioko vijiji hawatuelewi kwa kuchanganya lugha. Naomba Wizara hii itoe tamko na kuweka na kuendeleza mikakati iliyo bora ili lugha yetu ya Kiswahili isidhalilishwe na baadhi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la mchezo wa mpira wa miguu. Mashindano ya mpira huu kwa Mikoa, naomba yaboreshwe sana ili tupate wachezaji wengi na walio bora kutoka Mikoa mbalimbi kwani kuna wachezaji wazuri lakini uzuri na umahiri wao hauonekani wakibaki Vijiini tu. Hawa wachezaji bora wa Simba na Yanga pia wanatokea vijiji na sio mijini tu. Pia michezo ni sehemu ya ajira hata wakati mwengine anaweza akachukuliwa mchezaji wetu na timu toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono, ahsante.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Watendaji wote wa Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuleta bajeti nzuri iliyojikita katika mbinu mbalimbali zitakazosaidia kuboresha na kuinua tasnia ya utamaduni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti hiyo, nichukue nafasi kutoa ushauri katika baadhi ya maeneo. Jukumu la msingi kuruhusu utengenezaji wa sinema, maigizo, maonyesho na utoaji wa leseni. Sinema, maigizo na maonyesho ni burudani ambazo kama Serikali ingeweza kusimamia, kuwatia moyo vijana na kuwasaidia kulinda kazi zao, ingesaidia sana vijana kupata ajira nzuri endelevu na kukuza vipaji vya vijana walio wengi.

Mheshimiwa Spika, vijana walio wengi ambaao ni wasanii wamekuwa wanajitahidi sana kutengeneza sinema, nyimbo hata ngoma lakini wamekuwa wanapata shida sana, kuza huduma hizi kutokana na kuwa na mitaji midogo, elimu na hata upeo mdogo walio nao katika fani hiyo. Hata hivyo, wapo wafadhili wanaowafadhili lakini wanakuwa na lengo la kuwadumaza vijana kwa kununua kazi zao kwa bei ndogo sana na kuendelea kuisambaza na kuvuna fedha kwa kipindi kirefu. Naishauri Serikali kuwasaidia wasanii katika jambo hili ili waweze kuzipata haki za msingi za kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia kukazia suala la michezo mashule ili kuibua vipaji vya vijana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hiyo. Wizara hii ni nyeti sana ambayo inashughulika na kazi ambazo zinaweza aidha kuangamiza au kudumisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, habari ndiyo ilichochea mauaji ya Rwanda. Hali sasa hivi inaendelea kuwa mbaya. Waandishi wengi wanajihuisha na rushwa na wanaweza kuandika kitu chochote wanacholipwa kuandika. Hawajali habari hiyo itamuathiri mtu au nchi kwa kiasi gani. Sasa hivi magazeti ambayo yamekuwa uititri hayaaminiki kwa sababu mara nyngi sana yanaandika uongo. Serikali inalijua hilo, lakini hakuna sehemu yoyote wala wakati wowote Serikali ilipochukua hatua hata pale gazeti linaposema uongo dhidi ya Serikali yenyewe au kiongozi yeyote.

Mheshimiwa Spika, sera ya vyama vingi imezidisha hali hii mbaya kwa sababu waandishi au vyombo vyote vyaya magazeti na *television* wanasema uongo kusaidia kutoa sifa ya Chama chao na kukandamiza na kusema uongo dhidi ya vyama vingine. Tumeshuhudia vurugu nyngi zimechochewa na taarifa za uongo za vyombo hivyo vyaya habari. Kama kweli tunataka kudumisha amani nchini kwetu, basi Serikali ichukue hatua ya kudhibiti habari za uchochezi, vinginevyo amani tunayoringia Tanzania itatweka.

Mheshimiwa Spika, vijana ni zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania, vijana wapo kwenye makundi mawili ambayo yote yana matatizo na yanaweza kuleta madhara makubwa sana kwa Taifa. Kundi la kwanza ni kundi la vijana ambao kwa sababu moja au nyngine hawakupata elimu nzuri. Wengi wamemaliza Darasa la Saba (7) na kwa sasa wapo pia waliomaliza Kidato cha Nne (4) na 6. Hawa hawana ajira, hawana mtaji, hawana biashara au wanajihuisha na biashara ndogondogo ambazo hazikidhi mahitaji yao ya kila siku. Hawa vijana ndiyo walio wengi sana, matokeo ya hali hiyo, vijana hawa ni rahisi kuingizwa kwenye maasi ya aina nyngi kwa ujira mdogo sana. Ndiyo hawa utawakuta kwenye maandamano, ujambazi na fujo yoyote itakayokuja karibu yao. Tumeona fujo nzito nchini Uingereza na chanzo ni vijana kutokuwa na ajira kwa hiyo kitu kidogo kinachoanzisha vurugu wanakuza na kufanya Miji kutokalika.

Mheshimiwa Spika, tunasema wajunge waanzishe *SACCOS*, lakini wataanzaje ikiwa hawana kipato kinachoingia? Hata kama wanacho, itawachukua muda gani kuweza kutumia hisa zao kupata mikopo? Serikali ni lazima ibuni mpango mwagine wa kuwasaidia vijana hao ili waweze kujikimu na kupata maendeleo, wana mahitaji kama mtu mwagine yeyote. Serikali ianzishe mashamba na kuwagawia vijana, kuwasaidia mbegu, utaalalm mpaka watakapovuna mara mbili tatu, wanaweza kuchangia kwa mfumo wa mazao watakayovuna. Vilevile vijana wanaweza kusaidiwa zana za kufanya kazi kwa wale wenye ujuzi kama waliotoka *VETA* ili waweze kuanza kujiajiri. Kama Serikali haikuchukua hatua hiyo kuna hatari ya amani nchini kutoweka, vijana watakata tama, hakuna kinga ya hilo.

Mheshimiwa Spika, kundi pili ni vijana waliopata elimu nzuri ndani na nje ya nchi. Vijana hawa wamekuwa na tamaa ya maendeleo ya haraka. Hawa ndio wanaojihuisha sana na wizi wa kitaalam wa mabenki, *TRA* na sehemu nyngine za taasisi za fedha, sijui kama Wizara ina takwimu ya utajiri wa vijana katika kundi hili? Wana magari ya kifahari, nyumba za kifahari na wanashindana kwa utajiri. Serikali ni lazima illangalie kundi hili maana wengi ni wale waliotoka kwenye familia zinazojiweza na wanaleta tabaka la vijana walionacho na wasionacho, Serikali ilikemee suala hili.

**MHE. KAIKA S. TELE:** Mheshimiwa Spika, ni haki ya kila Mtanzania kupata habari kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, Ibara ya 18. Mgogoro wa ardhi wa Loliondo kati ya Mwekezaji na Wanavijiji, ulipata umaarufu/kujulikana ndani na nje ya Tanzania kutokana na kalamu ya Wanahabari na Wanaharakati walitembelea eneo hilo mara kadhaa. Nawashukuru sana kwa kazi yao nzuri ya kuwahabarisha Watanzania juu ya mgogoro huo hadi Kamati ya Bunge kwenda kuona.

Naomba kupitia kwako Mheshimiwa Waziri, Waandishi wa Habari (magazeti na television) waruhusiwe kuingia Hifadhi Mseto ya Ngorongoro na kuandika habari zinazohusu wananchi

waishio ndani ya Hifadhi hiyo ambayo pia ni urithi wa dunia. Kufanya hivyo kutaimarisha uwazi na kuondoa usiri wa matatizo ya wananchi wa Ngorongoro kufahamika nje ya mipaka ya Hifadhi.

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI:** Mheshimiwa Spika, ingawa vyombo vya habari pamoja na Waandishi wana dhima kubwa katika kuhabarisha jamii na kuburudisha, lakini mara nyingi imekuwa kwa baadhi ya wananchi wanawabeza Waandishi, kuwadharau na kuona hawana umuhimu katika jamii. Hivyo Waziri wa Habari namwomba suala hili kulichukulia hatua ili na wao wajisikie wako huru katika kufanya shughuli yao.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu, wakati wa kufuatilia habari za mtu humbidi afuate *story* hata kwa miguu. Hivyo naomba Waandishi nao wapatiwe usafiri hata kama vespa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira kwa vijana wetu Waandishi wa Habari imekuwa ni tatizo kubwa sana na tukiangalia sasa hivi vyombo vya habari vingi hapa nchini petu vinamilikiwa na vyombo binafsi hususan magazeti. Hivyo namuomba Waziri wa Habari kufanya mazungumzo na vyombo vya habari vya binafsi kuhusu Waandishi wa Kujitegemea na wao wawaajiri ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Wanahabari zisizo za Kiserikali. Miongoni mwa taasisi na vyombo vinavyosaidia katika kuboresha vyombo vya habari pamoja na Waandishi wa Habari hapa nchini ni Baraza la Habari Tanzania (*MCT*) na Wahariri wake kwa juhudhi kubwa wanazozichukua katika kuwapatia nafasi ya muda mfupi kwa waandishi waliorachanga kwa kuwapatia mafunzo ya kiuandishi. Hivyo naliomba Baraza hili la Habari nao kuwapatia ajira Waandishi hao katika maofisi ya vyombo vya habari hivyo. Namwomba Waziri pamoja na Serikali kulipa uzito suala hili.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa wanafunzi wa vuo. Hivi sasa vijana wetu wengi wanaosoma vyuoni wanasumbuliwa na tatizo la mikopo hususan wanafunzi wanaosomea Uandishi wa Habari. Sijui tatizo hili linatokea kwa kuwa Waandishi hawana umuhimu kwani mara nyingi wanafunzi hawa wanajisomesha wenye huku Tanzania Bara na kule Zanzibar. Hivyo basi, naiomba Bodi ya Mikopo kuliangalia suala hili katika utoaji wa mikopo kwani wanafunzi wote ni sawa. Hivyo namwomba Waziri wa Habari pamoja na Serikali yake kulichukulia hatua suala hili ili tatizo hili liondoke.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Waziri wa Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo kutohuna na hotuba yake nzuri yenye lengo la kusaidia vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi (Mb), kwa hotuba yake nzuri na yenye kutoa mwanga na dira wa tasnia ya Wizara kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, leo naomba kuchangia Wizara hii kwenye mambo mawili ya msingi ambayo ni Habari na Vijana.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari ni taasisi yenye nguvu. Vina uwezo mkubwa wa kujenga na vilevile kubomoa iwapo vikitumiwa vibaya. Hivyo basi vyombo vya habari vina wajibu wa kufanya kazi kwa kuzingatia umakini na kufuata kanuni za nchi yetu vizuri na sio kama sasa kwa vyombo binafsi kujali biashara zao zaidi.

Mheshimiwa Spika, ipo haja tena ya haraka Serikali kutunga Sheria mpya zinazoendana na wakati huu tulio nao na kufuatilia kwa karibu magazeti ya Serikali na Binafsi na machapisho mengine kuangalia (*contents*) maudhui yake. Nimesema haya kwa sababu ukiangalia vyombo vyetu vya habari vimepoteza uhalisia na baadhi ya lugha inayotumika iwe sahihi ili isipotoze maana nzima ya kupashana habari na kukuza lugha sanifu ya Kiswahili. Baadhi ya vyombo vya habari vimkuwa vikitumia lugha isiyo rasmi na yenye kuleta mkanganyiko miongoni mwa jamii kwani ni chombo kinachotegemewa na jamii katika kupashana habari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri yalijyopo katika Wizara yetu juu ya mikakati ya kuleta maendeleo kwa vijana, suala la kuwepo kwa Benki ya Vijana italeta heshima kwa nchi yetu na Serikali yetu kwa ujumla. Asilimia 50 ya Watanzania ni vijana. Ipo haja ya kuweka mipango madhubuti kwa Serikali yetu ili kupunguza walau kwa sehemu matatizo ya vijana waliopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalazimika kuitia Wizara hii kuweka mikakati na mipango mizuri ya kuondosha matatizo ya vijana. Huu mchakato wa Benki ya Vijana uharakishwe mara moja kwani utasaidia walau kidogo kupunguza na kuwajengea vijana uwezo wa kukopa katika vikundi ili kuweza kuijendeleza kimaisha kwa kuwa wajasiriamali wa shughuli mbalimbali na wengine wanaweza kutumia mikopo hiyo kuijendeleza kielimu. Mpango huu utawezesha kupunguza kwa sehemu tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, tatizo la vijana na ajira kwa sasa limekuwa tatizo sugu kwa nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla pamoja na dunia nzima. Wizara hii inatakiwa kuwa nguzo na mkombozi mkubwa wa vijana kwa malengo yao yajao. Naungana na vijana wa Tanzania kuwa tatizo la ajira kwa vijana ni tatizo lisiloweza kumalizika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hawahawa vijana, tumeshuhudia kuwa wengi wao ni wasanii wa sanaa mbalimbali kama muziki na maigizo. Naomba kuweka mkazo juu ya hatimiliki zao kama wasanii ili kulinda maslahi na jasho la kazi zao. Kuna haja ya kuipa meno zaidi COSOTA ili iwe huru na kuweza kuijendesha chini ya Wizara ya Habari kwani ndiko kazi kubwa ya kushughulikia kazi za wasanii iliko tofauti na sasa ilivyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Wizara ijitahidi kulinda kazi zao kwani kwa kufanya hivyo tutakuza uchumi wao binafsi na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia haitoshi kusikia watu wamekamatwa na kazi *fake* za wasanii, wameachiwa au kulipishwa faini. Ni lazima adhabu kali zitolewe ili iwe fundisho kwa wengine wenye adhima na nia ya kuwaibia wasanii kazi zao. Kuwepo na uboreshwaji wa Sheria ya Wizara hii ili kuwe na adhabu kali zaidi ya vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali na Wizara husika kuweza kuwasilisha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999 ili ifanyiwe marekebisho na kutekelezwa kwa faida ya wadau wa sekta ya sanaa na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima anaotujalia. Nikushukuru wewe binafsi kwa nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri na taarifa ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai yangu kwa vyombo vya habari, *television* zote, Waandishi kuitia magazeti yote, Wahariri na Wamiliki wa vyombo hivyo kuwa wanayo dhamana kubwa ya kuhakikisha maendeleo, amani ya nchi inakuwepo kwa ajili ya ustawi wa Watanzania. Vyombo vya habari visifanye kazi kwa upendeleo wa Chama fulani na kuacha Chama fulani bila kukzungumzia kwa mfano vyombo vingi hasa magazeti yamekuwa yanakipendelea CHADEMA kwa kiwango kikubwa huku Vyama vingine haviguswi kabisa.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vimekuwa vikitangaza hasa matukio ambayo si ya maendeleo badala yake "failures" tu kwa mfano matukio kama ya majambazi, moto, maangamizi na kadhalika na si mambo ya maendeleo kama vile Kilimo Kwanza, Kilimo cha Tumbaku, barabara nyingi na madaraja makubwamakubwa yanayaoendelea kujengwa na kadhalika. Vyombo vya habari hasa Tanzania Bara vilige mfano mzuri wa wenzao wa Tanzania Visiwani wameweka kipaumbele cha kutangaza habari za maendeleo yale yasiyo ya maendeleo ni machache.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai yangu kwa Serikali kuwa Watanzania tudumishe utamaduni wetu wa Tanzania hasa katika lugha ya Kiswahili fasaha kitumike na mavazi yanayoimarisha heshima ya Mtanzania yavalive. Ukilinganisha na miaka ya nyuma na sasa ngoma za utamaduni kwa makabila yote nchini zimekuwa hazitumbuizi sana katika maazimisho mbalimbali ya sherehe za Kitaifa hivi sasa muziki tu wa kizazi kipyra ndio unaotumika. Naiomba Serikali kuititia Wizara yenyewe dhamana isimamie kufufuliwa kwa ngoma za utamaduni wa Mtanzania, kila kabilia la Tanzania Bara na Visiwani lina ngoma zake za kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, michezo nchini imeanza kudorora, michezo ambao sasa umezingatiwa ni mpira wa miguu tu na katika hili ni timu za Simba na Yanga tu ndio zinatiliwa maanani ikifuatiwa na timu ya Taifa Stars. Umepotelea wapi ule mpango mzuri uliokuwa umeanza wa kushindanisha timu za Mikoani hadi kupatikana mshindi Kitaifa? Utaratibu huu ni mzuri maana unaibua vipaji kwa kizazi hiki na kijacho. Mpango ufufuliwe, utumike sana, uimarishwe, wapatikane wachezaji hodari ambao watakuwa wana-replace wale wanaong'atuka Simba, Yanga na Taifa Stars. Pia michezo mingine kama vile riadha, *netball, cycling, motorcar, safari rallies*, michezo mbalimbali mashulenii na hata mitaani izingatiwe.

Mheshimiwa Spika, vijana, *let us recruit the youth's* katika nyanja zote na katika mambo yote yanayohusiana na kazi, kilimo na maendeleo ya Taifa hili. Tuwashirikishe katika mambo mbalimbali, vijana ndio mambo yote, ndio wa kulifanya Taifa hili lisonge mbele kwa maendeleo. Vijana waenziwe na wale wanaopoteza mwelekeo warejeshwe kwenye mstari lakini vijana na wawaheshimu wazee kwani ndio kisima cha kuchota yote mazuri, hekima na busara.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Spika, Waandishi wa Habari na vyombo vya habari, ni suala muhimu sana katika nchi yetu lakini Waandishi wa Habari ni watu wabaya sana pale wanapopotosha habari kwa ajili ya utashi wao au kuelekea upande zaidi wanaouhitaji. Naiomba Wizara hii wawape mafunzo ya mara kwa mara ili wasiwe na uelekevu wa sehemu fulani au Chama fulani kwani wao wajijue kuwa ni Wanahabari wa nchi nzima na wasijikite upande mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, wasanii hawatendewi haki kutokana na hatimiliki, wao wanajitahidi kutengeneza mambo mbalimbali kama michezo ya kuigiza na kadhalika, lakini mafao mengi wanapata wanaouza kuliko wao wenye kuandaa. Naomba sana Wizara ifuatilie sana suala hili na pindi ikibainika dhuluma hiyo adhabu kali ya kisheria ishike mkondo wake ili iwe funzo kwa wengine wanaopenda kufaidika kwa migogo ya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, jengo la *TBC* litafutiwe ufumbuzi unaofaa kwa sababu ni muda mrefu sana liko vile na haipendezi kwa sababu *NSSF* wako tayari ila wanasubiri makubaliano na Serikali tu. Naiomba Serikali itekeleze hilo ili *NSSF* waendelee na utaratibu walioupanga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu bado inasuasua kufanya vizuri katika michezo ya riadha, mpira wa miguu na kadhalika. Tatizo ni maandalizi hafifu yanayotokana na uchache wa fedha. Naishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuwekeza katika michezo mbalimbali na ni vyema Serikali kuangalia kuwekeza katika michezo mingine ili tuweze kushiriki na kuwa na uhakika wa kushinda.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kupungua kwa maadili kwa vijana linaendelea kukua siku hadi siku na inaonekana kwamba vyombo vya habari baadhi ya vipindi vyake kwenye *TV* au kwenye magazeti yanachochea mmomonyoko wa maadili. Naiomba Serikali iwaeleze Watanzania ukomo, mipaka ya mavazi kwa wanenguaji wetu ambaao wanaonekana wakiwa nusu uchi, ni kero kubwa kwa familia katika nyumba wanapoangalia *TV*. Pia baadhi ya magazeti hayana mipaka ya kupima madhara ya picha wanazotoa kwenye magazeti hayo, hivyo, naishauri Serikali kuititia upya Sheria ya wanasanaa mbalimbali ikiwemo kuelewa mipaka ya Waandishi kutoa habari.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kero kwa wanamichezo kwa Serikali kutokuwaenzi kimaisha baada ya kustaafu, michezo mbalimbali hata kama waliletea sifa nchi hii na kuleta heshima kubwa ya kupata medali mbalimbali. Hivyo naishauri Serikali kufanya tathmini ya kuwatambua wanamichezo hawa walioletea sifa nchi hii na kuwasaidia kimaisha, Maveterani katika michezo.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Baada ya kuunga mkono naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana, Waziri, pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo matatu.

Mheshimiwa Spika, nianze na Vyombo vya Habari. Kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana katika Vyombo vya Habari na inasadikiwa baadhi ya Vyombo vya Habari vinaonekana, kufanya au kuandika habari kwa ajili ya maslahi ya kundi fulani, au Vyombo vya Habari vimikuwa vikitangaza kuititia *Television* au kuititia *Radio* taarifa za kundi fulani, cha kusikitisha mara nyangi umma wa Watanzania wameanza kuamini kuhusu hizo taarifa zinazoandikwa au zinazotangazwa na taasisi hizo na Serikali inakaa kimya.

Mheshimiwa Spika, huo ni upotoshaji mkubwa na unaharibu kabisa sifa za Vyombo vya Habari. Mheshimiwa Spika, naomba nipate kauli ya Serikali, itaendelea kukaa kimya katika eneo hili mpaka lini. Nataka kusikia kauli ya Serikali kukemea sana taasisi za habari ambazo zinafanya kazi ya maslahi binafsi badala ya maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali kuandaa vijana kwa lengo la kukuza vipaji vyao katika eneo la Michezo, hususan soka, riadha, ndondi, *netball*, *volleyball*, *basketball* na kadhalika bado dhana hii iko chini na cha kusikitisha zaidi tunazidi kushuka katika madaraja ya kimichezo kila kukicha, hususan katika michezo ya mpira wa miguu (soka), riadha, ndondi na kadhalika lakini jambo nillojifunza, kila siku Tanzania huwa kichwa cha mwendawazimu cha kujifunzia, kunyoa. Je, ni lini Serikali itakusudia kwa dhati kuboresha katika maeneo haya kwa kuajiri, walimu wazuri wenye uwezo katika maeneo haya? Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kusudi maandalizi yafanyike kwa uhakika. Je, ni lini Serikali itaboresha maeneo ya viwanja kwa maeneo husika kwa lengo la kuviwezesha vizazi vipyta vijifunze kwa uhakika? Je, ni lini Serikali itasaidia wapatikane viongozi bora wanaongoza hizi taasisi za michezo ambao wanatumia muda mwingi kushughulika na malumbano na ugomvi katika taasisi, hivi badala ya kushughulika na sera ya kuendeleza maeneo wanayoyaongoza?

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ninalotaka kuchangia kwa pamoja ni jinsi vijana na Maofisa Utamaduni walivopuuuzwa. Zamani vijana walikuwa wanashirikishwa katika mambo mengi ya msingi na hususan michezo na vijana walikuwa na uhakika wa maisha yao, kila kijana aliyepata nafasi ya kwenda shule alikuwa na uhakika kuwa atapata ajira, lakini sio sasa na Serikali bado hajatengeneza utaratibu wa uhakika wa kusaidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Utamaduni, wamesahaulika kabisa, kwa sababu hii wamesahau wajibu wao. Sasa hivi utamaduni wa Mtanzania hauthaminiki kabisa, hili tuliliona juzi tarehe 29 Juni, 2011 hadi tarehe 2 Julai, 2011 nilipokuwa Arusha kwenye Mkutano wa *East African Community* Watanzania walishindwa kabisa kuleta kikundi cha utamaduni wakati nchi nyingine zote zililetu. Hii ilikuwa ni aibu kubwa sana kwetu ukichukulia Mkutano huu ulifanyika katika ardhi yetu, lakini cha kusikitisha sana vikundi viliviyotoka Rwanda, Uganda, Kenya, Burundi viliteka Mkutano ule na sisi tukaonekana wageni katika nchi yetu. Naomba Serikali itoe tamko kwani tulidhalilika kiasi kile kwa nini wahusika wasichukuliwe hatua kwa kudhalilisha kiasi kile. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igulala, Wilaya ya Uyui, Mkoani Tabora limemaliza Mashindano ya Mpira wa Miguu Kata zote kumi. Mfutakamba Igulala *Super League Cup* na kupata washindi wa kwanza mpaka wa nne:-

- (a) Kata ya Igulala;
- (b) Kata ya Loya;
- (c) Kata ya Kizengi; na
- (d) Kata ya Nsololo.

Tumbaini vipaji kwa vijana 20 ambao tunawaombea, Wizara iwasaidie wakafanyiwe majaribio Timu (b) za Yanga *Sports Club*, Simba *Sports Club*, Azam *Football Club*, Mtibwa *Sports Club*, RUVU *Shooting Star* na kwingineko ili baadaye waende timu (a) na baadaye Kimataifa. Nawasilisha.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa kwa kuiongoza vema Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unahusu *TBC*. Inatakiwa kuimariswa maana ndiyo chombo pekee kinachotegemewa na wananchi kupata habari. Majengo yao ya Nyerere *Road*, Jengo la Utangazaji au Utawala limechoka sana. Majengo ya Ghorofa pale Mikocheni, Dar es Salaam ni magofu, Serikali inusuru hali hii.

Mheshimiwa Spika, tija kwa wafanyakazi wa *TBC*. Kazi yao ni kubwa, ujira mdogo. Naomba maslahi yao yaangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Lugha ya Kiswahili, watangazaji wengine hawana weledi wa Kiswahili fasaha, wanachanganya lugha pamoja na maneno, wapelekwe shule.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muziki, *TBC* isisitize muziki wenye nembo ya Kitanzania. Nyimbo nyingi sasa ni za kuigwa nje ila maneno ya Kiswahili. Midundo, mikogo sio, ni ya nje. Wasanii wetu wawezeshwe katika elimu, TASUBA itumike katika hiyo elimu ya muziki.

Mheshimiwa Spika, Muziki wa Dansi umedorora kwa vile Redio na *TBC TV* wameitosha, walinde muziki huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu ya kushauri ni:-

Kwanza, michezo. Eneo hili ni muhimu sana kwa Maendeleo ya Vijana na kwa kiasi fulani wazee. Linalosikitisha ni kwamba pamoja na juhudu kubwa ya Serikali kuboresha michezo bado nchi yetu inaonekana haipigi hatua ya kuridhisha. Je kuna tatizo gani? Michezo ni Furaha, Michezo ni Afya na Michezo ni Umoja.

Naomba Serikali isiiache *TFF*, mamlaka yote ya kusimamia michezo bila kutupiwa macho. Sera na mipango yote ya maendeleo ya Michezo iwe ni kazi ya kudumu ya Wizara, bila kuona haya wala huruma kwa wale ambao hawaitakii heri Sekta ya Michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, utunzaji wa maeneo ya kihistoria. Moja ya vivutio muhimu kwa watalii kote duniani ni maeneo ya kihistoria. Wilaya ya Lushoto (Usambara) ni moja ya maeneo yenye kumbukumbu muhimu za nchi yetu hususan kuhusu historia ya Wajerumani nchini Tanzania (Tanganyika), kwa leo kuna idadi kubwa ya watalii kutoka Ujerumani ambao wanatembelea maeneo ya milima ya Usambara.

Mheshimiwa Spika, nashauri historia hii itunzwe sana. Maeneo ya kihistoria yahifadhiwe mfano, Boma la Lushoto na kadhalika. Yako maandiko mengi kuhusu Usambara au madini yaliyoko Tanzania (Tanganyika) maandiko au nyaraka nyingi ziko Ujerumani au Uingereza. Naomba nyaraka hizo zitafutwe na kurejeshwa nchini kwa kuhifadhiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, tatu, Utumishi. Wizara ijitätidi kurejesha hadhi ya Maafisa Utamaduni na wapewe nyenzo za kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MONDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iboreshe utamaduni wetu wa Kiafrika ambao kwa nchi yetu unaweza kutoweka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iwe na mikakati ya makusudi ya kusaidia Wasanii wetu wasilbiwe kazi zao. Kwa sasa kuna mtu kajitolea kufanya kazi hiyo, kukamata wezi wa sanaa. Je, Serikali ina mpango gani wa kumpa mtu huyo ushirikiano? Naomba Wizara impe mtu huyo ushirikiano wa hali ya juu ili vijana wetu wanaoimba na kutoa filamu wapate faida.

Mheshimiwa Spika, Serikali itambue hizi ni ajira zao, wanaishi kwa kazi hizo, wanajajiri na wanaendeleza familia zao, ni lazima sasa kwa makusudi kazi hii tuifanye. Pia itainua uchumi wetu kwa kuwa watu hawa watalipa kodi. Naamini wakuza kihalali *CD, DVD* zao na kadhalika wataongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja yako ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Wizara kwa hatua nzuri waliyofikia juu ya Chuo cha Malya cha Michezo. Kwa kuwa hakuna Chuo chochote Kikuu cha Michezo katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Napenda kushauri Chuo hicho sasa kifanywe kuwa Chuo Kikuu cha Michezo. Kwani michezo sasa inahitaji elimu zaidi kuliko mazoweya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ligi kuu, Uwanja wa Taifa. Uwanja wa Taifa unaanza kupoteza maana yake kwani itafika mahali timu zitashindwa kuutumia kutokana na ghamama kubwa zinazotozwa na mamlaka ya uwanja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu riadha, naomba msukumo uwekwe katika timu za mashule na timu za majeshi. Kwani huko ndio kwenye vijana wanaoweza kuleta heshima ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Habari ihmizwe kuandaa *Code of Ethics* ili kudhibiti habari zisizo za kweli, habari za uchochezi na *character assassination* kwa viongozi (baadhi) zifanywazo na baadhi ya Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru wetu kama Taifa, Wizara iandae programme ya kuelezea Tunu Zetu kwa umma ili vijana wafahamu kwa kina *system of values* yetu.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni Baraza la Sanaa. Hapa nchini kuna wachoraji wazuri sana wajulikanao kama Tingatinga. Picha zao ni picha ambazo huvutia sana watalii na huuzwa kwa bei ya juu sana. Swali, je, ni kweli Kampuni kutoka *Disney USA* walikuwa Tanzania na kuwatumia

Wasanii wetu na kuondoka nchini bila kuwalipa haki zao? Je, kama Serikali inalijua hili inachukua hatua gani kwasaidia vijana hawa?

Mheshimiwa Spika, pili, miradi ya Vijana enzi za Chama kimoja kabla ya kuingia kwa vyama vingi palikuwepo na miradi ya vijana, kwa mfano, mradi wa kilimo kule Bagamoyo. Nina maswali yafuatayo: Je, bado mradi ule upo? Kama upo unamilikiwa na vijana gani? Je, ni lini Baraza la Vijana Taifa litaanzishwa rasmi?

Mheshimiwa Spika, tatu, ni utamaduni. Pamekuwepo na utamaduni wa aina tofauti katika nchi yetu. Naamini kabisa tukiwa tunawathamini Wazungu wa kale, kwa mfano, Mkoani Kigoma, pale alikopita *Livingstone* bado kumbukumbu ipo lakini sisi tulikuwa na Machifu. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuanza kuweka kumbukumbu kwa ajili ya machifu wetu ili kuenzi juhudii zao katika nchi hii?

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuhusu michezo. Viwanja vya michezo vingi vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi na vingine vimeuzwa kuwa masoko. Wote tunajua michezo ni afya na tunahimiza michezo, hivi michezo hii itachezewa wapi? Ni jukumu la Serikali yaani TAMISEMI na Wizara hii kuhakikisha viwanja hivi vinatumika kama viliviyokusudiwa na virudishwe kwenye Halmashauri husika ili kuzipatia Halmashauri hizo mapato.

Mheshimiwa Spika, tano, ni matumizi ya Lugha ya Kiswahili. Bunge ni chombo cha Wawakilishi wa wananchi na wananchi wengi wa Tanzania lugha tunayoitumia ni Kiswahili. Lakini Miswada yote inayoletwa Bungeni huandikwa kwa Kiingereza. Tunajua kabisa *information is power halafu Ignorance of the law is not defence* na sheria iliyopo ni English.

Mheshimiwa Spika, ni kwa jinsi gani Baraza la Kiswahili limetumika kuendeleza Kiswahili na kwa nini wasipewe jukumu la kutafsiri sheria zote kwa Kiswahili? Ni mchango wa Baraza hili la Kiswahili?

Mheshimiwa Spika, sita, ni kuhusu mila na desturi. Pamekuwepo na upoteaji wa mila na desturi zetu unakuta vijana wanavaa vibaya sana wengine kusahau kabisa mila zetu. Pamoja na Kiswahili kuntuunganisha kama Watanzania sio vibaya kuendeleza lugha zetu za kiasili, *our mother tongue* ili mila zetu zisipotee ikiwa ni pamoja na uasili wetu. Hii haiwezi kuleta ukabila hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ni kitu gani kinachochelewesha kuletwa kwa Muswada wa Habari hapa Bungeni? Je, kuna tatizo gani? Lazima zifanywe juhudii za makusudi uletwe ili waandishi wa habari waweze kuwa na sheria inayowalinda.

Mheshimiwa Spika, saba ni kuhusu vazi la Taifa ni lini mchakato wa kukamilisha vazi la Taifa utakamilika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni majengo ya Historia. Ni jambo la kusikitisha Jengo la Kihistoria kama lile la Mahakama ya Rufaa wanaliuza. Je, ni majengo mangapi yaliyokuwa yanalindwa yakabadilishwa na kuuzwa?

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya.

Mheshimiwa Spika, Bado *TBC* haisikiki vizuri Mkoa wa Singida hususan Jimbo la Manyoni Magharibi. Maeneo karibu yote wananchi wanategemea Radio Mwangaza kwa taarifa na matangazo muhimu. Naiomba Wizara iwasiliane na watumishi warekebishe hali hii. Si vema kwa wananchi kutopata habari za moja kwa moja kutoka chombo cha habari cha Taifa, *TBC*.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha BANGO si kibaya, kinatukumbusha juu ya wapendwa wetu waliotangulia mbele za haki na pia kinatukumbusha na sisi kuwa tayari kwa kifo. Lakini inapokuwa kila siku tunakuwa na kipindi cha majonzi hapo sasa si kumbukumbu tena bali kero ya simanzi

inazidi na kutufanya tusielewe kwamba (*life has to go on*), maisha ni lazima yaendelee na shughuli za kila siku lazima tuzifanye kwa nguvu tusonge mbele. Kumbukumbu za aina hiyo yatolewe kwenye magazeti na pale inapotokea msiba umetokea.

Mheshimiwa Spika, Pia sherehe za harusi zinazoonyeshwa kila siku kwenye *TV* nazo zinawafanya wengine kupanga sherehe kubwa za ushindani na za kifahari badala kuchangia kwenye shughuli za maendeleo ya familia. Matangazo mengi yatolewe katika magazeti ambayo ni mengi sana na *TV* ibakie zaidi na mambo muhimu ya maendeleo na habari za Kitaifa na matukio muhimu. Ku-commercialize kila siku vitatupa vipindi visivyo na tija katika kuhamasisha maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa pongezi kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu ngoma, Wilaya ya Mbinga ni maarufu sana kwa ngoma nyingi sana, chache ni kama zifuatazo: Mhambo, Mganda, Lizombe na Chihoda. Ngoma hizi zinapingwa na kuchewza kwa umahiri.

Mheshimiwa Spika, tatu, changamoto, ngoma hizi zinaanza kupotea lakini pia Wasanii hawa hawafaidiki kimapato zaidi ya kuombwa kuburudisha viongozi na pengine Mwenge.

Pendekezo, Wizara itusaidie kuchukua picha au filamu na kutengeneza *CD (video)* ili Wasanii hawa waone umuhimu wa kazi zao. Nitafurahi kupata maelekezo ya Serikali jinsi tutakavyosaidiana.

Mheshimiwa Spika, zipo sanaa za mikono kama visonjo ambazo sasa zinaelekeea kupotea ikizingatiwa kwamba wasusi ni wanawake wazee.

Mheshimiwa Spika, natoa pendekezo, naweza kushirikiana na Halmashauri kuwa na vikundi na naomba Serikali iandae semina au mafunzo kupitia pengine muziki wa utamaduni.

Mheshimiwa Spika, Mbinga *Youth Centre* vijana ndio Taifa la kesho, wanahitaji habari. Vijana wa Mbinga wanacho kiwanja na wameanza ujenzi ili awe na kituo chao ambacho kila kijana kutoka kijiji akifika Mbinga aende kwanza kwenye kituo chake ili aonane na wenzake, lakini pia kupata taarifa mbalimbali. Naomba nguvu za Serikali katika kuwatia moyo hawa vijana.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji husika kwa kuandaa bajeti nzuri na kuiwasilisha vizuri. Nawapongeza kwa kuendesha Wizara vizuri na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Wizara na vyombo vyake kwa kusaidia kufanikisha maonyesho ya "Siku ya Mnyambo" yaliyofanyika Makumbusho. Mheshimiwa Waziri aliungana nasi na utawala wa Makumbusho ulikuwa wa msaada mkubwa. Naomba waendelee hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo. Nashauri kuwa msisitizo uwekwe kwenye michezo mingine na siyo mpira peke yake (mpira wa miguu). Tunafarijika michezo mashuleneni imeanza tena, itiliwe mkazo, lakini bila ya kuathiri masomo na maadili.

Mheshimiwa Spika, tuangularie maadili ya vijana wetu, tuwaelimishe hasa juu ya *HIV* na madawa ya kulevyta. Kuwe na semina na matangazo juu ya masuala haya tuki-highlight madhara yake. Nyakati za mikusanyiko kama michezo, sanaa na kadhalika, haya masuala yatangazwe sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna ya kuanzisha mfumo wa kudhibiti na kuchuja (*filtration*) matangazo na habari mbalimbali hasa zenye upotoshaji katika jamii. Yaani uhuru wa habari uwe na mipaka pia.

Mheshimiwa Spika, vijana waelimishwe na wapewe taarifa za mikopo mbalimbali na namna inavyopatikana na pia waelekezwe namna ya kuandika *proposals* ili waweze kupata mikopo hiyo kirahisi na pia waweze kupambana na umaskini hasa vijana wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, ni lini ufungaji wa mitambo ya *TBC FM* na *TBC Taifa* utakamilika na lini matangazo yataanza kurushwa Mpanda?

Mheshimiwa Spika, Serikali ijikite sasa katika kuangalia kuwekeza katika mchezo mmoja ambao utakuwa kama kitambulisho cha Taifa na hivyo kulipatia Taifa pato la kigeni kwa mfano, riadha (Jamaica), Kenya USA (*BasketBall*).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kwa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro wa Shirikisho la Wasanii wa Filamu na Bongo *Movie*. Hivi sasa kumetokea mgogoro wa Shirikisho la Wasanii wa Filamu na kundi lingine la Wasanii wa Filamu (*Bongo Movies*). Makundi haya mawili yamehasiana na kila kundi lina kiongozi wake mathalani Shirikisho la Wasanii wa Filamu linaongozwa na Simon Mwakifamba na Kundu la Bongo *Movie* linaongozwa na Hartman Mbilinyi. Mgogoro huu umefikia hatua mbaya na hivi karibuni ilitokea hali ya sintofahamu na kupeleka Polisi wa kutuliza ghasia kuingilia kati. Tukio hili ilitokea *Leaders Club*. Naomba wakati wa kuhitimisha Waziri alitolee ufanuzi kwani mgawanyiko huu hauwasaidii Wasanii bali utatoa mwanya kwa wafanyabiashara kuwagawa Wasanii na kuwanyonya Wasanii kupitia kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuibua Vipaji vya Wasanii, Wanamichezo vijijini. Wizara iandae utaratibu wa kuibua vipaji vya Wasanii wa michezo mbalimbali vijijini. Hivi sasa Wizara kuitia Ofisi za Utamaduni, Wilaya hawajawezeshwa kufika vijijini. Kuna umuhimu wa kuweka programu ya makusudi kuwafikia Wasanii vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie suala hili, wapo vijana wengi vijijini wenye vipaji, lakini hakuna wa kuwaona na kuwasaidia kufikia malengo yao ya kisanii na michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongezea fedha Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*). Hiki ndiyo chombo cha Serikali kutoptaka na ushindani uliopo na utandawazi ni muda muafaka sasa Serikali kulisaidia shirika hili fedha za kutosha kukabiliana na changamoto.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri pamoja na timu yake, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufanuzi kwa nini *TBC1* ambayo ni chombo cha Taifa kinarusha vipindi ambavyo kwa kiasi kikubwa vinalenga kulidhalilisha Taifa na Serikali. Napenda kufahamu Kipindi cha "Huku ndo Kwetu" kinalenga hasa kufundisha nini au kutoa picha gani kwa wanaokiona hasa nje ya nchi ukizingatia kuwa *TBC1* inapatikana kwenye *DSTV*. Hivi *TBC1*

wanafahamu kuwa kipindi hicho kinaidhalilisha nchi nje ya mipaka na kama wanafahamu mnalifurahia hili na ni kwa faida gani.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu ni lazima *TBC1* kurusha vipindi nya Haki Elimu ambavyo siku zote kazi yake ni kudhalilisha Serikali, ina maana *TBC1* ilianzishwa kwa lengo la kudhalilisha Serikali, ina maana bila matangazo ya Haki Elimu *TBC1* itashindwa kujidhesha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijiji tumechoka kuona makala zenu (*TBC1*) za suala la mimba Mtwara Vijiji nendeni mikoa mingine na muanze kurusha Makala za Ukeketaji kwani ndio suala linalodhalilisha wanawake Tanzania kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuchangia bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa bajeti hii kwa utaalam mkubwa ikizingatia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasisitiza ubora wa hali ya habari ili kuendana na maendeleo yanayotokea duniani kila leo ikiwa ni nia pamoja na utawala bora katika uhuru wa habari. Kuandaa mipango mizuri ya kuwawezesha vijana kielimu, kimaadili, na kuwajengea uwezo wa kushiriki katika kupambana na umaskini. Kukuza na kuimarisha fani mbalimbali za utamaduni. Pamoja na kuhamasisha wananchi kushiriki katika michezo mbalimbali jambo ambalo linaimarisha afya zao.

Mheshimiwa Spika, maendeleo katika Sekta ya Habari pamoja na Uhuru wa Habari ni mambo ambayo nchi yetu imefanikiwa sana na tumepata sifa ya kuwa na utawala bora katika sekta hii.

Pamoja na sifa hii lakini tukumbuke kwamba sumu ya habari ni kali sana na kwamba uhuru huu ukitumika vizuri unaweza ukaleta maendeleo makubwa hivyo hivyo ukitumia vibaya unaweza ukadidimiza nchi pamoja na watu wake. Siku za karibuni kumekuwepo na tabia za Vyombo nya Habari pamoja na kundi la watu wanaoijiwa wanaharakati kutangaza habari za kila tukio baya linalotokea hapa nchini kwa kuzidisha chumvi hata kama jambo lenyewe limetokea kwa bahati mbaya au linafanywa uchunguzi wa kujuu kiini chake.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivi havijengi nchi bali vinapunguza sana sifa na kuathiri mahusiano na hasa ya misaada au watalii na wawekezaji kutoka nchi za nje wanaoingiza pesa za kigeni. Kumekuwepo pia na magazeti mengi ya kila aina na kila maandishi ambayo kazi yake ni kutoa habari za maisha ya watu binafsi kwa malengo mazuri lakini mengi yakiwa ni malengo ya kuwachafulia sifa zao au kuweka katika mashinikizo ya kutokuwa huru katika jamii. Tatizo hili ni kubwa na linachangia sana kupunguza maadili mema katika jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna sheria inayosimamia Vyombo nya Habari, lakini bado kuna matatizo makubwa ambayo yanawadhalilisha sana watu na si watu tu bali kuna kundi la watu amba wana nyadhifa mbalimbali ndio wanaolengwa. Aidha, mabinti zetu nao wamekuwa chambo cha kuchafuliwa na kuzuliwa kashfa mbalimbali katika magazeti na tovuti. Imefikia wakati wananchi wanajiuliza kweli mabinti hawa wanakutwa katika hali hiyo kwa ajili yao au wamewekewa mitego ili wadhalilishwe? Nashauri Serikali ikazie sheria ya kuwataka wamiliki wa Vyombo nya Habari na wanahabari kuheshimu fani yao na kuelekeza habari wanazozitoa katika mambo muhimu yatakayowaletea wananchi faida kama kutoa elimu kuhusu matokeo muhimu duniani yanayoweza kukuza uchumi na maendeleo ya nchi yetu na si kujikita katika kutoa habari za kuwachafua watu ili vyombo vyao ipate faida ya kuuza habari hizo.

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa ya vijana ni ukosefu wa ajira, mafunzo ya stadi mbalimbali yakiwemo ya ujasiriamali na mahitaji makubwa ya kuwepo na mipango ya kuwawezesha kukopesheka ili washiriki kikamilifu katika kuondoa umaskini. Napenda nichukue fursa hii kwa moyo kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi

kwa juhudu kubwa waliyofanya katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ya kujenga shule ya Sekondari angalau moja kwa kila Kata. Hili ni jambo la kuenziwa kwani limetoa fursa ya kuelimisha vijana wengi kupata elimu ya sekondari. Changamoto kubwa iliyobaki ni jinsi gani vijana waliopata elimu hii wanaweza kutumika kuchangia pato la Taifa, ukizingatia kuna wimbi kubwa la ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wamejingiza katika vitendo vya maadili potofu kama kutumia madawa ya kulevyaa, ujambazi na uzururaji si kwa kupenda bali wamekata tamaa ya maisha. Ni jambo la kawaida kabisa kwa vijana ambaao ni nguvu kazi ya Taifa kuondoka vijijini na kuhamia mijini wakifirkiria wanaweza kupata maisha bora. Hali ya umaskini na hasa vijijini inachangia vijana kuhamia mijini kwa sababu shughuli nyingi za kilimo na ufugaji hazileti tija na hivyo kuchangia hali ya maisha kuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya hali ya hewa (*Global Climate Change*), nayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kusababisha ukosefu wa mvua na ukame. Baa la njaa katika Mikoa mbalimbali hapa nchini, mfumuko wa bei, vita vinavyoendelea katika nchi za kaskazini mwa Afrika na Nchi cha Uarabuni na kupanda kwa kasi kubwa kwa bei ya Nishati ya Mafuta ya Petroli kumeongeza ugumu wa maisha hasa katika maeneo ya vijijini. Kutokana na hali hii, ili vijana wetu waweze kuendelea kuishi na kuwa nguvu kazi ya kuinua uchumi vijijini, ni lazima Serikali iwavezeshe kwa kuweka mipango na miradi mbadala itakayolenga kuinua pato lao waweze kuhimili changamoto za maisha ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kwa makusudi makubwa iboreshe mipango ya maendeleo ya vijana katika kukuza vipaji vyao mbalimbali, kuongeza na kuboresha vyuo vya mafunzo stadi (ikiwezekana kijengwe chuo cha ufundi stadi mbalimbali katika kila Kata) ili vijana wafundishwe stadi zitakazowawezesha kuajiriwa na kujajiri wenye. Serikali ianzishe Mfuko wa Maendeleo ya Vijana utakaoratibu shughuli za miradi ya maendeleo inayobuniwa na vijana na kuifadhili. Serikali pia iweke sheria ya viwanda na taasisi kuweza kuwapokea wanafunzi wa vyuo mbalimbali hapa nchini kwa mafunzo ya vitendo (*Practical Training*) ili wanapohitimu mafunzo yao waweze kuingia katika ushindani wa ajira wakiwa na uelewa wa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Taifa lisilokuwa na utamaduni wake ni kama lilitovia. Tanzania tunajivunia utajiri mkubwa wa utamaduni wa makabila mbalimbali ya nchi hii. Changamoto iliyopo ni jinsi ya kuendelea kuzihifadhi kwa kuimarisha fani mbalimbali zinazolezea tamaduni zetu kwa mfano, sanaa za kazi za mikono kama vinyago, mikeka, ngoma zetu za asili, nyimbo zenyenye maudhui na mafunzo mbalimbali ya jadi na nyiginezo nyingi. Hivi vyote ni alama za kielelezo cha nchi yetu. Tunazo mila nzuri sana katika kila makabila kama za kuwaandaa vijana kujua maadili mema katika maisha, ushujaa, kutunza siri na kujiamini. Pia tunayo makabila mengi yenye baadhi ya mila na desturi potofu ambaao zinaathiri maisha. Mila hizo ni kama ukeketaji, kurithiana, kuua watoto wanaozaliwa na ulemavu mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali pamoja na Asasi Zisizo za Kiserikali zimejitalidi sana kukabiliana na vitendo vya mila potofu katika jamii. Pamoja na juhudu hizo lakini bado kuna makabila mengine wamebuni mbinu na njia mbalimbali za siri zinazoendeleza mila hizo potofu. Napendekeza katika harakati za kutokomeza mila na desturi potofu, Serikali na asasi zisizo za kiserikali ziendelee kufanya utafiti na kutoa mafunzo zaidi kuelimisha jamii kuhusu athari za mila hizo kuititia Vyombo vya Habari, makongamano na mikutano mbalimbali ya Vyama vya Siasa, Taasisi za Dini, warsha, semina na katika mikusanyiko ya watu. Aidha, pale ambapo inagundulika kwamba vitendo hivi vimekithiri basi vyombo vya sheria vitumie kudhibiti vitendo vya mila na desturi zisizokubalika.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili ni moja ya kielelezo kikubwa cha utamaduni wa Tanzania. Lugha hii inapendwa sana na inawavutia watu wengi duniani kutaka kujifunza. Kinachoshangaza, Watanzania walio wengi hawaoni umuhimu wake na wala hawajivunii lugha hii. Nchi kama Korea, China, Japani, Ufaransa, Uturuki, Italiano, Nchi za Kiarabu, Ujeruman, Urusi na kadhalika. Wanajivunia sana lugha zao na hata kama wakienda kwenye mikutano ya Kimataifa wanatumia lugha zao. Kwa nini viongozi wetu ambaao ndio kioo cha jamii yetu na mfano mzuri wa kuongoza na kuigwa, wanapokwenda katika mikutano ya Kimataifa hawatumii lugha ya Kiswahili?

Mheshimiwa Spika, tunalo Baraza la Kiswahili BAKITA, hata wajitahidi vipi kuendeleza na kutoa mafunzo ya Kiswahili fasaha, kama watu hawatakuwa tayari kupenda, kujivunia na kutumia lugha ya Kiswahili kila wakati kama kielelezo cha utamaduni na lugha ya Taifa letu, kazi hii itakuwa bure. Serikali ifanye mikakati ya makusudi au kuweka sheria itakayohakikisha kwamba wananchi wanatumia lugha hii katika kila mikutano, makongamano, semina na kila penye mikusanyiko ya watu ili iweze kutambulika na kupewa heshima inayostahili Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, michezo ina faida nyingi sana kama kutunza afya zetu, mashindano ya Kitaifa na Kimataifa yanayovuta hisia za wapenzi na washabiki wengi. Vijana wetu wana vipaji vyta kucheza michezo mbalimbali. Wengi ambaao vipaji vyao vimeibuliwa wamejithadi sana kuiwakilisha nchi yetu kushiriki katika michezo ya Kimataifa na kuileteka nchi yetu sifa. Michezo inasaidia sana kutumia muda wa ziada au wa mapumziko kwa kucheza au kuangalia michezo hii. Inasemekana sehemu ambazo vijana wamevezeshwa kuwa na michezo ya mbio za magari, baiskeli na kadhalika, kumewasaidia sana kutumia muda wao katika kufanya mazoezi au mashindano na kukutana na watu mbalimbali ambaao wameweza kubadilishana mawazo. Michezo hii hii imewasaidia vijana kutumia muda wao vizuri na kupanga mambo ya maendeleo badala ya kukaalaa vijiweni kupanga uhalifu au kutumia madawa ya kulevyta na vitendo vya ukahaba. Kadhalika michezo imefanikisha kwa kiasi kutoa ajira ya hapa nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini tunalo tatizo kubwa la viwanja vya kufanya mazoezi ya michezo. Katika kupanga na kuchora ramani za mijji yetu, wataalam wetu wa maendeleo ya ardhi na makazi hawafikirii kutenga maeneo ya michezo kama huduma mojawapo muhimu kwa jamii. Aidha, katika sehemu zile ambazo ziliwahi kutengewa maeneo ya wazi kwa ajili ya kujenga viwanja vya michezo mbalimbali, kuna wajanja ambaao kwa kushirikiana na Maofisa wa Ardhi katika Halmashauri mbalimbali wamehujumu maeneo haya na tayari yamejengwa nyumba za kuishi au za biashara. Kweli ni fedheha kuona kwamba pamoja na utajiri mkubwa wa ardhi tulio nao, vijana wetu hawapati uhuru wa kukuza vipaji vyao kwa kukosa maeneo ya kufanya michezo. Nashauri Serikali iweke mikakati madhubuti ya kufuatilia maeneo haya kuhakikisha yanarudi mikononi mwa wananchi kwa malengo yaliyopangiwa awali hata kama waliovamia na kujenga nyumba hizo watapelekwa katika vyombo vya sheria kuhakikisha nyumba hizo zinabomolewa. Iwekwe sheria kwamba kila maeneo ya maendeleo ya makazi popote nchini yatakapokuwa yanachorwa ni lazima yatengwe maeneo ya viwanja vya michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha Tanzania ina uwanja wa kisasa wa mpira ambaao unakidhi viwango vya Kimataifa. Uwanja huu unatakiwa utunzwe na kuheshimiwa, hivyo, wanaousimamia uwanja ule wahakikishe hakuna wahuni ambaao watafanya vitendo vya kuuuhujumu kwa namna yoyote ile. Uwanja huu ni moja ya kivutio cha Taifa, napendekeza Halmashauri zishauriwe kutafuta wawekezaji wa kujenga uwanja kama huu katika kila Mkoa ili kuweza kuwa na nafasi zaidi ya kukaribisha wanamichezo kuja kutumia viwanja vyetu kwa malipo. Wachezaji hawa watakuja na washabiki na wapenzi wao na watapata fursa ya kutembelea katika sehemu za utalii na nchi itapata pesa za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kuna dhana kwamba michezo wa mpira wa miguu umewekewa kipaumbele zaidi kuliko michezo mingine hapa nchini. Nashauri kuna haja ya Serikali kuhamasisha na kuendelea, kukuza na kuibua vipaji vya michezo mbalimbali kwa vijana wetu ili michezo mingine ipate ari na msisimko wa kuwavutia washabiki na wapenzi wengi kama ilivyo kwa michezo wa mpira wa miguu. Serikali ihakikishe michezo ni moja kati ya masomo yatakayofundishwa mashulenii. Pia kipaumbele kiwe kwa michezo yote na si kwa michezo wa mpira wa miguu tu. Mikakati hii iende sambamba na kufundisha walimu na madaktari wa michezo mbalimbali hata ikibidi wapelekwe nchi za nje ili waweze kuja kuinua kiwango cha michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijiini ni Jimbo changa na lina maeneo makubwa sana ya ardhi na kwa Jilografia ni sehemu inayofikiwa kirahisi. Naiomba Serikali kwa makusudi kabisa watusaidie kutafuta wawekezaji au wafadhili katika fani ya michezo, kujenga viwanja vya michezo na vyuo vya michezo mbalimbali katika maeneo ya Mlandizi au Ruvu. Viwanja pamoja na vyuo hivi vitaleta maendeleo ya haraka kwani vitavutia watu wengi kuja kuwekeza katika shughuli mbalimbali za huduma ya jamii kama mahoteli, masoko, maduka na kadhalika. Maendeleo yatakayopatikana katika kujenga viwanja vya kisasa na vyuo hivi yatasaidia kutoa

ajira na kuongeza mzunguko wa pesa ambao utaondoa umaskini uliokithiri katika Jimbo la Kibaha Vijiji. Katika mambo ambayo Jimbo la Kibaha Vijiji limejaliwa ni pamoja na utajiri mkubwa wa utamaduni wa makabila mbalimbali yanayoishi katika Jimbo hili, Serikali iangalie uwezekano wa kujenga chuo cha kufanya tafiti za utamaduni wa makabila ya nchi yetu ili kuweka kumbukumbu za historia kwa vijana na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo inayofundisha maisha ya Mtanzania (Wakati huu Wizara hii inatakiwa iongezewe bajeti. Wanamichezo inakuwaje wanapendwa wakati wakishinda tu ndio wanaletwa Bungeni, lakini wakishindwa inakuwa lawama wakati hata bajeti yao ya michezo hamna. Je, watachukuaje mazoezi hadi wafike kiwango kama kimichezo.

Mheshimiwa Spika, waandishi hawatengewi fungu la kusomeshwa ili wawe wenye maadili.

Mheshimiwa Spika, waganga wa asili wanawasiliana na Wizara ipi kwani Wizara ya Afya wanafanya utafiti na kutoa vibali na utamaduni, wanatoa vitambulisho vya waganga na wakunga kwa nini wanayumbishwa tu Wizara moja itamke kuwa yenye we inahusika ili waganga wasisumbuliwe kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wasanii wanafananishwa na wahuni tu kwani hata mtu akikosea anaambiwa huyu si msanii tu, huu sio uungwana hata mara moja. Serikali inatakiwa iangalie viwanja vya michezo kama Tabora (Ali Hassan Mwinyi) Mwanza (Kirumba) Songea (Majimaji) Arusha (Shekhe Aman Abeid) viwanja vitengenezwe ili michezo iendelee na virekebishwe viwanja ili watu wasitegemee viwanja vya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ngoma za utamaduni zipo nyingi vijiji lakini haziangaliwi, tunaomba tuangalie ili nazo ziweze kujulikana katika Wilaya, Mikoa hadi Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kukupongeza na kukupa pole kwa majukumu mbalimbali ya Kitaifa. Nachangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, umuhimu wa Muswada wa Habari wadau mbalimbali walikaa na kujadili juu ya Muswada wa Habari na hata kuandaa Muswada huo. Je, Serikali italeta sera mpya na Muswada wa Habari lini?

Mheshimiwa Spika, pili, wahariri, waandishi na wamiliki wa Vyombo vya Habari. Napenda kupata majibu Serikali imeweka vigezo gani na inakagua kwa namna gani magazeti na Vyombo vya Habari vinakuwa huru na haviendeshwi kwa *influence* za wamiliki?

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu *TBC*. Napenda kujua ni lini mitambo ya *TBC* Radio na *TBC* Televisheni zitafika maeneo ya Pembezoni. Aidha, vyombo vingi vya Habari vinaripoti taarifa za baadhi ya maeneo. Je, lini Mitambo ya *TBC* itafika Kibondo? Pia Serikali ina mpango gani kuajiri waandishi kwenye kila Wilaya hususan Kibondo ambapo ni mbali sana na Kigoma Mjini?

Mheshimiwa Spika, nne, utamaduni na michezo. Napenda kupata majibu ya Wizara hii imeweka mkakati gani wa kubaini vipaji kuanzia ngazi ya Vijiji hadi Kitaifa? Pia napenda kupewa majibu katika utandawazi (*globalisation*), Serikali imejipanga vipi kudumisha na kuhakikisha utamaduni wetu haupotei? Je, sisi tunaathiri utandawazi au utandawazi umetuathiri na unaendelea kutuathiri? Je, tumejipanga vipi kuwa na sera itakayofanya tuathiri Mataifa mengine na sisi tunufaikie kiuchumi? Aidha, napenda kupata majibu, Serikali imetoea mwongozo wowote kwa Halmashauri zote nchini kutenga Bajeti zake kwa kuhusisha Idara ya Utamaduni?

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu vijana. Napenda kujua vijana wangapi katika nchi wana ajira na kivipi Wizara hii inahusika na kushirikiana na Wizara ya Ajira na kazi kujua vijana wangapi wana ajira na kujajiri kwa namna mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sita, ni kuhusu Taasisi za Kiswahili. Kuna taasisi mbalimbali za Kiswahili kama BAKITA na TUKI na kadhalika, napenda kupata majibu kwa nini taasisi hizi zisitafsiri vitabu vyote vya Kiingereza kuja Kiswahili ili wanafunzi wote nchini wasome kwa lugha hii kama sehemu ya utamaduni? Je, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, ubunifu na *Intellectual Property*. Napenda kujua tunapata hasara kiasi gani kwa watu wanaotengeneza kanda, *video*, *CDs*, *DVDs* za muziki na kadhalika bila idhini ya wamiliki? Je, watu au kampuni ngapi zimekamatwa?

Mheshimiwa Spika, napenda kupewa majibu hayo kabla ya kuunga mkono hoja hii.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kuunga mkono hoja ilioletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja naomba kuchangia kwenye baadhi ya maeneo kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokusikika kwa Redio ya Taifa (*TBC*) katika maeneo ya Mkao wa Rukwa na hususan katika Wilaya mpya ya Kalambo ambako usikivu wa *FM Radio* umekuwa wa tabu na hivyo kuwalazimu wananchi kukosa haki yao ya kikatiba ya kupashwa habari hususan mambo ya msingi yahusuyo nchi yao na kulazimika kusikiliza redio za nchi jirani za Zambia, Burundi na Malawi ambazo ndizo husikika bila tabu. Tatizo la usikivu hafifu ni kubwa zaidi katika maeneo ya mwambao mwa Ziwa Tanganyika hususan Vijiji vya Kasanga, Kipura, Kilewani, Somazi, Kipanga, Kisomba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia upatikanaji wa *television* umekuwa wa tabu kwa Mkao wa Rukwa hususan katika Wilaya mpya ya Kalambo na hasa ukizingatia kutokuwepo kwa nishati ya umeme kwa Wilaya mpya ya Kalambo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa habari kwa njia ya magazeti vijijini limekuwa ni tatizo kubwa kwa muda mrefu na hasa ukizingatia umuhimu wa chombo hiki katika kuelimisha, kuhabarisha na kutoa taswira.

Mheshimiwa Spika, Wizara hajafanya kazi kubwa kwa kuhakikisha vijana wanaandaliwa barabara kwa kuwa wazalendo kwa kuithamini kazi na kuwawezesha ili nguvu kazi hii itumike ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni hali ya kawaida kundi kubwa la vijana kukimbilia mijini na pale wanapokuwa vijijini wamekuwa wakashinda vijiweni bila ya kufanya kazi. Haishangazi hata kidogo kukuta rika la watu wazima ndilo linalojshughulisha na shughuli za shamba na si vijana. Hali hii ikiachiwa iendelee haipendezi hata kidogo na sijui kama tutakuwa tunajenga Taifa la namna gani.

Mheshimiwa Spika, hali ya ushiriki wa michezo ya Kimataifa imekuwa si ya kuridhisha hata kidogo, rekodi inaonesha kwamba katika michezo ambayo tulikuwa tukifanya vizuri kwa sasa hali imekuwa tofauti kabisa, hivyo ni wajibu kwa Wizara kujipanga upya ili kama Taifa tufanye vizuri.

**MHE. KASSIM M. MAJALIWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja kwa kuwa naamini mipango mingi ya Wizara itatekelezeka. Natoa mapendekezo kwa Vyombo vya Habari yakiwemo magazeti ambayo hayaitakii mema Serikali inayowawezesha kuendelea kufanya kazi zao. Vyombo vingi vya habari vimekuwa vikipotosha umma kwa kuandika mambo mengi ambayo hayana ukweli na kuwafanya wananchi kuichukia nchi yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yako mazuri kuhusu uboreshaji wa *TBC*, bado kuna usikikaji usiordhisha maeneo ya Ruangwa, Liwale jambo linalowalazimu wananchi kuunganisha nyaya ndefu kama *antenna* ili kupata msikiko ulio nafuu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia eneo hili la Mikoa ya Kusini (Mkoa wa Lindi) lipatiwe ufumbuzi wa kuboresha mawasiliano, nikiwa naamini kuwa uwezo upo kwani tayari kuna Kituo cha matangazo kilichopo Lindi mjini na mitambo yake iliyoko Nachingwea umbali usiozidi kilomita 60.

Mheshimiwa Spika, naamini inaweze kana. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nataka kutoa pongezi zangu kwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji kwa kazi na mipango mbalimbali katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo mashulenii. Ingawaje michezo imerejeshwa mashulenii bado hakuna jithada za dhati kuhakikisha kwamba kuna ufanisi wa kutosha. Matatizo ya wazi yanayojitekeza ni uhaba wa walimu wa michezo, ukosefu wa viwanja na bajeti finyu mashulenii kwa ajili ya kununua vifaa vya michezo na kujenga miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jithada hizo ni vema kama Taifa tukafikiria kuanzisha shule za michezo (*sports academics*). Kwa kuanzia, Serikali inaweza kuhamasisha vilabu vya michezo mbalimbali, majeshi na watu binafsi kuanzisha shule hizo kwa kuwachukua vijana wenye vipaji kutoka mashulenii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usikivu wa Redio ya Taifa. Hadi sasa kuna tatizo kubwa la usikivu wa Redio ya Taifa (*TBC*) katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Kati ya maeneo yenye tatizo hili ni Jimbo la Rombo. Wananchi wa Rombo wako kana kwamba ni raia wa Kenya, kwani redio ambayo inasikika sana huko (*KBC*) Kenya Broadcasting Corporation ya Kenya wananchi wa Rombo tunaiomba Serikali kuhakikisha kwamba redio hiyo muhimu kwa ajili ya uhamasishaji wa maendeleo ya wananchi inasikika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mmomonyoko wa maadili kuitia kwa Wasanii. Kwanza, tunafarjika sana na kazi ambazo Wasanii wanafanya katika nchi yetu. Wanafundisha, wanaonya na kuburudisha. Hata hivyo, baadhi yao wanatumia lugha na mavazi ambayo ni kinyume na utamaduni wetu. Baadhi yao huva nusu uchi, wengine wanalewa na kuvuta bangi kupindukia na baadhi mfano aliye kuwa katika *Big Brother* mwaka huu, wale wanaoshiriki mashindano ya urembo na wacheza filamu, wanatuhumiwa kufanya ngono hadharani. Vijana wengi wanawaiga, je, kama wakiachwa hivi wakati watoto huwaiga baadaye Taifa litakuwa la namna gani? Naomba Wizara kukemea ili fani hizi ziungwe mkono na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo yetu ya jadi ambayo ni bao, zumari, kucheza na ng'ombe, ngoma za asilia, makambi kama jando na unyago, yote haya yanapotea. Lazima tukumbuke michezo hii imebeba elimu, historia na ulinzi mkubwa wa maadili ya Taifa. Sijaona mahali ambapo mkazo umewekwa kwa ajili ya kuifufua na au kuiendeleza. Naiomba Serikali kuhakikisha michezo hii haifi kwani ni urithi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, narudia pongezi zangu za dhati kwa kazi inayofanywa na Wizara.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ili nami ijapokuwa kwa uchache sana niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo aliyoiwasilisha hapa Bungeni leo hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake, lakini pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano mzuri wanaompa Mheshimiwa Waziri kiasi cha kumwezesha kumudu vema kazi zake katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu napenda kuuelekeza zaidi upande wa vyombo vyetu nya habari.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama Taifa itakuwa na kumbukumbu isiyosahaulika juu ya nini kilichotokea nchini Rwanda katika miaka ya tisini (90s) ambapo maelfu ya wananchi wa Rwanda walipoteza maisha yao kutokana na vita nya wenyewe kwa wenyewe (*civil war*) ambapo mojawapo na sababu kuu zilizopelekea kuzuka kwa vita hivyo inasadikiwa kuwa ni uchochezi mkubwa uliotokana na Vyombo nya Habari. Hii ilitokana na kwamba vyombo vingi nya habari nya nchi hiyo vilikuwa vikiripoti taarifa ambazo nyingi hazikuwa na ukweli wowote hali hii ilifikia hatua ya kutengeneza chuki miongoni mwa wananchi wenyewe kwa wenyewe hali iliyosababisha baadaye kutokea kwa vita hivyo ambavyo ilikuwa kati ya makabila mawili makuu ya Wahutu na Watusi.

Mheshimiwa Spika, hali inayoendelea hivi sasa hapa Tanzania kuhusiana na vyombo vyetu nya habari yaonekana kushabihiana na ile iliyowahi kutokea nchini Rwanda. Hii ni kutokana na kwamba, vyombo vyetu nya habari hivi sasa vyaonekana kutokuwa na jipy la kuandika na hivyo kuonekana vingi nya vyombo hivyo kuelekea zaidi kuandika habari zinazohusiana na ukereketwa wa kisiasa. Ni vyombo ambayo vimekuwa havina la kufanya isipokuwa kushabikia siasa za kiupinzani nchini.

Mheshimiwa Spika, ni kawaida hivi sasa kusoma, kuangalia au kusikiliza kupitia vyombo vyetu hivi mfano, *Radio, TV* au magazeti, taarifa mbalimbali, lakini nyingi ya taarifa hizo ukiangalia undani wake zaidi, basi zitakuwa na mwelekeo wa kuleta mtifaruku wa kisiasa katika nchi yetu, kwa kuwa ni habari ambazo zinajenga mwelekeo wa chuki baina ya wananchi na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari kubwa inayolielekea Taifa letu. Kama hakutokuwepo na udhibiti utakaofahamika kisheria wa vyombo vyetu nya habari, basi ni wazi kwamba Taifa letu liko hatarini kuangamia kutokana na uandishi usiojali maadili ya kiuandishi na yale yaliyotokea kwa wenzetu wa Rwanda, nasi tuwe tayari kuyashuhudia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, kuhusu filamu zisizokidhi maadili. Hivi sasa nchini kumejaa filamu zinazokiwa maadili ya Mtanzania. Filamu hizi huangaliwa na vijana wadogo chini ya miaka 18. Vile vile kuna filamu nyingi za ngono zimezagaa nchini filamu, hizi zimetengenezwa humu nchini, Temeke na maeneo mengine. Serikali haijachukua hatua madhubuti kudhibiti filamu hizi na hivyo kulinusuru Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa JK. Mfuko wa uwezesaji maarufu, Mfuko wa JK haukuwaflikia vizuri vijana hasa vijiji. Lazima vijana watayarishwe kwa kupatiwa elimu ya ujasiriamali na wawekwe katika kundi ili iwe rahisi kuwapatia mikopo. Hatua hii itawanusuru vijana wetu na madawa ya kulevyo, wizi, ujambazi na mambo mengine mabaya.

Mheshimiwa Spika, lazima ifahamike kuwa vijana hawa wa hivi sasa ndio wazee wa kesho. Hivyo, ni muhimu sana kuwalea vijana katika mazingira mazuri.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi za Wilaya hazijali na hazioni umuhimu wa kuendeleza na kukuza utamaduni wa michezo hasa kwa kutokutenga fedha katika bajeti ili kusaidia kukuza utamaduni wa michezo. Sasa nashauri kwamba, Halmashauri sasa zielekezwe kuwa ni lazima kila Halmashauri itenge japo asilimia tatu ya bajeti zao ili zitumike kuenzi utamaduni na michezo kwa kuimarisha uwepo wake.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote zipangiwe wiki maalum kila mwaka ambayo itaitwa wiki ya utamaduni ili wiki hiyo itumike kufanya mambo mbalimbali yanayohusu utamaduni na michezo kama:-

Kwanza, kushindanisha vikundi nya utamaduni toka ngazi ya Kijiji, Kata na hatimaye Wilaya ili kupata washindi katika ngazi zote hizo na baadaye Mkoa nao upokee vikundi nya Wilaya

vilivyoshinda ngazi hiyo ili vishindanishwe kupata mshindi ngazi ya Mkoa. Baadaye Taifa ipokee vikundi vya Mikoa vilivyoshinda ngazi ya Mikoa ili vishindanishwe kupata mshindi ngazi ya Taifa. Hali hiyo pia ihusishe suala la michezo hata kama mashindano hayo yataishia ngazi hiyo ya Wilaya tu chini ya usimamizi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wakati wa nchi yetu kuwa na Vazi la Taifa umefika. Je, safari hii Mheshimiwa Waziri anatwambia nini juu ya nchi yetu kupata vazi lake rasmi la Taifa?

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia bajeti hii umuhimu katika utulivu na amani ya nchi. Hii ndiyo Wizara ambayo kwa kiasi kikubwa inahusika na utulivu na amani. Ni Wizara inayohusika na jukumu la kufunda na kulea vijana lakini zaidi ni mlezi wa utamaduni wa Taifa letu. Kama aliyosema baba wa Taifa: "Taifa ambalo halina utamaduni ni Taifa mfu." Pamoja na jukumu hili Wizara hii ni jicho na mboni ya rasilimali nyeti-habari. Dunia ya sasa kwa kiasi kikubwa inatawaliwa na habari, jinsi utakavyoitafuta miliki dhibiti na kutumia habari ndivyo utakavyoweza kupata faida ya kiushindani, *competitive advantage*.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo naomba na kushauri Serikali ijjandae ili siku za mbeleni rasilimali za kutosha (bajeti) zitengwe kwa ajili ya Wizara hii. Wizara hii ni muhimu na nyeti sana, hivyo, ni vema iimarishwe na kutumika kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili, ni kujenga mashirikiano ya nguvu na karibu kati ya Wizara na Wizara au idara mbalimbali zinazohusika na kulea vijana na kulinda utamaduni. Ipo haja ya msingi kabisa ya Wizara kufanya kazi na TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kuwalea na kuwaendeleza vijana. Mfano, ni suala la michezo na utamaduni. Kupitia Wizara tajwa vijana wanaweza kuandaliwa hili kupitia sekta ya michezo na utamaduni tujenge uwezo wa ajira zaidi.

Mheshimiwa Spika, mshikamano wa Wizara hizi utasaidia kupunguza ghamra ambazo zingehitajika kama Wizara hii ingeachiwa shughuli pekee. Lakini upande wa pili, ni sekta hii ambayo inaweza kutoa uelekeo wa kimkakati wa kuendeleza vijana na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ni watendaji wa Wizara waliko Wilayani, shughuli zao ziwekwe katika mipango ya Halmashauri ya Wilaya na bajeti ipangwe kwa ajili ya mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ili kuwakumbuka wachezaji wa soka wa zamani kuishia miaka ya 80 kwenda chini majina yao kama K. Manara, Omari Mahadhi, Lukongo, Mambosasa, Gobos, John Lyimo na kadhalika, yangewekwa kwenye ubao maalum katika uwanja mpya wa michezo ili iwe issue ya kuwahamasisha wachezaji wa leo, nao wawe na hamu majina yao yawekwe. Lazima tuwaenzi wachezaji hawa walioleta sifa na kutangaza jina la nchi yetu.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Baada ya pongezi hizi, naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwatayarisha vijana kiuchumi. Kila mwaka tuna vijana wengi wanaomaliza sekondari pamoja na vyuo mbalimbali wakitarajia kuajiriwa au kuingia katika Sekta isiyo rasmi ili kujishughulisha na maisha kiuchumi. Pamoja na takwimu za *unemployment* tunazopewa rasmi na juhudhi mbalimbali za kuwawezesha vijana bado kuna matatizo makubwa kwa vijana. Napendekeza yafanyike yafuatayo:-

- |     |   |
|-----|---|
| (i) | Kukusanya takwimu ya vijana kila Wilaya ambao wana uwezo wa kufanya kazi. |
|-----|---|

- (ii) Takwimu hizo zichambuliwe kimakundi ya walio na mafunzo ya sekondari, ufundi wowote na wale wasio na elimu ya sekondari lakini tayari wako kundi la vijana la kufanya kazi.
- (iii) Kila wilaya ifanye tathmini ya *economic analysis (present and potential economic opportunities)* zilizomo katika kila Wilaya mfano, kilimo, ufugaji, viwanda vidogo vidogo ili makundi ya vijana nchini ya item (2) juu yaweze kusaidiwa kuingia katika sekta hizo
- (iv) Vyombo vyta fedha vihamasishwe kuwakopesha wanavikundi mbalimbali watakaokubali kujishughulisha na sekta za uchumi zinazobainishwa katika Wilaya mbalimbali.
- (v) Jukumu la Serikali libakie kuhamasisha kuweka sera bora kufuatilia utekelezaji changamoto na kuwatafutia masoko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo. Hakuna haja ya kusitiza kwamba michezo ni afya, elimu, uchumi na ni nguzo kuu ya kujenga uhusiano kati ya mtu na mtu, kundi au nchi na nchi nyingine. Kwa bahati mbaya katika Tanzania inaonekana bado hatuna mfumo rasmi unaosaidia kukuza michezo mbalimbali kwa vijana na hata mashulenii hakuna michezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Filamu. Huu ni wakati Serikali kuhakikisha kwamba sheria ya kulinda haki ya Wasanii inakuwepo na kuona Wasanii wanufaika na kazi zao. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu vijana ndiyo wadau wakuu wa sekta hii na ndiyo walio wengi.

Mheshimiwa Spika, filamu zinazotengenezwa lazima zizingatie maadili ya Tanzania pamoja na uelimishaji wa jamii.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ijipange kama chachu ya kuwa chanzo cha ajira kwa vijana hususan kupitia michezo. Hata hivyo, ubunifu wa azma hii lazima uanzie ngazi za Vijiji hadi Wilayani. Tatizo la uhaba wa fedha hasa katika Ofisi za Utamaduni za Wilaya. Michezo huwa inadumaa kwa vile bado msukumo haujakuwa mkubwa katika ngazi ya Wilaya. Jithada binafsi bado hazijakidhi haja ya kufika malengo ya kutumia vipaji na uwezo wa michezo mbalimbali katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, uzoefu ulenge katika kutambua maeneo yenye vipaji vya michezo mbalimbali ili kuibua *potentials* zilizopo. Hususan mpira Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, tatu, uboreshaji wa Kiwanja cha Mkwakwani, Tanga kama Kiwanja cha Kimataifa, programu hii iendelezewa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii kwa kuanza na suala zito linalowakabili vijana (ajira). Mpaka sasa ajira kwa vijana imekuwa ni tatizo kubwa ambapo imepelekea vijana kuwa na maisha magumu. Je, Serikali inafanya mbinu zipi ili kuweza kukabiliana na tatizo hili? Maana llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 - 2010 iliahidi kuwapatia vijana ajira milioni pindi ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchangia upande wa utamaduni. Ukiwa upande wa utamaduni wetu, vijana ndio chachu kubwa ya kuendeleza utamaduni kwa kupitia njia mbalimbali zikiwepo nyimbo, mavazi na mengnayo. Lakini vijana wamekuwa wakishindwa kupita hatua hii ni kutoptana na kubiwa kazi zao, hizo kazi kukosa promosheni kwa soko la nje ya nchi pia Watanzania kutonunua kazi za Wasanii wa hapa nchini kwetu. Je, Serikali ina mpango gani kukabiliana na tatizo linalowakabili vijana wa hapa nchini kwa sasa?

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia katika Sekta ya Michezo, mara nyingi sana vijana wamekuwa wakishindwa kufanya vizuri pindi wanapokuwa ugenini ama ndani ya nchi yao, hii ni kwa sababu kuwa na maandalizi mabovu, ni kutokana na ukosefu wa *support* kutoka Serikalini ikiwa ni pamoja na kupatiwa wachezaji vifaa vyta michezo, mazingira mazuri ya michezo (chakula, afya na mengineyo). Lengo kuu la nchi yetu hii katika sekta ya michezo ni kutaka nchi yetu ifike mbali, je, Serikali kupitia Wizara ya Michezo na burudani umeandaa program zippi katika kuendeleza vijana kupitia sekta hii ya michezo maana vijana ndio tegemeo katika sekta hii ya michezo?

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali, iisaidie *TBC* iweze kujiendesha kwa faida, pia Serikali isaidie Shirika la Magazeti la Serikali kujpanua na hata kuanzisha *TV* na Redio pia haitoshi kuwa Serikali kutegemea *TV* moja au Redio moja. Ni vema hata *TBC* nao wakiwa na gazeti la kila siku ili kupanua wigo wa habari kwani wamiliki wa Vyombo vyta Habari hapa Tanzania wanamiliki *TV*, Redio na Magazeti kwa pamoja (yaani mtu mmoja anamiliki *TV*, Redio, na Magazeti). Kama mfanyabiashara mmoja anaweza, kwa nini Serikali imeshindwa?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wakuu wa Idara katika Serikali Ma-CEO wana Mashirika ya Umma wanapaswa wawe na *at least Masters Degree*, kwa nini *Daily News*, mtu anayekaimishwa *u-Chief Executive Officer (CEO)* hana hata degree wakati ndani ya *Daily News* kuna waandishi wa habari zaidi ya 18 wenye *Masters Degree* na zaidi ya waandishi wa Habari 50 wana *Degree* ya kwanza, iweje Wizara ya Habari imemkaimisha mtu asiye na hata *degree* moja kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *Daily News* na kuwaacha wasomi wengine? Hili ni Gazeti la Kiingereza linahitaji mtu msomi na si wa kubabaisha hasa katika lugha yenjewel! Ndio maana ukisoma *Daily News* siku hizi lina makosa mengi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kwa kuwa sekta ya michezo imekuwa ikifanya vibaya katika nyanja za Kimataifa, je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha *academy* na vile vile kuanzisha utaratibu wa kusomesha makocha wazawa nje ya nchi kwa kipindi fulani na kuepuka gharama ya kuajiri makocha wa kigeni mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kusema siungi mkono hoja hii, mpaka nitakapopata majibu mazuri.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya bajeti ya Wizara husika ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii haijapewa umuhimu kwani makadirio ya bajeti hii ni ndogo sana ya Shilingi bilioni kumi na nne (14,000,000,000/=) ambazo haziwezi kukidhi mahitaji mbalimbali yanayotakiwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana ukizingatia ina majukumu makubwa ya Habari, Vijana, Michezo. Kwa pesa ndogo zilizotengwa hakuna kitakachoteklezwa. Hivyo, naiomba Wizara kwenye *mini budget* iongezewe kiwango cha fedha ili iweze kufanya kazi kwa Sekta husika nilizozionyesha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vyta Habari vinatakiwa kuwa waangalifu kwa kuandika habari kwenye maslahi ya Taifa badala ya kuandika habari zenyet maslahi binafsi na zenyet mlengo wa kisiasa zaidi. Nliombe Wizara iangalie upya sheria ya habari ili kuweza kupitia baadhi ya vipengele vinavyopotosha dhana za Vyombo vyta Habari nchini.

Mheshimiwa Spika, Redio ni chombo muhimu sana katika nchi. Lakini katika Wilaya ya Mpanda, matangazo ya *TBC* Redio hayapatikani. Naiomba Serikali iharakishe mpango wa Kituo cha Redio kwa maeneo ya Wilaya ya Mpanda ili waweze kupata matangazo ya Redio ya Taifa ambayo ndio muhimu. Kwa sasa bado wananchi wa Wilaya ya Mpanda wanategemea sana *Radio Free Africa* na Redio Maria ndizo pekee zinazosikika katika Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, vijana ni kundi kubwa sana katika nchi hii na wengi wao hawana kazi. Naomba sana Serikali kupitia kwenye Wizara husika ili iweze kuwasaidia vijana waliojipanga kufanya shughuli za kiuchumi wasaidiwe na Serikali. Vijana hawa wakijengewa mazingira mazuri na Serikali vijana hawa wakijengewa mazingira mazuri na Serikali wanaweza kufanya mambo makubwa sana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara iweke mikakati mikubwa ya kuwasaidia vijana kuboresha shughuli zao na kuwapatia mitaji ambayo inaweza kuboresha maisha ya Watanzania. Lakini niishauri Serikali nguvu kubwa ilekezwe kwa vijana wengi waliopo vijiji. Kwani misaada mingi inaelekezwa mijini.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wanapenda sana michezo katika nchi hii lakini bado Serikali hajjalipa uzito mkubwa wa kusimamia shughuli za michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpira wa miguu (soka) ni michezo unaopendwa sana na Watanzania, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wachezaji wetu wa ndani kwa kuwajengea mazingira mazuri hasa kwenye vilabu wanavyochezea ambako kumekuwa na tabia mbaya ya kukumbatia wachezaji wa nje ya nchi kuliko vijana wetu. Kama hakutakuwa na mabadiliko basi soka letu linakwenda shimoni. Ni lazima tupange mkakati wa kuboresha vilabu kwa kuwapa kipaumbele wachezaji wazawa wa hapa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na michezo mingine ambayo inatakiwa maboresho ni riadha, ngumi, mpira wa mikono (*netball*) na mingineyo kwani michezo hiyo hajapewa uzito unaostahili na badala yake ni soko pekee ndio inayoangaliwa japo haitufikishi popote pale.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala la Wasanii. Waboreshewe mazingira yao ya kazi zao pamoja na kulinda haki zao ambazo wanaporwa na wajanja wachache.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali ingalie kuboresha shughuli za utamaduni katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA:** Mheshimiwa Spika, utumiaji wa TEHAMA kwenye sekta ya habari na utangazaji ni muhimu sana, lakini jambo la kushangaza ni kuona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri suala ya utumiaji wa TEHAMA kwenye sekta hii halikupewa kipaumbele kabisa. Hotuba hii kidogo tu imegusia *E-commerce project* (see pages 11, 36) *E-commerce* ni suala ambalo ni gumu utekelezaji wake. Kama kweli sekta hii inataka kupiga hatua haraka iwezekanavyo, suala la TEHAMA lazima lipewe kipaumbele husika.

Mheshimiwa Spika, suala la kutumia mkongo wa Taifa kwenye shughuli za utangazaji. Utumiaji wa Mkongo wa Taifa kwa shughuli za Utangazaji inapunguza gharama za utangazaji na pia inaongeza ubora wa shughuli hii hasa kwenye kurusha picha. *Quality* ya picha kupitia *backbone broadband* ni bora kuliko kupitia ya *satellite*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa njia yetu ya mkongo baina ya Dar es Salaam na Dodoma, Dar es Salaam na Arusha na kadhalika inafanya kazi. Ni jambo la kushangaza kuona matangazo ya Bunge yanapitia mtandao wa *Satellite*, wakati Ofisi za Bunge zimeunganishwa na Mkongo wa Taifa mita 1000mb/s. Mimi mwenyewe niliwahi kuwaita viongozi wa *TBC* kuhusu matumizi ya *NICTBB*, lakini kwa bahati mbaya sana walipotea bila ya kutupatia jibu. Sisi Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, tuko pale kuisaidia Wizara, Idara au Mashirika kuongeza ufanisi wa utendaji wa kazi kwa kutumia TEHAMA. Naiomba tena Wizara ihamasisha *TBC* itumie *NICTBB*, pale ambapo Mkongo upo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu *Local Digital Content Development* wakati umefika kwa Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia zianze kutengeneza *Local Digital Content* hasa kwenye *Information Entertainment* na kadhalika au tuanje kuhamasisha wadau mbalimbali kuhusu utengenezaji wa *Local Digital Content*.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kuipongeza timu ya Kilimanjaro Stars kwa kuchukua Ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (*CECAFA*) hapo 2010. Pamoja na kuipongeza timu hii bado tuna safari ndefu ya kupandisha soko letu katika anga za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, soka letu la Tanzania kwa kiasi kikubwa linazidi kudidimia, ni kweli tumechukua ubingwa huo lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya hasa ya kuwaandaa vijana wetu walio chini ya miaka 10 ili kuwaweka katika shule za *academy* ambazo zitawaandaa watoto hawa katika tasnia hii ya soka na pindi watakapokuwa wakubwa waweze kuwa wachezaji mahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa zipo shule chache za *academy* ambazo zinaendesha programu hii ya mchezo wa soka. Tatizo liliopo ni kuwa shule hizi zinawachukua wanafunzi ambao tayari wameanza kukomaa kwa maana ya kuanzia miaka 13. Vijana hawa tayari viungo vyao vipo katika kukomaa na kusababisha kutofuatilia vema mafunzo hayo. Naiomba Serikali hata sekta binafsi wawaandae watoto ambao watafundishika zaidi, nao ni wale ambao wako chini ya miaka 10. Kwa kufanya hivyo, watoto hao watakuwa na uwezo mkubwa si tu wa kupokea vema mafunzo hayo bali pia kuwa wachezaji bora hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, ili watoto hao waweze kuelewa vema mafunzo ni vizuri vituo hivyo vikaajiri walimu wazuri si wa hapa ndani tu bali hata wa nje.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri nikimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa jitihada kubwa anazozifanya za kuendeleza michezo hapa nchini hasa mchezo wa soka. Jitihada hizi ni pamoja na kuajiri makocha wakiwemo Marcio Maximo pamoja na Poelson. Makocha hawa wamefanya kazi kubwa ya kuendeleza timu yetu ya Taifa. Kwa upande wa Marcio Maximo alionesa nia ya dhati ya kuendeleza soka hapa nchini. Jitihada zake binafsi na kwa kushirikiana na Serikali na wadau wa soka nchi yetu iling'aa katika medani za Kimataifa na hatimaye kuweza kufikia kuwa ni nchi ya 98 katika kusakata soko hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, kutoptaka na mizengwe mingi kocha huyo alimaliza muda wake na kuondoka bila kurudia tena mkataba. Tangu alipoajiriwa Poelson nchi yetu inazidi kudidimia na hadi leo hajaonesha jitihada binafsi kama alivyofanya Maximo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali pindi inapotaka kuajiri makocha, ni vizuri wakawa na vigezo vingi vikiwa ni pamoja na *commitment* yake kuwa kweli ataliendeleza soko la nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee niipongeze sana timu ya Yanga kwa kuchukua ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati. Timu hii kwa mara nyingine imetutoa kimasomaso Watanzania kwa kutwaa taji hilo. Aidha, nawaomba waendelee kufanya mazoezi ya kutosha ili waweze kufanya vema katika mashindano mbalimbali yatakayofanyika hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vya umma yaani vya TBC (*Television* na *Redio*) viboreshe usikivu wake. Kuna sehemu nyingi hasa nje ya mji kule vijijini, vyombo hivi havisikiki kabisa au vinasikika kwa tabu. Ni lazima vyombo hivi viboreshe usikivu wake na visikike nchi nzima. Hivi sasa kuna Vyombo vya Habari vingi vya binafsi. Mara kadhaa vyombo hivi vinatoa habari zisizokuwa sahihi za kupotosha na zinazoweza kuhatarisha amani ya nchi hii. Vingine ni vya Vyama vya Siasa na hivyo vinatoa habari kwa malengo ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo, ni muhimu sana kwa Vyombo vya Habari vya Serikali vijiimarisho ili kuweka mustakabali mzuri wa habari na usalama wa nchi.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Waziri wa Habari na Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa kuzungumzia kuhusu Vyombo vya Habari. Vyombo vya Habari vinapewa nafasi kubwa kiasi cha kuwa vinachochea zogo, vinaleta mtafaruku katika jamii zetu. Kwa mfano, hivi karibuni waliandika kashfa nyingi zinazowahusu baadhi ya Wabunge ambazo hawawezi kuzithibitisha. Kashfa hizi haziwakashfu wale Wabunge waliowataja bali hata sisi Wabunge wengine basi tunajisikia vibaya. Mfano mwagine, hivi karibuni wameandika: "Bunge ni Nguvu ya Soda." Hili pia haliletii picha nzuri kwa Wabunge. Wabunge tunajadili kitu tunatofautiana kwa hoja lakini baadaye tunakubaliana kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mila, desturi na maadili ya Mtanzania yanakiukwa, tunapoteza mila zetu, leo watoto wa Kitanzania wanakaa katika barabara ya TAZARA wanauzu CD na Kaseti za ngono. Ukipita na gari basi pale gari iko kwenye foleni wanakuja kutembeza CD za ngono na zina picha nje za matusi na wanakuletea kwenye kloo cha gari wanakuonesha zile pitcha za uchi na wala hawajali kama uko na nani kwenye gari hilo. Wakati mwagine unashindwa hata kuwaangalia wale walimo kwenye gari pengine ni baba yako au mama yako au watoto wako.

Naiomba Serikali ifuatilie kwa kina suala hili ambalo linaleta aibu na kashfa kwa nchi yetu na linavunja mila, silka na utamaduni wetu wa Kitanzania.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa Wizara kwa mwaka 2011/2012 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt Emmanuel Nchimbi kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika kutusaidia sisi kama Wabunge, lakini pia utekelezaji wa majukumu ya kila siku kiutendaji kwa Serikali na wananchi kwa ujumla bila kuchoka na bila woga. Nampongeza pia Naibu wake Dkt Fenella Mukangara kwa uwajibikaji mzuri na utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, nimeipitia na kuelewa kwa makini sana hotuba, lakini kutokana na hotuba hii kujumuisha mengi ambayo naomba nichangie machache kufuatana na hali halisi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sasa Tanzania imekuwa haifanyi vizuri katika michezo hususan katika medani ya Kimataifa. Hali hii imetokana na ukweli kwamba, Tanzania kama Taifa imeshindwa kuwekeza katika maeneo ambayo ndio chachu na kitovu cha uibuaji wa vipaji vya vijana ambaa ndio rasilimali muhimu katika maendeleo ya michezo katika Taifa lolote.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mbalimbali ambayo klabu na vyama vya michezo kwa kushirikana na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali, yanapaswa kupewa kipaumbele endapo Tanzania ina nia thabitii na ya dhati ya kuleta mapinduzi katika mchezo. Kwa mfano, walimu (Makocha) kwa takriban miaka mitano Serikali sasa imekuwa ikitumia kiasi kikubwa sana cha pesa karibu wastani wa *USD 32,000* kwa mwezi mmoja kuwagharamia makocha wawili wa kigeni kwa ajili ya timu za Taifa, Taifa *Stars* na Serengeti *Boys*. Lakini kiasi hicho cha fedha au zaidi kidogo kingeweza kuwasomesha au kuwapa mafunzo ya ukocha wachezaji waliong'ara zamani wapataao 30 kupitia mpango wa ushirikiano au mahusiano ya kitamaduni baina ya Tanzania na nchi marafiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka isiyozidi mitatu wachezaji hawa wa zamani ambaa tayari wamepewa mafunzo ya kitaalam, wangeweza kutawanywa katika mikoa yote ya Tanzania kwa ajili ya kutekeleza mpango madhubuti wa kuibua vipaji vinavyojificha katika maeneo mbalimbali vijiji na mijini ikiwamo Kilwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, uboreshaji wa michuano ya vijana kama *Copa CocaCola* endapo ikishirikishwa kuanzia ngazi ya mashule ya msingi na sekondari ungesaidia na kuchochea mwelekeo sahihi wa kufanikisha mipango ya kuleta mapinduzi katika michezo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Elimu ili kuharakisha mapinduzi ya michezo na hatimaye kufikia malengo yaliyokusudiwa kwa wakati na njia muafaka, Serikali haina budi kwa kushirikiana na vyombo nya wadau wengine kutenga shule maalum kwa ajili ya michezo.

Mheshimiwa Spika, jambo au mpango huu ukiandaliwa kwa umakini wa hali ya juu katika kila Mkoa, ni dhahiri kwamba itakuwa chemchem ya uibuaji wa vipaji nya vijana nchi nzima, hali ambayo itasukuma kwa kasi kubwa ujenzi wa timu zenye ushindani na sio kama zinavyoshiriki sasa.

Mheshimiwa Spika, mkakati maalum (*Special Request to Foreign Aid*) Serikali inaweza pia kutoa au kupeleka ombi kwa nchi marafiki na ambazo zimepiga hatua kimichezo, kupokea vijana wetu katika vituo vyao nya ukuzaji vipaji kupata ujuzi na uzoefu. Ili kutekeleza mkakati huu Serikali inaweza kufanya mazungumzo na Mataifa kama Ufaransa, Hispania, Ujeruman, Uingereza na kadhalika. Ikumbukwe nchi nydingi za Afrika zimefanikiwa sana katika utaratibu kama vile Burkina Faso, Benin, Nigeria, Senegal na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ubunifu wa kuibua vipaji lipate suluhu kwa maana tunaweza kuwatumia vijana ambao kwa kiasi kikubwa wanaweza kuliletea taifa sifa kubwa katika michezo. Yapo maeneo kama uogeleaji na uendeshaji balskeli, ni vema tukaangalia vijana hawa kwa kuwapa ujuzi na mbinu za kimichezo wakaenda kutuwakilisha katika michezo sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ifike wakati Serikali iwe na dhamira ya dhati kuwasaidia Wasanii wa Kitanzania hasa kuwalinda kwa haki kwa kazi zao lakini pia iangaliwe namna bora ya kuzuia kazi za Wasanii wa nchi nydingi ambazo zinaingizwa holela kabisa. Kama Nigeria na kwingineko huwezi ukaingiza kazi zako na zikapata fursa za soko la moja kwa moja. Ikiwa kwao haiwezekani kwa nini kwetu iwezekane. Yaangaliwe pia maadili ya jamii yetu yanapotoka sana kutokana na tamaduni zisizo bora kutoka ughaibuni. Hakuna nchi ambayo haijaweka ukomo wa kuonesha kila kitu. Vyombo vyetu nya habari na jamii zielimishwe na kuona kuwa kuna umuhimu wa kuthamini utamaduni wetu lakini tuone kuwa utamaduni wa kigeni utatuvuruga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mingine endelevu, utaratibu na mipango niliyoeleza unaweza kubadilisha taswira ya michezo nchini mwetu kwa kasi ambacho italitoa Taifa katika dimbwi la usindikizaji.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa sana katika tasnia ya habari, uhuru wa kupindukia kwa Vyombo nya Habari utalipeleka Taifa letu pabaya. Ikumbukwe hata Amerika ambao wanasiifika kwa demokrasia hawana uititiri wa magazeti na Vyombo nya Habari ambavyo vinakuwa *across the country* zaidi ya viwili ama vitatu. Television *CNN local*, *ABC News* na *News 4*, Gazeti ni moja tu *US today*, sasa tujulize sisi tumeiga wapi?

Mheshimiwa Spika, tatizo la madeni na utumiaji mbaya wa madaraka katika Vyombo nya Habari nya Umma (*TBC* na *TSN*) ni tatizo sugu sana. Mashirika haya yanakabiliwa sana na malimbikizo makubwa sana na ucheleweshwaji wa kulipwa malimbikizo tena hawa kutoka katika taasisi zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanya kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri. Namwomba Mungu atulinde sote

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia sote kufika siku ya leo na kuweza kuchangia machache tu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Michezo na Vijana ni Wizara yenye kushirikiana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naipongeza Wizara na majukumu mazito na changamoto zinazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara inashirikiana na Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kwa Kihistoria na utamaduni kipindi cha uhuru kizazi hiki na kabla ya uhuru, ni muhimu tukilinganisha na kujiangalia hapa tulipofikia. Kwa ajili ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho. Kwa kuwa mila na desturi za nchi yetu hazituruhusu kugeuka kanuni za nchi. Mtu mzima kumbaka mtoto mdogo, kwa kuwa Wizara yako inashirikiana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vinatangaza kila mara suala la ubakaji, je, huoni sasa mkashirikiana kuanzisha sheria za kulinda mila na desturi na Wenyeviti wa Vitongoji, Mitaa hasa ngazi zote za chini kutambua matukio kama hayo mfano, mwanzoni mwa mwaka huu tumeona Vyombo vya Habari vikitangaza na kuandika magazetini, mtoto mdogo wa kimasai aliyolewa akiwa na miaka sita na kuzaa akiwa na miaka 11.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni wakati wa kuzielimisha mila zingine zenye udhalilishaji wa kijinsia na ubakaji na ni moja ya mauaji, tunao wengi wamezalishwa na hawajaripotiwa ipo haja kubwa kwa sasa kushirikiana kukomesha tabia hii kwani humdhalilisha mwanamke, mila zisizozingatia sheria za haki za binadamu zielimishwe kwani mwanamke ni moja ya jamii yenye uwezo wa kushauri na kupata elimu katika familia. Unapomkosesha masomo kwa ndoa za utotonni ni kumnyima haki na kumpatia maradhi ya kudumu bila tiba.

Mheshimiwa Spika, suala la mirathi ni kero, elimisheni umma uelewe haki ni ya kila mtu, mwanamke anayo haki ya kurithi mali ya mume na mume halikadhalika kurithi mali ya mke na mtoto wa nje ya ndoa naye ana haki pia lakini utaona watu wanagombana wanauana na vyombo vya habari vinatangaza kwa nini tusiwe na vipindi vya elimu ya familia kwa ndani na uwazi? Utakuta watu wanaelemea sana mila ambazo zingine zimepitwa na wakati, hivyo kugeuka mila za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, michezo ni moja ya afya. Michezo ni burudani, michezo ni ajira ni uchumi, sasa tuangalie kuanzia ngazi za chini kabisa hasa mashulenii mitaani na kuwa pamoa hawa watoto kuanzia nchini ili wajitambue mapema ajira yake ni ipi, kipaji chake ni kipi, kwani kufanya hivyo uwezekano mkubwa wa vijana kuwa tegemezi utatoweka katika nchi yetu na wimbi la wizi na ujambazi halitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, waandishi wa habari niwapongeze kwani hufanya kazi ngumu kwa kukutana na misukosuko na wengine kupoteza maisha. Ningishauri Wizara kuwawezesha vizuri na kuwawekea ulinzi kwani hii kazi inaingia sehemu nyingi zingine ni za hatari, hivyo Serikali iwave uwezo mkubwa kwa kila hali na ushirikiano.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uandishi wa Habari. Kwa kipindi kirefu Serikali imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi ya kudhalilishwa Serikali yao katika Vyombo vya Habari. Hivyo, nashauri sasa Serikali iweke sheria kwa waandishi wa habari, ye yote anayeandika taarifa zisizokuwa na ukweli achukuliwe hatua za kinidhamu ikiwemo hata kufungiwa leseni yake na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mchezo wa *Football* nchini. Ni muda mrefu nchi yetu imekuwa katika harakati za kuinua mchezo huo bila ya kupata mafanikio mazuri yanayohitajika. Aidha, tatizo hilo limetokana na utaratibu wetu wa Tanzania ni kwamba kila mchezaji anataka kuwa mchezaji wa Yanga na Simba na mtu akifika hapo mpira wake unakufa. Hivyo, naishauri Serikali kuanzisha vyuo maalum vya ukuzaji wa mpira huo na vile vile Wizara ianzishe ligi za mikoa kama zamani ili kupata wachezaji bora. Aidha, Wizara irejeshe utaratibu wa kuchezwa kwa ligi kuu ya Muungano kwani kutaweza kuinua mchezo huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Wasanii, naishauri Wizara kuweka utaratibu kisheria wa kuwasaidia Wasanii wa Tanzania kwa sasa usanii huo umekuwa ukilipa hadhi Taifa letu nje ya nchi. Aidha, Serikali iweke Mfuko Maalum wa kuwasaidia Wasanii wetu.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, napongeza kazi za Wizara. Lakini kuna changamoto zifuatazo:-

- (a) BASATA hawapewi hela za kutosha kwa nini? Sababu BASATA ipewe nguvu, fedha na watumishi wa kutosha.
- (b) Mfuko wa Utamaduni nao haupewi fedha wala utaalalm (*Human Resources, Experts*).
- (c) Vijana hawana utaalalm wa shughuli za michezo, lini michezo utaanishwa mashulenii au vyuoni hata mitaani. Kamati za michezo, Maafisa Utamaduni wa Wilaya wapewe *Skills* za kuanzisha vikundi vya michezo.
- (d) Michezo ni ajira kwa vijana, Serikali inapaswa ku-coordinate kila mtaa kuwepo na michezo.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa namna nzuri alivyowasilisha hotuba yake kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri inachanganua vizuri mchango wa Vyombo vya Habari vya umma na vile vya Binafsi katika kuimarisha utoaji wa Elimu, kuburudisha na kuhabarisha. Vyombo vya Habari vinahusisha magazeti, redio na *television* mchango wake katika maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara katika kusimamia maendeleo ya tamaduni za nchi yetu. Hata hivyo, ni wajibu wa Serikali kuongoza fungu kwa Wizara hii ili kuisaidia kuendeleza tamaduni zetu ambao zinaweza kuchangia pato la Taifa kuititia utalii wa ndani na nje. Nchi yetu ina wajibu mkubwa wa kuchukua hatua za makusudi za kuwawezesha vijana ambao wengi hawajaweza kupata fursa za kujajiri.

Mheshimiwa Spika, uratibu wa Mbio za Mwenge wa Taifa kila mwaka umekuwa ukifanyika kwa umahiri mkubwa, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ni mojawapo ya nguzo za Umoja wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala la uendelezaji wa sekta za filamu linapaswa kupewa kipaumbele ili hatimaye mchango wake katika pato la Taifa uweze kuonekana.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili kama lugha ya Taifa na Kimataifa kinatakiwa kupewa kipaumbele na heshima ya pekee na mipango ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu. Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lionegezewe uwezo wa kuweza kufanya utafiti na uendelezaji wa lugha yetu ya Taifa Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Wizara iyafanyie kazi mapungufu yaliyomo katika sheria ya haki miliki ya mwaka 1999 na uwepo utekelezaji wa sheria yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee kushirikiana na Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) kuondoa hujuma kwenye kazi za Wasanii wetu.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza viongozi wote wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu kuna changamoto nyingi ambazo zimo katika Wizara kadri nionavyo.

Mheshimiwa Spika, mchango wa soka, timu zetu zimeendelea kufanya vibaya na kutusononesha Watanzania. Ushauri vijana waandaliwe toka utoto wao katika shule za msingi, michezo ikiwa kama somo maalum na sio ziada.

Mheshimiwa Spika, kuajiri wachezaji wa kulipwa ipigwe marufuku. Kwani wana vipaji vya wazawa au idadi ya wageni iwe isiyozidi watatu tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hati miliki ya wanamuziki. Itungwe au sheria ya kulinda kazi za Wanamuziki au Wasanii inabadilishwa ili watakaopatikana wafungwe kifungo cha miaka 30 na zaidi ili kukomesha tabia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Lugha ya Taifa (Habari), kwa mtazamo wangu wanahabari wetu wanapoteza sifa ya uandishi wa habari, wanaandika mambo mengi ya kubuni na tumeshuhudia baadhi ya magazeti kuomba radhi kwa wasomaji watuhumiwa. Ushauri wangu, adhabu na vyombo vilivyopewa majukumu ya kusimamia mambo ya uandishi wa habari wakae walete mkakati wa kuwabana watu wengine au baadhi ya waandishi wa habari wasiokuwa waaminifu wapewe adhabu kali ikiwemo kufungiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu riadha. Tanzania iliyahi kufikia katika nafasi nzuri katika mchezo wa riadha lakini sasa tumerudi nyuma. Maoni yangu tukajifunze kwa wengine wanaofanya vizuri.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri - Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii, ambayo imeanisha jinsi itakavyoendeleza sekta zote zilizomo ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuajiri Maafisa Utamaduni na Michezo Mikoa na kwa kila Halmashauri. ni ukweli usiopingika kuwa Maafisa Utamaduni na Michezo wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana, kwani hawana fedha za kuendeshea, mara zote wamekuwa wakiomba kwa Makatibu wa Mikoa na kuomba kwa wahisani mbalimbali wapenda michezo na wenye moyo wa kujitolea.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini Serikali itanza kutenga fedha kwenye Idara ya Maafisa wa Utamaduni na Michezo kwa ngazi ya Halmashauri na Mkoaa ili Maafisa hawa waweze kufanya kazi zao vizuri kwa kuinua michezo na sanaa kwa nchi nzima. Vile vile wachezaji wataondokana na tabia ya kuombaomba wakati wanapenda kushiriki michezo ya ligi mbalimbali nchini na nje ya nchi. Hii itasaidia hata Wabunge kuacha kubebeshwa mizigo ya kusafirisha wachezaji na Wasanii.

Mheshimiwa Spika, napenda kurejea ushauri wa Wabunge nikiwa miongoni mwao kupitia bajeti zilizotangulia kwa njia ya maswali kuwa wanamuziki wengi wamekuwa wakivaa mavazi yanayoonyesha maeneo ya siri ya mili yao na kuwafanya vijana kuiga mila mbaya. Pamoja na Wabunge kuongea sana, bado wanamuziki wanaendelea kuvala nguo fupi, nyepesi na kuacha wazi maeneo nyeti ya mili yao hususan wanawake.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini Serikali itatoa kauli ya kukemea na kusitisha tabia hiyo sasa? Ninasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana au Naibu Waziri wakati watakapokuwa wanajibu hoja.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali na Bunge kwa uamuzi wake wa kuwatambua wachezaji wa *Yanga Sports Club* walipochukua ubingwa wa *Kagame Cup* mwaka huu, pamoja na wanafunzi waliofanya vizuri kwenye matokeo ya Kidato cha Nne kwenda Kidato cha Tano na wanariadha kwa Bunge liliopita.

Swali: kwa nini Serikali isitambue mwanzo mzuri wa Timu ya Taifa Queens ya wanawake ambayo ilichukua ushindi wa tatu huko Afrika Kusini ili kuwatia moyo kama ilivyofanya kwa timu ya Yanga iliposhinda? Nina uhakika wanawake watafarijika, watapata nguvu mpya na hatimaye kuchukua ushindi wa kwanza kwenye michezo ijayo. Nitafarijika sana kupata maelezo yenye kutia moyo ya Waziri au Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naisonikia raha sana kuona lugha yetu ya Kiswahili inakuwa mionganoni mwa lugha zinazotambulika kimataifa. Jambo la kusikitsha ni wale Watanzania wachache wanaokosa uzalendo wa kutumia lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni lini Serikali itapeleka wakalimani kwa kila nchi rafiki na nchi yetu ili kuwasaidia Watanzania wanaosafiri kwenda nje kwa sababu mbalimbali ikiwemo kwenda kutibiwa? Nitashukuru kupata majibu ya Waziri au Naibu Waziri, kwani wapo wagonjwa wanaokwenda kutibiwa au kibishara wanapopata shida ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa waandishi wa habari wengi wanashindwa kutambua wajibu na mipaka ya kazi yao. Wengi wao wanaandika habari kwa maslahi yake au kwa maslahi ya wachache badala ya kuandika habari yenye kuelimisha au kuwahabarisha Watanzania walio wengi kujua mambo yenye maslahi na Taifa au Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua, Serikali ina utaratibu gani wa kutoa semina, warsha, kozi fupi na kozi ndefu kwa waandishi wa habari?

Mheshimiwa Spika, napenda kuihabarisha Serikali kuwa vijana wengi hawanufaiki na mfuko wa JK, kwani mikopo hiyo inapitia kwenye Mabenki na Mabenki haya yanayo masharti magumu na ukiritimba usio na tija. Kwa kuwa *SIDO*, yaani viwanda Vidogo Vidogo imeonyesha kuwa karibu sana na Watanzania wa Vijiji ni wakiwemo wanawake na vijana, kwanini Serikali isipeleke fedha nyingine *SIDO* ili vijana wengi waweze kufaidika? Naomba maelezo, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha *SIDO*, ili vijana waweze kujiajiri kuondokana na uzururaji, ulevi wa madawa ya kulevyia, wizi, majambazi na kadhalika? Vile vile asilimia tano inayopelekwa kwenye Halmashauri, usimamizi wake siyo mzuri, kwani fedhahaziendi kwa mfululizo mzuri kwenye Halmashauri na marejesho ya vijana siyo mazuri kutokana na elimu ndogo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu nikiwa na imani kuwa Serikali itathamini mchango wangu ikiwemo kuwachukulia hatua waandishi wa habari wanaokikuka miiko au maadili ya Uandishi wa Habari. Ninamalizia kwa kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja hii na kuwatakia kila la kheri kwa utekelezaji wa bajeti hii.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Jimbo la Babati Vijiji. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kazi ya mfano wa kuigwa katika kuendeleza yanayotekelizwa na Wizara hii; huru wa Vyombo vya Habari, Maendeleo ya Vijana, utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, anaweza kuboresha Sekta ya Habari, Utamaduni na pia Michezo. Ni muhimu pia kuisaidia vijana hasa wasanii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali katika Wilaya ya Babati, Jimbo la Babati Vijiji, huko miaka ya nyuma tuliweza kutoa wanariadhwa wa kitaifa na kimataifa. Leo hii hatuna kabisa wanaoshinda hata kitaifa. Naomba tupate wataalam wa kufundisha wanariadhwa wetu wenye nia ili vijana wengi wandelee kupata ajira katika Sekta ya Michezo. Pia tuna uwanja mtupu Babati, tunaomba Serikali itsaidie namna ya kuboresha uwanja huo angalu ufanane na uwanja wa michezo.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba tusaidiwe katika masuala ya michezo mashulenii kwa elimu na vifaa vya michezo. Pia tuna masuala mengi ya utamaduni mbalimbali, Serikali ingeweka siku maalum ili kila Mkoa na Wilaya kila mwaka tuweze kuonyesha utamaduni wa makabila mbalimbali Tanzania. Tunaweza kuwa na utalii wa kitamaduni. (*Cultural Tourism*) mfano ni ule wa Brazili, *Carnival festival*/inayofanyika kila mwaka kwa wiki moja.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Serikali iangalie Sekta ya Habari. Ni Sekta muhimu sana, ni Sekta kama Sekta nyingine kuweza kuchangia maendeleo na kuwa kichochezi kikubwa cha maendeleo. Tunaomba katika Wilaya ya Babati na Mkoani Manyara tupatiwe vifaa vya kufanya kazi waandishi wetu. Pia ushirikiano kati ya Maafisa Habari wa Serikali na waandishi uboreshwe,

elimu zaidi itolewe. Pia ni muhimu Serikali iangalie namna ya kuboresha mitaala ya Shule za Uandishi wa Habari.

Mheshimiwa Spika, wengi wanavyofundishwa sasa na ukiangalia habari zinazotolewa, maadili hakuna, wanaandika na kutoa habari potofu bila utafiti, mradi waandike. Elimu kwa umma pia itolewe zaidi. Wengi sasa huamini kilichoandikwa na kutangazwa katika redio na TV ndiyo ukweli bila kujua ni habari za ukweli na ina lengo gani. Nchi za Magharibi pia hufanya sense ya habari zao, lazima tufundishe uzalendo wa nchi na waandishi wawe *investigative* na kuweza kusaldia kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na tunaomba Waziri aje Mkoani Manyara Wilaya ya Babati Vijiji kututembelea.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Habari kwa hotuba yake iliyokusanya mambo mengi yanayohusiana na Wizara hii, pia utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa bajeti iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji wa kazi zao kwa ufanisi hadi kukamilika kwa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Wizara hii ina majukumu mengi yakiwemo kuhakikisha kwamba mtandao wa habari kupitia vyombo mbalimbali vya habari iwe magazeti, televisheni, redio, vipeperushi na mengineyo, visambae kote nchini na kuhakikisha kwamba habari hizo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuleta amani ya Taifa letu bila kusababisha fujo au ugomvi wa namna moja au nytingine.

Mheshimiwa Spika, napenda nilipongeze Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) kutokana na jitihada zake za kusambaza mawasiliiano ya habari nchini kwa njia ya redio, televisheni na kutoa elimu kwa kiasi kikubwa kuhusu maendeleo ya nchi yetu kwa kuainisha jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali nchini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli usiofichika kwamba sasa hivi wananchi waliowengi wameweza kuelimika zaidi kupitia jitihada zinazofanywa na shirika hili nchini kwa wale waliko mijini na vijiji. Wengi wanaweza kufahamu jitihada za maendeleo ya miundombinu yaliyofikiwa na nchi yetu, vituo vya afya na utendaji wake wa kazi, shule kila kata, na hatua nytingine zilizofikiwa nchini tokea uhuru hadi leo hii.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuendelea kuliwezesha Shirika hili, kwani linaleta mchango mkubwa wa Taifa letu ili liendeleee kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, fedha inayotengwa kwa ajili ya kuendeleza Shirika, Serikali itilie mkazo na nguvu upatikanji wake kama ilivypangwa ili kuboresha mipango iliyokusudiwa na kuendelea kutuletea sifa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mishahara ya wafanyakazi pamoja na waandishi wa habari nchini. Tutambue mchango mkubwa wa waandishi wa habari wale walipo ofisini hata wale walio nje ya ofisi ambao hawaaja jiriwa (wakujitegemea).

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie kwa umakini mkubwa jitihada hizo kwa kuwaboreshea mishahara yao kulingana na kazi zao wanazozifanya. Wale wa kujitegemea, tuangalie uwezekano wa kuandaa sheria itakayowawezesha kuwekewa viwango vyao vya malipo kutokana na kazi zao. Pia kwa waandishi wanaokwenda kinyume na maadili ya nchi yetu, waweze kudhibitiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuwekwa kwa viwango vinavyoendana na kazi zao ndiko kutakakozidisha kutukuza kazi wanazozifanya na kuonekana zina maana nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa bajeti nzuri na utekelezaji mzuri wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuishukuru Wizara hii kwa kufikiria kuanzisha Kituo cha Television cha *TBC* katika Mkoa wa Shinyanga. Nawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awatangulie katika shughuli hii isiishie njiani.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Wizara hii kupitia vitengo vyake niwakaribishe katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini kuja kujonea msanii ambaye anaimba kwa kutumia zana au vifaa vya kawaida kabisa kama ngoma, vinanda vya kimila na siyo vya madukani.

Mheshimiwa Spika, lakini cha zaidi, msanii huyu ana uwezo wa kumtazama mtu kwa mara moja na akamchonga kama alivyo au kitu chochote, iwe jengo, mnyama; kwa hakika ana uwezo mkubwa wa kipaji hiki alichopewa na Mwenyezi Mungu bila kusomea popote. Msanii huyu anaitwa Mzee Tangaulizi, anapatikana katika Kata ya Mwamalo Wilaya ya Shinyanga Vijijini. Karibuni sana mjifunze kwa mzee huyu na mwone maajabu anayoyafanya katika sanaa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niishukuru Serikali kwa kurudisha michezo katika mashule yetu. Pamoja na kurudisha michezo, hebu sasa naomba shule zetu zote za mzingi na sekondari ziwe zinapelekewa vifaa vya michezo ya kutosha, kwani tunaona namna ambavyo wanafunzi hawa na walimu kuwa wakihangaika hapa na pale kutafuta vifaa vya michezo kwa wafadhili wa ndani na pengine hata kwa kuchangishana fedha.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya, ajira na ni viburudisho. Naomba sana tuwakumbuke watoto wetu mashulenii na kuibua vipaji vyao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuishauri Serikali iangalie sana matumizi ya lugha yetu ya Kiswahili, iendelezwé kwa kasi, lakini pia mwendeleze juhudí katika kuziendeleza ngoma zetu za asili kwenye televisheni pamoja na radio.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya bajeti hii ya Wizara ya Habari, vijana, Utamaduni na michezo. Ahsante.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Dkt. Nchimbi, Naibu Waziri – Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri inayoleweka.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hii, nachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, nimesoma hotuba yote kwa makini, lakini sikuona mstari hata mmoja uliolezea michezo kwa watu wenye ulemavu. Naomba ieleteweke kwamba wenye ulemavu huwa wanashiriki katika michezo ya riadha, kuinua vitu vizito, kitaifa na kimataifa, mfano michezo ya Jumuiya ya Madola, *Olympic* na kadhalika. Kinachofariji ni kwamba mara zote wanaposhiriki huwa wanarudi na medali ambayo inakuwa ni sifa kwa Taifa letu. Tunapaswa kuwaenzi.

Mheshimiwa Spika, ingawa wenye ulemavu hao wanashiriki michezo mbalimbali, wanajitoo kwa kudhamiria ushindi, lakini ushindi wao hupatikana baada ya taabu nyingi wanazozipata wakati wa maandalizi ya mashindano mbalimbali, wanamichezo na makocha wao. Kwa mfano, kilichotokea kwenye Kambi ya Wanamichezo wa Olympiki Maalum ulikuwepo *Salvation Army* Dar es Salaam, huduma hazikuwa nzuri, chakula, vifaa muhimu, wasaidizi wachache na kadhalika.

Kwa msingi huo, natoa rai kwa Serikali kwamba iwe inawezesha timu zetu hasa zinapojiandaa kwa mashindano ya kimataifa kwa sababu sifa ya ushindi inakuwa ya Taifa. Isiwe

tunafurahia tu medali, lakini kwenye maandalizi, tunaachia vyama husika vya michezo kwa wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, napongeza kazi inayofanywa na Vyombo vya Habari kwa kutoa habari za michezo ya wenyewe ulemavu kwa vile taarifa hizo zinasaidia jamii kutambua vipaji vya michezo walivyonavyo wenyewe ulemavu nchini.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kusikia kuwa angalau walimu kadhaa walihudhuria mafunzo ya michezo kwa wenyewe ulemavu. Ila nasisitiza kuwa wachezaji husika nao wathaminiwe na kuwezeshwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha Mfuko huo kifedha na kiufuatiliaji. Hata hivyo, naishauri Wizara itoe mwongozi kwa Maafisa Vijana kwenye Halmashauri zetu wajibu wao wa kuelimisha vijana wenyewe ulemavu kuhusu mfuko huo ili wafaidike nao kwa kujunga kwenye SACCOS.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi - Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Fenella Ephraim Mukangara kwa kushirikiana na watumishi wengine wa Wizara hii kuandaa bajeti hii ambayo tunajadili leo. Shukrani hizi ziwe kichocheo cha kuleta maendeleo, mafanikio pamoja na ufanisi mkubwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Sekta ya Habari imekuwa kwa kasi sana hapa nchini, Tanzania, lakini bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukosefu wa maadili mema katika uandishi na utangazaji wa habari, hii ina maana kuwa waandishi na watangazaji wetu wa vipindi mbalimbali hawana maadili mema na sio waadilifu kwa ujumla. Hali hii inapelekea kuandika hata taarifa za uongo, uchochezi, majungu na unafiki.

Mheshimiwa Spika, sekta hii bado haina wataalam waliobobea na badala yake waandishi wengi au watangazaji wengi ni vijana wa mitaani tu wasio na ujuzi wowote ambao hata kwa kiasi kikubwa hawajui kufanya utafiti wa kina kwa kile wanachokusudia kukiandalia makala au kipindi maalum katika televisheni/redio.

Mheshimiwa Spika, suala la waandishi kutoa nukuu za semi za uongo, limeleta uchochezi na hii ni kwa sababu hakuna sheria yoyote inayowabana waandishi au watangazaji wa habari. Pia uelewa mdogo wa waandishi na wahariri wa habari katika vyombo mbalimbali hupelekeea hali hii. Naishauri Wizara ihakikishe kuwa inaweka sheria inayowabana waandishi na wahariri wa habari, wahakikishe kuwa wanapofanya nukuu ya maneno aliyosema kiongozi au mtu ye yote yaye yale aliyojasema na wala siyo kuongeza chumvi au kumbambikia mtu maneno ambayo hakuyasema.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio dhahiri kuwa Sekta hii inanuka rushwa. Hali hii inapelekea kutokuwa na maadili katika tasnia hii. Hali hii pia husababisha kazi zinazoandikwa katika magazeti au kutangazwa katika televisheni au katika redio kuwa za upendeleo, uchochezi, fitina na hata majungu. Pia hali hii imepelekea baadhi ya wanasiasa kujitafutia umaarufu uchwara kupitia sekta hii ya habari. Naishauri Serikali ikomeshe mara moja hali hii kwa kutoa adhabu kali kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vyombo vya habari kutumia Kiswahili kisicho Sanifu na hivyo kuwa kikwazo katika ukuzaji wa Kiswahili. Vyombo vya habari hasa magazeti, redio, televisheni vinatakiwa kutumia Kiswahili sanifu na siyo Kiswahili cha Mitaani. Kiswahili cha mitaani mara nydingi hutumiwa na magazeti ya udaku! Hivyo naishauri Wizara ihakikishe kuwa inavibana vyombo vya habari ili vitumie Kiswahili sanifu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya magazeti hasa yale ya udaku huandika na kuchapisha picha ambazo zinakwenda kinyume na maadili ya Mtanzania. Picha hizo mara nydingi hulenga udhalilishaji wa kijinsia hususan wanawake wanaokutwa katika nyumba za kulala wageni wakiwa na waume. Kitendo hiki ni kinyume na haki za binadamu. Sijui Waziri wa Wizara husika anatoa kauli

gani juu ya picha za uchi zinazoonyesha maungo ya mwanamke kwa jamii zinatoa kiashiria gani kwa jamii!

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ihakikishe kuwa magazeti ya Serikali hasa lile la Uhuru na *TBC*:Radio na Televisheni, vyombo hivi vimeendelezwa na kuboreshwa ili kufikisha habari kila kona ya nchi. Serikali ifahamu wazi kuwa bila *TBC*, imara nchi yetu itayumba katika Sekta ya Habari.

Mheshimiwa Spika, katika maandishi yangu ya Kitaaluma niliwahi kuandika haya kuhusu kijana wa sasa wa Afrika. Naomba kunukuu: "Kijana wa leo nina balaa...! Nikitaka kutafuta elimu, hakuna madarasa...! Nikitaka ajira, naambiwa uzoefu miaka mitano au kumi zaidi. Uzoefu nitaupata wapi? ...Nikijiunga na siasa; wimbo maarufu kote ulimwenguni ni demokrasia. Demokrasia ina mizengwe, umajigambo, ukabila, udini, ubabe, rushwa, ubabaishaji, utapeli na kushindana bila kukubali kushindwa! ...Nikitaka kusema, naambiwa mjinga! ...Chochote ninachokitaka kukifanya, kinanikatisha tamaa! Nikiwa "deiwaka", mpiga debe; kila siku nitaamkia korokoroni! ...Nikiamua kuokoka; wokovu hauonekani. Nimebaki njia panda..! Nimeitambua nafsi yangu. Naahidi kupambana hadi kufa na kupona." Mwisho wa nukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi nukuu hiyo hapo juu inajumuisha matatizo ambayo vijana hukumbana nayo katika jitihadi zao za kupambana na maisha.

Mheshimiwa Spika, naomba waziri anijibu maswali yafuatayo:-

- Kwa nini malezi ya vijana siku hizi yameporomoka sana?
- Tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, Wizara inalikabilije?
- Ukosefu wa elimu ya ufundi kwa vijana, Wizara inakabilianaje nalo?
- Vijana wanaotumiwa vibaya katika siasa, Wizara inawaokoaje?
- Je, Wizara inawasaidiajje vijana wengi Tanzania wanatumiwa kama kondomu katika biashara haramu ya madawa ya kulevy?
- Vijana wa mipakani mwa Tanzania wanasaidiwaje na Wizara hili kukabiliana na changamoto za dunia ya sasa?
- Wizara inawaandaje vijana wa Tanzania kuukabili utandawazi ulioiteka dunia ya vijana kwa kazi zaidi?

Mheshimiwa Spika, utamaduni ni namna watu wanavyoishi. Kuishi huko hutokana na mfumo wa siasa, imani za dini, mfumo wa sheria, mila, desturi, nidhamu, miiko, lugha, uzalishaji wa mali pamoja na jitihada zote za kuyakabili maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utamaduni unahusu kila kitu ambacho mwanadamu anakifanya katika maisha yake ya kila siku, naomba kumwliza Waziri maswali haya:-

- Ni jitihada gani Wizara imechukua ili kuundeleza na kuuensi utamaduni wetu?
- *BASATA* inasaidiajje kukuza utamaduni wa Mtanzania?
- Ni nini nafasi ya tafsiri katika kukuza utamaduni wa Mtanzania?
- Utamaduni na lugha haviwezi kutenganishwa. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa utamaduni wa Mtanzania unaienzi lugha ya Kiswahili kama lugha ya utambulisho wa Mtanzania?

- Je, *Cultural Tourism* katika nchi yetu ya Tanzania ina nafasi gani? Kwa nini isianzishwe na kuendelezwa?
- Waandishi wa Fasihi ya Kiswahili wanathaminiwaje na Wizara husika?
- Mfuko wa utamaduni unasaidiaje kukuza na kuhifadhi utamaduni wa Mtanzania? Je, kuna faida yoyote ya kuwepo kwa mfuko huu?
- Serikali inatoa kauli gani juu ya filamu za Kibongo ambazo zinakiuka maadili ya utamaduni wa Mtanzania?

Mheshimiwa Spika, binafsi pamoja na pongezi kemkem zinazotolewa kwa baadhi ya timu zetu za mpira wa miguu, nashangaa kuona kuwa soka katika nchi yetu haikui. Naomba majibu ya maswali yafuatayo:-

- Je, Serikali ina mkakati gani mbadala wa kuhakikisha kuwa timu yetu ya Taifa, *Taifa Stars* inashiriki na kushinda michezo ya kimataifa?
- Vipi hali ya *Twiga Stars*?
- Vili hali ya *Kilimanjaro Stars*?
- Kwanini migogoro haiishi kwenye vilabu vya soko hapa Tanzania?
- Licha ya soka, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza michezo mingine kama vile kukimbilia, kuruka, kuogelea, na kadhalika ili itambulike kimataifa?
- Je, mashindano ya Miss Tanzania yanasaidia kukuza pato la Taifa au yanasaidia kukuza matumbo ya waandaaji?

Mheshimiwa Spika, mwisho wa yote, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, timu zetu pamoja na kuchangiwa pesa nydingi na Wadau wa michezo, lakini bado mafanikio ni madogo mno. Tumekuwa tukiambilia sifa tu za Yanga na Simba tu, lakini mafanikio ni madogo. Mafanikio yetu ni pale ambapo tutaweza kuzifunga timu za nje. Kwa hiyo, naishauri Wizara ikaze kamba.

Mheshimiwa Spika, katika Timu ya Taifa kunakuwa na ubaguzi. Unapozungumzia Taifa, tunazungumza Tanzania nzima, Bara na Visiwani. Lakini uteuzi wa timu ya Taifa hauzingatii pande mbili, hakuna Mzanzibari ambaye anatoka vilabu vya Zanzibar anayechzeza Timu ya Taifa. Naelewa kuna Wazanzibar wanachezeza *Taifa Star* lakini wanatoka vilabu vya Tanzania bara. Huu ni uonevu mkubwa unaofanywa. Je, vilabu vya Zanzibar havina uwezo wa kuchezea timu ya *Taifa Stars*.

Mheshimiwa Spika, pesa zinazotolewa na *FIFA* kuja *TFF* ambazo ni kwa nchi wanachama wa *FIFA*, *TFF* huwa hawatoi, wanawakilisha kama Tanzania na siyo Tanganyika au Tanzania Bara. Hizi pesa zinatakiwa baadaye zisaidie vilabu, lakini kwa makusudi *ZFA* hawapewi ili vilabu vyao vizidi kwenda chini na visije juu na huu ni uonevu mwagine wanaofanyiwa Wazanzibar. Miaka 48 hivi sasa *ZFA* hawajapata mgao huo na Kocha wa Taifa. Naomba nipatiwe maelezo.

Kocha wa timu ya *Taifa Star* ni kocha wa timu ya Taifa ya Tanzania na yeye mkataba wake ni kuja kufundisha timu ya *Taifa Star* tu na siyo timu nydingine yoyote. Lakini cha ajabu huyu kocha anaonekana anafundisha *Kilimanjaro Star*. Mbona haendi akafundisha timu za Zanzibar? Lakini kwa makusudi, anafundisha *Kilimanjaro Star* ili iifunge timu ya *Zanzibar Heroes*, na huu ni uonevu ikiwa kaamua huyu kocha kufundisha timu nydingine, basi na Zanzibar zipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TV*, kwa kweli baadhi ya vituo vya TV vinakuwa vikirusha picha ambazo haziendani na utamaduni na maadili ya Mtanzania na pia kila siku huwa wanaonyesha

michezo ya nje kama vile michezo ya Angelo. Ina na michezo yetu ya Tanzania huwa inaonyeshwa mara mbili kwa wiki na yao, kila siku? Hili ndilo tatizo letu Tanzania huwa tunathamini mambo ya nje au vitu vya nje kuliko vitu vyetu vya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vijana ni nguvu kazi ya Taifa, lakini hivi sasa vijana wengi wameamu kujihusisha na madawa ya kulevyia na uzururaji na huku wakilalamika maisha magumu. Naishauri Serikali kupitia Halmashauri, iongeze juhudhi ya kuwaelimisha vijana juu ya dhana ya kujiajiri wenyewe hasa kupitia kilimo kwanza.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri katika majumuisho yake anieleze juu ya mgao wa *FIFA* kwa ZFA, uteuzi wa Zanzibar kuchezea *Taifa Stars*, na Kocha wa Taifa kuchezesha mechi nyingine, Shirikisho la Michezo la Taifa tunamtaka aende akafundishe.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na malalamiko yote haya niliyoyataja na mengine, naishauri Serikali iunde Shirikisho la kusimamia Timu za Taifa na shirkisho hili live na wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani na ndiyo live na jukumu la kusimamia uteuzi wa wachezaji wa Taifa na mgao wa mapato ya *FIFA* na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utitiri wa magazeti hapa nchini, lakini habari ambazo nyingi hutolewa na magazeti, ni zile ambazo kichwa cha habari huwa hayalingani na yale maelezo, huo ni wizi mtupu, kwani mteja anaponunua lile gazeti huwa halilingani na zile habari alizozitarajia. Pia kuna upotoshaji wa baadhi ya habari, kwani huwa wanaandika bila kufanya utafiti wa kutosha. Naishauri Serikali kuwa makini na magazeti hayo.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu wa maandishi kwa yale ambayo sikupata fursa ya kuyatoa pale nilipochangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza michezo katika nchi yetu, ni lazima tuboreshe vyuo vyetu tulivyonavyo hapa nchini kwa kuvipatia ruzuku ya kutosha kama Chuo cha Malya ili kiweze kuchukua wanachuo wa kutosha ili kila Wilaya tukidhi mahitaji ya walimu wa michezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Wilaya zetu hasa Wilaya ya Masasi, wazee wetu kupitia ofisi ya Utamaduni wana mpango wa kusimamia tamaduni za makabila yaliyopo katika Wilaya hii. Serikali ingeangalia kwa ukaribu mno kwa kuboresha ofisi yao, kuwapatia vitendea kazi, usafiri na ruzuku ya kutosha kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na hasa ukizingatia kuwa masuala ya utamaduni kwa sehemu kubwa yanahitaji kufuatia vijijini.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa, bado hatujaweka mikakati mizuri juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili, mfano mzuri ni hapa Bungeni ambapo tumekuwa tukishindwa kuwasilisha kwa lugha ya Kiswahili na kuwasilisha kwa lugha ya kigeni, hivi kweli mpango huu tumedhamiria kuuboresha?

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni tuna timu ya Michezo ya Bunge, lakini hadi sasa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri naona hawajatambua kundi hili kama wana wajibu wa kushirikiana katika kuboresha michezo ndani ya Bunge.

Vilevile Bunge lilikuwa na mpango wa kutengeneza jengo lililopo katika mlango wa Wabunge kwa kuweka vifaa mbalimbali kwa ajili ya mazoezi ya viungo na masuala mbalimbali: Je, Mheshimiwa Waziri haoni jambo hili ni muhimu kwa afya za Wabunge na wafanyakazi? Ningeshauri suala hili Mheshimiwa Waziri angesimamia katika Ofisi ya Bunge ili waweze kukamilisha mpango ambaeo ulishaandalowi, kilichobaki ni utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba Mheshimiwa Waziri ajue ni jukumu lake kutafuta wadau wa michezo ili kuisaidia timu hii ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuendeleza michezo pamoja na vijana katika kujipatia maendeleo na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Vyombo vya Habari binafsi vina mchango mkubwa kwa Taifa letu, lakini umefika wakati kuangalia upya vyombo vya binafsi maana vingi vyao haviendi na maadili ya nchi yetu, pia huenda vikaleta madhara yaliyowapata wenzetu nchi ya jirani kama Burundi. Kwa kuepusha hayo, naomba Wizara ikishirikiana na Serikali kuu, iwe makini katika kutoa leseni kwa vyombo vya habari binafsi, pia kuweka sheria kali ambazo zitawenza kudhibiti vyombo hivyo ili visilete madhara kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, *TBC* ndio chombo chetu kikuu tunachokitegemea katika habari kwa Taifa letu. Iko haja ya kukiimarisha na kikitengenezea mazingira mazuri ya kufanya kazi. Wizara ikishirikiana na Serikali kuu, iko haja ya kuipatia dhamana Shirika hili kutoka *NSSF*, ili ipate kujengewa jengo lake ambalo muda mrefu lipo halijamalizwa. Katika bajeti ya mwaka huu: Je, Wizara itaishinikiza Serikali kuu ili kupatikana dhamana kwa *NSSF* ili jengo la *TBC* litengenezwe?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iweke kipaumbele katika kuhifadhi kanda zetu za zamani ambazo ni hazina kubwa kwa Taifa letu, na baadhi ya nyingine zimeshaanza kuharibika. Sehemu hii ya hifadhi ya Rekodi za Asili, ni mbovu. Sasa itengewe fedha nyingi zitakazowenza kuhifadhi hazina zetu hizi. Ushauri wangu huu ni kwamba wakati wa teknolojia sasa umefika, wakati wa kubadilisha mbinu za uhifadhi wa rekodi zetu, kutoka *analogue* kwenda *Digital* ili tuwe na uhakika wa kuhifadhi rekodi zetu kwa muda mrefu tena bila ya kuharibika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa kwa wasanii wetu kukosa mapato yao yanayotokana na kazi. Iko haja Wizara kuweka mikakati madhubuti ya kulinda kazi za wasanii na kujulikana. Hii itasaidia wasanii kupata mapato yao yanayotokana na kazi zao, pia Serikali itapata pato lake linalotokana na wasanii wetu na pia kutapunguza kuvuja kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. DAVID M. MALOLE:** Mheshimiwa Spika, Mchezo wa Bao ni mchezo wenye historia kubwa sana hapa nchini. Kupitia Bao, Baba wa Taifa Marehemu Julius Kambarage Nyerere aliweza kuhamasisha wananchi kuona umuhimu wa kujitawala wenyewe. Kwa vile mchezo wa Bao huchezwa na watu wenyewe umri wa utu uzima, watu waliweza kuelewa, kuhamasika na wao wenyewe kuhamasisha wengine, na mwisho uhuru ulipatikana. Bao bado linachezwa sana hapa nchini. Katika Jimbo la Dodoma Mjini na linachezwa kwa nguvu sana kwenye vituo vingi vya migahawa. Ni burudani kubwa sana kwa watu wa heshima na wazee wengi hata vijijini. Hata hivyo, mchezo huu unaonekana kukosa msaada (*support*) kutoka Serikalini na watu binafsi. Wacheza Bao hawana sehemu maalum za kuchezza bao. Wengine huchenza chini ya miti, na kuendelea kuhamisha bao ili kufuatilia kivili cha mti kinakoelekea.

Aidha, mvua zikija, mchezo huvurugika na kusimama hadi mvua zitakapokatika. Baadhi ya mabao pia yamechakaa na baadhi ya Kete za Mabao hayo kupungua. Ili kuenzi historia ya nchi yetu na mchezo wa bao, naomba Wizara yako Tukufu iangalie uwezekano wa kuweka angalau vibanda vidogo vya gharama nafuu, vyenye heshima kwa ajili ya mchezo huu, maeneo ya mjini na vijijini. Aidha, Serikali isaidie kununua mabao mapya na kete mpya. Natambua ufinyu wa bajeti, lakini Serikali ingeweza kuanza kwa awamu, hasa kwenye Mikoa ambapo Bao lilitumika sana kuhamasisha uhuru wa nchi yetu, ikiwemo Mikoa ya Dodoma na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Mataifa ya nje pia yanapenda sana utamaduni. Wafadhili wangeweza kutafutwa ili kufadhili mchezo huu wenyewe heshima na historia kubwa sana katika nchi yetu. Mashindano makubwa yangeweza kufanyika pia nchi nzima, siku ya "Nyerere Day" na yangeweza kuhusisha hata michezo mingine inayofanana na mchezo wa Bao, yaani michezo ya ZUMNA na Karata.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina utajiri mkubwa sana wa tamaduni mbalimbali ambazo hujieleza kwa mfumo wa michezo. Hapa Dodoma kuna michezo mbalimbali ya kiutamaduni na inasisimua na kuvutia sana. Michezo hiyo ni pamoja na Nindo, Misunyunho, Marimba, Mazeze na mingineyo mingi.

Wakati wa Uhuru wa Msumbiji Wagogo walitia fora na kuacha simulizi kubwa huko Msumbiji. Naomba Wizara yako Tukufu ifufue mashindano haya ya michezo ya Nindo, Misunyunho, Mazeze na Marimba, ili kukuza na kudumisha michezo ya utamaduni wa Taifa letu. Dkt. Zawose alitia fora katika michezo ya ala za muziki, kumbukumbu zake zipo hadi nchi za nje. Tuenzi utamaduni wa nchi yetu unaosifika mahali pote duniani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wimbo wa Taifa ni alama muhimu sana katika nchi na wengine maana yake hawajui, bali hufikiri ni wimbo tu ulio mzuri kuimba, na wakati wa kuimba watu huwa katika staili tofauti, mwingine ananyooka na kadhalika. Tatizo hilo ni kubwa zaidi hasa kwa vijana wetu ambao hawajapitia jeshini au JKT.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri kutumia bajeti yake kulelimisha Bunge kwani Wizara hii pia ni muhimu katika kutunza utamaduni na heshima ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika kuendeleza michezo mashulen, walimu wamekuwa wakijienendeza kupitia Diploma za michezo, lakini wanaporudi shulen Diploma hizo zimekuwa hazitambuliki, tofauti na nyngine za ualimu, hivyo wenzao kupandishwa vyeo na wao kubaki wakiangalia tu na kukatishwa tamaa.

Je, Waziri unalifahamu hilo? Kama ndiyo, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha tatizo hilo linaloleta kero katika uendelezaji wa sekta hii ya michezo hususan katika Shule za Sekondari hasa baada ya kurudisha michezo mashulen? Naomba jibu ama sivyo nakushika katika kifungu.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kumpongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo - Mheshimiwa Emmanuel J. Nchimbi kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza Naibu Waziri - Mheshimiwa Fenella E. Mukangara, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, lipo kundi kubwa sana la vijana ambalo linalalamikia kutokuwa na ajira na hivyo linashinda vijiweni kucheza Kamari, Karata na *Pool table*, na wanafanya hivyo kwa kisingizio cha "hakuna ajira" wakati zipo njia nyngi za kujajiri. Vijana wengi hawajiungi katika vikundi nya ujasiriamali. Ushauri wangu, naomba Serikali ipange mkakati madhubuti na kuratibu mienendo ya vijana, kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ili iweze kupata elimu ya ujasiriamali ili vijana hao waweze kuelimika na baadaye waweze kujajiri wenye.

Mheshimiwa Spika, michezo ni afya na michezo ni ajira, na Mheshimiwa Rais wetu amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha michezo inapewa kipaumbele. Ni kwanini katika Halmashauri zetu hakuna fungu la michezo linapangwa kwa ajili ya kusaidia wachezaji wa mpira wa miguu, *Netball*, Maigizo na sanaa mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, Wachezaji wa timu zilizopo katika Halmashauri zetu na timu za Mikoa huishia kuombaomba michango kwa watu mbalimbali na hali hii kuwapelekea kukata tamaa, na wakati mwingine kushindwa kushiriki katika mashindano mbalimbali. Je, isingekuwa vizuri Serikali kuagiza Halmashauri kupanga kifungu cha kusaidia michezo wakati wa bajeti ili kuweza kusaidia kukuza vipaji nya michezo katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nawatakia kheri Waislam wote wanaofunga katika mwezi huu wa Ramadhan. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo inayoweza kutoa msukumo wa ziada katika matumizi sahihi na fasaha ya lugha yetu ya Kiswahili. Pamoja na kwamba Serikali inatoa tamko kwamba Kiswahili kiwe ndiyo lugha rasmi ya kiofisi na sehemu mbalimbali, lakini cha kushangaza, viongozi hao hao ndiyo wa kwanza kuhutubia Mikutano kwa Kiingereza na hata sheria tunazotunga bado zinaletwa kwa Kiingereza na hatupati tafsiri zake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa Serikali ilete Sheria ya Vyombo vy'a Habari. Hii itasaidia sana kumlinda Mwanahabari, mwenye kumiliki vyombo vy'a habari, Mtoa habari na Mtolewa habari kwani sasa hakuna sheria yoyote inayolinda katika taaluma hiyo. Je, ni lini sheria hiyo italetwa?

Mheshimiwa Spika, maslahi ya wanahabari ni vyema yakaangaliwa vizuri, kwani kuna vyombo ambavyo havilipi vizuri, matokeo yake, mianya ya rushwa ndogo ndogo hutokea na kupelekeea kutokuwa na maadili kwenye fani, kwani Mwandishi atalazimika kuandika kile anachoona kitamfurahisha aliyemضا.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Habari lipewe mamlaka ya kisheria ni vipi Serikali inajipanga na ni lini Baraza hilo litapewa mamlaka hayo?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kujipanga katika kubuni ajira kwa vijana maana ongezeko lao ni kubwa sana?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, Taifa lolote lisilo na utamaduni wake ni Taifa liliokufa. Taifa lisiloenzi tamaduni zake na kuzithamini, Taifa hilo lina tatizo. Taifa linalofyonza tamaduni za Mataifa mengine na kupuuza tamaduni zake kadhalika lina matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo maandiko na maneno matamu kwamba tunaenzi utamaduni wetu. Kuuendeleza na kuulinda, kunatia mashaka sana, hakuna juhudzi zinazoonekana za kutimiza hayo tunayoimba kila siku. Ni jitihada zipi za makusudi ambazo zimeelekezwa katika ngoma zetu na michezo yetu ya jadi, lugha zetu za asili na hata lugha ya Taifa Kiswahili, mavazi yetu na mengi mengineyo ambayo ni utambulisho wa Taifa hili? Tumefikia wapi Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika mfumo wa elimu wa nchi yetu? Tumefikia wapi juu ya Vazi la Taifa? Hivi vimini na *short pants* ndio utambulisho wa Taifa hili?

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu ususi na ufinyanzi. Tumepiga hatua gani au tumeridhika na nywele za Wazungu wanazovaa dada zetu? Ni kwanini tunadekeza kila kitu hata tamaduni za ovyo ovyo? Leo wanawake wengi katika nchi yetu, hata viongozi wanaukana uafrika wao kwa kisingizio cha utandawazi, maendeleo na vurugu za makundi ya wanaharakati ambaa wanapoteza hadhi na heshima ya mwanamke na hususan mwanamke Mtanzania na kama Taifa tumepiga magoti kwa fikra ambazo zinapoteza heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hatufanyi juhudzi kubadili na kuuendeleza michezo, tuna programu ambazo hajizaleta tija na wala hatuoni kama zinahitaji kuangaliwa upya. Hakuna mkakati wa mafunzo kwa walimu wa michezo kuwa na mwalimu mmoja wa Taifa ambaye anashughulikia timu moja tu badala ya kufundishia walimu wa timu za Mikoa au vilabu ili kuwa na mfumo unaoeleweka nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naamini tutaendelea kubakia hapa tulipo kwa kuwa na timu ya Taifa wanatoka katika vilabu vya Simba na Yanga badala ya nchi kavu ulivyokuwa huko nyuma, ukiona mchezaji wa Timu ya Taifa akitoka Mwanza au Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuwa na mjadala mpana, tunalipeleka wapi Taifa letu?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, niruhusu nimpongeze kwa dharti Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Pamoja na pongezi hizi, ninayo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, Wadau wa habari nchini kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakidai kutungwa sheria mpya ya habari na Serikali iliahidi kuleta Muswada wa habari hapa Bungeni, lakini hadi sasa hatujaletewa Muswada huu ili tuupitishe na uwe sheria ya habari. Naiomba Serikali ilete mswada huu haraka iwezekanavyo kwa ustawi wa Sekta ya Habari nchini. Waandishi wa Habari nchini (walio wengi) hawajaajiriwa rasmi bali hupewa vibarua kwa kuandika makala kwenye magazeti. Waandishi hawa wanalipwa kiasi kidogo sana cha fedha kisichotosheleza mahitaji yao ya msingi kama chakula, malazi, mavazi na kadhalika. Je, Serikali kuitia Wizara hii inajipanga vipi kutatua matatizo ya ajira na mafao ya wanahabari wetu?

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kurejesha michezo katika Shule zetu za Sekondari na Shule za Msingi. Tatizo liliopo ni uhaba wa vifaa vya michezo, mfano jezi, mipira, nyavu hata walimu wa michezo. Serikali itenye fedha kwa ajili ya kununua na kupeleka vifaa mashulenii.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumekuwa tukishuhudia magazeti mengi yakiandika habari za uchochezi yanayoweza kuleta uvunjifu wa amani nchini. Je, Serikali inachukua hatua gani za kuondoa kabisa tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, miji mingi hapa nchini ina kiwanja kimoja cha michezo na mara nyingi wananchi wa kawaida hawapati nafasi ya kufanya mazoezi katika viwanja, hivyo kutokana na uongozi wa viwanja hivyo kutoruhusu wananchi kuingia: Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuongeza viwanja Mikoani, Wilayani na hata kwenye Tarafa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kabla sijaanza kuchangia hoja hii, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mimi naanza kuchangia kuhusu maadili ya vijana wetu yalivyomomonyoka hasa kwa upande wa kivazi hasa wasichana. Kwa sababu vijana wa kike kivazi wanachovaa ni kivazi ambacho hakiendani na heshima yetu ya kitanzania, na hakuna chombo chochote ambacho kinatoa elimu au kukaripia kivazi hicho.

La kushangaza, kwa upande wa wasanii wanaume, wanavaa nguo za heshima, lakini wasanii wanawake ndio wanavaa kivazi cha kuwdhalilisha kabisa. Kwa sababu wanavaa nguo ambazo ni sawa na kutovaa nguo. Sehemu ya mwili wao ambao wanatakiwa wauenzi, ndio wanaouacha uchi kabisa bila nguo.

Mheshimiwa Spika, sasa umefika wakati wazee wa watoto kukemea jambo hili, lakini hata Serikali isimamie neno na kulikomesha kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kujitahidi sana kukuza michezo wa mpira wa miguu kwa kuleta walimu wa michezo huo.

Mheshimiwa Spika, nasikitishwa na mtindo ulioingia hivi sasa hapa Tanzania, wananchi, Watanzania wanathubutu kuzishangilia timu za nje kuliko timu ya nyumbani. Kama Yanga itacheza, basi wapenzi wa Yanga watashangilia timu ya Yanga, lakini wapenzi wa Simba wote wataishangilia timu ya nje ya Tanzania. Vilevile kama Simba itacheza, basi wapenzi wa timu ya Yanga wote wataishangilia timu ya nje ya nchi. Kwa kweli staili hii inavunja moyo wa kizalendo. Nadhani ni vizuri sasa Watanzania tubadilike.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa timu za nje ya nchi hazina shida ya kutafuta mashabiki wa kushangilia wakati wakija hapa Tanzania, mashabiki wao wanatokea hapa hapa Tanzania nao ni Watanzania. Tunajikaanga kwa mafuta yetu wenywewe.

Mheshimiwa Spika, Waandishi wetu wa habari na vyombo vya habari hivi sasa wana mfumo wa kushabikia zaidi jambo lenye utata kuliko jambo la maendeleo na jambo la kujenga

nchi yetu, na hata wananchi nao wako hivyo hivyo. Ni bora vyombo hivyo viwajibike kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa mambo ya kujenga nchi yetu pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kwa yale ya kuwaweka wananchi wetu wawe na imani na nchi yao, siyo ya utata tu.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vina mtindo wa kuegemea baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wengine hawana habari nao. Hata wachangie vizuri, basi aah, hawana habari nao kabisa jambo ambalo linatia wasiwasi. Kwanini wawe na upendeleo wa hali ya juu? Au wanapata kitu fulani? Lakini nashauri vyombo hivi vya habari vinaona Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar hawana haki kwenye vyombo hivyo kwa sababu hata wachangie pipi hapa Bungeni, basi hawana habari nao, labda wachangie jambo la utata, hapo ndipo wataeleza kwa kirefu kwa sababu ni la utata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naviomba vyombo hivyo vibadilike, vitoe haki kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Ahsante.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya kukuza michezo, kuhabarisha Watanzania na kukuza utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada ya Serikali kuleta makocha wa Mpira wa Miguu, Ndondi na kadhalika kutoka nje ya nchi, bado hatujapiga hatua kubwa katika michezo. Nafasi tunayoshikilia katika orodha ya dunia katika mpira wa miguu bado ni mbaya. Bado riadha hajaturudisha pale tulipofika miaka ya 70, wakiwa akina Filbert Bayi, Nyambui na kadhalika.

Kwa ujumla, Sekta ya Michezo inahitaji kujipanga vizuri zaidi kutoa picha kamili, ni pipi itatufikisha huko tunakotaka kufika? Ni muhimu matayarisho ya michezo yaanze ngazi za chini ili kuibua vipaji. Ni vizuri pia kutenga bajeti ya kutosha katika kuandaa timu ili tuwe washindani katika michezo ya kimataifa na sio wasindikizaji siku zote. Tuifanye michezo iwe sehemu ya kazi ili wachezaji wafaidike na michezo waichezayo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imepiga hatua kubwa katika kutoa habari kutokana na kuwa na vyombo vingi vya habari kama TV, redio na magazeti. Tatizo kubwa katika wanahabari wetu ni kuwa sio "professional" katika habari wanazoiandika. Mwandishi wa michezo au uchumi ni vizuri awe amejikita zaidi katika fani hizo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine, waandishi wengi hawaandiki taarifa zilizofanyiwa utafiti wa kina, badala yake kujikita kuandika habari za viongozi wa Siasa wanapotembelea maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni "*quality*" ya habari zinazoandikwa. Habari nyingi zina mwelekeo wa kibashara kuliko taaluma. Hivyo hazisaidii sana kuwaelimisha Watanzania na badala yake zinaandika mipasho, malumbano, tuhuma na kuwgawa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, japo Wizara inajitahidi kudumisha utamaduni wa Mtanzania, lakini vipindi vingi vya redio na TV vinamomonyoa maadili ya Mtanzania. Naomba vipindi vyote vya TV zote viangaliwe na Wahariri kabla ya kurushwa hewani, kwani vipindi vingine ni aibu hata kuangalia ukiwa na familia yako nyumbani.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, natoa hongera kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kazi nzuri inayofanya, pia kwa hotuba nzuri. Kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha michezo nchini kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni, imedhihirika wazi kwamba Serikali ikiweka msisitizo katika michezo, sekta hii inaweza kuimarika zaidi na zaidi. Hivyo, naishauri Serikali sasa itilie mkazo uanzishwaji wa "*Sports Academy*" nchini ili kukuza vipaji vya michezo kwa vijana wetu tangu wakiwa wadogo mashulenii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na ukarushaji wa baadhi ya taarifa za magazeti kwamba siyo za kweli. Je, Serikali imeandaa vipi mazingira ya kuwawezesha waandishi wa habari kuzithibitisha taarifa hizo kuwa ni za kweli kabla hazijatolewa magazetini?

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia vijana, tuna maana ya vijana wasichana kwa wavulana. Lakini kuna tatizo kwamba wanapoitwa vijana wanaojitokeza wengi wanakuwa wavulana. Ni ushauri wangu Serikali ihamasishe vijana wote wa kike na kiume kujitokeza kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imeweka mpango gani wa kutekeleza mkataba wa kimataifa kwa kuhifadhi utamaduni usioshikika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, michezo katika ulimwengu wa leo siyo tu ni burudani bali pia ni ajira takatifu kwa wachezaji walio na vipaji kulipwa hadi USD 150,000 kwa wiki. Hivyo ni vyema Serikali ikajipanga kibiashara ili mfumo wa umiliki wa klubu zetu uwe wa kikampuni inayomilikiwa ama na mtu, watu au wanachama wote (*Public Co.*) Aidha, Serikali itafute Mshauri Mwelekezi wa namna ya kubadilisha mfumo wetu wa michezo hasa mpira wa miguu ili tuweze kutoa vijana wenye vipaji.

Mheshimiwa Spika, Taasisi za Habari zimekuwa kama mhimili wa nne wa mfumo wa utawala katika dunia ya leo. Hivyo, nashauri Serikali ifanye yafuatayo:-

- (1) Kuvihakiki vyombo vyote vya habari kama vinatimiza viwango kama sheria inavyotaka;
- (2) Kuvielekeza vyombo vya habari kujiepusha na upendeleo wowote, kwani wao kazi yao kubwa ni kutoa elimu na taarifa kwa umma;
- (3) Vyombo vipunguze matangazo na nyimbo zinazoonyesha nusu uchi wanasanaa;
- (4) Serikali ijipange vizuri katika kuititia sheria ya habari ili kila upande uwe na ulinzi unaostahiki.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona suala la *FIFA* na *ZFA* limechukua muda mrefu wakati nchi kama *United Kingdom* nchi zilizomo ndani ya umoja huo zinashiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa: Je, inashindikanaje kwa Serikali ya Muungano kuiruhusu Zanzibar ijiunge na *FIFA* ili tuwe na fursa ya sisi wawili kushiriki katika mashindano yanayoandalishi na *FIFA*? Mbona Zanzibar inashiriki katika michezo ya Afrika Mashariki? Wakati umefika kwa *SMT* kumaliza mgogoro huu.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Wizara ya Michezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuendeleza michezo na utamaduni. Pamoja na jitihada zake, upande wa utamaduni jitihada ni ndogo. Mfano Wizara imesimamia ngoma za asili tu. Tuna mengi ya utamaduni wetu, mfano kuna majigambo, matambiko, mila na desturi. Jambo hili ni muhimu ili kusaidia wananchi na kizazi hiki kijue utamaduni wetu badala ya kuenzi utamaduni wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la upotoshaji wa habari kwa makusudi, hii kwa mtazamo wa haraka, vyombo hivi huwa wanaangalia maslahi yao binafsi ili wauze magazeti yao. Naomba Wizara ilisimamie jambo hili na kuhakikisha lisendelee tena maana ni chanzo cha kuvuruga amani.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo, nashauri lirudishwe mashulenzi, vyuoni na kwa wananchi nchi nzima. Kulikuwa na mashindano ya michezo mbalimbali wakati wa Sherehe za Kitaifa, na ilikuwa inahamasisha kuleta mshikamano na amani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia na kutoa maoni yangu. Michezo ya kimataifa mfano *Olympic* wahakikishe washiriki wanatafutwa au washindanishwe kuanzia ngazi ya *Kijiji* hadi Taifa. Hii itasaidia kuibua vipaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na utukufu wake kwa kutuwezesha kuwa hai na uzima.

Mheshimiwa Spika, nami nachangia mada iliyopo mbele yetu kwa kuanza na Chama cha Mpira cha Tanzania (*TFF*). Kwa maoni yangu binafsi, Tanzania ni Muungano wa nchi mbili, Zanzibar na Tanganyika. Kwa maana hii, kama siyo Muungano huu, Tanzania ingekuwa hapana Chama cha Mpira wa Miguu (*TFF*). Chama hiki ndicho kinachoongoza michezo wa mpira Tanzania. Lakini ukiangalia vizuri, utakuta chombo hiki cha *TFF* kimechukua jukumu la Tanzania, lakini utendaji wake ni upande mmoja tu wa Tanzania Bara, upande mmoja wa Tanzania Visiwani unalalamika hautendewi haki.

*TFF* imevaa koti la Tanzania, lakini kwa sababu ambazo nitaweka wazi, utaona chombo hiki kinafanya kazi upande mmoja, upande mwininge wa Muungano haufaidiki. Sababu ambazo naweka wazi ni kama ifuatavyo:-

- (i) Katiba yake inazungumzia Tanzania Bara peke yake;
- (ii) Viongozi wake wanaoongoza, wote wanatoka Tanzania bara;
- (iii) Waliowachagua kuongoza *TFF* ni Tanzania Bara peke yao;
- (iv) Mipaka ya *TFF* ni Tanzania Bara peke yake Mikoa 21 tu;
- (v) Utendaji wa nje ya Tanzania *TFF* inawakilisha Tanzania Bara tu; na
- (vi) Misaada yote kutoka *FIFA* na *CAF* inatumika kwa maendeleo ya Tanzania Bara pekee.

Mheshimiwa Spika, hii ni baadhi tu ya mifano, lakini ipo mingi zaidi na zaidi. Kutokana na mfumo huu na utendaji huu, utakuta Mdau mwenza wa Muungano amekuwa ni mdandiaji tu na sio mshirika.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, lakini pia inadumaza maendeleo ya mpira wa miguu hasa Zanzibar. Vile vile Zanzibar inaathirika kama ifuatavyo:-

- (i) Kutokupata Zanzibar fursa ya kuwa mwanachama *FIFA* na *CAF*;
- (ii) Zanzibar kutotambulika katika anga za kimataifa;
- (iii) Kutoshiriki Zanzibar katika program zozote endelevu kutoka *FIFA* na *CAF* zinazohusu Zanzibar kama nchi;
- (iv) Vijana kukosa fursa ya kushiriki mashindano yote ya kimataifa na yale ya michezo kutoka *FIFA* na *CAF*;
- (v) Zanzibar inatoweka kidogo kidogo katika ulimwengu wa soka; na
- (vi) Chama cha mpira wa Zanzibar kukosa misaada yote kutoka *FIFA* na *CAF* na kuwa na wakati mgumu katika utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, TFF kuvaajohoh la Tanzania kuunda Chama cha Mpira na huku ikijua kwamba Tanzania ni nchi mbili zilizoungana, halafu chombo hiki kikafanya kazi upande mmoja, hii ni dhuluma ya makusudi. Mimi namwomba Waziri atakaposimama kwa majumuisho anifafanulie vizuri kuhusu tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa leo ni hayo tu. Nasubiri jibu. Ahsante.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani, ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la Habari, kumekuwepo na uhuru mkubwa sana wa vyombo nya habari ambavyo kwa namna nyngine vinafikia mahali sasa badala ya kuelimisha jamii, imekuwa ni kupotosha jamii na saa nyngine kuleta picha au taarifa za aibu kwa jamii hususani magazeti ya udaku. Magazeti haya yanapotosha kabisa na kutuletea utaratibu ambao ni tofauti na mila na desturi zetu. Magazeti haya yanachapisha picha za utupu kuandika habari ambazo zinapelekea kuwa za kimahaba zaidi ambazo siyo za kujenga maadili, hususan kwa watoto. Serikali iangalie utaratibu wa kurelesha maadili ya vyombo hivi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, bado kuna maeneo katika nchi yetu hayafikiwi na mawimbi ya radio yetu kongwe ya *TBC*. Naomba chombo hiki kihakiki tena masafa ya mawimbi yake kwani bado tuna wananchi ambaao hawana uwezo wa kununua *7V* pamoja na hili tatizo sugu la ukosefu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, karibu asilimia 60 ya wananchi wote ni kundi la vijana. Na katika hao asilimia 14 hawana ajira rasmi. Ni kweli kuwa vijana wengi wanategemea ajira ya kuajiriwa maofisini, lakini Serikali hii ina wajibu wa kutafuta mbinu mbadala ya kupunguza kundi hili la vijana vijivjeni.

Hii inawezekana kwa kufufua viwanda vyatia *VETA*, *FDC* na pia kujali vipaji mbalimbali vyajijana hawa. Kuna vijana wana vipaji vyatia uchoraji, ufundi mbalimbali, lakini bado hawapewi nafasi katika shughuli mbalimbali ili kuonyesha vipaji vyao ili viweze kuthaminiwa na kupewa kipaumbele na Serikali. Sasa ni muda muafaka wa kuyaangalia makundi haya kwa karibu sana na kuyasaidia kuendeleza vipaji hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala la utamaduni wa nchi hii limeachwa nyuma kabisa. Leo hii hatuna kumbukumbu za makabila yetu, mila zetu na tamaduni zetu za asili. Kizazi tulichonacho sasa hakina kumbukumbu ya mambo haya, ukizingatia watoto wetu wanasoma shule za bweni tangu shule za misingi mpaka vyuo. Hivyo muda wa malezi toka kwa wazazi (*parental care*) unakuwa kidogo. Naiomba Wizara sasa kutengeneza mpango mahsusini wa kukusanya na kuhifadhi kazi na taarifa za tamaduni zetu ili ziwafae watoto hawa kuelewa wapi asili yao na tamaduni zao. Mfano, Mwanahabari Suleiman Mkufya alivyofanya tafiti katika kabilo Wasubi ambao asili wao ni wakazi wa Wilaya ya Biharamulo, iapo sasa hivi kuna mwingiliano wa makabila.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo limepeewa umuhimu, lakini kwa kipaumbele cha mpira wa miguu na mpira wa pete. Tanzania tunayo michezo mingi na mingine ikiwa ni ya asili. Michezo hiyo ni kama kuvuta kamba, ngoma zetu za asili na kadhalika. Lakini umekuwepo ule mfumo ambao siyo rasmi wa kumiliki viwanja vya michezo hii katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo sasa Serikali inapaswa kulifanyia kazi kwa haraka. Kuna viwanja vingi sana ambavyo vipo katika Halmashauri mbalimbali za Wilaya ambavyo kimsingi ni mali ya Halmashauri. Lakini viwanja hivyo sasa vinasemekana kumilikiwa na Chama cha Mapinduzi. Viwanja hivi vimechakaa sana, havina matengenezo wala uendelezwaji na hii imepelekea kudumaa kwa michezo kwa sababu ya kukosa viwanja bora. Naiomba Wizara/Serikali kutoa kauli kuhusiana na viwanja hivi. Viwanja virudishwe kwenye mamlaka ya Halmashauri na vikarabatiwe ili kukuza michezo, kwani michezo ni afya, michezo ni akili na michezo ni ajira.

Mheshimiwa Spika, ni wakati sasa Serikali inaweza kupunguza tatizo la ajira kwa kuendeleza sekta ya michezo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa nimechangia hoja hii kwa kuongea, naomba niongeze yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wasambazaji wa kazi za sanaa hasa Muziki na Filamu wamekuwa wakiwanyanya wasanii na pia kuwanyonya kwa mikataba ambayo ni batili, pia hukataa kazi za wasanii wapya kwa kuwataka wawe wameshirikisha wasanii wenyе majina makubwa ndipo wakubali kazi zao. Sasa je, Wizara haioni kwamba umefika wakati wa kuunda chombo maalum cha Serikali na kutoa leseni kama ilivyofanya kwenye suala la mafuta kwa kutoa leseni *TPDC* ili waokoe jahazi na kuondoa ukiritimba kwa wasambazaji? Hivyo naomba, jamani toeni leseni kwa chombo cha Serikali ili kiwe kinasambaza kazi za sanaa, na ukiritimba utakwisha, hata wizi utapungua, ama kwisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la waandaaji wa tuzo mbalimbali za wasanii, ni vyema wakawa na utaratibu wa kupitia kwenye shirikisho husika, mfano, kama ni Muziki au filamu, ili kuwe na nidhamu na haki kwa usawa na mashirikisho yote yawewe kuwa na uzito.

Mheshimiwa Spika, je, kwanini Serikali huwalipia wachezaji wa michezo mingine kama Mpira wa miguu na kadhalika, wanapokwenda nje au riadha na kadhalika, lakini hakuna Msanii yejote ambaye amewahi kulipiwa? Yaani labda kikundi kinachokwenda kuwakilisha nchi kwenye matamasha ama vinginevyo vyovoyote, kwanini, na hali huenda huko wakipeperusha bendera ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna Msanii wa kike toka Tanzania, Yvone Cherry (Monalisa) ameteuliwa kugombea tuzo ya *Pan African Actress of the year (East Africa)* katika tuzo za *NEA (Nigeria entertainment Award) September New York*, lakini nashangaa hata Watanzania hawajahabarishwa jambo hili. Kwanini? Yaani Wizara tuwafanye nini ili mtuthamini? Huyu dada anatakiwa apigiwe kura ili ashinde, atashindaje hata watu wake hawajui, hali amebeba jina la Tanzania? Jamani, hebu Waziri naomba basi angalau ultambue hilo, utangaze na Watanzania wajue, wampigie kupitia [www.nigeriaentaward.com](http://www.nigeriaentaward.com), kwani kura zao, zitaitangaza Tanzania katika ulimwengu wa sanaa, na mwisho wa kupiga kura ni mwisho wa mwezi huu, wako wasanii sita toka Afrika. *Please!* Kila mpiga kura atumie jina lake halisi la Yvone Cherry, kwani la Monalisa ni la kisanii tu.

Mheshimiwa Spika, tafadhali ninaomba *Studio* zote zitambulike kwa kupata cheti cha *BASATA* ili kudhibiti ubora wa kazi.

Mheshimiwa Spika, wasambazaji wote, *DJ's* ambao wengi huunganishwa na *MC's Promoters*, Mameneja wa Wasanii wote hawa naomba watambulike *BASATA* na walipe fee *BASATA* ili kudhibiti udhulumwaji wa wasanii.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi – Waziri Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Mheshimiwa Dkt. Fenella Mkangara - Naibu Waziri kwa jitihada kubwa wanazofanya kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za sekta zilizo chini ya Wizara ili kuleta ustawi na maendeleo ya vijana, wanamichezo, wasanii na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Katibu Mkuu - Bwana Sethi Kamuhanda na Watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nafuatialia kwa karibu jitihada zinazofanya na wadau mbalimbali kwa lengo la kuwezesha vijana kujiedeleza na hivyo kujitegemea. Hata hivyo, sijaona mikakati ya muda mrefu ya kuwezesha vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi ili wachangie maendeleo ya Taifa na kijiwekea msingi wa maisha ya baadaye. Nashauri hatua zifuatazo zichukuliwe ili kulinda na kukuza maslahi ya vijana nchini.

- (a) Sekta zote nchini zijumuise kwenye mipango yao ya maendeleo, program za kuendeleza vijana kijamii na kiuchumi;
- (b) Program ya Kilimo Kwanza iweke sehemu maalum itakayohudumia vijana kupata ardhi na mtaji ili washiriki kuzalisha mali na kuchangia maendeleo ya Taifa; na
- (c) Serikali itambue maendeleo ya vijana kuwa kipaumbele na hivyo itenge fedha za kutosha kwa Idara ya Vijana kwa ajili ya kuwaendeleza kitaalamu, ajira, kimichezo na kiutamaduni ili wajenge uwezo wa kuliongoza Taifa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maendeleo yaliyofikiwa duniani, hivi sasa michezo imethibitika kuwa siyo upotezaji wakati na rasilimali, bali kuchangia maendeleo ya afya ya mchezaji, hujenga umoja mionganoni mwa wachezaji, watazamaji na hata wasikilizaji kuptitia redio na chanzo kizuri sana cha mapato. Miaka iliyopita, Serikali ilikuwa na Maafisa michezo kwenye ngazi ya Wilaya. Maafisa hao waliratibu na kufuatilia uanzishwaji wa vilabu na kuwezesha vilabu hivyo kutokana na bajeti ya Serikali. Hivi sasa wakati ambapo michezo imepata umuhimu mkubwa zaidi kwa kuwa ajira kwa vijana, Serikali inaipa michezo umuhimu mdogo sana. Naomba Serikali iajiri Maafisa michezo na watengewe fedha za kutosha ili kuwaandaa vijana na watu wote kushiriki michezo.

Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili ina msingi wake nchini Tanzania. Hata hivyo, inasikitisha kuona kuwa fursa zinazopatikana katika mashirika ya Kimataifa huenda kwa Wakenya na Wanigeria. Tatizo nililoliona ni Serikali yetu kutokuwa na mpango wa kusaidia wahitimu wa Shahada za Kiswahili wajenge uwezo kuwa Wakalimani na kuwahamasisha (kupitia Balozi zetu na Wizara) kuomba kazi zinapotangazwa kwenye mashirika ya kimataifa. Nashauri kuwa Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Diplomasia ianzishe kozi maalum ya kuandaa wahitimu wa lugha kutoka vyuo vyetu kujandaa kushiriki katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Magazeti ya Serikali limekuwa likisimamiwa na Kaimu Mhariri Mtendaji kwa muda mrefu sana. Nini kinakwamisha uteuzi wa Mhariri Mtendaji? Kama anayekaimu amemudu, kwanini hajathibitishwa? Kama hajamudu, kwanini nafasi hajiazwi?

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa magazeti haufanyiki ipasavyo, magazeti yanachapisha lolote lile bila kujali athari zake kwa mahusiano kwenye jamii na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Idara ya maelezo ya jamii kwa ujumla, Idara ya Maelezo iimarishwe na watumishi waongezewe maslahi kwani wanasmamia tansia tete sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri zinazofanya ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu inagusa vijana ambao ndiyo nguvukazi ya Taifa inayotegemewa sana. Katika Sekta ya Madini vijana wengi wanajishughulisha na kazi ya kuchimba madini, kuchenjua. Kazi hizi ni ngumu na ni hatari, wakati mwingine vijana wetu wengi huathirika na kufa ndani ya mashimo kwa kukosa teknolojia na vitendea kazi vya kisasa. Sekta ya Madini imeajiri vijana wengi sana kutokana na *nature* ya kazi yenye. Wanaofanya kazi ya kuchimba madini zaidi ya asilimia 70 ni vijana. Nimetembelea sana sehemu za machimbo hasa jimboni kwangu Busanda kwenye machimbo ya Nyaruguru, Rwangasa, Nyakagwe Mgusu wanaochimba kwenye duara ni vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara inashughulikia masuala ya vijana, ninaomba mkakati maalum uwepo wa kuwaendeleza vijana wanaojishughulisha na uchimbaji madini.

Napendekeza watengewe bajeti maalum itayowawezesha kujengewa uwezo ili wawe na teknolojia za kisasa, pia kuwepo na mtaji ili kuwakopesha wanunue vifaa vya kisasa ili kuboresha

mazingira ya utendaji kazi kwa vijana hawa. Mikopo kwa vijana kupitia Halmashauri ni kidogo sana, hivyo haziwezi kukidhi mahitaji makubwa wanayohitaji wachimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Wizara ibaini makundi maalum ya vijana wanaofanya shughuli maalum ili ione namna ya kuwasaidia vijana hawa. Kwa kuanza ni hawa wachimbaji wadogo wadogo, vijana, na makundi mengine. Mfano, vijana wanaojishughulisha na uvuvi, na michezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba Waziri aseme atawasaidiaje vijana wangu wa Busanda wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini, hasa katika bajeti ya mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka kipaumbele katika kuleta uhuru wa habari hapa nchini. Napenda kupendekeza yafuatayo yafanyike ili kuongeza tija katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Utamaduni wa Wilaya wawezeshwe ili michezo iweze kushamiri kutoka ngazi za chini kabisa. Kwa sasa Maafisa Utamaduni wamesahaulika kabisa.

Mheshimiwa Spika, nashauri vijana wawezeshwe kupatiwa mikopo maalum ya kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia Serikali isimamie viwanja vya michezo ili viweze kuboreshwa na kuwawezesha vijana kupata sehemu za michezo. Pia kusimamia vyema maadili ya Mtanzania, michezo kama ya *Big Brother* na mingineyo yenye sura hii inadhalilisha utu wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vijikite katika kujenga misingi ya uzalendo ili kujenga utaifa badala ya kujikita katika kuchochea migogoro nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanzishwe Sera ya Habari hapa nchini ili kuwe na agenda maalum zenye maelekezo ya kulijenga Taifa letu badala ya kulibomoa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. ANGELAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu, ni lini, Muswada wa Sekta ya Habari ambao umechukua muda mrefu uteletwa katika Bunge lako Tukufu? Muswada huu ukipitishwa, utasaidia sana kudhibiti sekta hii ambayo kwa hivi sasa hauko sawa hata kidogo. Utasaidia, kuboresha maadili ya wanahabari.

Mheshimiwa Spika, namna Mfuko wa Maendeleo ya vijana unavyogawa/kopesha pesa kwa vijana kupitia *SACCOS* siyo mfumo mzuri hata kidogo. Ni vyema Taasisi za Fedha (*Microfinances*) kwani kupitia Taasisi hizi vijana watafikiwa kwa urahisi zaidi. Masharti ya *SACCOS* yanayomtaka mkopaji awe na akiba ya kiasi cha takribani nusu ya hela anayotaka kukopa, kwa kweli vijana wengi hawana akiba, hivyo ni bora mfumo wa ukopeshaji ukabadiishwa ili vijana wengi waweze kukopa tena riba iwe nafuu, angalau kwa asilimia kumi na ikibidi muda wa marejesho kuwa miili na *grace period* ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, vilevile kutokana na hotuba ya bajeti ambayo imewasilishwa na Wizara ya Fedha iliyokopeshwa Sh.1,210,000,000/= na kiasi kilichorudishwa ni kidogo sana ikilinganishwa na kiasi kilichokopeshwa (Sh. 46,350,000/=). Vilevile, utaratibu wa ukopeshwaji haufahamiki kwa vijana, hivyo basi, ni vyema utangazwe ili vijana wanaohitaji wafahamu. Sambamba na ukopeshwaji, ni vyema mikopo ikaambatana na elimu ya ujasiriamali na kuwatafutia masoko ya bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, BAKITA ni Baraza muhimu sana, lakini taasisi hii ina hali mbaya sana. Wanapaswa kutoa huduma za ukalimani, pamoja na kutoa tafsiri ya hati mbalimbali. Nimefurahishwa kuona kwamba kwenye bajeti hii, BAKITA itapata majengo mapya yaliyopo Kijitonyama.

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho ya hotuba yake, alieleze Bunge lako Tukufu ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ukarabati huo na ni lini BAKITA watahamia katika majengo hayo mapya?

Mheshimiwa Spika, BAKITA vile vile inashirikiana vipi na Wizara ya Katiba na Sheria katika kutafsiri Miswada ya Sheria? Je, Wizara imewashirikisha kutafsiri Miswada mingapi ya sheria?

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo ningependa kupatiwa maelezo, ni kuhusu Vazi la Taifa. Tuna mipango gani kama nchi/Serikali kuhakikisha vazi hili linakuwepo mapema iwezekanavyo na ni lini vazi hili litaanza kutumika, na hatua gani zimeshachukuliwa na Wizara katika kukamilisha mchakato huu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri, Katibu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi pevu ya kuandaa na kukamilisha kwa mafanikio makubwa hotuba hii yenye mwelekeo wa kukidhi matakwa au matarajio kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado tuna changamoto nyingi kwenye Wizara hii, hususan kwa upande wa vijana, vijana ni nguvukazi ya Taifa na ni vijana wa Taifa la leo. Naiomba Wizara iwe na program maalum kwa ajili ya kuwahamasisha na kuwaelimisha vijana ili wajue umuhimu wao katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuwe na mpango mahsus wa kuwawezesha hususan kwenye sekta binafsi kama ujasiriamali, tuongeze nguvu kwenye viwanda vyetu vya *SIDO* ili waende vijana kwa wingi kujifunza ili kuongeza ujuzi na hatimaye kuweschewa mitaji kwa masharti nafuu ili waweze kujajiri.

Mheshimiwa Spika, Wizara iwe na mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa mikopo inayokusudiwa kuelekezwa kwa vijana, basi inafika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la utamaduni, Wizara iwe makini kuhakikisha utamaduni wetu unaendelezwa ili urithiwe na vizazi vijavyo, Wizara ikemee matendo yote yanayoharibu na kubomoa silka na tabia nzuri za wazee wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, tuwe na mpango wa kila mwaka kupeleka makocha wetu wazalendo kwenda kujifunza nje kwa maslahi ya nchi yetu na siyo kutegemea wageni kuja kutufundishia wanamichezo wetu, tuwe na vyuo vya kisasa hapa nchini vya kutoa mafunzo kwa wanamichezo.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ni muhimu Serikali kuanzisha Shule za Michezo katika kila Mkoa ili tuweze kuwajenga watoto wenye *interest* ya michezo hasa mchezo wa soka. Ni vyema Mikoa ya kuanzia ile inayoonyesha inatoa wachezaji wengi katika fani mbalimbali za michezo mfano, Kigoma ni mahiri kwa mchezo wa Mpira wa Miguu, Singida na Arusha riadha na mingine mingi. Hii itasaidia kuwa na wanamichezo ambaio ni *professional* na wataweza kuendeleza Sekta ya Michezo ambayo itasaidia kuongeza pato la Taifa na ajira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, viwanja vya mpira vimetelekezwa, mfano mzuri ni kiwanja cha mpira cha Lake Tanganyika Kigoma, Abeid Aman Karume Arusha, Ally Hassan Mwinyi Tabora na vingine vingi. Viwanja vingi vimehodhiwa na Chama cha Mapinduzi, lakini chama hicho kimeshindwa

kuviendeleza. Ni dhahiri upo umuhimu wa kuvirejesha viwe vya Serikali kwa maana ya umiliki wake uwe wa Watanzania wote, kwani vilijengwa kwa jasho la Watanzania bila kujali itikadi zao.

Mheshimiwa Spika, vazi la Taifa bado ni ndoto. Suala hili limeongelewa muda mrefu, mashindano mbalimbali ya kutengeneza vazi la Taifa yamefanyika, lakini mpaka leo hatuna vazi la Taifa. Naitaka Serikali itueleze ni lini Tanzania tutapata vazi rasmi la Taifa ili tuweze kutambulika kama zilivyo nchi nyingine?

Mheshimiwa Spika, Baraza la Vijana la Taifa, siyo jambo jipya. Toka nimeingia ndani ya Bunge hili tunauliza lini Baraza la vijana litaundwa? Naitaka Serikali ituambie, lini litakuwa tayari ili iwe *forum* ya vijana wa kitanzania? Hii itawasaidia kukutana na kujadili mambo yanayowahusu vijana bila kujali itikadi, na kama mnavyofahamu matatizo ya vijana yanafanana. Naomba majibu, lini vijana watapata Baraza lao?

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu kuilinda na kuiendeleza lugha yetu kwa kuitumia katika Mikutano mbalimbali. Vilevile sheria zetu ziandikwe kwa Kiswahili, kwani zinatumwi na wote wasomi na wasiosoma, wajuzi na wasio wajuzi wa Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi ilioendelea kwa lugha ya kukopa. Tutumie lugha yetu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwanza kwa kumponeza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuwahabarisha wananchi pamoja na kulinda tamaduni zetu.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba ndani ya Bunge lako Tukufu, tumepitisha azimio la kuridhia kutumika kwa lugha yetu ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali kama vile Makongamano, Semina na mambo mengine yote kwa nia ile ile ya kuidumisha na kuienzi lugha yetu ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha yetu ya Taifa. Je, utekelezaji wa azimio lile umefikia wapi? Mbona hatusimamii maamuzi yetu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania sasa tunapoteza maadili, mila na tamaduni zetu kutokana na kuvutiwa na kuiga zaidi tamaduni za wenzetu. Hii inaonyesha kwamba hatimaye tutapoteza uasilia wetu, kwa mfano, zile jando na unyago ziliikuwa zikitoa mafundisho mbalimbali kwa vijana, leo hii tunashuhudia vitendo vingi vya utovu wa nidhamu vinavyofanywa na vijana wetu ambavyo vinadhihirisha kwamba watoto hawa wamekosa mafunzo fulani yanayotokana na mila na tamaduni nzuri za asili. Kwa hiyo, naishauri Wizara kwamba utamaduni wetu wa asili tusiudharau, kwani ndiyo unaoweza kuwalea watoto wetu na kupata makuzi yenye mafundisho ya mila na desturi nzuri za kitanzania. Tusione kwamba utamaduni ni mtu kuishi apendavyo kwenda atakapo na kufanya apendavyo tu, la! Hivyo sivyo kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wasanii ni watu amba mara nyingi wanatoa fundisho ama katika maigizo yao, ama katika tungo zao. Sasa kama kweli wanaelimisha, basi waelimishe mambo ya maana, lakini ikiwa mwalimu anavaa ovyo anapoingia darasani anawafundisha nini wanafunzi wake? Hivyo basi, Wasanii wetu hasa wanawake wasivae uchi, wasionyeshe mili yao, kwani wanapotisha jamii na wao wenyewe wanajidhalilisha. Naiomba Serikali ilisimamie hilli.

Mheshimiwa Spika, hata hawa vijana wetu wanaogombea U-miss tunaomba wavae nguo za heshima, yaani wasitiri maungo yao.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Habari ni eneo muhimu sana katika Taifa lolote, na watu wa habari tunawategemea katika kutoa ama kutupa habari, ama ziwe nzuri au mbaya, lakini ni lazima zitoke na zipatikane. Pamoja na kazi nzuri wanayofanya watu wa habari, tunaomba watende haki kwa wote, wasiwe na upendeleo katika kutekeleza kazi zao na watoe habari zilizo sahihi, wasitoe habari kwa utashi na wala wasiandike habari kwa kukashifu mtu fulani. Hilo siyo jambo zuri. Waandishi wajenge mahusiano mazuri na jamii wasikaribishe mpasuko baina yao na jamii ambayo wanaihabarisha.

Mheshimiwa Spika, siyo jambo zuri hata kidogo kumpiga picha Mheshimiwa Mbunge ambaye kwa bahati mbaya amesinzia Bungeni, kwani yeye ni sawa na binadamu yeote tu. Kwa maana hiyo, usingizi unaweza kumpata wakati wowote.

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kwa mawasiliano makini ya hoja ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, riadha nyakati za Uhuru na mara baada ya Uhuru ililettea nchi yetu sifa kubwa. Ilitokea nini? Hatujachelewa sana, naomba tuanze kuhamasisha mchezo huu shulenii pamoja na Mpira wa Miguu na *Netball*. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumewajenga vijana wetu na michezo na nchi vile vile.

Kuna bingwa wa mbio aliyeletea Tanzania sifa sana aliposhiriki mbio za *Olympic* aliweza kukamilisha mbio/mashindano aliyeshiriki hadi mwisho hata pale alipoumia mguu. Serikali ya China ikataka kumjengea nyumba na kiwanja cha kisasa pale atakapochagua, lakini mpango huu umeishia Wizarani: Je, ni nani anayehujumu juhudhi hizi? Mheshimiwa Rais alipotembelea Mbulu katika ziara zake aliwajulisha wananchi baada ya kuzuru China taarifa hii. Mchezaji huyu anaitwa John Stephen, naomba kujua nani hapendi nchi na mchezaji huyu mpaka wanafikia kuhujumu haki yake? Pia naelewa hii siyo mara ya kwanza. Naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamati watusaidie, nami nitafuatilia kwa karibu sana. Tafadhalii naomba tuwe watu wa haki, na kwa kuwa watu wa haki tutawajengea vijana wetu matumaini, sasa Wasanii wanadhulumiwa sana. Ahsante.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa hotuba nzuri ya bajeti. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu ya wizara na asasi zilizomo katika Wizara hii na bajeti iliopangwa kwa huo mtindo wa ukomo ni dhahiri kuwa haitoshi. Tatizo kubwa ni ukomo wa bajeti katika miradi ya maendeleo. Tatizo hili linakwamisha sana utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Serikali ni vyema ingeona umuhimu wa kupokea ushauri wa vipaumbale vinavyotolewa na Kamati husika kwa mfano, fedha zilizotengwa kwa *TBC* ni kidogo sana, haziwezi kufanya miradi na ukarabati wa vifaa vya kurushia matangazo (*OB VAN Equipment*) vya *Television* bado hauwezi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Jengo la *TBC* ulianza miaka mingi takribani muongo mmoja umepita. Ni aibu sana kuwa jengo hilo limesimama kwa kipindi kirefu. Kwanini Serikali imepoteza resource kubwa kwa kuanzisha ujenzi wa jengo lile na kupoteza fedha nyngi. Serikali kwanini haitoi dhamana kwa ujenzi wa jengo la Mikocheni ambapo likimalizika litawezesha shughuli zote za shirika zifanyike katika jengo moja? Serikali haioni faida nyngi za kumalizia mradi ule kuliko hasara nyngi za kutoendelea kumalizia? Inasikitisha kuona Mlima wa mamilioni ya pesa pale Mikocheni.

Mheshimiwa Spika, uchakavu wa mitambo katika vituo vya radio unaongeza bei ya umeme. Kwa sasa fedha nyngi zinatumika kulipa bili za umeme, kwa mfano kwa mwezi mmoja bei ya umeme kwa kituo cha redio Nachingwea ni Shilingi milioni mia moja na hii inatokana na uchakavu wake. Kwa sasa mitambo yote imechakaa sana, lakini Serikali inawataka *TBC* watoe huduma kwa wananchi kwa upana. Watawezaje?

Mheshimiwa Spika, asasi zilizopo katika Wizara hii, *TBC* na *TSN* zinadai fedha nyngi katika Wizara na Idara za Serikali. Kwa mfano, *TBC* inadai Serikali na Serikali za Mitaa ikiwa ni gharama za matangazo kwenye *Daily News* na Habari Leo.

Mheshimiwa Spika, hali hii kwa kiasi kikubwa inachelewesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuufinya mtaji wa *TSN*. Serikali inapohudumiwa, halafu hailipii, inatarajia nini? Kama Serikali inaona inafaa kutolipa, itumie vyombo vya binafsi kama wanawenza kuwavumilia. Ikumbukwe kuwa deni linavyoendelea kuwa kubwa, ndiyo uwezo wa vyombo hivi unavyopungua.

Mheshimiwa Spika, siyo vema, inazorotesha, inarudisha nyuma, inavunja moyo harakati zote za watoa huduma kama huduma zinazokopwa hazilipwi.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa watumishi ni tatizo sugu katika Wizara hii. Kila mwaka Asasi zake zinakuja na kilio hiki cha upungufu wa watumishi. Kwa mfano, TBC ina upungufu wa watumishi 33, Kituo cha vijana – llonga wana upungufu wa wakufunzi, Kituo cha Mafunzo ya Vijana – Sasanda hawana Maofisa Ugani na Kituo cha Marangu hakuna *Professional Instructors*.

Mheshimiwa Spika, kama hali ndio hiyo, tunatarajia kupata matokeo mazuri kwa uhaba huo. Kwanini Serikali inaachia upungufu huu wa watumishi? Mpaka lini? Kwanini isitoe kibali cha kuajiri kwa mahitaji yaliyopo?

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikachukua jukumu la kuwezesha vituo hivyo vikafanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoona wiki iliyopita sikuwepo. Tulikuwa na Mkutano, ooh! Sikukuona Mheshimiwa Dokta. Tulikuwa na mkutano wa Maspika ambao wanatokana na nchi ambazo ni Wajumbe wa Jumuiya Madola. Kwa kuwa kunakuwa na kikao cha namna hii kila baada ya miaka miwili huwa vikao hivyo vinafanyika katika nchi mojawapo katika nchi mojawapo inayohusika. Safari hii ilikuwa ni Malawi ndiyo waliotukaribisha. Katika ule mkutano tunajadiliana mambo yanayohusiana na mambo ya nchi zetu na Maspika huwa wanazungumza mambo ambayo tuseme wanashirikiana kupeana usoefu wa nchi moja na nchi nyingine kuhusu mambo yale ambayo yanakubalika kwa pamoja. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu sisi wa *Commonwealth* mambo yetu mengi yanakwenda karibu sawa sawa, kwa hiyo, tuna-share usoefu. Moja ya mada ambayo tulikuwa tunazungumza kule naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge ilikuwa nafasa ya Vyama vyta Upinzani katika Bunge kuweza kuimarishe demodrasia na kufanya maendeleo ya nchi yaonekane, ndiyo moja ya mada iliyofanyika. Mada hiyo kwa ujumla wote tulikuwa tunazungumza na Waheshimiwa Wabunge napenda kuwashukuru, kwa sababu hamuwezi kuwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halafu mkawa Wabunge wa CCM, Wabunge wa CHADEMA, Wabunge wa NCCR, Wabunge wa nani, kwa maslahi ya wananchi hatufanyi sawa. (*Makofi*)

Ndiyo hivi sasa mlivyoanza kwa mfano, jambo mkikubaliana kwamba hili ni la *national interest* mnasimama kama Wabunge wa Tanzania, kitu ambacho ni kizuri. Lakini tuwe na hoja ya msingi ya kuwasaidia wananchi wetu wanaotusikiliza sisi. Kwa hiyo, mimi nasema hili lazima tutofautishe. Ama kwa mfano mnapitisha *Bill* ya nchi, Sheria ya nchi haiwezi kuwa ya CCM au ya CHADEMA lazima iwe Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Ubaya wake uzungumzwe, uzuri wake uzungumzwe, manufaa kwa wananchi yazungumzwe bila hata kukopesha. Tusifanyi mchezo usiokuwa na akili nzuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ttatungaje Sheria ya CHADEMA, utatungaje Sheria ya CCM? Hakuna kitu kama hicho. Kwa hiyo, nawaomba kama ile ninayosema *net working* ni muhimu. Ila tuwe *genuine*, tuwe wakweli, hii kwa maslahi ya wananchi. Ama ni maslahi ya siasa tu. Haya mambo ya siasa tuna muda mwingi wa kufanya huko nje, wapi, lakini hapa tutunge Sheria zinazowalinda Watanzania wa leo, wa kesho na wengine na hii sote tukumbuke. (*Makofi*)

Sisi hapa tunatumia Sheria zingine za miaka ya 1960, kama zingekuwa zimetungwa na chama fulani tu sasa zisingekuwa sheria za nchi. Kwa hiyo, ndiyo maana tutofautishe Waheshimiwa kwamba tunapofikia jambo la *national interest* ni lazima ku-argue kama tunataka kuwafaidisha wananchi wa Tanzania, hili naliomba sana. Hili ndilo ninalolisema kila siku, ninyi bishaneni humu ndani, mkitoka ni marafiki, hakuna uadui kati yetu. Hicho lazima mkiangalie na wananchi watusikie hivyo. Kwa sababu kuna wakati mwengine wanashangaa wewe ukishirikiana na mtu mwengine wanawaambia haa, mbona wanashirikiana. Jamani hakuna ugomvi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sheria ya vyama vyote tumeitunga humu ndani kwamba viwepo vyama. Kwa hiyo, si kwamba vile ni kwa bahati mbaya. Kwa hiyo, tunabakia ni Watanzania,

marafiki, tutashindana kwa hoja na si vitu vinginevyo ambavyo vinastahili. Kwa hiyo, ninaiomba hii tabia na mwelekeo tulioanza uendelee hivyo hivyo. (*Makofi*)

Hivyo hivyo na Waheshimiwa Mawaziri itabidi mfanye kazi mliyopewa. Itafika mahali mtageukwa na ukumbi mzima. Wanasema *back bencher rebellion* ipo. Kwa hiyo, ni vizuri na nyie mkafanya kazi zenu kwa uhakika na mkafanya kazi zenu kwa kujihamini kwa sababu mmepewa *instruments* za kufanya kazi. Mkifanya hivyo hakuna *rebellion* na kama *wata-rebell* na nyie wananchi mtasema hili pengine tulipeleke kwa namna ambayo mnafikiria inafaa kwa maslahi ya wananchi. Kwa hiyo na ninyi upande wenu fanyeni kazi yenu kama inavyostahili. (*Makofi*)

Nimesema hayo yote kwa sababu mna muda wa kuweza kusema hivyo. Lakini kwa sababu leo ni siku ya Ijumaa wenzetu waende kuswali kama kawaida na Waziri na Naibu wake wakajiandae vizuri majibu mchana mtaingia kuanza ku-wind up halafu tuingie kwenye Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni. (*Makofi*)

(*Saa 6.30 mchana Bunge lilitishwa mpaka saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

(*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

(*Majadiliano yanaendelea*)

**NAIBU SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, sasa naomba nimuite Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyangi na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kuongoza nchi kwa awamu ya pili na kwa uongozi wake bora katika kusimamia ipasavyo llani ya Chama cha Mapinduzi, ili kutekeleza shughuli za chama na Serikali. (*Makofi*)

Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dokta Gharib Bilal kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuendelea kutumikia wadhifa wake baada ya kuthibitishwa rasmi na Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Spika, Mheshimiwa Anna Makinda, Mbunge wa Njombe, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Ni imani yangu kuwa tutatekeleza wajibu wetu katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika jitihada anazozifanya za kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa letu. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na wananchi kuwa wawakilishi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunitfea kuwa Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Naamini kwamba uteuzi wake umezingatia imani aliyonayo kwangu na uwezo nillionao nikishirikiana na Waziri katika kutekeleza majukumu yaliyo chini ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia uniruhusu nichukue nafasi hii kushukuru CCM, UWT kwa ujumla kwa kunijengea maadili na mazingira mazuri ya kijamii na kisiasa. Kipekee nashukuru UWT Mkoa wa Dar es Salaam na UWT Taifa Baraza Kuu. Napenda pia kushukuru familia yangu, mume wangu Profesa Daudi Mukangara na vijana wetu Cleopatra, Natasha na Jackson kwa upendo na ushirikiano wanaonipa katika utendaji wa kazi yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Dokta Emmanuel Nchimbi, kwa ushirikiano mkubwa alioonesha kwangu na pia kuniongoza katika kufanya maamuzi sahihi yanayohusu utekelezaji wa shughuli zinazohusu sekta za Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. (*Makof*)

Nampongeza pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Bwana Sethi Kamuhanda, Naibu Katibu Mkuu Bibi Sihaba Nkinga, Wakurugenzi wote wa Idara, watendaji wakuu wa taasisi na wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa katika kusaidia kusimamia utekelezaji wa sera na majukumu ya kila siku ya Wizara. Sitakuwa nimetenda haki pasipo kuwashukuru pia Maafisa Waandamizi na wahudumu wa Wizara yetu na taasisi zilizo chini yake kwa kazi nzuri na ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo nirejee katika eneo muhimu na la msingi linalohusu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza kabisa nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, maswali na maelekezo mbalimbali walyotoa kuhusiana na hotuba ya Bajeti ya Makadirio na Matumizi ya Wizara yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumtambua Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Niwatambue pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Kutokana na muda mchache niliopewa sitaweza kutaja majina yao wote, lakini Waziri wangu atawezu kufanya hivyo atakapoibju hoja zao walizotoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa maelekezo mbalimbali yenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara na hivyo kuleta mafanikio yanayotarajiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, nitajibu hoja zilizolenga sekta ya vijana na kwa kiasi kidogo michezo zitakazowezekana kwa muda nilionao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maoni ya kutoka Kamati ya Bunge. Maoni ya kutoka katika Kamati ya Bunge yamehusu hoja mbalimbali na yamegusia masuala ya vituo vya vijana pamoja na Mfuko wa Uwekezaji, mamilioni ya Kikwete, lakini pia umuhimu wa kujitahidi tuwe na sheria ambayo itatuwezesha kuzuia vigenge vya vijana wasio na kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema tu ushauri wa kutoka katika Kamati tutauzingatia na tutajitahidi kuufanya kazi. Lakini niseme tu kwamba mengi ambayo wameyazungumzia katika maoni na maelekezo ni kwamba tumeshaanza kuyafanyia kazi katika maeneo yaliyoainishwa kufanyiwa kazi ndani ya sekta hii ya vijana, kwa mfano maeneo ya afya bora na malezi ya vijana, mafunzo na uendelezaji ujuzi wa vijana, uvezeshwaji kiuchumi, ushirikishwaji na uhamasishwaji wa vijana. (*Makof*)

Niruhusu pia nizungumzie kidogo kuhusu maoni kutoka Kambi ya Upinzani, lakini niseme tu kwamba baadhi ya ushauri wao tutauzingatia lakini yale mengine yaliyojiteza kwa maana ya benki ya vijana pamoja na mchakato wa Baraza, Waziri wangu atazungumzia wakati atakapokuwa anawasilisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nitaanza kuzungumzia sekta ya vijana, nizungumzie kwa ujumla wachangiaji wa sekta hii. Wachangiaji wa sekta hii ya vijana kwa maandishi walikuwa

ni wengi, nadhani wanazidi 80 na katika hao 80 karibu kila mmoja amezungumzia vipengele mbalimbali, yote yanagusa masuala ya vijana, lakini wengi wametoa maoni, maelekezo lakini pia maombi. Hoja nyingi zimejikita katika maeneo ambayo tayari nimesema kwamba Wizara inayafanya kazi katika kulenga vijana. Katika hayo maeneo la kwanza ni eneo la malezi na afya bora kwa vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili napenda niseme tu kwamba na kuwajibu wale ambao wamezungumzia masuala yale ya kuwahusu vijana na mwelekeo wao na kutokuwa na maadili mazuri, kwamba Wizara yetu inao mwongozo wa stadi za maisha kwa vijana na huu mwongozo wa stadi za maisha kwa vijana unalenga taasisi mbalimbali hapa nchini kuweza kuutumia kama mwelekeo wa kutayarisha vijana mbalimbali wanapotayarisha mitaala, lakini pia hata wakati wanapofundisha masomo yao mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara pia, programu ya stadi za maisha kwa vijana, imetengenezwa na imeanza kutekelezwa na hiyo programu ina malengo ya kuwatayarisha vijana kuweza kujitambua, kujiamini, kuwajibika, kupenda kazi, kupenda uzalendo, kupenda utaifa na kadhalika. Lakini pia katika kuhakikisha utekelezaji wa hii programu, mafunzo kwa Maafisa Wilaya na Mikoa umefanyika ili kuwawezesha kuufahamu, kushirikiana na kusimamia utekelezaji wake. Kwa hiyo, kwa wengi waliochangia ambao walikuwa wanalamika kwamba hata na maofisa vijana hawapo karibu nao, ningependa tu wakirudi kule waweze kusisitiza katika mikoa yao na Halmashauri zao, kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kwa karibu na hao maafisa vijana pamoa na Afisa Michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya mwongozo wa stadi ya maisha, masuala ya UKIMWI na uchangudoa na athari za dawa za kulevyta na ulevi kwa ujumla yanaelekezwa vizuri. Kwa hiyo, hapa ninachotaka kusisitiza ni kwamba katika eneo la malezi na afya bora kwa vijana, wengi wamechangia masuala ya wengine kuwa machangudoa, nadhani hili suala Mheshimiwa Vick Kamata ameliusia, Mheshimiwa Ester Bulaya na wengine wengi wamegusia kuhusu maadili kuhusu vijana kukaa katika vijiwe, Mheshimiwa Jenista Mhagama pia aligusia kwa machungu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka niseme tu mwongozo upo na nafasi kama ingewezekana, Wabunge mbalimbali wajitahidi kuweza kuhakikisha wanaupata huo mwongozo, lakini pia kufuatilia Halmashauri mbalimbali na vyuo vilivypopo katika sehemu zao kuhakikisha kwamba huo unatekelezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Wizara yetu imejikita na ambalo masuala mengi au maoni au hoja mbalimbali zimejitokeza, ni katika suala la mafunzo na uendelezaji wa ujuzi wa vijana. Katika hili Wizara yangu imejikita hasa katika kutayarisha vijana kukabiliana na suala la ukosefu wa ajira. Lakini hasa kulenga kuhakikisha tunatayarisha vijana wenye kuweza kujajiri na kuajirika na katika hili ni kuhakikisha kimsingi kabisa kwamba mafunzo yanayotolewa yanajikita katika masuala ya vitendo na katika kusimamia stadi ya maisha, vituo vyetu vya vijana vinatoa mafunzo ya ujasiriamali ambayo yanatolewa huko llonga, Sasanda na hata Marangu, hivi ni vituo vyetu ambavyo tumeviainisha na kuweza kuvisimamia kama Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa ujasiriamali suala linaloangaliwa hasa ni kuhusu tabia na mwenendo na hulka ya mtu kuwa na moyo wa kujituma na kuthubutu hasa kujituma kwa malengo na hili ndilo jambo kubwa zaidi ambalo tunalismamia kama Wizara kuwatayarisha vijana kusudi hata wanapopata mafunzo ya ujasiriamali, waweze kujua hasa cha kufanya. Mafunzo yanayotolewa hasa yanahu uanzishwaji, usimamizi na uendeshaji shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji mali kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili wafadhili wa *ILO* na *UNFPA* wanasaidia na vituo vya mafunzo kama nilivyosema vipo pia kule Marangu. Kituo cha Marangu hasa kinashughulika na mambo ya ujasiri, ukakamavu, maadili na uzalendo, uwajibikaji, utaifa, uthubutu, lakini pia masuala ya kujitegemea na kupenda kazi, masuala ya kujituma bila kuanza kusukumwa sukumwa. Kwa hiyo, masuala ya vijana katika mambo ya vijiwe yanaweza yakaisha kama kweli tukizingatia

na kufuatilia haya mafunzo na kupeleka vijana wetu huko na wale Wabunge wanaohusika kwa sehemu hiyo, kuweza kusimamia kwa dhati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo kingine cha Sasanda, kinahusika na mambo ya kilimo, mambo ya uvuvi na mambo ya ufugaji na kituo kingine cha llonga ambacho kiko Morogoro, kinahusu stadi za maisha kinachobeba sana sana masuala ya ujasiriamali, masuala ya teknohama, lakini hasa kuanzisha masuala mbalimbali pamoja na miradi. Pamoja na kusema haya ni lazima nikiri kuwa vituo vinahitaji kuboreshw, kama ushauri ulivyotolewa na Kamati ya Bunge na sisi kama Wizara, tunatambua hilo na tunajitahidi kwa kadri tunavyoweza kuweza kuhakikisha kwamba kila mara tunatenga hela kiasi cha kuweza kushughulikia hivyo vituo, lakini tutambue kabisa kadri tunavyojitahidi kuitengeneza hivyo vituo vikawa katika hali nzuri, ndio inatupa nafasi zaidi ya kuweza kufikia vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo lingine ambalo ninaweza kusema labda ni eneo la tatu, ni eneo la uvezeshwaji kiuchumi, ushirikishwaji na uhamasishwaji wa vijana. Katika hili wachangiaji wengi wamegusia sana haya maeneo matatu, na tuna zaidi ya wachangiaji kama 80 na karibu wote wengi wao kwa namna moja au nyininge wamegusa suala la ajira, wamegusa suala la vijana kukaa katika vijiwe kwa kukosa kitu cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kwamba Wizara imejipanga sawasawa na kuhakikisha tangu mwanzo kuanzisha masuala ya vijana waanzishe *SACCOS* huko katika Halmashauri, katika Kata zao ambako wanawenza kupata na kufaidika na kutoka katika ule Mfuko wa Vijana. Na tunasema uvezekano wa kuanzisha Benki ya Vijana, unawenza kutokana na hizo *SACCOS* kama zikzikita sawasawa na zikaanza kuweza kukopa au kukopeshwa kutoka katika hiyo benki itakapoanzishwa. Mpaka sasa hivi zaidi ya shilingi 1,000,210,000/= zimekwishatumika na *SACCOS* 242 zimeshapata msaada, lakini pia Manispaa 121 zimefaidika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusema hilo lingine ambalo ningependa nilizungumzie kidogo kama eneo kubwa ambalo Wizara pia imejitahidi kuhakikisha kwamba vijana wanapewa nafasi katika nyanja mbalimbali za utendaji wa kazi ndani ya Serikali au kuwaziwa vizuri ndani ya Serikali ni kwamba Wizara yangu inalibeba na kuhakikisha kuwa kila Wizara inawajibika kuwa na dirisha la vijana. Katika nyanja hii kila Wizara inatakiwa kuwa wazungu wanasema kuwa-*pro active and enovative*, katika kubeba suala la vijana katika kuendelea kuwaendeleza kiuchumi na kijamii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika hili tayari mazungumzo mbalimbali ingawa sio *formal*, tumeweza kukutana na kuzungumza kidogo na Mawaziri wengine wa Ardhi, Kilimo, kuweza kuwaelezea kabisa kwamba katika programu ya kilimo au katika masuala ya biashara na viwanda katika Wizara ya Ardhi, Wizara ya Uvvi, Utalii, ziwekwe kwa makusudi programu za kuendeleza vijana kiuchumi na kijamii na hili Wizara yangu inafahamu kabisa kwamba inalo hilo jukumu la kusimamia kwamba hizi Wizara pia zinabebe huo mzigo, ndio maana ya kuwa sekta ya maendeleo ya vijana kuwa sekta mtambuka ambayo ina-cut across na hizo Wizara nyininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Sheria pia tunasema kwamba ijiweke sawasawa kwa sababu kadri tunavyokwenda kuna vitu vingi ambavyo vitaendelea kubadilika kuweza kuhakikisha kweli tunaweza kuwajumuisha vijana katika masuala mbalimbali ambayo watahitaji mabadiliko ya sheria ambayo itabidi kuwe na mkakati rasmi kabisa wa kuhakikisha hizo sheria zinabadilika kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nzungumzie kidogo pia masuala ya vijana, nimezungumzia kwa jumla jumla lakini na mengi ya hawa waliochangia yanagusa katika hizo nyanja nne, ambazo nimezungumzia. Kwa hiyo, napenda nianze tu kwa kusema kwamba Mheshimiwa Ester Bulaya, amezungumzia kuhusu vijana na ajira; na hilo nimelizungumzia na hasa tunawasaki vipi katika sekta ya kilimo. Hilo nimelizungumzia na ninasema kabisa kwamba mkakati upo tunautayarisha kuhakikisha kwamba kila Wizara inayohusika hasa zile sekta kubwa tulizozipa kipaumbele, kuweza kuweka mkakati rasmi kabisa katika mipango yao ya kushughulikia *window* ya vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mariam Kasembe wa Masasi, amezungumzia pia kuhusu kikundi chake. Wizara inashauri vikundi hivi vianzishe *SACCOS* ili viweze kupata mkopo wa masharti nafuu kuititia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mifuko mingine ya uwezeshaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vick Kamata aligusia swali la kuhusu Geita kama na yenye we haikuwezekana kuwemo katika ule mpango wa kutayarisha vijana kwa mambo ya ujasiriamali?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa ni sema tu awamu hii ya huu mpango Geita haikuwemo. Lakini awamu ya pili kama ikianzishwa tutahakikisha kwamba Geita itakuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, anazungumzia masuala ya vijana kuhitaji kufundwa. Hilo nadhani nimelizungumzia, lile la kiujumla la masuala ya maadili pamoja na afya ya vijana. Anazungumzia kuhusu JKT irudishwe na sisi tunasema ushauri wake tumeupokea na utafanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, anataka Afisa wa Vijana kuwa karibu na vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ninasema ni sawa kabisa, tutawasiliana na mamlaka ya Mkoa wa Rukwa ili kuhakikisha Maofisa Vijana wa Wilaya, wanakuwa karibu na vijana wao. Lakini pia tunamuomba ahakikishe hao vijana wanajunga katika *SACCOS* na wanapitia mafunzo rasmi, ikiwezekana wapitie mafunzo hayo ya stadi za maisha ili kusudi waweze wakianzisha *SACCOS* zao, zinaweza kudumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Margareth Mkanga wa Viti Maalum, anazungumzia kuhusu vijana walemavu. Nasema ushauri wako tumeupokea na tutaufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Martha Mlata, anahitaji Chuo cha Kufundishia Wanariadha kutoa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri tumeuzingatia lakini tungeomba pia na ye ye kama Mbunge wa hiyo sehemu atusaidie pia kuzungumza na Wabunge pamoja na Halmashauri pale, ili kuangalia uwezekano wa kuweza kuanzisha hicho chuo hapo kikawa kama ndio picha na bendera ya ye ye kama Mbunge wa hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sabreena Sungura wa Kigoma, amezungumzia tatizo la Afisa Vijana Kigoma, hajawaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba Kigoma inaye Afisa Vijana wa Mkoa ambaye ameajiriwa na Sekretarieti ya Mkoa. Kwa hiyo, ni muhimu ahakikishe amfuatilie kusudi aweze kuwa naye karibu pamoja na Maafisa wa Utamaduni pamoja na Maafisa wa Michezo kama wapo katika huo mkoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanamrishi Taratibu Abama na ye ye pia amezungumza vitu vingi, amezungumzia masuala ya *SACCOS* ambayo tayari nimeshayazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maryam Msabaha, anazungumzia kuhusu vijana kuwa na maadili na hayo yenye we nimeshayazungumzia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, nasema kuhusu mfuko wa JK na vijana wengi hawapati mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema ushauri tutaupeleka kwa Wizara inayohusika na sisi pia itabidi kufuatilia kwa sababu, tuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba vijana hela zinapotengwa kusudi waweze kufaidika, wanafaidika kikweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichungulie kidogo waliochangia kwa maandishi kama nilivyosema kwa upande wa vijana wengi na kwa kweli sitoweza kuwamaliza wote ni zaidi ya 80 na kama nilivyosema nimeweza kuweka kidogo maeneo kama manne, matano ambayo yanawabeba hawa wote akina Mheshimiwa Lucy Owenya, anazungumzia Baraza la Taifa la Vijana, hili atazungumzia Waziri. (*Makof*)

Pia amezungumzia kuhusu mradi wa kilimo Bagamoyo na tunapenda kusema tu kwamba ule mradi kama ulianzishwa wakati wa chama kimoja (Chama cha Mapinduzi) huo ni mradi na ni mali ya Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo inabidi kuweza kufuatilia kwa kuweza kujua kwa karibu kitu gani kinachoendelea, lakini mimi nataka niwapongeze kama Chama cha Mapinduzi bado kinasimamia huo mradi kikahakikishe kweli vijana wanafaidika vizuri na huo mradi. (*Makof*)

Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbanga Mashariki, anazungumzia kuhusu vijana wa Mbanga, nawapongeza vijana wa Mbanga kwa jitihada zao za ujenzi wa kituo cha vijana nawashauri hiyo *Mbanga Youth Center* wahakikishe wanawasiliana kwa karibu pia na Wizara labda mawasiliano kuhusu mambo ya *ICT*, lakini pia na kitengo chetu kile cha llonga kusudi waweze kupata labda mafunzo au namna yoyote ile ya kuweza kusaidiana nao kusudi tuhakikishe tunafanikisha hiyo *center* isije ikashuka chini zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, alizungumzia ukosefu wa ajira, hiyo hoja nimekwishaizungumzia, hoja ya kwamba Serikali iboreshe mipango ya vijana tunasema kwamba ushauri tumepokea na tayari unafanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Neema Hamid, Mbunge wa Viti Maalum amezungumzia ajira za vijana kuwa ni tatizo, kama nilivyosema hilo tumekwishiwekeea mikakati mbalimbali chini ya maeneo makubwa manne ambayo nimeyazungumzia mwanzoni kulenga wote kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum anataka vijana waelimishwe na wapewe taarifa hivi vyote kama wakiweza kufikiwa na huo mradi ambao nadhani ni muhimu pia wajitahidi wahakikishe unawafikia, maana yake hivi vitu wakati mwininge ni wewe mwenyeewe unatakiwa kuwa unaviona ni vya muhimu lakini unavisimamia kwa niaba ya hao vijana na kuhakikisha kwamba hao vijana wanaweza kufaidika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie pia kidogo kwa mfano, Mheshimiwa Diana Chilolo pia anazungumzia masuala hayo hayo. Napenda pia niingie upande wa michezo ambayo na yenyecheo mijadala mingi ya uhakika kutokana na *data* nilizonazo ni zaidi ya wachangiaji 34 kuhusu michezo peke yake kwa maeneo tofauti tofauti. Lakini nianze kwa Mheshimiwa Juma Nkamia, alizungumza juu ya BMT kupewa ofisi uwanja wa Taifa, napenda niseme kwamba utaratibu wa kuwapatia ofisi BMT unaandalila. Pia amezungumzia uwepo wa Kurugenzi ya Michezo unasababisha mgongano wa majukumu. Tunasema kwamba hilo kimsingi hakuna muingiliano mpaka sasa hivi labda kwa nje mnaona kama kuna muingiliano lakini sisi kama Wizara tunaona vitu vinaenda vizuri tu ni kiasi cha kuhakikisha tu kwamba BMT inajengewa uwezo vizuri pamoja na Kurugenzi ya Michezo ndani ya Wizara na yenyecheo inajengewa uwezo ambao unahitajika.

Lakini pia uteuzi wa Baraza jipya la BMT, tunasema hilo tunalizingatia sasa hivi. Suala lipi katika hatua za mwisho mwisho. Mheshimiwa Nkamia, Mheshimiwa Khatib pia pamoja na wachangiaji wengi wamezungumzia kuhusu Serikali kutenga fedha kwa wataalam wa Wizara kupata mafunzo na hilo tunasema ushauri tumeupokea na tunauzingatia. (*Makof*)

Pia wataalam wa nje kutoa mafunzo kwa wataalam wazalendo, hiyo tunasema tumeupokea na taratibu zinaendelea kuandiliwa na kwa kifupi wataalam wengi wanaotoka nje kwa kweli hutoa mafunzo na kulipwa na pamoja na kukochi au kufanya nini na wao pia wanatoa mafunzo kwa wataalam wa kizalendo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kwa Baraza kupunguza uitiri wa vyama ili kuleta ufanisi, tumepokea ushauri na utazingatiwa kwa kadri ya sheria zilizopo na kuhakikisha kweli vyama ambavyo tunavipa dhamana ya kubeba masuala ya kusimamia michezo mbalimbali Kitanzania

au Kitaifa kweli inakuwa na sura ya Kitaifa na inawajibika kama sura ya Kitaifa na hilo kwa kweli imekuwa ni changamoto moja kubwa. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo tunalichukua kwa makini na tutalifanya kazi. (*Makofi*)

Hoja ya maafisa michezo katika mikoa na wilaya kutokuwa na fungu la kutekeleza majukumu yao, tunaendelea kuhimiza mamlaka za mikoa na wilaya kutenga fedha kwa majukumu yao kila hali itakapaoruhusu. Serikali pia itaendelea kutenga pesa kuhakikisha kwamba timu zetu zinaenda na zinawakilishwa Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, alizungumzia kuhusu kocha wa *netball* aliyeondoka pamoja na Waheshimiwa kama watatu, wanne, walizungumzia hili suala lakini napenda iwe wazi kabisa kwamba kocha aliondoka kutohana na kucheleweshwa utekelezwaji wa baadhi ya masharti ya mkataba na kutoridhishwa na namna mchezo wa *netball* unavyoendeshwa kwa ujumla wake. Ucheleweshaji na utekelezaji wa masharti ya mkataba ultokana na kocha huyo kuletwa kabla ya kukamilisha maandalizi kwa mujibu wa taratibu zilizopo, hivi sasa maandalizi yanaendelea kwa ajili ya kupata kocha mwingine.

Kuhusu makocha wazalendo wapatiwe ujuzi, hili tumelizungumzia. Hoja ya kuanzishwa mamlaka ya viwanja vya michezo, nieleze kuwa mchakato wa kuunda wakala wa kuendesha viwanja tayari unaandaliwa na utakamiliwa mwaka huu. Aidha, ushauri wa ujenzi wa vituo umepokelewa na utafanyiwa kazi. Pia ushauri kwamba tujitahidi tuwe wenyeji wa Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ligi ya ndani (*CHAN*) 2008 pamoja na *CAN* 2019 na timu ya Taifa kushiriki fainali ya Kombe la Dunia la 2014, tunasema kwamba ushauri tumeupokea na tutazingatia endapo hali halisi ya uchumi itaruhusu na kuwepo na uwezo wa kimchezo, kwa maana ya kuwa katika ile ngazi ya kuweza kushiriki fainali tunaomba kabisa tuweze kufikia huko. (*Makofi*)

Hoja ya viwanja vinavyomilikiwa na CCM kurejeshwa Serikalini hili tunasema haliwezekani, viwanja hivyo ni mali ya CCM hivyo ni hiari yao kuvirejesha au laah! Lakini kama Wizara na Serikali tungewaomba CCM wavishughulikie ili kusudi viendelee kufanya kazi na kuweza kuhakikisha hata wale wenye kujitolea kuhakikisha kwamba wanafundisha vijana wetu katika ngazi mbalimbali wanawenza kuvitumia badala ya kukwama kwa kukosa nafasi za kutumia michezo. (*Makofi*)

Hoja ya kuzipongeza Simba na Yanga kufikia fainali Kombe la Kagame, naunga mkono na mimi naifikisha pongezi hizo vizuri kabisa kwa dhati na nawapongeza pia Yanga kwa kuchukua hilo kombe labda wajitahidi walishikilie hapo hapo. (*Makofi*)

Hoja ya malipo kwa makocha wazalendo, Mheshimiwa amezungumzia malipo kwa makocha wazalendo kwamba makocha wazalendo malipo yao ni tofauti na wale wa nje. Katika enzi napenda kusema tu kwamba Shirikisho la Mpira wa Miguu (*TFF*) lipo katika mchakato wa kuandaa mikataba kwa makocha wazalendo wanaofundisha timu za Taifa. (*Makofi*)

Hoja ya uanzishwaji wa shule za michezo na watoto (*sport academy*) hili ni suala ambalo limezungumziwa na wachangiaji mbalimbali ambao kwa kweli nadhani ni jambo la muhimu lizingatiwe kusudi vipaji vya watoto viweze kukamatwa tangu zile ngazi za chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi tutajitahidi kama Wizara, kama Serikali kuhakikisha tunatayarisha mazingira, uwepo wa makocha, lakini pia uwepo wa mkakati endelevu wa Kitaifa wa kuweza kusimamia hivi vitu kimsingi kusudi tusiwe muda mwingi tunahusisha wachezaji katika ngazi za juu wakiwa wachezaji tayari katika *levels* za *competitions* tu lakini katika ngazi za kuwakamata kuweza kupata vipaji inakuwa ni vigumu. Kwa hiyo, tunataka kama Serikali kuhakikisha kwamba huo mkakati unakuwepo na tunashirikiana na Wizara zinazohusika mpaka sasa hivi tunafanya kidogo kidogo kwa ngazi ya *project* na *programs* ndogo ndogo kwa misaada ya kutoka kwa wafadhili. Kwa hiyo, hilo tunajitahidi tuhakikishe kwamba tunabidlilisha. (*Makofi*)

Hoja hii Mheshimiwa Sabreena Sungura amezungumzia, Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib wamezungumzia hilo, pamoja na kutaka vilabu vya soka kuwa na timu za vijana na sisi tunasema ushauri tumeupokea na tunauzingatia. Mheshimiwa Ester

Bulaya na Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, wanataka tuwe na fungu Serikalini la kusimamia hawa *Twiga Stars* ambao wanasema kwa kweli hawathaminiwi kama *Taifa Stars*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la hoja hii ni kwamba mkakati wa kuendeleza mpira wa mguu kwa wanawake *TFF* wana mpango huo na tunavyoendelea labda katika mwisho wa mwaka 2012 *Twiga Stars* itakuwa kama anavyosema Mheshimiwa Bulaya na yenye we inapata sura ambayo *Taifa Stars* inayo. Hili hata mimi nilikwishalionna na tumekuwa katika nafasi ya kuipa kipaumbele *Twiga Stars* kuweza kuitafutia wafadhili mbalimbali waweze kushughulikia masuala yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir hoja yao inahusu viwanja vya michezo na hilo tumeshalizungumzia, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Margaret Mkanga, michezo kwa watu wenye ulemavu nimeshaizungumzia na nimeigusia kidogo wakati nilipokuwa nazungumzia vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Murtaza Mangungu Mbunge wa Kilwa, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Sabreena Sungura wamezungumzia masuala ya makocha, pia Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, amezungumzia kuhusu masuala ya makocha kutoka nje. Haya tayari nimeshajibu Mheshimiwa Ahmed Ali Salum na Mheshimiwa Donald Max kuhusu hoja ya Serikali ifute ushuru kwenye vifaa vya michezo na sisi tunasema ushauri tunaupokea na tutawasilisha kwenye mamlaka husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wachangiaji ni wengi na mengi nimejaribu kuyakusanya niweze kuyaweka katika sehemu mbalimbali ambayo kwa ujumla wake nadhani yamejitokeza vizuri. Kuna suala lile la *TFF* kwamba wanapata dola laki 500, mimi napenda tu kuliweka wazi kwamba si dola laki tano, ni dola laki 250 kwa mwaka na fedha hizo zinaletwa kwa maelekezo maalum. Hata hivyo hivyo *TFF*, ina programu ya kuendeleza vijana kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile *NMB*, *VODACOM*, *Coca Cola*, *SS Bakhresa* na kadhalika. Kwa hiyo, mimi nadhani cha msingi ni kuhakikisha tu tunafuatilia na *TFF* na vijana wetu wanaofaidika na *TFF* tuwaunge mkono ili *TFF* iweze kutimiza malengo yake vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niishie hapo kabla sijapigiwa kengele ya pili, niweze kuruhusu Mheshimiwa Waziri wangu aweze kuelezea hizo sekta zingine, ahsante. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, tunakushukuru sana kwa kuchangia hoja hiyo. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenye we, Wenye viti wa Kamati pamoja na Spika kwa kusimamia kwa umakini mkubwa majadiliano ya hotuba ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2011/2012. (*Makofii*)

Naungana na Bunge lako Tukufu, kutoa pole za dhati kwa familia na Watanzania wote kwa kifo cha shujaa wetu Luteni Jenerali Silas Peter Mayunga, kilichotokea tarehe 7 Agosti, 2011, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Jenista Mhagama na wajumbe wa Kamati hii kwa michango yao makini ambayo itasaidia kuboresha utekelezaji wa majukumu yanayoihusu Wizara na Asasi zake. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa maoni na mapendekezo aliyoyatoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote walipata nafasi ya kuchangia ama kwa kuongea ama kwa maandishi, kwani michango yao imeiwezesha Wizara yangu kwa kiasi kikubwa kutambua maeneo ambayo yamefanikiwa na yale ambayo bado ni changamoto na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Katibu Mkuu Bwana Seth Kamuhanda, Naibu Katibu Mkuu Bibi Sihaba Nkinga, wakurugenzi, wakuu wa asasi na watendaji wote kwa kazi waliyoifanya katika kufanikisha uwasilishaji hotuba nilioitoa hapa Bungeni na pia kwa majibu ya hoja mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo, kwanza kabisa katika mjadala huu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 160 walipata nafasi ya kuchangia na kati yao Waheshimiwa Wabunge 30 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja na Waheshimiwa Wabunge 130 wamechangia kwa maandishi, kwa idhini yako niruhusu niwatambue kwa majina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wa kwanza ni Mheshimiwa Juma Nkamia, Naibu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Moza Saidy, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo na Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, hawa ni waliochangia kwa mdomo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue waliochangia kwa maandishi, wa kwanza ni Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa *Engineer Athuman Mfutakamba*, Mheshimiwa Kepteni John Komba, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Munde Abdallah, Mheshimiwa Ismail Rage, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Abuu Jumaa, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwi, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Omar Badwel, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Mussa Azzan, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Neema Hamid, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

Wengine ni Mheshimiwa Moza Saidy, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Azza Hamad, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*, Mheshimiwa Mussa Khamis Silima, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Sara Ally, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Rose Sukum, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Mendrad Kigola,

Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee na Mheshimiwa Dkt. David Malolle. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vullu, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Dokta Anthony Gervase Mbassa, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo na Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Mhonga said Ruhwanya, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Dokta Mary Michael Nagu, Mheshimiwa Agness Elias Hokororo, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Dokta Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Naomi Amy Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwatambua wachangiaji kwa majina naomba sasa nianze kujibu na kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge nikianza na hoja za jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia masuala muhimu ya ujumla yanayohusu Wizara yangu. Napenda kutambua Waheshimiwa wote waliochangia katika eneo hili. Tunathamini sana michango yao ambayo imelenga katika kuongeza ufanisi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara na maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezwa kwa bajeti ya Wizara. Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia kwa maandishi na kwa kuongea ndani ya Bunge lako Tukufu wamesisitiza kuhusu umuhimu wa kuongezwa kwa bajeti ya Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na mafanikio zaidi. Tunakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii, tutaendelea kujenga hoja Serikalini ili bajeti ya Wizara ijayo iweze kuongezwa kama mlivytushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ni kuhusu Wizara kuleta Bungeni mapendekezo ya kutunga Sheria ya kusimamia vyombo vya habari, Sheria ya haki ya kupata habari na Itifaki za Kimataifa zinazohusu sekta tunazosimamia ambazo nitaziongelea muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hoja ya tatu ni juu ya uhusiano kati ya *TFF* na *ZFA*. Lakini kama ambavyo utakumbuka mtoa hoja wa habari hii alitusomea barua mbele ya kikao chako ambayo ilionesa mawasiliano kutoka *ZFA* kwenda *TFF* kulalamikia masuala mbalimbali ambayo walikubaliana lakini hayajatekelezwa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba viongozi wa timu hizi mbili wamekutana tarehe 6 Agosti, ili kushauriana kuhusu barua hiyo. Mimi na Waziri mwenzangu wa michezo wa Zanzibar tutafuatinilia kwa karibu mazungumzo hayo ambayo yameshaanza huku tukiyapa uzito maoni ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile katika hoja hiyo iliyozungumzwa ililhusu haja ya timu ya Taifa kuwa na uwakilishi wa kutosha wa pande zote mbili za Muungano. Kwa upande wa Wizara sina pingamizi na jambo hilo kwa sababu hili linaonyesha umuhimu wa sisi kutambua kwamba nchi yetu ina sehemu mbili za Muungano pamoja na wataalam kuangalia uwezo na vipaji vya wachezaji lakini wasipuuze hoja ya kuwa na sehemu mbili katika Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitazipitia hoja za Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa haraka kama ifuatavyo:-

Kwanza nirudie kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa jinsi ambavyo inatusimamia vizuri lakini pia inavyosimamia kwa nguvu sana kuhusu hoja ya *TBC* kuwezeshwa zaidi. Naomba niseme kwamba Serikali inalichukua jambo hili kwa uzito na tutahakikisha kwamba tunajipa nafasi ya kutosha kuona umuhimu wa *TBC* unaonekana kwa vitendo katika bajeti zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mkopo la udhamini wa *Star Media* nataka niihakikishie tena Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kama ambavyo nilifanya kwenye kikao chake kwamba maelekezo ya Kamati kuhusu haja ya uharaka wa Serikali kuchukua hatua ya kutoa udhamini huo haraka tumeyachukua na vile vile kwa misisitizo uliowekwa ndani ya Bunge kutoka kwa Wabunge mbalimbali tunaipa uzito unaostahili na tutafanyia kazi kwa haraka kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nytingine ilihusu ukamilishaji wa majengo ya *TBC Mikocheni*. Nataka pia niishukuru Kamati kwa kuiona hoja hii. Ni kweli jambo hili limechukua muda mrefu na tatizo liliopo ni suala la kuwa na uhakika wa kupata dhamana kutokana na fedha ambayo ingetolewa na shirika la *NSSF*. Nataka niihakikishie Kamati kama nilivyoofanya kwenye kikao cha Kamati hiyo, kwamba Serikali inatoa kipaumbele cha pekee na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa yale mambo ninayoongea hapa kwamba Serikali inafanya kipaumbele cha pekee, siyo kwa ajili ya kupitishia bajeti, kwa sababu uongo si sehemu ya sera zangu za kazi. Kwa hiyo, muwe na hakika kwamba ninaposema tunalipa uzito wa pekee, namaanisha ninachokisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba, suala hili la kukamilisha jambo hili, tumeshaanza mazungumzo. Nimefanya mazungumzo na Waziri wa Fedha lakini pia nilipata nafasi ya kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu kuhusu jambo hili na uzuri wake ni kwamba Waziri Mkuu kaniambia niendelee na mazungumzo na Waziri wa fedha, nikiona nakwama nikamuone. Ukipewa ujumbe huu huna sababu ya kutojamini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuhusu suala la madeni ya *TBC*. Nataka kwa namna ya pekee kwanza niishukuru Kamati ya Bunge, lakini pia Kamati inayosimamia Hesabu za Serikali ambayo kwa pamoja wameshirikiana sana kusukuma vyombo vinavyohusika na kudaiwa na *TBC* viweze kulipa na matunda yameonekana kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo, nawashukuru kwa namna ya pekee walivyotusaaidia. Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu naye kwa namna ya pekee amesimamia sana madeni ya *TBC* kutoka sehemu mbalimbali, naye matunda yake yameonekana. Timu hizi kwa pamoja zikiendelea kwa utaratibu huu mambo yatakwenda kwa kasi na kwa haraka sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya Kiswahili katika mabango, dhifa na Miswada ya Sheria. Wizara yangu inaunga mkono matumizi ya Kiswahili na tunaunga mkono kwa sababu ndiyo lugha tuliyokubaliana kuwa lugha yetu ya Taifa. Nakumbuka siku chache zilizopita kulikuwa na kikao cha Umoja wa Nchi Huru za Afrika na kulikuwa na *agenda* inayohusu vijana, kwa hiyo, ilibidi kama Waziri wa Vijana niende na kule tulikuwa na Mheshimiwa Rais. Katika shughuli moja Rais alimualika Rais wa Sao Tome kwenye kikao chetu. Rais wa Sao Tome akaongea kwa lugha ya kwao kukawa na mkalimani na wote tukaamini hajui Kiingereza. Lakini yule Bwana Mkalimani alipokosea akasema ambacho Rais hakusema, Rais akasema *I have not said that!* Akasema sitaki tena ukalimali naongea kwa lugha ya Kingereza. Inaonyesha tu ambavyo anajivunia lugha yake. Mliopata bahati ya kwenda China mtagundua ni hivyo hivyo, mkikaa na Wajumbe mbalimbali wa watu wa China, wanaongea lugha yao halafu anakuwepo Mkalimani, lakini ukikaa peke yako unaweza ukadhani kwamba hawajui Kiingereza. Lakini ni ile hamu ya kuongea lugha yao na kujivunia lugha yao. Kwa hiyo, nadhani na sisi tunaweza kufanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilitoa maelekezo ambayo ni muhimu kwamba BAKITA ishirikishwe katika kuandaa vitabu vya bajeti katika Wizara mbalimbali ili kupata usanifu wa

Kiswahili. Sisi kama Wizara hatuna pingamizi na jambo hili, wakati wowote ambapo Wizara mbalimbali zikihitaji usaidizi wa BAKITA basi BAKITA ipo na ina uwezo wa kufanya kazi hiyo na itakuwa tayari kusaidia ingawa lugha ya Kiswahili inazidi kukua kwa kasi, maana nilikuwa naona rafiki yangu mmoja alikuwa anachangia leo hapa alichanganya lugha nyingi kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria Namba Saba ya mwaka 1999 kuhusu hatimiliki. Niwahakikishie kama ambavyo siku ya bajeti ya Wizara ya Viwanda, Mawaziri wake walilihakikishie Bunge kwamba, jambo hilo litashughulikiwa kwa karibu sana. Naomba niwahakikishie kwamba nitaendelea kuwa karibu sana na Wizara hiyo ili kuona kwamba jambo hili linashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uingizaji na usambazaji wa filamu holela. Tumeshaanza kuchukua hatua ya kuona kwamba kunakuwa na udhibiti wa filamu zinazoingizwa bila utaratibu na ndiyo maana tulikuwa na Sheria ya mwaka 1976. Tumekwishazitengeneza Kanuni na Kanuni zimeanza kufanya kazi ili tuweze kuziweka filamu zote katika madaraja. Filamu hizo zikiwa kwenye madaraja itakuwa rahisi kuzidhibiti na kujua zipi zinaingia na zipti zinatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mirahaba ya kodi na kazi za wasanii, nataka niseme, ni kweli kwamba, sasa hivi usimamizi wetu wa mirahaba au mapato ya jumla ya wasanii uko chini ya kiwango na vilio vya Waheshimiwa Wabunge wengi tumevisikia na kwa kweli hata vikao vyangu vyote na wasanii wamekuwa wakililia jambo hili sana. Jambo hili linatugusa sana sisi kama Serikali na tuneshaanza kuchukua hatua. Nimefanya vikao vya kutosha na wasanii hawa ili kupata maoni yao lakini pia nimeshafanya kikao na Waziri wa Viwanda na Biashara, nimeshafanya kikao na Waziri wa Fedha na tumekubaliana kushirikiana Wizara hizi tatu kutafuta ufumbuzi wa mapoteo au kupotea kwa kazi za wasanii. Tukishalipatia ufumbuzi tatizo hili tutakuwa na uhakika kwamba, mapato ya Serikali yatapatikana lakini hasa mapato ya wasanii wetu. Hili ni jambo la mapambano ya kufa na kupona kuona kwamba tunakomboa hali za wasanii wetu. Nimelisema hili kwenye Kamati na nalisema tena mbele ya Bunge kwamba, tumedhamiria kulikomesha, tupewe muda tutalifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kidogo kuhusu maoni yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani. La kwanza ni suala la uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa *TSN*. Naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba mchakato wa kumteua Mtendaji Mkuu wa *TSN* uko katika hatua za mwisho, siku chache zijazo Rais atamteua Mtendaji Mkuu wa *TSN*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kufutwa kwa Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na hili rafiki yangu Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni alilisemea kwa nguvu sana. Akasema Serikali tunaionya isije ikachakachua. Sasa niseme tu kwamba ujasiri aliokuwa nao Ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi wa kusema tunaionya Serikali isije ikachakachua ni kwa sababu ni mtu makini, anajua tayari tupo kwenye mpango wa kushughulikia jambo hili. Kwa hiyo, ilikuwa ni sehemu tu ya kuunga mkono jambo hili jema. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba tupo katika utaratibu huo katika hatua za mwisho za Baraza la Mawaziri na Waziri wangu kivuli tunashirikiana sana, anayajua mambo haya, sasa nikimpa siri na yeye anakuwa mkali humu ndani. (*Makofî/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Serikali kutishia vyombo vya habari, naomba niwahakikishie kwamba, Serikali haijajenga utamaduni wa kutishia vyombo vya habari na tuna uhusiano wa karibu sana na vyombo vya habari. Pia nataka niwahakikishie kwamba uhusiano huo tutaendelea kuudumisha kwa muda wote ambao tutakuwa tunafanya kazi za wananchi. Nia ya Serikali ni kuona wananchi wanapata habari za kweli zisizotiwa chumvi, zisizo na madhara kwa jamii na zenyenye kuunganisha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni alilalamikia tahiriri ya *Daily News* kwamba ilisema Dokta Slaa hawezi kuwa Rais. Rai hii imenipa tabu sana, naijibu namna gani? Imenipa taabu kwa sababu kweli hajawa Rais. Lakini huyu Mhariri nina hakika kama angekuwa Rais, basi huyu Mhariri angekoma. Lakini ndiyo hivyo, mpaji Mungu na rafiki yangu Sugu anajua mpaji Mungu, hajawa! Ila tu jambo la kweli na la dhahiri kwamba tunataka vyombo vyote vya habari wakati wote wa uchaguzi vihakikishe kwamba haviegemei

upande wowote, vitoe taarifa za kweli za kila upande na bila kutoa maoni yao binafsi. Tukifanya hivyo tutafanikiwa sana katika kujenga umoja wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pendekezo la kuundwa Kamisheni ya Rais ya kusimamia na kutunza historia yetu. Kwanza, nikubaliane naye Msemaji wa Upinzani kwamba hii hoja ni nzuri na ni muhimu na nataka tu nimhakikishie kwamba tumeanzisha Program ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika ambayo inaungwa mkono na *AU*. Maoni yake tutayaingiza pia katika mchakato wa *program* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kutaka *COSOTA* iwe Mamlaka nayo ni wazo la maana totalifikisha Wizara ya Viwanda na Biashara ili ionne maana hoja yenyewe ya msingi anayotaka kujenga Ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ni hoja ya *COSOTA* kuwa na nguvu zaidi, iwe na meno ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi kuliko inavyofanya sasa. Kwa hiyo, hii ni hoja ambayo Waziri mwendawazimu tu anaweza akaikataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwa na mradi wa *Stickers* kwa kazi za wasanii, jambo hili pia tumewahi kuzungumza na Ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na tumelizungumza sana Kiserikali na kwenye Kamati nililitolea taarifa kwamba, tumeanza kutafakari baada ya kupata maoni ya kutosha kutoka kwa wasanii wenyewe. Wanaamini kwamba, utaratibu ule ndiyo utakaowafikisha katika hatua ya kuziokoa kazi zao kuibwa. Mimi binafsi nauamini utaratibu ule kuwa utafaa. Kwa hiyo, naendelea kushirikiana na wenzangu kuona kwamba tunaufanikisha kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ya nakshi za Ofisi na samani za ndani ya nchi zitokane na sanaa. Wazo hili pia ni zuri, sina pingamizi kama Wizara, tunatoa wito kwa watu mbalimbali kufanya hivyo kwa sababu ukitumia sanaa za ndani kwanza unazifanya ziendelee kudumu katika historia yetu, zinaendelea kuwepo. Lakini pia unatengeneza soko la ndani kwa wanaofanya kazi hizi na kukuza uchumi wetu. Kwa hiyo, tunakubaliana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu wa kurudisha masomo ya sanaa katika shule, pia Wizara yangu haina pingamizi na jambo hili, tutawasiliana na Wizara inayohusika kwa sababu tunaamini pia ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyininge ambayo Kambi ya Upinzani Bungeni ilisema ni suala la *Mastering Studio*. Sasa sijui maana hili nalo ni gumu kweli! Sugu hataki kuiacha yaani yeye Sugu ni Sugu kweli! Leo tunalisema sijui mara ya tatu. Rafiki yangu tukimaliza leo tusiliseme tena maana tunalisema na kulisema mwisho nikaanza kufikiria sijui kuna dawa ya kumchoma mtu sindano halafu anasahau ugomvi wa zamani!

Mheshimiwa Naibu Spika, habari yenyewe ni kwamba wakati *THT* ikisherehekea miaka mitatii ya kuanzishwa kwake mgeni wao rasmi alikuwa ni Mheshimiwa Rais na katika shughuli ile msanii moja anaitwa Lady Jay Dee alisoma risala kwa Mheshimiwa Rais kumwomba msaada wa *Mastering Studio*. Mheshimiwa Rais alikubali risala ile na baadaye akawapatia wale waliomwomba, lakini walishauriwa kwamba ni vizuri wakaunda Taasisi yao badala ya kushika mtu mmoja maana hofu ilikuwa ni kwamba ukisema tu umewapa atachukua mtu yeyote atajidai ni cha kwake. Kwa hiyo, cha msingi wakaambiwa waanzishie Taasisi yao halafu ile Taasisi ndiyo imiliki chombo hicho na ndiyo walianzisha kitu kinaitwa *Tanzania Flavour Unit* ambayo imesajiliwa kisheria kama Taasisi isiyo ya Kiserikali. Kwa hiyo, ndiyo inayomiliki chombo hiki kwa sasa na kilinunuliwa kwa karibu sh. 50,000,000/= za Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nirudie tu kusema kwa wale wote ambaa wanaamini kwamba chombo hiki ni mali ya *THT*, chombo hiki si mali ya *THT*, ni mali ya *Tanzania Flavour Unit* na kwa utaratibu wa kawaida mtu ambaye ana hamu ya kujuwa *Tanzania Flavour Unit* ina akina nani, kuna Msajili wa Taasisi anaweza kwenda kumuona akapata taarifa kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kulikuwa na hoja kwamba Serikali imetoa nyumba kwa *THT* na imesemwa na Wabunge karibu watatu. Mwezi huu Mtukufu siyo vizuri kusema mtu mwongo, katika mwezi huu Mtukufu tunaseme alipotosha kidogo, habari hii siyo ya ukweli. Kwa hiyo, ukweli

ni kwamba THT wamekodi nyumba wenyewe na wanalipa na si nyumba ya Serikali, kwa hiyo, habari kwamba wamepewa nyumba na Serikali si ya kweli. Kwa hiyo, waliotupa taarifa hizi ndani ya ukumbi wa Bunge ni wazi tu kuna watu waliokuwa nje, waliwapa taarifa ambazo siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya umuhimu wa kukuza Kiswahili. Nakubaliana kama nilivyosema awali na Kambi ya Upinzani kwamba Kiswahili chetu sisi ndiyo wenyewe dhamana ya kukikuza na siyo watu wengine kwa hiyo, lazima tushirikiane katika kukikuza.

Nikienda kwa wachangiaji wengine na naomba mniwie radhi sitaweza kuwataja wote, nitajielekeza kwenye hoja mbalimbali kwa sababu nikiwataja muda wote utaishia kwenye kuwataja majina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ni kuhusu maslahi ya waandishi. Nakubaliana na wachangiaji kwamba maslahi ya waandishi wetu ni madogo sana na wito tunaoweza kutoa kwa wamiliki wa vyombo vya habari mbalimbali, kuendelea kukuza mfumo wao wa masoko ili waweze kumudu gharama za kuwashudumia waandishi wao kwa sababu ni kweli pia kwamba ukiruhusu waandishi wasiwe na mapato kabisa unawageuza kuwa mateka na wakiwa mateka wataandika mambo yasiyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwa na weledi na uzalendo kwa waandishi wa habari. Nakubaliana moja kwa moja na waliochangia hoja hii. Ni kweli tunapotaka kujenga Taifa letu lenye umoja na mshikamano, ni lazima tuwe na utaratibu wa kuwa na waandishi wanaoandika kwa kufuata weledi na uzalendo kwa nchi yao na uzalendo siyo maana yake kupendelea Serikali maana wakati mwingine hata ukisema uzalendo mtu anadhani ni kupendelea Serikali au kupendelea Chama cha Mapinduzi. Uzalendo ni kutoandika mambo ambayo yana madhara kwa nchi yako, uzalendo maana yake kuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nilikuwa nawaambia waandishi wa habari kwamba ukienda ukamtafuta Shehe mahali ukamuuliza maswali halafu ukatengeneza swalii la uchokozini, Askofu fulani alichukua mali zisizo zake, huyo Askofu unamuitaje? Si atakujibu ni mwizi! Halafu wewe unaacha kwenda kusema ulichomuuliza unaandika Shehe asema Maaskofu wezi na yeye Askofu akienda kuulizwa Shehe amesema wewe mwizi atajibu nini? Atasema, mwizi mwenyewe, siyo! Wewe unakwenda kuandika, unaendelea na mchezo huu wa kuchonganisha katika akili yako unadhani unaauza gazeti kumbe unaauza uhuru wa usalama wa nchi yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokutana na waandishi wa habari niliwaambia kwamba hata viongozi wa Serikali tunayoyasema ambayo mnahisi yanahatarisha umoja na usalama wa nchi yetu msiyaandike. Mtu anasema hapa tutamwaga damu, halafu wewe unarudia kwenye televisheni mara tatu, hapa tutamwaga damu! Hapa tutamwaga damu! Hapa tutamwaga damu na unaona raha kama chizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndiyo tunasema kwamba hapa huyu mwenzetu siyo mzalendo, yeye haoni kabisa kwamba Taifa hilli likivurugika yeye anayo hisa ya usalama wa nchi yetu, ana hisa na maisha katika nchi yetu. Kwa hiyo, niseme wito huo wa Bunge letu kwamba waandishi wa habari wawe wazalendo na namshukuru sana Mungu kwamba katika michango hii ya maandishi wito huu haujatoka upande mmoja. Wabunge wa CCM wameongelea uzalendo, CHADEMA wameongelea uzalendo, CUF wameongelea uzalendo kwa uzito mkubwa na wote neno uzalendo mlikuwa mnalipigia misitari kuonesha mnalitambua neno hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, tusichoke kuongea kuhusu uzalendo kwa nchi yetu. Maana si muhimu nani yuko madarakani au nani yuko chama cha upinzani. Wenzetu kama Marekani kule huwezi kujua hata nani kaingia madarakani, nani katoka! Ukienda kuvitazama vyombo vya habari kuna mambo makubwa ya nchi yote wanayachukua kwa uzito ambaa unafanana kwa magazeti yote, kwa kipindi chochote na sisilazima tufike mahali tuseme Tanzania ni nchi yetu. Kila Mtanzania ana nafasi sawa na Mtanzania mwenzake katika nchi bila kubaguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya vipindi nya redio kwa wanafunzi. Niseme tu kwamba, hoja hii ni ya muhimu. Jambo hili limekuwa likifanyika lakini kama mnavyofahamu vipindi hivi vinahitaji ufadhili mara nyingine na tumesema tutashauriana na wenzetu waliokuwa wanafadhili kuhusu jambo hili, tuone kama wanaweza kuendelea kutufadhili ili viendelee kutoka kwa wingi. Lakini na sisi tunavifanya mpaka sasa, japo si kwa muda wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kumalizia *studio* ya kuweka nyaraka ambazo ni *digital*. Kulikuwa kuna malalamiko kwamba Serikali iliishatoa shilingi milioni mia sita (600,000,000/=) bado shilingi milioni mia sita (600,000,000/=) ili shughuli hii ikamiliike. Niwaambie tumelichukua hilo kwa uzito unaostahili na lenyewe tutaona namna ya kulimaliza haraka. Lakini pia tutaweka nguvu zetu zaidi katika kumaliza jengo la Mikocheni ili ikiwezekana nyaraka hizi zianze kwanza kuwekwa mle. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watumiaji na wasambazaji wa *cable TVs* ambao tumeambiwa kwamba maeneo mengine wanarusha matangazo bila kuhakikiwa. Nataka niwahakikishie kwamba *TCRA* inafuatilia kwa karibu sana na wengi wamekamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria na nimewaelekeza Kamati ya Maudhui waendelee kufanya jambo hili la kufuatilia kwa karibu. Lakini pia *TCRA* imenihakikishia kwamba wataongeza kasi ya ukaguzi kwa sababu vipindi hivi visiporatibwa vinaweza kuwa na madhara makubwa kwa nchi yetu kama hatutakuwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wanawake kudhalilishwa katika *TV* mbalimbali. Hili nalo ni suala gumu. Kwanza nakubaliana na wasemaji kwamba jambo lenyewe halivutii tunapoona dada zetu wakiwa kwenye vipindi ambavyo havileti heshima. Unajua Mwfrika ana heshima yake. Kuna namna ambavyo Mwfrika anajisikia vizuri kutoka nje na kuonekana. Lakini msingi wa heshima ya mtu unaanzia ndani yake yeye mwewewe. Naambiwa zamani watu walikuwa wanakamatwa na kuvishwa khanga na nini, lakini leo tukisema tunakamata na kuvisha khanga, wengine watakamata na kuvua, maana kila mtu anaitumia sheria kwa staili yake. Ila tunasema msingi wa heshima ya mtu unaanzia ndani yake mwenyewe, unaanzia kwenye malezi katika familia yake, malezi katika jamii anayoishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza, tuwatake wazazi wasipuuze mikao na namna watoto wanavyotoka nyumbani. Wazazi ni lazima watekeleze wajibu wao. Kwa hiyo, tunawaomba wazazi wa Tanzania wafanye wajibu wao huo bila haya. Kumwambia mtoto umuhimu wa kuishi kwa maadili si kero, hata akitasirika wewe mwambie, ni wajibu wako kumwambia. Wajibu wa mzazi ni kumkumbusha mtoto kila wakati bila kujali atanuna, atakasirika, huo ndiyo wajibu wa mzazi. Kwa hiyo, nawaomba wazazi wa Kitanzania wote tushirikiane na kuwafanya watoto wapende kuva mavazi yenye heshima. Lakini nawaomba nao binti na dada zetu watambue kwamba heshima yao ni heshima yetu, wanapojidhalilisha wanatudhalilisha. Wajilinde, watulinde na sisi ili na sisi tupite barabarani tukiwa tunajisikia vizuri, tunalindwa na ndugu zetu hawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyombo nya habari kutozingatia habari ya kutangaza kwa namna ambayo walemau wanaweza nao wakaelewa kinachotangazwa. Naomba niseme kwamba, nimeuchukua wito huu kwa uzito mkubwa na tunaviomba vyombo nya habari vichukue hatua za kulirekebisha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vyombo nya habari kutangaza matangazo kwa maslahi binafsi. Tunaomba na vyenyewe vijitahidi kutangaza kwa maslahi ya umma. Kuhusu upotoshaji wa habari kwa kuzingatia makundi ya kisiasa. Hili nalo ni jambo la heshima tu kwamba katika nchi ambayo demokrasia yake bado inakuwa, katika nchi zetu ambazo bado ni changa magazeti yana nafasi ya pekee katika kuimarisha utilivu au msingi wa nchi yenye au kuua na hasa katika mazingira kama ya nchi yetu. Mpaka sasa tunakwenda vizuri, lakini tunaviomba vyombo nya habari vijiepushe na makundi ya kisiasa, vizifanyie utafiti vyenyewe taarifa vinazopata. Maana wakati mwengine ni kweli unakuta habari imetengenezwa riwaya lakini jamii inataka iaminishwe kwamba habari hii ni ya kweli. Walikutana pale, kulikuwa na kikao, alikuwepo Sugu, Mbwe na Zitto Kabwe, wamekubaliana moja, mbili, tatu na *minutes* za mikutano hizi hapa. Kumbe uongo

mtupu! Yaani mtu mzima anakaa, anaandika uongo halafu anauweka kwenye gazeti. Sasa tufike mahali wanaofanya hivyo wajue kwamba mchezo wao ni maafa kwa Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka katika Bunge liliopita kuna Mbunge mmoja na Waziri mmoja wameanza kuongea mwezi uliopita. Mmoja alipewa habari kwamba mwenzake kakaa kwenye kikao na ndiye aliyejua anachangia mada ya kummaliza akisema; huyu mpuuzi, hana maana, ana nini, kumbe hicho kikao hakijawahi kuwepo. Huyu anayetajwa wakati huo alikuwa yuko nje ya nchi, lakini wanasema alikuwa yuko kwenye kikao, mpaka kampelekea mwenzake tiketi ya ndege kumuonesha alikokuwa na risiti za hoteli alikofikia na taarifa ya mwaliko aliouputa. Ndipo mwenzake anatambua aah, kumbe habari ile nilidanganywa! Lakini Mtanzania wa kawaida ukimwambia habari hii si ya kweli anasema haiwezekani! Habari hii ni kweli kwa sababu nimeiona mwenyewe kwenye gazeti. Nimelona mwenyewe kwenye gazeti! Hii ni kwamba Watanzania wanaamini magazeti kwamba kila yanachoandika ni kweli!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ni heshima kubwa sana kwa vyombo vyetu vya habari kwamba Watanzania wanaviamini. Viitumie fursa hiyo vizuri, viendelee kujenga kuaminiwa. Hiyo ndiyo namna pekee ya kuwa na vyombo vya habari vinavyowajibika kwa umma na sisi umma tuwajibike kwa vyombo vya habari. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mafunzo kwa waandishi wa habari nakubaliana na hoja iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa kuna malalamiko kuhusu *Big Brother Africa*. Nataka nikubaliane na wote walilalamika kwamba kile kipindi ni kero! Kile kipindi ni kero! Tunataka Watanzania wanaotusikiliza wajue kwamba Serikali haikiungi mkono, wala Bunge halikiungi mkono! Kinaonesha mambo ya fedheha waziwazi, hatujui kinataka kufundisha nini watoto wetu. Ni bahati mbaya tu kwamba utaratibu wa kualikana unafanywa kwa njia ya *internet*, si utaratibu unaopitia Serikalini. Lakini tunataka Watanzania wanaotaka kwenda kule wajue kwamba, hawana baraka za Serikali. Hatuwashabikii! Hatuwaungi mkono na ndiyo maana hatujawahi kwenda kuwapokea. Kwa hiyo, wazazi wajitahidi kushauri watoto, kipindi kile hakina maana yoyote, kinamharibu anayekwenda na kinaharibu ndugu zake waliobaki nyumbani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja kuhusu umuhimu wa kuimarisha muziki wa Kitanzania. Tunakubaliana na hoja hiyo. Muziki wa dansi umedorora! Tutashirikiana kuona tunauamsha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hoja nyingine ni juu ya maadili ya vipindi vyetu vya *TV*. Tutaendelea kutoa wito kwa vyombo mbalimbali vya Televisheni kuona kwamba vinazingatia maadili yetu vinaporusha vipindi vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matangazo ya lugha mbalimbali kwenye *TBC*, mchangiaji mmoja alisema ni vizuri lugha mbalimbali za jadi kama Kingoni, Kbarabaigi, zitumike kwenye *Tlevisheni* ya Taifa. Nasema kwa sasa, wazo hili la kutumia lugha zetu si baya sana lakini lisubiri nikishatoka kuwa Waziri, sababu siamini kama lina tija. Hatari ya jambo hili ni kujenga misingi ya ukabila katika nchi. Maeneo mengi tumeshuhudia kwamba, waliporuhusu lugha za kikabila zitumike ndizo zilizochochea misingi ya vurugu katika nchi, kwa sababu wengine mnasikia, wengine hawasikii kumbe mambo yanayoongewa ni ya kuvunja nchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu Baraza la Vijana, niwahakikishie kwamba tunachukua hatua zinazostahili kuhakikisha kwamba linaundwa mapema inavyowezekana. Benki ya Vijana na yenye kwa kifupi kwamba, tunayo nia na nillisemea hii kwenye Kamati juu ya kuona kwamba tunatengeneza *SACCOS* za vijana katika nchi nzima, lakini tunataka *SACCOS* ndiyo ziwe wateja wa benki hiyo na siyo mtu mmoja mmoja, huo ndiyo mwelekeo tunaoupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgogoro wa CHANETA, tutaufutilia kwa karibu tuone namna ambavyo unakwisha. Hili ni jambo ambalo halivutii kwani tukiwa na migogoro hatuwezi kufanikiwa katika shughuli hizi za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijamaliza nimirambue mchangiaji kwa maandishi Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, naye alichangia katika hoja ya leo

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwanza nakushukuru sana wewe kwa kutuongoza vizuri kufikia hatua hii tuliyofikia, lakini pia wakati Naibu wangu alipoipongeza timu ya Yanga, nilipata hofu nikasema, sasa huyu Naibu Spika, atatumaliza maana huwa anapata mshituko wa moyo akisikia Yanga inatajwa. Lakini natumaini Mheshimiwa Naibu Spika, haitakuwa sababu ya kutushughulikia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo nakushukuru sana na naomba kutoa hoja. (*Makof*)

(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Dokta Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; kwa ufanuzi wa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri ametoa hoja na imeungwa mkono. Katibu!

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### FUNGU 96 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Kif. 1001 - *Administration and General..Sh. 1,702, 286,000/=*

**MWENYEKITI:** Kule Songea wanasema tunaanzia palepale penyewe pale! Tuanze na Mheshimiwa Waziri Kivuli, Joseph Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naona Waziri amejitahidi kunionya kwamba tusilizungumzie tena hili suala, lakini hili suala ni nyeti kuliko yeye anavyofikiria kwa sababu kama nilivosema *issue* hapa siyo *studio*, mimi ningekutana na *President* Jakaya Kikwete angeniuliza, Wasanii niwasaidie nini? Nisingemwambia *studio*, ningemwambia, arekebishe *policy* ambazo zingenifanya msanii kama mimi niwe na uwezo wa kununua *studio* za sh. 50,000,000/= kama kumi kwa mwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema Lady Jaydee alikuwepo Tanzania *House of Talents (THT)* ndio maana nikasema kwamba inatemegea, Rais anaweza kutoa *order* au ahadi popote kwa sababu Lady Jaydee siyo msanii wa *THT*. Kwa hiyo, ndio maana nikasema kwamba ile ahadi hata kama imetolewa katika viwanja vya *THT* ni kwa wasanii wote kama ambavyo Rais alikwenda *Diamond Jubilee Hall* kuongea na wazee lakini alikuwa anaongea na watu wa *TUCTA*, nafikiri ndivyo inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anasema Rais aliwaagiza waunde chombo, kuna chombo kiko chini ya Serikali yake, chini ya BASATA, kwa nini aagize kiundwe chombo kingine! Ndiyo maana nasema siwezi kuamini kama hicho kitu kinaweza kikafanyika! Rais anajua kwamba kuna chombo kiko chini ya Serikali yake, chini ya BASATA kwa mujibu wa sheria, halafu alete watu wengine. Naomba maelezo! Kama wanasema ile nyumba siyo ya *THT*, Rais alisema ametoa pango, hilo pango alimpa nani na liko wapi? Je, hizo fedha alizotoa ni za binafsi au ni za Serikali?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbilinyi. Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru ndugu yangu Mbilinyi kwa swali lake zuri. Wakati akichangia katika mchango wake asubuhi nilimkariri akisema kwamba jambo hili si muhimu sana ila ametafuta tu *weak point* na sisi kama Serikali hatushughulikii *weak point*.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize swali Bwana Waziri. Ni miaka mingi sasa ni lini hasa Sheria ya Vyombo vya Habari italetwa Bungeni?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhanikishie na Bunge lako kwamba tunafanya jitihada haraka inavyowezekana. Ikiwezekana katika mwaka huu wa fedha tuweze kulifanikisha jambo hili.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningependa kumwuliza Waziri kufuatilia ahadi ya Rais aliyoitoa ya Kuunda Kikosi Kazi kwa ajili ya kufuatilia wizi wa kazi za wasanii wetu. Je, Kikosi Kazi hicho kimeundwa na kama kimeundwa ni taratibu gani zilifuatwa kwa sababu bado wasanii wanalamika?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Kiwelu kama ifuatavyo: Suala la ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuundwa Kikosi Kazi ahadi hiyo ni sehemu ya maelekezo na ndiyo maana mimi, Waziri wa Fedha na Waziri wa Viwanda na Biashara tumekutana wakati wa utekelezaji wa agizo hili.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nchi nydingi zinakuwa na utaratibu wa kukumbuka wachezaji wao mbalimbali. Kwa mfano, Uingereza kuna alama za Stanley Mathew, ukienda Urusi kuna Raviation, Wajerumani wana Caisar ambaye ni *Franceback Empower*. Sitaki twende huko hivi kwa nini Wizara isishirikiane na *TFF* ili wachezaji wote wa soka wa Tanzania kama vile Kitwana Manara, kina Hemed Seif, John Lyimo, Tenga majina yao yakawekwa kwenye ubao maalum kwenye Uwanja mpya wa Taifa ili *inspire* za wachezaji wengine na wao watake kuwekwa kwenye ubao ule na iwe kumbukumbu kwa Tanzania, wachezaji wa zamani wa Taifa *Stars* ambao walileta sifa kubwa sana nchini mwetu.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Zungu, ushauri wake ni mzuri kwa sababu utafanya vijana nao waone kwamba mchezo huu unaweza kufanya uheshimiwe na Taifa baadaye. Kwa hiyo, tumeuzingatia tutatafuta namna nzuri ya kuufanya kazi.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Yako malalamiko kutoka vyama vya michezo kwamba hawapati msaada wowote kutoka Baraza au Serikalini hasa kwa mashindano ya Kimataifa. Siku za nyuma kulikuwa na vyanzo vitatu ambavyo vilikuwa vimeomba Baraza la Michezo kusaidia vyama vya michezo ambavyo havina fedha. Kwa mfano, mapato yanayotokana na bahati nasibu, kuna asilimia fulani ilikuwa inakwenda Baraza la Michezo vinasaidia vyama hivyo.

Halafu vile vile katika mechii za *Football* zinazochezwa Uwanja wa Taifa, asilimia moja ilikuwa inakwenda Baraza la Michezo inasaidia vyama vingine hivi ambavyo havina fedha. Lakini vile vile kupitia bajeti yetu, Wizara ilikuwa inatenga kitu kinaitwa *International Participation Fund*. Hivi vyanzo vitatu vilikuwa vinakaa Baraza la Michezo na vinasaidia vyama vingine kama *netball*, sijui riadha, *cricket* na kadhalika ukiacha *football* ambao kiasi fulani wana fedha. Je, vyanzo hivi bado viwo? Kama havipo sasa Serikali inafanyaje kusaidia vyama hivi ili viweze kuwaandaa timu zao vizuri na viweze kushiriki mashindano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Missanga kwa suala lake zuri. Niseme tu kwamba, Serikali inaendelea kusaidia timu mbalimbali zinapotoka nje, lakini kwa kiwango kidogo sana. Kinachotuhangaisha sasa ni namna ya kuboresha mapato haya ya Serikali ili tuweze kusaidia zaidi. Kwa kweli huwa inaleta tabu sana hasa inapokuja *issue* zinazohusu timu zetu kwenda nje. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tunalipa uzito unaostahili na tutalifanyia kazi kwa nguvu zaidi kuliko mwanzo.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kuchangia nilitoa ushauri kuundwe Shirikisho la Michezo la Taifa, liwe na Wajumbe kutoka Bara na Visiwani. Kwa hiyo, naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, hilo la kuhusu uwezekano wa kuunda Shirikisho. Nadhani hilo ni wazo zuri na tumesema tutalishughulikia na ushauri wako tutauzingatia. Ahsante.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Uwanja wa Lindi ujulikanao kama Lindi *Stadium*. Tangu uwanja huo ujengwe mwaka 1957 na Bwana Sir Edward Twining mpaka leo uwanja huo uko vile vile. Zamani ulikuwa na taa na walikuwa wanacheza mpira Kanda ya Afrika Mashariki, lakini leo hata Kanda ya Kusini hawachezi mpira pale. Tunaomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Ufanuzi, uwanja wa Lindi hali mbaya sana kama uwanja wa Kaunda.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Fatma Mikidadi kama ifuatavyo: Kwanza tunasikitika pamoja naye kuhusu hali ya uwanja huo. Kwa sasa tunataraja siku za karibuni kuwa Wakala wa Kusimamia Miundombinu ya Michezo nichini. Lakini wakati tukitarajia sisi kufanya hivyo tunaomba Halmashauri ya Wilaya inayohusika pia itimize wajibu wake kule kwa mambo ambayo yako ndani ya uwezo wake.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya ukosefu wa matangazo ya radio Tanzania kuititia Shirika la *TBC* maeneo ya Wilaya ya Mpanda hayasikiki. Ni sababu gani zinazofanya mpaka sasa wananchi wa Wilaya ya Mpanda wasipate matangazo hayo?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo: Suala la matangazo kupatikana katika eneo la Mpanda ni katika yale niliyoyasemea katika hotuba yangu ya bajeti. Katika *transmitter* tulizonunua ni pamoja na *transmitter* kwa eneo la Mpanda. Kwa hiyo, tunaomba wavute subira kwa sababu vifaa tayari vipo zoezi lillobaki ni la kufunga tu.

**MHE. KULIKOYELA K. KAIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimefurahi Waziri alipokubali kuwa mabango, Miswada ya Sheria Bungeni na hata rekodi katika Mahakama za Juu ziandikwe kwa Kiswahili. Sasa nilichokuwa nataka kumwuliza ni kwamba anaweza kutupatia dokezo la ratiba ya utekelezaji wa jambo hili. Kwa sababu ni jambo ambalo lilipaswa kutekelezwa toka zamani hata Waziri aliyejita nadhani ni Mheshimiwa Mkuchika alishalizungumzia kwamba jambo hili lilipaswa kutekelezwa, lakini hakukuwa na ratiba. Tunaomba atupatie ratiba ili tatizo hili liishe tufanye mambo mengine.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Kahigi kama ifuatavyo. Maeneo mengi yameanza utaratibu huo. Kwa kweli Profesa ye ye anajua, ye ye ni mtaalam katika sehemu ya taratibu za kazi ya Waziri akifika hapa kuanza kutoa ratiba wataalam wake watamshangaa sana, maana watashangaa wao watabaki wafanye kazi gani kama Waziri ndio anatoa ratiba. (*Makofu/Kicheko*)

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningombwa kupata ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Serikali hii ina utaratibu gani ya kuwaenzi wanamichezo waliostaafu ambao wameletea sifa nchi hii na medali mbalimbali ama za dhahabu au za shaba, lakini inaonekana hali zao za maisha sio nzuri? Sambamba na hilo ni kwa jinsi gani ambavyo wale wengine ambao wataletea sifa nchi hii ambaobado wako hai. Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu Serikali inatambua sana umuhimu wa hawa ambao wanatuwalilisha kwenye shughuli za Kimataifa, kama aliyosema Mheshimiwa Masoud. Tumekuwa tuna upungufu katika kuwaonesha namna gani tunajali. Pengine pia tukifanya utaratibu wa kuimarisha mapenzi ya wananchi kwa michezo hiyo ili inapokuwa kwa mfano, na viingilio waweze kushiriki vya kutosha. Lakini pia wadhamini waweze kushiriki vya kutosha kwa sababu wakati mwagine tukiwatengenezea mazingira mazuri ya sasa yatawatengenezea wao mazingira mazuri ya akiba za baadaye.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati wasanii wakiwa wanapata shida kupanga foleni na kubembeleza kuuziwa kazi zao kwa wasambazaji ambao wanataka kazi zao ziwe na majina ya wasanii wakubwa wakubwa kumbe Serikali imeamua kugawa jengo ambalo lilikuwa linatoa tija na manufaa lilitolewa na Mwalimu Nyerere kwa ajili ya kusambaza kazi zao. Namtaka Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi jengo hilo wameligawa kwa nani na kwa nini wameligawa na hatma yake ni nini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Jengo lipi Mheshimiwa Mlata ili sote tuelewe swali?

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Jengo la Nyumba ya Sanaa.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mlata kama ifuatavyo: Jengo hilo analolizungumzia Mheshimiwa Mlata liko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na kwa kuwa Mungu ni mwema Wizara ile bado siku yake.

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nitofautiane na wenzangu nimpongeze Mheshimiwa Waziri alivyokuwa na umahiri mkubwa sana katika kujibu hoja zilizotolewa na Wabunge wakati wa kuchangia hotuba hii ya bajeti. Lakini tofauti na Mheshimiwa Naibu Waziri majibu yake mengi yalikuwa ni majibu rahisi sana kwa maswali magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, majibu kama Serikali imelipokea, Serikali bado inatafakari, bajeti ikiruhusu tutalifanya kazi, tuko mbioni, ushauri umepokelewa, ushauri tunauzingatia. Nadhani sio majibu mazuri kwa Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lako hili. Ningependa basi hata Waheshimiwa Mawaziri wengine wajaribu kuiga mfano wa Mheshimiwa Waziri Nchimbi jinsi alivyo na umahiri katika kuliweka suala zima vizuri na watu wangeweza kuelewa na mimi mwenyewe kwa kweli nimefarijika sana Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, swali sasa la msingi naomba kuuliza, je, Mheshimiwa Waziri uko tayari sasa kushirikiana na Mawaziri wengine ili uweze kuwaelekeza jinsi ya kuwa wanajibu maswali hapa Bungeni? (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini katika mchango wangu wa maandishi pamoja na umahiri ambao ameuonyesha Mheshimiwa Waziri kwenye kujibu hoja nilisema kwamba Serikali itumie fedha ambazo tunazipoteza kuwalipa makocha wa kigeni kuwaenzi na kuwaendeleza wachezaji wetu au wana michezo wetu kuwapa ujuzi nje ya nchi. Je, suala hili amelichukuliaje na sikupata majibu yake?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mangungu kama ifuatavyo: La kwanza ni kwamba, ushauri wake tuliusikia, lakini kwa bahati mbaya sana Makocha wale wa kigeni tunawahitaji na sio sisi peke yetu hata nchi kubwa zinaita Makocha wa kigeni na zinawapa mshahara mkubwa. Hoja kubwa pale ni kufundisha Makocha wetu. Kwa hiyo, tutawatumia Makocha hawa pia kufundisha ndani ya nchi lakini vile vile tutatengeneza programu za kuona kwamba Makocha wetu wanafundishwa ili baadaye tuwe na Makocha wazalendo wa kutosha. Kwa sababu ni ukweli ulio wazi kwamba hatuwezi kumudu kuweka Makocha wa kigeni kila sehemu. Mwisho wa siku lazima Watanzania wenyewe wawe wengi zaidi, tutaweza kuwamu du kuwagharamia, lakini pia watafundisha kizalendo zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo karibu sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu kuhusiana na suala zima la kuboresha maslahi au mazingira ya kazi ya wanamuziki wetu, tuna wasanii kwa ujumla alitoa majibu ambayo yalishatolewa pia na Mheshimiwa Mary Nagu wakati akiwa Waziri wa Viwanda na Biashara miaka mitano iliyopita. Sasa naamini labda wewe una mtazamo wako mpya na nakutakia kila la kheri. Lakini kumekuwa kuna watu ambao wanatuhumiwa kuiba hizi kazi za wasanii na Kampuni ya *Steps Entertainment* imekuwa inatajwa kabisa na hawa wasanii. Sasa kama Wizara mmechukua ama mna mpango wa kuchukua hatua gani kutumia vyombo vyetu vya dola kwenda kuanza kufanya uchunguzi wakati hiyo mipango mingine inaendelea ili hawa watu wasiendelee kufanya wanayoyafanya?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mdee kwa swali lake. Labda niseme tu kwa sheria tulizonazo sasa sisi hatuna chochote cha kufanya isipokuwa *COSOTA* inacho cha kufanya. Ndiyo maana katika maelezo yangu nimesema kwamba tutashirkiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kwamba *COSOTA* inapata meno ili iweze kufanya kazi vizuri. Lakini kwa vyovoyote vile hatuwezi kuwa tunapuuza jambo hili liendelee kutokea kwa kusubiri sheria mpya. Kwa hiyo tutachukua hatua.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeuliza mkakati wa Wizara namna ya kusaidia Halmashauri zetu za Wilaya na Mkoa kuhusu Idara ya Utamaduni na Michezo kwani zinashindwa kuijidesha hata kusafirisha timu na wasanii wanapokwenda kushiriki michezo ya Kitaifa.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Chilolo kama ifuatavyo: Suala la maaifisa hawa ambao wako katika Halmashauri zetu za Wilaya, kimuundo tunalishughulikia katika ngazi ya Serikali kuliweka vizuri zaidi. Lakini suala la namna wanavyofanya kazi niwaombe Waheshimiwa Wabunge watumie ushawishi wao kwenye Halmashauri zao kuona kwamba zinatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kusaidia shughuli hizo.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa kanuni hairuhusu kurudia yaliyokwisha semwa swali langu limekwishapata ufumbuzi.

**MWENYEKITI:** Nakupongeza sana kwa kuzingatia kanuni.

**MHE. LOLESEA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilijaribu kuonyesha jinsi ambavyo sekta ya madini imeajiri vijana walio wengi. Lakini katika hotuba siaona mahali popote ambapo panazungumzia suala la wachimbaji wadogo wadogo hasa vijana. Kwa hiyo, ningependa kufahamu kwamba Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuwawekea mkakati hawa vijana ili kuwaendeleza. Nahitaji ufanuzi katika hilo?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Bukwimba kama ifuatavyo: Kwanza ni kweli kwamba vijana wanajishirkisha sana katika sekta hii. Jambo ambalo kwa sasa Serikali imepata uzoefu wa kutosha ni kwamba vijana wale kila fedha wanazopata hawana utaratibu wowote wa kufanya waendelee kuwa na fedha hizo. Kwa hiyo, tumeanzisha mtaala wa stadi za kazi kwa kushirkiana na wafadhili ambao tunajitahidi kuusambaza lakini uwe ni sehemu ya mafunzo kwa vijana hao na vijana wengine. Kwa hiyo, tunaomba, muda utakapofika basi Mheshimiwa Mbunge atupe ushirikiano katika eneo lake.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilipenda kujua tatizo la Jimbo la Manyoni Magharibi kutosikia *TBC*. Tuna ujo wa watu wa *TBC* Singida, lakini sehemu kubwa ya Mkoa wa Singida na hasa Jimbo langu hatusikii kabisa *TBC*. Tunategemea redio moja tu Redio Mwangaza na hizi redio zingine hatusikii kabisa. Sasa tungependa kujua *TBC* wana utaratibu upi wa kuweza kuisambaza hii huduma Mkoani Singida?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe Mheshimiwa Lwanji atuachie jambo hilo, tunajua umuhimu wa usikivu kwa faida ya watu wake. Tatalifanyia kazi tuone namna ya kulitatuwa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa mchango wangu niliomba ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri mpwa wangu, kwamba Serikali imejenga Uwanja wa Taifa kwa zaidi ya shilingi bilioni 50 kwa mambo mawili. Ili kwanza, kukuza michezo wa mpira na michezo mingine hapa nchini. Lakini kuweka kitega uchumi cha *ku-invest* kwenye kukuza michezo. Baada ya kujenga mashine za kuhesabu watu *Turnstiles machines*, bei yake moja ni dola

35,000. Kwa nini Serikali haiweki hizo mashine ili tuweze kupata mapato yanayopaswa pale uwanjani?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwambalaswa kwanza amenifarji kwamba mjomba yupo kwenye karne ya sayansi na teknolojia. Lakini la pili, hoja yake tumeichukulia kwa uzito unaostahili isipokuwa kwa sasa ambapo tunategemea kuunda wakala wa kuendesha viwanja vya mipira ni jambo la busara wakala akishakuwa ameanza kufanya kazi ndiyo achukue huo utaratibu. Kwa hiyo, nimwambie tumeuchukua huo utaratibu lakini pia tutawashirikisha wadau wengine ili waweze kuuelewa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Wakati nilipokuwa naongea hapa jana nilisema kwamba, Bunge hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nikaiomba Serikali kwamba na waandishi mbalimbali wa habari wanakuja hapa lakinii nikaiomba Serikali ishauriane na Wizara kama hii ya Zanzibar ili waandishi wa habari wa Zanzibar nao waje hapa na waweze kuripoti matokeo mbalimbali ya Bunge. Ahsante.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Faida Bakar kwamba tunafanya kazi kwa karibu sana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hiyo, tutatafuta muda mapema inavyowezekana na kwa kuwa kikao chetu cha ushirikiano kipo siku za karibuni kati ya sisi na Wizara ile ya Zanzibar moja ya ajenda ya kwanza ambayo nitahakikisha inazungumzwa ni hiyo ili kuona waandishi wanapata fursa ya kushiriki katika Bunge letu.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru Mheshimiwa Waziri kanijibu swali langu la *Big Brother* lakini sasa tatizo lipo kwa *Miss Tanzania*. Hawa *Miss Tanzania* wanaingizia Taifa pato gani na kwa nini kushiriki kwao mpaka watembee uchi ndiyo tupate *Miss Tanzania*? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Maryam Msabaha na kwa kuwa sikusudii kuiharibu swaumu yake naomba niliambie Bunge lako kwamba toka michezo hii ilipoanza ya U-miss katika nchi yetu kama mtaitazama mtagundua kwamba tumepiga hatua kubwa. Mwanzo ilikuwa mambo ya hovyo zaidi na Serikali imekuwa muda wote ikiwaelimisha nini cha kufanya. Kwa hiyo kuna mabadiliko makubwa na hatutaacha iishie hapo. Tutaendelea kuwaelimisha na kuhakikisha kwamba watu wakiwa wenye staha zao wanaweza wakatazama na wakafurahi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri *Miss Bunge* lini? Tunaendelea na Mheshimiwa Zarina Madabida. (*Kicheko*)

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia kuhusu vijana ambao ndiyo kwanza wamemaliza chuo au wale ambao wamemaliza Chuo Kikuu ama hawa wa kutoka kwenye vyuo mbalimbali, hawana kazi, hawana hela. Kwa hiyo unapomwambia aende akajunge *SACCOS* ili aweze kupata mtaji, hana mtaji. Wizara ina njia gani ya kuwasaidia? Katika mchango wangu nilisema kwa nini basi wasiwakopeshe vifaa kufuatana na fani zao ili kusudi na wao waweze kujikimu na kuchangia katika pato la Taifa?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna tatizo kubwa la vijana wetu kupata ajira hata waliosoma na kwa pendekeso kwamba wale waliokuwa na elimu watafutiwe uwezekano wa vifaa ni jambo ambalo linazungumzika, tunaweza tukakaa na wataalam wakatushauri namna ya kufanya, maana jambo lenyewe ni kubwa na la kitalaam linahitaji kushauriwa vizuri.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kwamba kwa kuwa wachezaji wengi wa soka hapa nchini wengi wanaacha kwa sababu tatu muhimu. Kustaifu, kiwango kushuka na wengine kwa kuumia na kwa kuwa yapo Mashirika ya Hifadhi ya Jamii kama *NSSF*, Wizara haioni umuhimu wa kuwachangia kwenye *NSSF* ili wakistaifu au wakiumia waweze kulipwa pensheni zinazotolewa na mashirika haya.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba wachezaji wetu wale hawana utaratibu wa maisha yao ya baadaye, hawana utaratibu wowote wa hifadhi. Lakini jambo lenyewe kwa uzito wake na umuhimu wake na wenyewe wataalam wetu watalifanyia kazi ili waone kama linatekelezeka.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Naomba nizungumzie suala la uhuru wa habari pamoja na kwamba nimepata majibu lakini upande wa pili sikupata jibu. Kwamba uhuru wa vyombo vya habari kuingiliwa na viongozi wa Serikali, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwanyanya waandishi wa habari na kuwaweka ndani na mara nydingi hukatazwa kwamba wasitoe habari fulani. Je, hawa viongozi hawatakiwi kuchukuliwa hatua na ni hatua ipi?

La pili muhimu, Mheshimiwa Waziri kwenye viambatanisho vya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, *sub-vote* 1001, ukurasa wa 61, kinga ya maambukizi ya UKIMWI ilitolewa bajeti yake mwaka 2011. Lakini haikupatikana fedha hata kidogo. Je, mmewatendea haki wale ambao ni waathirika na walipata fedha kutoka wapi kwa ajili ya matumizi yao kwa ajili ya kujikinga UKIMWI?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rose Ijibiwe lipi, la kwanza au la pili?

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Yote, kwa sababu ni muhimu lakini nataka hili la viongozi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa mama Kamil kwamba kwa vigezo vyovyote atakavyotaka kuvitumia katika nchi za Afrika Mashariki na kati hakuna sehemu ambayo uhuru wa vyombo vya habari upo kama Tanzania na hata Sheria tunayokusudia kuitunga haiwezi kutoa uhuru kuliko uliopo sasa. Vyombo vya habari ni shahidi wa jambo hili.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri aweze kunipa ufanuzi juu ya jambo moja. Tangu uhuru na hata baada ya uhuru michezo imeonekana kuwa ni moja ya vitu muhimu sana hapa nchini na ukipita katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu utakuta kwamba kuna tatizo la viwanja vya michezo. Lakini inaonekana kuna baadhi ya viwanja ambavyo vilikuwa vikimiliwa na Serikali toka enzi za mfumo wa chama kimoja. Leo hii viwanja hivyo vinaonekana baadhi yao vinamiliwa na Chama cha Mapinduzi hali ambayo inawanyima fursa baadhi ya watu ambao pengine wanataka kwenda kuchezea viwanja vile hawapati fursa. Naomba kauli ya Serikali ni kwa nini viwanja hivyo visichukuliwe na kumiliwa na Serikali ili kusudi vikaweza kutumiwa na Watanzania wote kwa kuwa hata enzi za chama cha *TAA*, wakati *TAA* bado ni *Tanganyika Africans Association*, kikiwa kama chama cha wafanyakazi na ikaja *TANU* kilikuwa ni chama cha Watanzania wote na hata baada ya uhuru *TANU* kilendelea kuwa chama cha Watanzania wote. Kwa nini viwanja hivi vinaendelea kumiliwa na Chama cha Mapinduzi, mfano kiwanja cha CCM Kirumba kule Mwanza? Sina imani kwamba CCM ndio walijenga peke yao ila ni kodi za Watanzania wote wa enzi hizo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Sidhani kama nimemwelewa Mheshimiwa Machali, yaani viwanja vya CCM vichukuliwe na mtu mwininge?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu sana nikiulizwa maswali na rafiki zangu. Labda niseme tu kwamba, kwanza nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo kimeweza kusimamia kujengwa viwanja vile na kuvitunza mpaka leo. Lakini la pili, Chama cha Mapinduzi hakikuishia kujenga viwanja tu wakati wa Mfumo wa Chama kimoja. Kilifanya kazi pia ya kumwandaa Dokta Slaa kuwa mwanasiaya mzuri ndio maana alikuwa sehemu ya viongozi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, niseme tu hata katika mfumo wa kawaida wa chama chochote katika Chuo cha Kujenga Viongozi ambacho kinakusudiwa kujengwa na CHADEMA mwanachama wa CCM Sabodo amechangia. Atakuwa mwehu kweli mtu wa CCM akija kudai kile chuo ni chake kwa sababu Sabodo kachangia. Kwa hiyo, niseme tu CCM itaendelea kumiliwi viwanja hivyo lakini itakapotekea mahitaji ya kuvimarisha kwa ajili ya wananchi wote kuvitumia Serikali haitasita kushirikiana na CCM. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu, kwamba na vyama vingine vijenge. Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nilipochangia kwa maandishi nilitaka kujua mkakati wa Serikali katika uibuaji wa vipaji vya vijana wetu katika ngazi za vijiji na shule za msingi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kama ambavyo tumekuwa tunasema mara kwa mara. Katika mkakati wa kuinua vipaji ndio maana Serikali imefanya uamuzi wa kurudisha michezo mashulen na sasa hivi tunatengeneza mikakati ya muda mrefu zaidi ambayo tunaita *community sports* ambayo itatusaidia sana katika jambo hili. Kwa hiyo, Wabunge watupe muda tunawahakikishia kwamba tutalifanya hilo.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Kwa sababu hii Wizara inaitwa ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kule Wilayani kwetu tuna Maafisa Utamaduni. Hawa maafisa utamaduni wamesahaulika kabisa na Serikali wanachukulwa kiraishi rahisi kiasi cha kwamba wanaonekana ni washehereshaji na Serikali naomba itoe maelezo ina mpango gani katika kuwajengea uwezo Maafisa Utamaduni hawa wa Wilaya ili angalau waweze kuwa hata Wakuu wa Idara?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la kuboresha muundo wao ili waweze kuifanya kazi yao kiufasaha linafanyika kama nilivosema kwenye maelezo ya awali, lakini pia nirudie kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kutumia ushawishi wao kwenye Halmashauri zao kuona kwamba Halmashauri zinawapa uzito na vitendea kazi Maafisa Utamaduni ili wafanye kazi zao vizuri.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kwa nini kuna tofauti kubwa ya mishahara kati ya makocha wa kigeni na makocha wazawa kitu ambacho kinapelekeea kukatisha tamaa makocha wazawa na wakati wana ujizi na uwezo mzuri wa kuweza kufundisha timu zetu za ndani?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa makocha wa Kimataifa wapo kwenye soko, usipomchukua wewe watamchukua wenzako na ndio maana nimesema kwenye maelezo yangu ya awali kwamba tutawatumia makocha hawa wa kigeni kusaidia na kuwajengea uwezo makocha wetu. Tukikaa hapa na kusema makocha wetu wana uwezo, tutaendelea kuwa nyuma. Sasa hivi nchi yetu iko nyuma kwelikweli kwenye michezo na tunatakiwa kutoka hapa tulip na hatuwezi kutoka kujisifiasifia.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona. Wanasaikolojia wanasema watu wanaweza kushughulikia yale matatizo yanayoonekana au kusikika kwenye redio. Sasa kuna Wilaya nyingi ambazo haziripotiwi. Kwa hiyo, Serikali kwa kushirkiana na *TBC* na vyombo vingine vya habari, ina mpango gani wa kuajiri waandishi kwenye Wilaya kama Kibondo ambayo inaweza ikakaa mwezi mzima bila kupata habari yoyote.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu mwanasaikolojia Mheshimiwa Mkosamali kama ifuatavyo: Serikali ina waandishi wa kutosha katika mikoa lakini ni kweli kwamba hatuna waandishi katika ngazi za Wilaya. Kwa sasa tulionao hawa wa Mikoa wa *TBC* tutawapa maelekezo ya kufuatilia zaidi habari za maeneo ya Wilayani na hasa hasa kwa rafiki yangu Mkosamali.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kutokana na shule zetu za sekondari kuweka michezo kuwa ni sehemu ya mitaala yake na walimu kupata nafasi ya kupata nafasi ya kwenda kusomea *Diploma* za Michezo. Lakini walimu hao linapokuja suala la kupandishwa vyeo *Diploma* hizo zinasemekana kwamba hazitambuliki na hivi kuwakatisha tamaa kabisa. Leo nimepata simu kutoka kwa walimu wa Manyara, Ruvuma na Mbeya na kwenye maandishi nililuliza. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze atalifanya vipi suala hilo ili

kutokuwakatisha tamaa walimu hao na hasa ikizingatia kwamba amesema sasa hivi kuna viwanja veya *community* vitajengwa na vitahitaji walimu kama hao.

**MWENYEKITI:** Leo Mhandisi amevaa hijabu au? Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba yapo malalamiko ya walimu kwamba wakishapata mafunzo ya michezo hayazingatiwi katika utaratibu wao wa kupanda yleo. Serikali inayafanya kazi malalamiko hayo tuone namna ya kuyaondoa.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Katika mchango wangu wa maandishi nilitoa ushauri kwa Serikali kwamba kwa kuwa utamaduni wa Kitanzania ni mkusanyiko wa tamaduni za makabila mbalimbali yaliyoko hapa nchini na nyenzo kubwa ya kuhifadhi tamaduni hizi ni lugha za makabila haya. Je, Serikali iko tayari kuenzi utamaduni wake kwa kuanzisha vipindi nya matangazo kwa radio nya makabila mbalimbali kupitia *FM Radios* zilizoko katika Mikoa?

**MWENYEKITI:** Lakini kuna makabila mengine kama Kisukuma inawezekana? Mheshimiwa Waziri ufanuzi. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haiko tayari kuanzisha utaratibu wa kutumia lugha za makabila katika radio zetu.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa lengo la Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulilenga kwa mikoa yote Tanzania. Je, Mheshimiwa Waziri anaahidi vipi kwa ile Mikoa ambayo haikupata fursa hiyo na hususan Jimbo la Kalambo?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ni kweli Mfuko wa Vijana ulilenga kuhudumia maeneo yote ya Tanzania lakini kutohaka na uchanga wake umeshindikana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Kandege kwamba tutakapokuwa tunaingia kwenye awamu nyingine ya Mfuko huu tutazingatia maeneo mengine ambayo hayajapata hususan katika Jimbo la Kalambo.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kupata ufanuzi wa Serikali kwamba ina mpango gani wa kujenga kiwanja cha kisasa cha michezo wa ngumi na ukizingatia pale Kibaha tuna eneo kubwa sana la kujenga kiwanja hicho?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kiwanja cha michezo wa ngumi kitakuwa katika mpango wa awamu ya pili ya ujenzi wa uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ningependa tu kupata ufanuzi, ni hatua gani Wizara imechukua kwa uzembe na aibu kubwa ambayo mlilitia Taifa hili wakati wa Mechi ya Tanzania na Morocco, Wimbo wa Taifa haukupigwa, jambo ambalo limejirudia. Kwa sababu kwanza, Brazil, ilikuwa hivyo hivyo na mkaomba radhi hapa. Hilo limejirudia. Lakini hata na mashindano ya Kagame, Uwanja wetu mzuri, mechi zilizokuwa zinaonyeshwa na *SuperSports*, ilikuwa inaonyesha kabisa kwamba nyavu za golini zimechanika na zilikuwa zinafungwa na kamba ya katani iliyooza. Lakini na bomba la chini halikuwepo. Ile ni aibu kwa Taifa letu. Nataka kujua hatua mlizochukua ukiachilia mbali ile hatua ya kumsimamisha kazi yule kiongozi wa *TFF*, Kajage, yule siyo mfanyakazi wa Serikali. Ninii watu wa Serikali ambao mliwajibika kuhakikisha ziara ya Rais inafanikiwa, mmechukua hatua gani kwa watendaji wenu? (*Makof*)

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwanza kumshukuru Mheshimiwa Azzan kwa swali lake zuri. Nnimevutiwa na ufundi wake wa kutambua nyavu zilizooza kupitia kwenye *TV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiliacha hilo, niseme tu, suala la Wimbo wa Taifa lilishachukuliwa hatua kwa wale ambao walitakiwa washughulikie jambo hili. Sisi kama Serikali tumeridhika na hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatizo la nyavu, sisi kama Serikali tumekwishalifanya kazi tatizo hilo, limekwishaondolewa. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Azzan, amekuwa akifuatilia sana ubora wa Uwanja wa Taifa, nitaendelea kushirkiana naye kuona matatizo hayo hayarejei.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa orodha yangu naona kama nimekwisha-cover wote, lakini kama kuna Mheshimiwa Mbunge yejote ambaye sikumgusa, asimame mahali pake! Nawashukuruni sana, wamekwisha wote.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*.....Sh. 206,556,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1003 – *Policy and Planning* .....Sh.1,142,494,200/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Subvote 1003*, kifungu kidogo 271200, ambayo ni *current grants to households and unincorporated business*, jumla milioni 729 na ushee.

**MWENYEKITI:** Uko kwenye *subvote* ipi Mheshimiwa Cheyo?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** *Subvote*, kwanza, tunaanza na 1003 ambayo ni *subvote* ya *Policy and Planning*, halafu tunateremka pale chini unaingia *subvote* 271200. Kwanza, nashukuru kwa kunikaribisha. Nilikuwa na shughuli ambazo ilikuwa lazima nizifanye pamoja na za Taifa. La pili, ukiwa nje kule, naliangalia Bunge hili, unaona umuhimu wa kuwa hapa. Lakini nawashukuru Wabunge, nawapongeza kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Hongereni sana wote! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nauliza, nimeangalia hii *sub vote*, ukiangalia zote ni milioni 16, mara moja ni milioni 769 na zote zinakwenda kwa *current grants to households and unincorporate business*. Mheshimiwa Waziri anaweza kulipa Bunge hili ufanuzi, haya ni matumizi ya vitu gani? Nilikuwa na fikir labda ni matumizi ya kutengeneza sera mpya au sheria mpya ya habari, lakini naona kama hizi fedha zinakwenda kwenye *households* na vitu vingine. Labda tueleze ili tuelewe fungu hili ni vitu gani hivi na zaidi kwa sababu havikuwepo zamani, mwaka huu ndio vimejitokeza. Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba fungu hili linatokana na Idara ya Maendeleo ya Vijana ambayo katika mwaka uliopita haikuwepo katika Wizara hii. Sasa, kwa sababu ya utaratibu wa Kiserikali, *subvote* yake inayojitegemea ilikuwa haijandaliliwa, kwa hiyo, ikawekwa kama *online item*. Kwa lugha hii Mzee Cheyo atanielewa.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1004 – *Information, Education and Communication*..... Sh. 123,783,000/=

Kif. 1005 – *Procurement Management Unit* .....Sh. 149,146,000/=

Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* .....Sh. 130,419,000/=

Kif. 1007 – *Information and Communication Technology* .....Sh. 343,933,000/=

Kif. 6001 – *Culture and National Languages* .....Sh. 2,798,560,800/=

Kif. 6004 – *Sports Development* .....Sh. 2,005,779,000/=

Kif. 7003 – *Information Services* .....Sh. 6,068,920,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 96 - Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Kif. 1001 – *Administration and General* .....Sh. 40,000,000/=  
Kif. 1003 – *Policy and Planning* .....Sh. 982,469,000/=  
Kif. 6001 – *Culture and National Languages* .....Sh. 952,984,000/=  
Kif. 6004 – *Sports Development* .....Sh. 1,365,398,000/=  
Kif. 7003 – *Information Services* .....Sh. 540,000,000/=

(*Bunge ilirudia*)

## TAARIFA

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi na ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja! (*Makofii*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)  
(*Hoja illamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Yalipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba ya Bunge zima, naomba niipongeze sana Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kupitia Mheshimiwa Waziri Dokta Emmanuel Nchimbi na Naibu wake Mheshimiwa Dokta Fenella Mukangara, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara hii pamoja na mashirika yake na taasisi nyingine ndani ya Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo mmekuwa mkilifanya kwa mwaka mzima. Tunawatachia kila la heri kupitia bajeti hii ambayo tunawapa, tunatarajia ufanisi utaongezeka, tija itaongezeka na tukikutana mwakani wakati kama huu, *Inshallah*, tunaamini kabisa kwamba tutakuwa tumepiga hatua kubwa katika maeneo yote ya vijana, utamaduni, habari na michezo. Kwa hiyo, tunawatachia kila la heri katika kutekeleza bajeti tuliyopitisha mbele yetu leo.

Baada ya maelezo hayo, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho kuanzia saa 3.00 tutaendelea na utaratibu ule ambao tuliyopitisha leo asubuhi baada ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi kuleta mapendeleko ambayo tuliyauinga mkono kwamba kesho siku ya Jumamosi tuendelee na kazi ya Bunge kama tuliyokubaliana kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini nayo iweze kutendewa haki yake na ratiba yetu iweze kuendelea kama tuliyopanga tangu mwanzo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, kwa kuwa basi, ratiba ya leo ya Kikao cha 45 cha Mkutano wetu wa Nne imekamilika, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(*Bunge illahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 13 Agosti, 2011 Saa Tatoo Asubuhi*)